**30 MEI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

_________

## MAJADILIANO YA BUNGE

__________

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Thelathini na Sita – Tarehe 30 Mei, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wa Kumi na Moja, Kikao cha Thelathini na Sita, leo tarehe 30 Mei, 2023. Tunaanza na Hati za Kuwasilisha Mezani, Waziri Mkuu, Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummy Nderiananga, karibu.

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):**

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya nchini ya mwaka 2022.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2022/2023, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Muharami Mkenge, kwa niaba ya Mwenyekiti.

Katibu tuendelee.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mbunge wa Ukonga aulize swali lake.

Na. 466

**Ujenzi wa barabara ya njia nne, Pugu – Viwege, Dar es Salaam**

**MHE. JERRY W. SILAA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Pugu - Majohe - Viwege njia nne na Kampala - Bwera - Rada hadi Chuo?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mbunge wa Jimbo la Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikizifanyia matengenezo barabara za Jimbo la Ukonga zikiwemo barabara za njia nne Pugu – Majohe hadi Viwege na Kampala – Bwera – Rada hadi Chuo ambapo katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 jumla ya shilingi milioni 701.67 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo yenye urefu wa kilomita 20.7 na kazi zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la matumizi katika barabara hizo limesababisha matengenezo yanayofanyika kutokudumu kwa muda mrefu. Hivyo Serikali imeingiza barabara hizi katika mpango wa uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam *(DMDP)* awamu ya pili, ili barabara hizo zijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa mradi upo katika hatua za awali za kufanya usanifu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jerry William Silaa.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naishukuru Serikali kwa majibu mazuri ya kuona mahitaji ya barabara za lami kwenye Jimbo la Ukonga. Naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mvua zinazoendelea kunyesha Jijini Dar-es-Salaam zimeharibu sana miundombinu ya barabara ikiwemo Jimbo la Ukonga, barabara nyingi zimekatika ikiwemo barabara ya Banana – Kitunda – Kivule – Msongola. Nini mpango wa Serikali wa kuzikarabati kwa dharura, hasa kipindi hiki ambacho wananchi wanapata taabu na barabara hizi?

Swali la pili. Barabara ya Mwembe Supu – Kwakupepeteka – Bangulo CCM mpaka Mwembe Kiboko kwenye Kata ya Pugu *Station* haijawahi kutengenezwa kwa kiwango chochote. Je, Naibu Waziri yuko tayari kuambatana na mimi kwenda kuona barabara hii na kuweza kutoa kauli ya Serikali mbele ya wananchi wa Kata ya Pugu *Station? (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Jerry Silaa kwamba, Mheshimiwa Mbunge amekuwa akilifuatilia sana hili suala, hasa la kupata fedha kwa ajili ya *emergency* kwenye barabara zake Jimboni kule.

Ninalitaarifu Bunge lako tukufu kwamba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Angellah Kairuki amekuwa akifanya vikao mbalimbali na wenzetu wa *TARURA* na Wizara ya Fedha kuhakikisha *TARURA* inaongezewa bajeti ya kutoka bilioni 11 ya *emergency* mpaka bilioni 46, niwatoe mashaka vikao hivyo vinaenda vyema na Wizara ya Fedha imeahidi kutafuta fedha hizo kwa ajitihada za Mheshimiwa Angellah Kairuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, nipo tayari kuongozana na Mheshimiwa Jerry William Silaa kuelekea katika Jimbo lake la Ukonga na kuzikagua barabara zake. Ninamuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaangalia ratiba hata *weekend* tutoke hapa tuelekee Jimbo la Ukonga tuweze kukagua barabara hizo na kuona ni kipi Serikali inaweza ikafanya.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Josephine Genzabuke na Mheshimiwa Christine Ishengoma.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika Halmashauri ya Kasulu Vijijini ipo barabara ya kutoka Mgombe kwenda Kagerankanda, barabara hiyo hutumika kwa wakulima kupitisha mazao kupeleka majumbani kwao.

Je, ni lini Serikali itatoa pesa kwa *TARURA* ili barabara hiyo iweze kutengenezwa?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Genzabuke kuhusu hii barabara ya Mgombe iliyopo kule Kigoma:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari inafanya jitihada kubwa sana za kuhakikisha *TARURA* inakuwa na fedha ya kutosha ya kufanya matengenezo ya barabara mbalimbali hapa nchini. Tukirudi katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 *TARURA* ilikuwa ina bajeti isiyozidi bilioni 226, lakini kwa jitihada za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, *TARURA* imeongezewa fedha zaidi ya mara tatu na kwenda kuwa na bilioni mia saba na sabini na kitu. Hivyo nimtoe mashaka Mheshimiwa Genzabuke kwamba, *TARURA* itafikia barabara hizi na kuhakikisha zinatengenezwa kwa wakati kadri ya upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga Barabara ya kuanzia pale *SUA* mpaka Mzinga Jeshini - Magadu, katika Manispaa ya Morogoro Mjini? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaangalia katika bajeti hii iliyopitishwa na Bunge lako tukufu ya 2023/2024 kwa *TARURA*, kuona kama barabara ya *SUA* kwenda Mzinga imetengewa fedha. Kama haikutengewa fedha katika mwaka huu wa fedha basi tutaiangalia ni namna gani inaweza ikatengewa fedha katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 467

**Ujenzi wa barabara za mitaa na mifereji Mkoa wa Dar es Salaam**

**MHE. JANETH M. MASABURI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuubadilisha Mkoa wa Dar es Salaam kwa kujenga barabara za mitaa, mifereji na miundombinu mingine?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Janeth Maurice Masaburi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2021/2022 – 2022/2023 Serikali ilitenga shillingi bilioni 100.06 kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara ambapo kilomita 47.77 za lami, kilomita 1,896.966 za matengenezo ya barabara, madaraja na makalvati 70 pamoja na taa za barabara 862. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, jumla ya shilingi bilioni 48.68 zimetengwa kwa ajili ya kazi ya barabara katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango uliopo sasa ni wa kuanza utekelezaji wa Mradi wa Uendelezaji Jiji la Dar es Salaam Awamu ya Pili *(DMDP II),* pamoja na maboresho ya Mto Msimbazi na Daraja la Jangwani. Miradi hii itahusisha ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya barabara, mifereji ya maji ya mvua pamoja na madaraja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janeth Maurice Masaburi.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ambayo sijaridhika kidogo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na bajeti kuwa ndogo ambayo haikidhi mahitaji halisi ya barabara za Mkoa wa Dar es Salaam, ukizingatia Dar es Salaam ina wakazi wengi ambao unaweza kulinganisha na Mikoa minne, mitano ama sita katika nchi hii.

Je, Serikali haioni haja ya kuunda mamlaka itakayoshughulika na barabara za Mkoa wa Dar es Salaam? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa, Mkoa wa Dar es Salaam hatuna ruzuku ya pembejeo, mbolea, shida yetu ni barabara, mifereji, madaraja, labda na *panya road.*

Je, Serikali haioni huruma kwa adha wanayoipata wananchi kwa kuhangaika na ukizingatia sasa hivi barabara nyingi zimejengwa kutokana na ujenzi wa reli na barabara zile za *BRT? (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Massaburi:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la bajeti ndogo kwa Barabara, nimuarifu Mheshimiwa Masaburi kwamba ni jitihada za Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuhakikisha barabara za Jiji la Dar es Salaam zinapitika wakati wote na kutengenezwa kwa kiwango cha lami, kwanza kwa kuweka shilingi bilioni 800 na zaidi ya hapo katika Mradi wa *DMDP I.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa siku hizi mbili hapa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Angellah Kairuki, amewakaribisha Wabunge wote wa Dar es Salaam kwenda kushuhudia utiaji saini wa mikataba ya *consultants* katika mradi wa *DMDP II* ambapo nao ni *commitment* kubwa ya Serikali katika Jiji la Dar-es-Salaam, kuhakikisha barabara zote zinapitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninakuomba Mheshimiwa Massaburi uwe na subira na wananchi wa Dar es Salaam Serikali inaweka fedha zaidi tena ya bilioni 800 katika kutengeneza miundombinu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili la kwa nini Serikali isiongeze miundombinu kama reli na kadhalika. Hili tunalipokea kama Serikali na tutakaa na wenzetu wa Wizara ya Ujenzi kuona ni nanma gani tutaboresha zaidi miundombinu, lakini tayari kama nilivyosema hapo awali katika mradi huu wa *DMDP II,* Dar es Salaam inakwenda kupendezeshwa chini ya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha barabara

zinapitika, mito inajengwa vizuri na mifereji ya kupitisha maji ili wananchi wa Dar es Salaam waweze kufanya shughuli zao za kiuchumi bila kupata bughudha yoyote ya kiusafiri.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mheshimiwa Tumaini Magesa na Mheshimiwa Furaha Matondo.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia fursa ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mkoa wa Dar es Salaam ni Mkoa mkubwa na ni Jiji la kibiashara, kwa kuzingatia vigezo vyote, kwa maana ya idadi ya watu, kiuchumi na idadi ya magari ni kubwa sana. Je, nini mtazamo wa Serikali wa kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi na Kuendeleza Jiji la Dar es Salaam kwa maana ya Dar es Salaam *Metropolitan Authority*?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Ndugulile la kwa nini Serikali isianzishe Mamlaka ya Usimamizi wa Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tunalipokea kama ushauri na tayari Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa maelekezo yake Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Angellah Kairuki, kuna timu ambayo inaliangalia hili na kuona ni namna gani linaweza kufanya kazi, pale timu hii itakapowasilisha ripoti hii kwa Mheshimiwa Waziri, basi tutaona hatua zinazifuata za kuchukuliwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tumaini Magesa, nilikutaja na Mheshimiwa Furaha Matondo.

**MHE. TUMAINI B. MAGESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi ya swali moja la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara, mitaro, mifereji na madaraja katika Mji Mdogo wa Katoro ambazo ni Kata tatu za Ludete, Katoro yenyewe na Nyamigota ni mbovu. Je, nini mkakati wa Serikali…

**MWENYEKITI:** Sauti, sema vizuri Mheshimiwa Waziri akusikie vizuri.

**MHE. TUMAINI B. MAGESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara, mitaro na madaraja katika Mji Mdogo wa Katoro ni mibovu, katika Kata tatu za Ludete, Nyamigota na Katoro yenyewe. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba miundombinu hiyo inatengenezwa ili wananchi waweze kuhudumiwa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kwamba, taasisi yetu ya *TARURA* ambayo inasimamia barabara za Mijini na Vijijini inakuwa na fedha ya kutosha kwa ajili ya kutengeneza barabara hizi, zikiwemo za Mji Mdogo wa Katoro, ndiyo maana Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeiongezea fedha *TARURA* mara tatu ya bajeti iliyokuwepo 2021. Hivyo, tutakaa na Mheshimiwa Mbunge kuona katika barabara hizi za Mji Mdogo wa Katoro kama zimetengewa fedha kwenye mwaka huu wa fedha tunaoenda kuuanza Julai na kama hazijatengewa fedha basi tutahakikisha zinatengewa fedha katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Furaha.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Jimbo la Ukerewe limekuwa likipata wakati mgumu sana wa kupata Wakandarasi na Wakandarasi kushindwa kuja Ukerewe kwa sababu ya gharama kubwa ya kusafirisha vifaa vyao. Nini mkakati wa Serikali wa kuichukulia Ukerewe kama eneo maalum la kibajeti kwa ajili ya barabara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, tayari kuna timu ambayo inafanya tathmini kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuangalia jiografia ya nchi yetu, kuona bajeti inayopelekwa kwa ajili ya barabara na kama kuna uwiano ambao ni sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, timu ile tayari ilikuwa imemaliza kazi yake na sasa imepelekwa kwa *independent consultants* kuweza kuiangalia vilevile taarifa ile na kisha mapendekezo yale yakirudi basi *formula* ya kutoa fedha iweze kubadilika kadri ya mapendekezo ambavyo yatakuja kwa ajili ya utengenezaji wa barabara. Hivyo, basi nimtoe mashaka Mheshimiwa Mbunge kwamba, naamini katika maeneo yenye jiografia ngumu ya ufikaji kama ya Ukerewe na yenyewe timu hii itakuwa imeangalia hayo matatizo ambayo yapo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Swali la Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, Mbunge wa Singida Mjini, litauliulizwa kwa niaba  na Mheshimiwa AYsharose Matembe.

Na. 468

**Mradi wa *TACTIC* Singida Mjini**

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE K.n.y. MHE. MUSSA R. SIMA** aliuliza:-

Je, lini Mradi wa *TACTIC* utaanza Singida Mjini?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, Mbunge wa Singida Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Manispaa ya Singida ni miongoni mwa Miji 45 ambayo imepewa kipaumbele cha kupata ufadhili wa Mradi wa Uboreshaji Miundombinu ya Miji, Manispaa na Majiji ya Tanzania ambao unaitwa Tanzania *Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness (TACTIC) Project*. Ufadhili huu ni wa Serikali Kuu kupitia mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia ambapo unaratibiwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mradi huu unatekelezwa katika Miji ya Tanzania kwa awamu tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya pili ina Miji 15 ikiwemo Halmashauri ya Manispaa ya Singida. Serikali inatarajia kutangaza zabuni za kuwatafuta wasanifu *(Design Consultants)* mwishoni mwa mwezi Mei, 2023 ambapo wasanifu watakapopatikana wataanza kazi ya usanifu mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2023/2024 na ujenzi utaanza mwishoni mwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aysharose Mattembe.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja la nyongeza. Napenda kufahamu: Je, mradi huu utazingatia ujenzi wa soko la vitunguu na Soko Kuu la Ipembe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sima ambalo limeulizwa kwa niaba yake, mradi huu unazingatia miradi ile ambayo ilipendekezwa na Halmashauri za Manispaa, Halmashauri za Majiji na *Town Councils* wenyewe. Kwa hiyo, huwa mapenekezo yanaletwa kwa wenzetu wa *TARURA* kupitia waratibu wa mradi huu wa *TACTIC*. Yanapoletwa, basi wanachambua na *30 percent* ya miradi ile iliyoletwa, ndiyo ambayo inapitishwa na kutengewa fedha. Kwa hiyo, kama wao wenyewe Manispaa walileta soko hili la vitunguu na soko kuu, basi naamini itakuwemo katika mradi huu wanapopatikana hao *Consultants* kufanya usanifu.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Priscus Tarimo.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri; je, Manispaa ya Moshi katika Mradi huu wa *TACTIC* itaanza lini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotoa maelezo kwenye majibu yangu ya msingi, hivi sasa wapo katika kuwapata *consultants* wa ku-*design* miradi hii na pale watakapopatikana, basi *designs* zitafanyika na ndipo mradi huu utaanza mwisho wa mwaka wa fedha 2023/24.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mradi huu pamoja na mambo mengine utahusisha ujenzi wa miradi ambayo itakuwa chanzo cha mapato katika hiyo miji 45; na kwa kuwa huu ni mkopo: Je, Serikali haioni umuhimu wa kukaa na Benki ya Dunia ili awamu ya pili na awamu ya tatu zote zikaenda pamoja ili utekelezaji wa mradi huu uanze mapema? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tunalipokea. Tutakaa na wenzetu wa Wizara ya Fedha ambao ndio wanzungumza na *World Bank* kuona kama hili linaweza likafanyika, lakini kwa sababu ya ukubwa wa miradi hii ni lazima iende kwa awamu ili kuhakikisha *monitoring* ya miradi hii inakuwa ni nzuri ili fedha zinazoletwa, kama alivyosema yeye mwenyewe, Mheshimiwa Chumi, kwamba ni mkopo, hivyo basi Watanzania watalipa, zisitumike vibaya. Kwa hiyo, ni vyema tuka-*monitor* miradi hii kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Chumi kwamba miradi hii itafika katika maeneo yote ya majiji haya 45 kwa wakati ambao umepangwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ni lini sasa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni nayo itaingizwa kwenye Mradi wa *TACTIC*? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, tukimaliza tathmini ya hizi *tier* tatu za miji hii 45, ndipo tutaangalia kama Serikali kuona uwezekano wa kuongeza Miji, Halmashauri za Manispaa na Halmashauri nyingine *DC* ambazo zipo nchini, ikiwemo ya Manyoni. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge avute subira, na pale ambapo tutakamilisha mchakato huu, kama nilivyokuwa nimemjibu Mheshimiwa Chumi, basi tutaangalia na maeneo mengine ya nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, Mbunge wa Hanang; aulize swali lake.

Na. 469

**Kuihamishia bararaba ya Hilbadaw – Bashnet *TANROADS***

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA** aliuliza:-

Je, lini barabara ya Hilbadaw – Bashnet itahamishiwa *TANROADS*?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Samweli Hhayuma, Mbunge wa Jimbo la Hanang kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007, kifungu cha 11 na Kanuni za Usimamizi wa Barabara ya mwaka 2009 Kifungu 43(1) na (2) na kifungu 44(1) kupitia Tangazo la Serikali Na. 21 ya tarehe 23 Januari, 2009, imeainisha vigezo vya utaratibu wa kuhamisha barabara ili iwe chini ya *TANROADS* ambapo barabara inaweza kupandishwa au kuteremshwa kutoka daraja moja kwenda daraja lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na sheria hii, barabara ambayo inakidhi vigezo kutoka daraja la barabara ya Wilaya kwenda daraja la barabara ya Mkoa (kusimamiwa na *TANROADS)* inatakiwa ijadiliwe kwenye kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa na ikionekana inakidhi vigezo, Bodi hiyo kupitia Mwenyekiti itamshauri Waziri mwenye dhamana na barabara husika, kwamba barabara hiyo imekidhi vigezo na kupandishwa hadhi. Hivyo, nashauri kwamba utaratibu huo uzingatiwe katika kupandisha hadhi barabara ya kutoka Hirbadaw – Bashinet kwenda *TANROADS*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la barabara hii ambayo inapita Lukhumeda – Setet kwa upande wa Babati, ambayo kwa Hanang inapita Bassodesh – Dang'aida – Hilbadaw, lakini ukienda upande wa Singida inaenda Singa – Ilongero – Singida, imejadiliwa kwenye kikao cha Bodi ya Barabara mwaka 2021. Hapa Bungeni nimeshaisema hii barabara zaidi ya mara tano; je, Serikali ina kauli gani juu ya nini kifanyike ili barabara hii iweze kufanyiwa kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwenye bajeti ya mwaka 2021/2022, tuliongeza bajeti ya *TARURA* kwa uwiano kwa majimbo yote, lakini kwa majimbo yale makubwa ambayo mtandao wa barabara ni mkubwa, fedha hizi ni kidogo; kwa mfano kwa Hanang tuna kata 33 na vitongoji 414; je, Serikali ina kauli gani kuziongezea bajeti zile Halmashauri kubwa au majimbo makubwa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Hhayuma, hili la kwanza la kauli ya Serikali juu ya barabara hii ya Hilbadaw – Bashnet iliyopo kule Hanang kupandishwa hadhi; kama nilivyoeleza kwenye majibu yangu ya msingi, hili ni takwa la kisheria la kupitisha barabara hii kwenye vikao hivi. Mheshimiwa Mbunge ameshasema barabara hii ilipitishwa mwaka 2021, hivyo basi, kwa sasa litakuwa

chini ya Waziri mwenye dhamana na barabara ambaye ni Waziri wa Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilitakiwa timu ije kufanya tathmini ya barabara hiyo kabla ya kuipandisha hadhi na kumshauri Waziri wa Ujenzi. Kwa hiyo, tutakaa na wenzetu wa Wizara ya Ujenzi na kuona hili limekwamia wapi? Pale lilipokwamia basi hatua ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili kuhusu uwiano wa bajeti ya barabara za *TARURA* katika majimbo mbalimbali hapa nchini, ikiwemo na Jimboni kwake Hanang; hapa wakati najibu swali mojawapo la nyongeza, nilisema tayari kuna timu ambayo inafanya tathmini ya maeneo yetu hapa nchini juu ya bajeti ya barabara ambayo inatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa *TARURA* ilirithi mfumo ule ule uliotoka kwenye Bodi ya Barabara wakati taasisi hii inaanzishwa. Tathmini ile itakapokamilika kuangalia maeneo ya kijiografia, kiuchumi na masuala ya kilimo yanayotokana na maeneo mbalimbali hapa nchini, basi *formula* mpya itatolewa. Kama nilivyosema, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, analifanyia kazi na timu yake muda siyo mrefu itamshauri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Manispaa ya Moshi, barabara inayotoka *YMCA* kwenda *KCMC* ni barabara ambayo ina msongamano mkubwa sana. Kuna Chuo cha Ushirika, kuna Chuo cha *CCP* Moshi na kuna Chuo Kikuu cha Katoliki, lakini kwenda pale hospitali kwenyewe watu wanaoenda kuona wagonjwa wanachelewa na wakati mwingine pia wanapata matatizo; bajaji zimo humo humo, bodaboda zimo humo humo, vi-*hiace* na hata magari binafsi; kutokana na majibu ya msingi, kwamba vikao vifanyike na ni matakwa ya sheria, vyote vimeshafanyika: ni lini

Serikali itaona umuhimu na udharura wa kubadilisha barabara hiyo kutoka *TARURA* kwenda *TANROADS*? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa barabara ya *YMCA* kwenda *KCMC* katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi. Tutakaa na wenzetu wa Wizara ya Ujenzi kuona hatua zipi ambazo wamezifikia katika kwenda kupandisha hadhi barabara hii kuwa barabara ya mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali kwenye majibu yangu ya msingi, kwamba haya ni matakwa ya kisheria, na yakishapita kutoka kwenye vikao hivi vyote na vikipitishwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Barabara ya Mkoa ambaye ni Mkuu wa Mkoa, sasa yanakwenda kwenye mamlaka ya Waziri wa Ujenzi ambaye ndiye mwenye dhamana ya barabara. Kwa hiyo, Serikali inalichukua na tutakaa na wenzetu wa barabara kuona imefikia wapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Noah Lemburis.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Jimbo la Arumeru Magharibi hivi karibuni mvua kubwa zimenyesha na kuharibu miundombinu kweli kweli yakiwemo madaraja, barabara na sasa wananchi hawana mahali ambapo wanapita katika maeneo haya ambapo yalitakiwa kujengwa maradaja mapya.

Ni lini sasa Serikali itapeleka hizo fedha za dharura ambazo tumeziomba kwa ajili ya kuokoa wananchi ambao hawana jinsi ya kwenda shambani, hospitali au popote wanapohitaji kupata huduma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa sasa kupitia Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini *(TARURA)* inaangalia namna ya kupata fedha za ziada za dharura. Bajeti ya *TARURA* kwa ajili ya dharura kwa mwaka ni shilingi bilioni 11. Kama nilivyosema hapo awali, tayari Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kairuki, ameshakaa na Waziri wa Fedha kuona ni namna gani *TARURA* inaweza ikaongezewa fedha za dharura kwenda shilingi bilioni 46 ili barabara hizi zilizoharibika katika kipindi hiki cha mvua ziweze kutengenezwa, zikiwemo hizi za kule Arumeru Magharibi kwa Mheshimiwa Lemburis. Pale ambapo Wizara ya Fedha itaridhia *TARURA* kuongezewa fedha hii, basi barabara hizi zitaanza kutengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, nimalizie tu kwa kusema kwamba tunakwenda kuanza kutekeleza mwaka mpya wa fedha mwezi mmoja na siku kadhaa zijazo (mwezi Julai), hivyo basi, wataona barabara hizi zitengenezwe katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Katika kikao cha Barabara cha Mkoa wa Kilimanjaro na Kikao cha *RCC* cha Mkoa wa Kilimanjaro, tulipitisha barabara kadhaa tangu mwaka juzi kupandisha hadhi kutoka *TARURA* kwenda *TANROADS;* na tayari kikoa cha mwisho cha *RCC* Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa alituambia ameshawasilisha Wizarani ili barabara hizi ziweze kupandhishwa hadhi.

Je, ni lini sasa barabara hizi za majimbo yote ya Mkoa wa Kilimanjaro na Hai zitapandishwa hadhi kutoka *TARURA* kwenda *TANROADS?*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni takwa la kisheria kwamba barabara hizi na vikao vyote vinavyokaa kule vya kisheria katika ngazi ya wilaya na mkoa zinafikishwa kwa Waziri mwenye dhamana na barabara ambaye ni Waziri wa Ujenzi. Hivyo, tutakaa na wenzetu wa Wizara ya Ujenzi kuona ni hatua zipi ambazo zimefikiwa na kupandisha hadhi barabara hizi za Mkoa wa Kilimanjaro, na Jimbo la Hai kule kwa Mheshimiwa Saashisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, kwa majibu hayo kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Tunaanza na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero.

Na. 470

**Mafunzo ya JKT kwa viongozi ngazi ya Wilaya na Mkoa**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Viongozi wa Serikali ngazi ya Wilaya na Mkoa wanashiriki mafunzo ya JKT ya muda mfupi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa

Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Kujenga Taifa linaendesha mafunzo kwa kundi la lazima *(compulsory),* kundi la kujitolea *(voluntary)* na kundi maalum *(special)*. Mafunzo ya kundi maalum hutolewa kulingana na mahitaji yanayowasilishwa na taasisi au Wizara husika na huendeshwa kulingana na maelekezo yanayotolewa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu kundi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu unaotumika katika kuendesha mafunzo ya makundi maalum ni kwa Wizara au taasisi kutuma maombi Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kisha Jeshi la Kujenga Taifa huelekezwa kuendesha mafunzo hayo, ambapo taasisi ama Wizara husika huyagharamia. Hivyo, endapo kuna uhitaji wa viongozi wa ngazi za wilaya na mikoa kuhudhuria mafunzo ya JKT kwa kundi maalum, basi Wizara au taasisi inayohusika na viongozi hao iwasilishe maombi hayo ili Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iweze kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naipongeza Serikali kwa nia yake ya kuwa tayari kwa mafunzo haya, na Wabunge wengi tulioenda katika yale mafunzo tulikuwa tunapata maswali mengi sana ya Wakuu wa Idara na baadhi ya Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wanaotaka kwenda kwa kujitolea, walikuwa wanauliza ni utaratibu gani ambao wanaweza kuufuata ili kushiriki mafunzo haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru sana Kambi ya Makutupora hapa, imetupa mafunzo mazuri sana na tunatoa ombi kwa Wabunge ambao hawajaenda waende kwa sababu kila siku wanatuambia kwenye *group* kwamba vifaa vyao viko pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yangu mawili ya nyongeza. La kwanza: Je, ni lini *intake* nyingine ya Wabunge na viongozi wa wilaya ambao wako tayari itaenda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kama nilivyosema, Kambi ya Makutupora iko hapa Dodoma, ni kaibu: Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza fedha ya bajeti kwa sababu JKT ni taasisi ya Kiserikali ili Kambi ile jirani ya Makutupora iweze kutoa mafunzo vizuri zaidi na kwa ufanisi zaidi, ikiwemo kujenga mabweni, vitanda na kadhalika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mara kadhaa wamekuwa wakienda kwenye kambi hizi kwa ajili ya kushiriki kwenye mafunzo haya ambayo yana nia ya kuwajenga Waheshimiwa Wabunge. Ni kweli kwamba wapo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hawajapata fursa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa niwaambie tu kwamba mara nyingi sababu zinazosababisha hizi, kwanza ni nafasi yetu sisi kama Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya majukumu ambayo tunayo. Lingine kubwa ni kutokana na utaratibu. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge kupitia Bunge hili, kama tulivyoeleza katika jibu la msingi, iombwe ruhusa, kwa maana ya kwamba tuombwe kibali maalum ili Jeshi la Kujenga Taifa liweze kutoa fursa hiyo ya Wabunge wengine kuweza kuendelea ama kupata mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niseme tu kwamba, kwa kuwa mafunzo haya yamelenga katika kuwajengea uzalendo, kuwajengea utayari, ukakamavu na ujasiri Waheshimiwa Wabunge na viongozi wengine wa taasisi nyingine, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutajitahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyoelezwa katika jibu langu la msingi, kwamba suala la uchangiaji gharama ni jambo la msingi; na kwa sababu tunatakiwa tuchangie gharama hizi kwa sababu ya mahitaji maalum yakiwemo afya, matibabu, chakula na vifaa vingine, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti inayofuata tutajitahidi tuongeze fungu maalum kwa ajili ya kutoa huduma hizi za mafunzo kwa Waheshimiwa wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Kusini, aulize swali lake.

Na. 471

**Kufungua benki katika miji ya Kalemie na Uvira nchini Congo**

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itashawishi mabenki kufungua benki nchini *Congo DRC* katika Miji ya Kalemie na Uvira ili kurahisisha biashara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo Mei, 2021 Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania iliipa Benki ya *CRDB* kibali cha kufungua kampuni tanzu Lubumbashi, nchini Congo ambapo inatarajia kuanza kutoa huduma za kibenki mara tu itakapopewa leseni na Benki Kuu ya nchi hiyo ya Congo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkakati wa Miaka Mitano wa Biashara wa Benki ya *CRDB* wa mwaka 2023 - 2028 unaonesha kuwa benki hiyo inatarajia kufungua kampuni tanzu zitakazotoa huduma za kibenki kwenye Miji ya Bukavu, Uvira na Kalemie nchini Congo. Hivyo, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kutoa ushirikiano kwa benki za biashara za hapa nchini kuanzisha kampuni tanzu nje ya nchi ili kusambaza huduma za kibenki katika nchi mbalimbali kwa lengo la kurahisisha ufanyaji wa biashara baina ya nchi na nchi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Kalemie na Uvira ni miji ambayo iko karibu sana na Mikoa ya Kigoma, Katavi na Sumbawanga: Je, Serikali haioni haja ya kufanya haraka kuhakikisha kwamba maeneo haya ya Uvira na Kalemie yamefunguliwa hizo *branches* za *CRDB?* Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Serikali imeona haja hiyo na ndiyo maana kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi,

kwamba Benki Kuu ya Tanzania ilishatoa kibali kwa *CRDB* sasa, lakini tumetoa wito kwa benki nyingine zote nchini ambazo ziko tayari kuwekeza katika miji hiyo ya Congo, basi Serikali imetoa idhini ya kufanya zoezi hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, kwa majibu hayo kwa maswali ya Mheshimiwa Mbunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo; Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 472

**Kurejesha Ardhi ya Kijiji Iliyochukuliwa na Kituo cha Utafiti wa Kilimo – Igeri**

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itarejesha kwa wananchi wa Kata ya Luponde Ardhi iliyochukuliwa kwa ajili ya Kituo cha Utafiti wa Kilimo Igeri ambayo kwa miaka mingi imekuwa haitumiki?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haina mpango wa kurejesha shamba la Utafiti wa Kilimo Igeri kwa kuwa kama nchi kuna uhitaji mkubwa wa uzalishaji mbegu. Shamba hilo lina ukubwa wa hekta 816, kati ya hizo, hekta 350 ni misitu ya kiasili, hekta 450 ni eneo linalofaa kwa kilimo na hekta 16 ni eneo lenye barabara na nyumba. Kwa sasa shamba hilo linatumika kwa shughuli za utafiti na kuzalisha mbegu za mazao mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imelima hekta 400 za mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imepanga kusafisha, kuweka fensi, kuchimba visima na kulima shamba lote kwa kuzalisha mbegu za awali na za msingi za mazao ya ngano na pareto kwenye hekta 348 na utafiti hekta 88.8. Lengo ni kujitosheleza kwa mbegu za zao la ngano na pareto kwa wakulima wa Njombe, Makete na sehemu nyinginezo. Aidha, natoa rai kwa wananchi kuacha kuvamia mashamba ya utafiti na uzalishaji wa mbegu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deodatus Mwanyika swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu ya Serikali hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza kwa kuwa kuna uhaba mkubwa sana wa ardhi maeneo ya Kata ya Luponde ambako ndiko shamba kubwa hilo lipo na mashamba makubwa ya chai yako kule, na vijana ni wengi sana ambao wanauhitaji wa ardhi;

Je, kwa nini Serikali isifikirie ndani ya eneo hili ikagawa sehemu kuwapa vijana katika mpango wa *BBR* au *BBT*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kituo cha utafiti cha Igeri ambacho ndicho kimekuwa na shamba hili kwa muda mrefu sana kimekuwa *dormant* kwa miaka mingi sana hakujakuwa na uwekezaji, na vile vile kituo kidogo cha Ichenga ambacho ni cha utafiti eneo hilo hilo na chenyewe cha matunda kimekuwa *dormant* na hakina fedha na hakifanyi shughuli yoyote wakati tuna zao la parachichi ambalo linahitaji sana utafiti;

Je, Serikali ina mpango gani kutoa fedha za kutosha kwenye vituo hivi vya utafiti?

**MWENYEKITI:**Mheshimiwa Waziri majibu ya maswali hayo mawili.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza kuhusu vijana na ushiriki wa vijana kwenye kilimo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ya kwamba ni dhamira ya Serikali kuhakikisha vijana wengi zaidi wanashiriki kwenye kilim,o na ndio maana tumekuja na programu ya *BBT.* Na kwa kuwa kuna changamoto ya ardhi kama alivyosema, mimi nitaandaa safari kwenda jimboni kwake Mheshimiwa Mbunge tukakae na uongozi wa wilaya kwa pamoja tutafute namna bora ya kuweza kuwawezesha vijana hao washiriki kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili la kuhusiana na kituo hiki cha utafiti. Kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, mwaka wa fedha unaokuja wa 2023/2024 tumetenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunalima eneo lote kwa ajili ya kutayarisha mbegu zile ambazo ni *pre-basic seeds* na *basic seeds* ili baadaye tusaidie kwa ajili ya kuzisambaza, hasa kwenye zao la ngano na zao la pareto. Kwa hiyo nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba hatujakitelekeza, tumeshakitengea fedha, kitaanza kuwa *operational* kuanzia mwaka wa fedha ujao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Mohamed Monni nimewaona.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa changamoto kubwa ya wakulima wetu nchini ni upatikanaji wa mbegu bora; je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba mbegu bora zinapatikana kwa wakati ukiwemo Mkoa wangu wa Iringa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mkakati wa Serikali kwa kutumia Wakala wa Mbegu Tanzania *(ASA)* na wazalishaji binafsi kuhakikisha tunazo mbegu za kutosha kuweza kuwahudumia wakulima wa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya mbegu za kilimo katika mpango wetu ule wa Agenda kumi thelathini ifikapo mwaka 2030 ni kuwa na uzalishaji wa tani takriban laki sita na Hamsini elfu. Hivi sasa tupo katika uzalishaji wa tani 61,000 kama asilimia kumi ya mahitaji yetu katika mwaka 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, hivi sasa kwenye mashamba yetu yote ya *ASA* tumeweka mifumo maalum ya umwagiliaji ambayo itatuhakikishia uzalishaji wa mbegu zaidi ya mara mbili ndani ya mwaka mmoja, na hivyo wakulima wetu watapata mbegu kwa wakati kwa sababu hivi sasa tumeboresha mashamba yetu 16 na mbegu zitaanza kuzalishwa zaidi ya mara moja ndani ya msimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Monni nilikutaja, tutamalizia na Mheshimiwa Amar.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wilaya ya Chemba imetenga maeneo kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu na tafiti, na tunafahamu Taifa hili lina changamoto ya upungufu wa mbegu;

Je, nini mkakati wa Serikali wa kuyatumia maeneo haya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Chemba kwa utayari wao wa kutenga ardhi kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu na utafiti. Hivi sasa tuko nao katika mazungumzo ya mwisho kwa ajili ya kuanza kuanzisha shamba kubwa la uzalishaji wa Mbegu za mtama mfupi ambao una soko kubwa kwa kampuni ya bia Tanzania pamoja *WFP* na wakulima wakubwa wanapatikana ndani ya Mkoa wa Dodoma na Singida. Kwa hiyo

shamba hili ndani ya Chemba litakuwa kama mwokozi kwa wakulima wa kanda ya kati.

**MWENYEKLITI:** Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, nilikuona na Mheshimiwa Butondo.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kuwanyanyua vijana kupitia kilimo na Wilaya ya Nyang'hwale hatuna mazao ya kudumu ama ya kibiashara;

Je, Serikali ina mpango gani kufanya utafiti wa udongio ili na sisi tuweze kupata miche ama mazao ya kibiashara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hussein Nassor Amar rudia kwa ufupi.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie, Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia vijana wa Wilaya ya Nyang'hwale kupitia mpango wake wa kuwanyanyua vijana kupitia kilimo? Wilaya ya Nyang'hwale hatuna mazao ya kudumu ya kibiashara; je, Serikali ina mpango gani wa kuchukua udongo na kufanya utafiti ili na sisi tuweze kuwa na miche ama mazao ya kibiashara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mkakati wa Serikali wa kuhakikisha ya kwamba tunawahusisha vijana wengi kwenye kilimo na ndio maana tumekuja na programu hii ya *BBT*. Hatua ya awali ambayo tunaifanya kwanza kabisa tunashirikiana na mamlaka za mikoa husika kwa ajili ya utengwaji wa maeneo; na eneo la pili hivi sasa tumeanza kuichora ramani ya Tanzania kwa afya ya udongo ili tujue sehemu gani wanaweza kulima zao gani na sisi tuwasaidie jambo gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari njema ni kwamba katika mwaka ujao wa fedha tumekwenda kununua mitambo ya kisasa ya upimaji wa afya ya udongo. Badala ile ya mahabara tu tutakuwa pia na *mobile laboratory* ambazo zitakuwa zinatembea kupima afya za udongo. Tukija kukupimia kwako mkulima tutapima hapo hapo na nitakupa cheti hapo hapo kitakwambia kwamba katika udongo huu unaweza kulima mazao ya aina gani na utumie mbolea aina gani, na hiyo ndio itakuwa mkombozi kwa wakulima wan chi yetu ya Tanzania.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Butondo kwa ufupi.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Wilaya ya Kishapu na Mkoa wa Shinyanga unajihusisha sana na kilimo cha zao la kimkakati la pamba, lakini zao hili katika msimu huu limeshuka sana bei, kutoka shilingi 2,200 hadi shilingi 1060. Wakati huo gharama kubwa za uendeshaji ama uzalishaji wa zao hili umekuwa ukiongezeka ikiwemo pembejeo na gharama zingine;

Je, ni nini mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba inafanya kila jitihada kuona kwamba bei hii inapanda ili kumtia moyo na kumhamasisha mkulima ilimradi aweze kuondokana na gharama ya uendeshaji wa zao hili na hivyo kupata manufaa kutokana na zao hili la pamba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya bei ya mazao mengi hapa nchini inatokana na kwamba wakulima wetu wanatumia nguvu kubwa ya wanachokiingiza shambani na wanachokipata havilingani. Sisi kama Serikali tumekuja na mkakati ufuatao. Tunaamini kabisa mkulima wa Tanzania akilima kwa tija suala la bei halitakuwa changamoto kubwa sana. Kwa hiyo mkakati wetu wa kwanza kabisa wa kuanzia ni kuhakikisha kwamba wakulima wetu wanalima kwa tija na hivyo tumefanya yafuatayo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza tunasaidia kuendelea kufanya utafiti kwa ajili ya kuwapatia mbegu bora, cha pili ni kuwasaidia pia katika teknolojia ambayo itamsaidia mkulima aweze kulima kwa tija, na cha tatu ni usambazaji wa pembejeo kwa wakati ili mkulima aweze kufikia malengo yake. Hii itatusaidia sana kwenye kuhakikisha kwamba wakulima wetu wanalima kwa tija na hatimaye hata akienda sokoni bei ikiwa imeporomoka lakini atakuwa na uwezo mkubwa wa kuweza kufidia changamoto ambayo anaipata katika uwekezaji alioufanya shambani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi kuuliza swali;

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga benki ya kuhifadhi mbegu asilia zisije kupotea kabisa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka ya afya mimea na viuatilifu pale Arusha tayari tunayo benki ya uhifadhi wa mbegu za asili, na tunaendelea kufanya utafiti. Lengo letu ni kuzitunza na kuhakikisha kwamba zinaendelea kutumika na kuwaletea tija wakulima wetu wa nchi ya Tanzania.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Naibu Waziri Wizara ya Kilimo ahsante sana kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendela na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Mwakasaka Mbunge wa Tabora Mjini aulize swali lake.

Na. 473

**Wazee kukosa dawa katika hospitali nchini**

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua tatizo la ukosefu wa dawa kwa wazee wanaopata huduma ya matibabu bure katika hospitali nchini?

**MWENYEKITI:**Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na ukosefu wa dawa kwa wazee, Serikali imeamua dawa ambazo zinatumika sana na wazee zilizokuwa hazitolewi kwenye vituo vya afya na zahanati zianze kutolewa katika ngazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imewajengea uwezo watumishi wa vituo vya huduma za afya ili kuweza kufanya maoteo halisi kulingana na mahitaji ya dawa ya vituo husika.

**MWENEKITI:** Mheshimiwa Adamson Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa sasa Serikali imekiri kwamba kuna tatizo kubwa la upungufu wa madawa kwenye zahanati;

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapa wazee bima maalum ya afya ambayo inaweza ikawasaidia kupata dawa katika maduka ya watu binafsi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa sasa kuna mmomonyoko wa maadili miongoni mwetu kijamii wazee wakiwa wanaenda hospitali wengi hawawapishi katika zile foleni wanawaacha wazee wanapata shida.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kila hospitali inakuwa na madirisha maalum ya wazee kupata huduma haraka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake hili muhimu sana kwa ajili ya afya za wazee wetu. Kwanza nianze kwa kumwambia Mheshimiwa Mbunge, moja tuliposema tunakuja na Bima ya Afya kwa Wote, ndilo lilikuwa suluhisho la hili jambo, na unajua kwamba kwenye Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote tulikuwa na kipengele cha kuwalipia watu wasio na uwezo, kwamba wanakuwa na bima ya afya, maana yake na kuwa wazee wako sehemu ya hili. Lakini suala la kusema kwamba wapate bima maalum ili wakikosa ndani ya hospitali zetu dawa waweze kupata kwenye maduka binafsi; mimi nafikiri cha msingi hapa ni hospitali zetu, kwa maana ya vituo vya afya, hospitali za wilaya na zahanati zetu ziwe na dawa zote ambazo zinaweza kuwasaidia wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mikakati imefanyika; nafikiri Mheshimiwa Mbunge unajua jinsi ambavyo sasa hivi dawa zikifika kuna kamati za vijiji za kupokea dawa, Waheshimiwa Wabunge wanapewa ripoti na kila mtu anashiriki kwenye mchakato huu. Nina hakika hakutakuwepo na upungufu mkubwa na wazee watapata dawa zao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Charles Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize swali la nyongeza fupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Vunjo kuna vituo vya afya vinne tu licha ya kwamba tuna kata 16. Na hivi vituo vya afya vikiwemo Unyika Msae, *Marangu Head Quarter* ambacho ni kipya, Kilua Vunjo na Kahe havina uwezo wa kutoa huduma ya upasuaji, hususan kwa wanawake ambao ni wajawazito na hivyo wanalazimika kupewa rufaa kwenda kwenye hospitali za Mawenzi ambapo ni mabli au KCMC ambapo pia kuna usumbufu mkubwa;

Je, ni lini Serikali itatoa vifaa na madaktari ili vituo hivi viweze kutoa huduma hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Serikali ya Doctor Samia Suluhu Hassan ilipopeleka vituo vya afya kule kwa kweli lengo lake ni kufika mahali vile vile viweze kufanya upasuaji waweze kuwasaidia akina mama kule kule badala ya kuwapeleka mbali kama hospitali ya Mkoa anavyosema Mheshimiwa. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge kama suala ni ukosefu tutakuja kuangalia vituo vyako *specifically* kama *theater* ipo na vitu vingine vipo. Kama ni ukosefu wa vifaa tutashirikiana na wenzetu TAMISEMI tuone namna vitakavyoweza kupatikana ili huduma hiyo iweze kutolewa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Godwin Mollel, Naibu Waziri Wizara ya Afya ahsante sana kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Daud Protas Venant Mbunge wa Igalula aulize swali lake.

Na. 474

**Hitaji la Chuo cha VETA Jimbo la Igalula**

**MHE. VENANT D. PROTAS** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha VETA katika Jimbo la Igalula?

**MWENYEKITI:**Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Venant Daud Protas Mbunge wa Jimbo la Igalula kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa vyuo vya ufundi stadi katika kuwasaidia wananchi kupata ujuzi utakao wasaidia kutekeleza kazi zao za kiuchumi. Kwa sasa Serikali inatekeleza azma ya kujenga chuo cha ufundi stadi katika kila mkoa na wilaya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Igalula lipo katika Wilaya ya Uyui na kwa sasa Serikali inakamilisha ujenzi wa Chuo cha Wilaya ya Uyui. Ujenzi huo umefikia asilimia 97 na chuo hiki kimeshaanza kutoa mafunzo ya muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilisha ujenzi wa vyuo vya *VETA* katika wilaya zote nchini, Serikali itaangalia uwezekano wa kujenga vyuo vya *VETA* katika ngazi za majimbo na ngazi zingine za chini kadri ya upatikanaji wa fedha na uhitaji, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Protas Venant.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze Serikali kwa majibu mazuri. Ni kweli Wilaya ya Uyuwi tumepata chuo cha *VETA,* lakini kutokana na jiografia ya Wilaya ya Uyuwi na kuwepo kwa majimbo mawili, wananchi wa Jimbo la Igalula kwenda kuifata *VETA* ni zaidi ya kilometa 200.

Je, Serikali haioni haja sasa ya kunipatia upendeleo maalum wa kunipatia angalau hata shule ya ufundi ili niweze kuwa na shule

ya ufundi na wanachi wa Jimbo la Igalula wakanufaika na matunda ya Mama Samia Suluhu Hassan?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Venant Mbunge wa Igalula kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti,kama nilivyoeleza kwenye majibu ya swali la msingi kwamba ni azma ya Serikali kujenga vyuo hivi katika wilaya zote ikiwemo Wilaya ya Uyuwi, hivyo nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali wakati inajenga miundombinu hii vile vile tunatoa huduma za mabweni pamoja na zile za kutwa. Lakini vile vile tunafahamu, inawezekana huduma hizi za mabweni kwa wale wanafunzi wanaotoka mbali zinaweza zikawa sio toshelezi. Serikali vile vile inatambua kwamba kuna Wilaya ambazo ni kubwa na jiografia yake ni kubwa na zina majimbo zaidi ya moja. Nitoe tu mfano wa hiyo Wilaya ya Uyuwi lakini tuna Wilaya ya Bagamoyo, tuna Wilaya ya Lindi kuna Wilaya ya Bariadi kwa hiyo kuna Wilaya nyingi ambazo zinachangamoto aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, tunauchukua ushauri wake. Serikali ina mipango mingi endelevu na Serikali hii ya Mama Samia tunakwenda kufanya mambo makubwa kwa lengo la kusogeza huduma za elimu pamoja na elimu ya ufundi karibu. Kwa hiyo andaa tu eneo kwa ajili ya ujenzi wa hiyo shule uliyozungumza na Serikali ya Mama Samia ni sikivu. Tuna amini baada ya kukamilisha ujenzi wa vyuo hivi tunakwenda sasa katika ujenzi wa shule hizi za ufundi katika maeneo ambayo yamekosa vyuo vya *VETA*, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamga kwa ufupi.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa mpango Mkakati wa kujenga Vyuo vya *VETA* kila wilaya. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa kujenga Chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Simanjiro?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asia, Mbunge kutoka Mkoa wa Manyara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Simanjiro wenzetu wa Taasisi ya Upendo walijenga chuo kilikuwa hakijakamilika miundombinu yake lakini baada ya kujenga waliikabidhi Serikali. Chuo ambacho kipo katika Wilaya ya Simanjiro kipo katika Kijiji Engalakash katika Kata ya Emboret, lakini kilikuwa kimejengwa kweli na wenzetu wa Upendo na wamekwisha kabidhi Serikali na kilikuwa na miundombinu ifuatayo: Karakana mbili; Madarasa; Bwalo; Mabweni mawili; na Kisima cha maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha Serikali imepeleka pale milioni 190 kwa ajili ya kuongeza miundombinu ambayo tunakwenda kujenga Bweni moja, tunajenga nyumba za watumishi, lakini kulikuwa na changamoto za umeme. Kwa hiyo, tunasambaza umeme ndani ya majengo pamoja na nje ya majengo na tutaendelea kufanya hivi. Kwa hiyo, sasa hiki ndiyo kitakuwa Chuo cha Wilaya ya Simanjiro kinachomilikiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwondoe hofu tutaendelea kuongeza majengo kama tunavyofanya katika maeneo mengine kama vile Urambo, Nanyumbu na maeneo mengine ambayo tulikuwa na vyuo vya zamani vilikuwa na miundombinu ambayo sio toshelezi, tutakwenda kujenga miundombinu ili kutosheleza kutoa huduma ile ya *VETA* katika maeneo yote ya wilaya zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Juma Kipanga, Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

Na. 475

**Usambazaji wa maji Kata za Mbezi Juu, Wazo na Mabwepande – Kawe**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA K.n.y. MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha usambazaji wa maji Mitaa yote ya Kata za Mbezi Juu, Wazo na Mabwepande katika Jimbo la Kawe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha huduma ya maji safi na salama kwa wakazi wa maeneo ya Kawe, Kata za Mbezi Juu, Wazo na Mabwepande. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2022, kazi ya ulazaji wa mtandao wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilometa 391.306 ilikamilika kupitia mradi mkubwa chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi inayoendelea sasa ni ulazaji wa mabomba ya maji umbali wa kilometa 64.3 kuanzia ulipoishia mradi mkubwa kwenda maeneo ya Mpiji Magohe, Mbopo, Mbopo Chekanao na Kinondo na itakamilika mwezi Desemba, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilika kwa kazi hiyo, maeneo yote katika Kata za Mbezi Juu, Wazo na Mabwepande yatakuwa yamepata huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muuliza swali alisisitiza ukosefu wa maji katika maeneo ambayo ameyataja ya Mabwepande, Wazo pamoja na Mbezi Juu. Swali la kwanza; je, ni lini Serikali itaongeza *speed* ya kumaliza hiyo kazi ili wananchi Waheshimiwa Wabunge, pale waweze kupata hayo maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Mradi wa Maji kutoka Masoko katika Wilaya ya Rungwe unafanana kabisa kama ambavyo wanahangaika watu wa Wazo.

Je, ni lini watahakikisha watu wa vya Kasyeto, Mpumbuli pamoja na Segela wanapata maji kwa sababu ilipoanzishwa maji katika Mto Masoko tulitegemea sana watu wa maeneo haya wapate maji safi na salama na kwa wakati sahihi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge Viti Maluum, yaliyoulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lini Serikali itaongeza kasi? Tayari tumejipanga na na kuanzia sasa tunaongeza kasi na kuhakikisha maeno haya yote tunakwenda kuyafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Mradi wa Masoko Rungwe, Mheshimiwa Mbunge ni shahidi mimi na yeye tulishawahi kuongea tukiwa Mbeya na hili tutalifanya pamoja mimi na yeye baada ya Bunge hili na kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge

wa Jimbo, tutahakikisha hili suala la Mradi wa Masoko sasa linafikia mwisho wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Catherine, swali fupi la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu ya wakazi wa Jiji la Arusha kuletewa bili za maji tofauti na matumizi yao na hivi juzi Mamlaka ya Maji ya Jiji la Arusha imetangaza kuongeza gharama za maji kuanzia kesho. Je nini kauli ya Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Catherine Magige, Mbunge Viti Maalum kutoka Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nipende kumpongeza amekuwa akifuatilia sana suala la hizi bili za maji kwa Jiji la Arusha na maeneo yote. Hata hivyo, kwenye suala la ongezeko la bei ambaho imetangazwa hapo kesho ni utaratibu tu ambao upo kikanuni na tayari *EWURA* waliweza kufuata taratibu zote na kushirikisha wananchi kupitia mikutano mbalimbali ya hadhara ambayo iliweza kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na manung'uniko haya sisi kama Wizara tumelipokea na kuona namna gani tutalifanya. Lengo ni kuona huduma za maji zinabaki kuwa endelevu na zinaboreshwa kwa kutumia hizi fedha zinazochangiwa na wananchi, lakini vile vile kuhakikisha wananchi wanatumia katika gharama tunaziweza.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, Mbunge wa Karatu.

Na. 476

**Bei elekezi kwa *unit* moja ya maji – Karatu**

**MHE. DANIEL A. TLEMAI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatoa bei moja elekezi kwa kila *unit* moja ya maji Wilayani ya Karatu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, Mbunge wa Jimbo la Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya majisafi na usafi wa mazingira mjini Karatu inatolewa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu *(*Karatu *Urban Water Supply and Sanitation Authority - KARUWASA).* Awali kulikuwa na changamoto ya kuwepo kwa Taasisi mbili zinazotoa huduma ya maji ambazo ni Karatu *Village Water Supply (KAVIWASU)* na *KARUWASA* na kila moja ilikuwa na bei yake. Mwezi Agosti 2022, Serikali iliziunganisha taasisi hizo na kuwa na taasisi moja inayoitwa *KARUWASA* na kutoa bei elekezi ya maji ya shilingi 1,300 kwa *unit* moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa eneo la Karatu Vijijini linalohudumiwa na *RUWASA*, Serikali ilitoa bei elekezi kulingana na teknolojia inayotumika kuwafikishia wananchi maji na bei hizo zinafuatwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daniel, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Serikali nina swali moja la nyongeza. Kama katika Mji wa Karatu waliweza kushusha bei kutoka shilingi 3,500 mpaka shilingi 1,300 kwa *unit*. Je, inashindikana nini katika jimbo hilo

hilo katika eneo la *RUWASA* vijijini majini kuuzwa kwa shilingi 2,500, kwa nini kwenye jimbo moja isishushwe bei ikawa ya uwiano Karatu Mjini na Karatu Vijijini ikawa na bei moja kuliko kuwa na bei mbili katika Mji wa Karatu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, Mbunge wa Karatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei za maji hazifanani kwa sababu ya teknolojia zinazotumika kusambaza maji. Teknolojia ambayo inatumika eneo la *RUWASA* ni tofauti na pale mjini. Kwa hiyo sisi kama Wizara tunachokifanya ni kuhakikisha bei zinakuwa rafiki kwa wananchi wa eneo husika. Kwa hiyo, kwenye maeneo haya ambayo yanahudumiwa na *RUWASA* bei ziko tofauti kwa namna ambavyo maji yanasukumwa na gharama za uendeshaji.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Maryprisca Mahundi, Naibu Waziri wa Wizara ya Maji.

Waheshimiwa kutokana na muda tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Neema Gerald Mwanadabila, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 477

**Ukomo wa upelelezi wa kesi**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA** aliuliza:-

Je, ni lini Muswada wa Ukomo wa Upelelezi wa Kesi utaletwa ili kupunguza msongamano wa kesi unaotokana na upelelezi kutokamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 225(4) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20, ukomo wa upelelezi katika baadhi ya makosa ni siku 60 na kwa mujibu wa kifungu 225(5), Mahakama imepewa mamlaka kuifuta kesi ambayo upelelezi wake haujakamilika baada ya siku 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilifanya marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.1) ya 2022 kwa kuongeza kifungu cha 131A kilichoweka masharti kuwa isipokuwa kwa makosa mazito na makosa yote yanayosikilizwa na Mahakama Kuu watuhumiwa wasifikishwe Mahakamani hadi upelelezi uwe umekalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mkurugenzi wa Mashataka imetoa Waraka Na. 1 wa mwaka 2022, kuhusu Ufunguaji wa Mashtaka na Ukamilishaji wa Upelelezi wa Kesi za jinai uliotolewa tarehe 30 Septemba, 2022 na ulishaanza kutumika tarehe Mosi Oktoba, 2022. Waraka huo unataka upelelezi wa kesi za mauaji, kesi za makosa mazito na kesi zote zinazosikilizwa na Mahakama Kuu ambazo hazihitaji utaalam kutoka taasisi nyingine usichukue zaidi ya siku sitini (60) na zile zinazohitaji utaalam kutoka taasisi nyingine upelelezi usichukue zaidi ya siku tisini (90).

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mwanadabila, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Serikali ni mazuri na imeonesha kwamba sheria ipo, lakini ukweli ni kwamba utekelezaji wa sheria hii umekuwa ni hafifu sana. Pia kama hivyo ndivyo, Watanzania wengi wamekuwa wakiathirika

na utekelezaji huu hafifu wa hii sheria, kitu ambacho kinawafanya waathirike kisaikolojia, kijamii na hata kiuchumi. Vilevile wanapotoka na kuja mtaani baadaye watu hawa wanakua wamepoteza uelekeo sana lakini tunajua utekelezaji huu hafifu wa hii Sheria umeipa mzigo mkubwa sana Serikali kwa kuwahudumia watu ambao wanakaa muda mrefu rumande. Kitu ambacho tulivyofanya ziara mbalimbali tumeona kabisa kuna watuhumiwa wengi…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema, uliza swali.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wananchi wengi wako gerezani kwa zaidi ya miaka 15. Swali la kwanza; je, Serikali ina mkakati gani wa kuwalipa fidia watuhumiwa wote waliokaa mahabusu muda mrefu na kushinda kesi hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, nataka kufahamu ni nini kauli ya Serikali katika kufuta kesi zote za watuhumiwa waliokaa zaidi ya miaka mitano mahabusu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Naomba sasa nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Neema Gerald, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sio kweli kwamba haya tunayoongea hapa hayatekelezeki, ndio maana ukiangalia kwenye takwimu zetu za masijala za mahakama hadi jana tarehe 29/5/2023 mashauri ni 1,863 lakini *backlogs* ambazo hazijafanyiwa kazi ni asilimia nne tu. Hapa maana yake ni nini? Maana yake Mahakama imekuwa ikizisikiliza kesi hizi na zimekuwa zikihukumiwa na kuondoka na sasa katika mahakama zetu hakuna kesi ambayo mtuhumiwa yuko mahabusu mpaka sasa zaidi ya miaka mitano hajahudumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumshukuru Mheshimiwa Rais, amekuwa akiboresha mahakama zetu, amekuwa akiteua Majaji, amekuwa akitoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama Kuu na mwaka huu wa fedha tunakwenda kujenga Mahakama za Mikoa zaidi ya 14 ili Majaji hawa wakasikilize kesi hizi. Kwa hiyo, naomba nilihakikishie Bunge lako tukufu kwamba kwenye Mahakama kesi hizi zinasikilizwa na kasi imeongezeka ndio maana *backlogs* zimebaki asilimia nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, anataka kufahamu kama watu hawa waliokaa zaidi ya miaka mitano wanaweza wakafidiwa. Taratibu za kisheria na *principles* za kesi kwamba pale ambapo unaona kwamba mashtaka haya yamekamilika na unaona ulibambikiziwa kesi na imechukua muda mrefu unaweza kurudi Mahakamai kufungua kesi ya madai.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Pauline Gekul, Naibu Waziri Wizara ya Katiba na Sheria kwa majibu yako kwa Mheshimiwa Mbunge.

Tunamalizia Wizara ya Madini Mheshimiwa Kabula Enock Shitobela, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 478

**Njia mbadala ya matumizi ya matimba**

**MHE. KABULA E. SHITOBELA** aliuliza:-

Je, Serikali haina njia mbadala ya matumizi ya matimba kama ngazi ambayo yanamaliza miti na hivyo kuharibu mazingira?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Doto Biteko, majibu.

**WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabula Enock Shitobela, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa magogo ya miti ni moja ya teknolojia rahisi na muhimu katika ujenzi wa migodi ya chini ya ardhi kwenye shughuli za uchimbaji mdogo wa madini nchini, ambapo miti hiyo hutumika katika ujenzi wa kuta na dari za migodi ili kuweka mazingira salama ya migodi midogo kwa wachimbaji. Wachimbaji wadogo hununua miti hiyo kutoka kwenye hifadhi za misitu na mashamba ya miti kupitia mawakala wa miti kwa kufuata taratibu za uvunaji wa miti. Teknolojia ya matumizi ya magogo ya miti imeenea zaidi kwa wachimbaji wadogo kwa kuwa inasaidia kuimarisha usalama wa migodi na haihitaji uwekezaji mkubwa wakati wa ujenzi wa migodi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia zipo teknolojia nyingine zinazotumika kwenye ujenzi wa migodi ya chini ya ardhi ambazo hutumia zege na vyuma ili kuimarisha kuta na dari za migodi hiyo. Teknolojia ya zege na vyuma hutumiwa zaidi na Wachimbaji wa Kati na Wakubwa kwa sababu ni ghali ukilinganisha na wachimbaji wadogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabula Shitobela.

**MHE. KABULA E. SHITOBELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuna uwepo wa teknolojia mbadala, je, Serikali Serikali itaanza lini kutoa elimu ya matumizi ya matumizi ya teknolojia mbadala?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba matumizi ya teknolojia mbadala yapo na yanafanyika kwa wachimbaji wa kati na wakubwa lakini wapo pia wachimbaji wadogo ambao wana

uwezo wa kununua mahitaji hayo, wanaendelea nayo. Sasa, sisi kama Wizara tunaendelea kutoa elimu ya uchimbaji salama kwenye migodi ikiwemo matumizi ya teknolojia mbadala.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko, Waziri wa Madini kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umefikia ukomo kwa siku ya leo. Tunaanza sasa na matangazo yaliyoko mbele yetu leo. Kuna matangazo kwanza ya wageni ambao wako Bungeni asubuhi hii.

Tutaanza na wageni walioko kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika. Kuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Stegomena Tax, Waziri wa Mambo ya Nje na uhusiano wa Afrika Mashariki, tunaye Balozi Dkt. Samwel Shelukindo, Katibu Mkuu, karibu sana Katibu wetu Mkuu wa Wizara na Balozi Fatma Rajabu Naibu Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Tuna Luteni Gererali Ancelim Sanyatwe - *High Commissioner, Republic of Zimbabwe;* Ndugu Charles Kadonya, kwa Niaba ya Katibu wa Bunge wa *EALA;* Colonel Mumbi Mulenga- *Acting Coordinator, Southern African Development Community - Regional Counter Terrorism Center;* Balozi Radhia Msuya Mtengeti- Balozi Radhia Msuya Mtengeti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Bodi ya *APRM*; na Balozi Began Taj, - Mwenyekiti wa Bodi – *AICC*. *(Makofi)*

Vilevile kuna Balozi James Msekela - Balozi Mstaafu; Mhe. Jaji Imani Dauod Aboud - Rais wa Mahakama ya Afrika; Profesa Wineaster Anderson - Makamu Mkuu wa Chuo *UDOM;* Mheshimiwa Shogo Mlozi - Mbunge wa *EALA;* Mheshimiwa James Ole Millya - Mbunge wa *EALA;* Ndugu Ephraim Mafuru - Mkurugenzi Mwendeshaji *AICC;* Ndugu Felex Wandwe - Kaimu Mkurugenzi *CFR;* Ndugu Lamau Mpolo- Katibu Mtendaji *APRM*; Ndugu Haji Janabi - Mkurugenzi wa Sera na Mipango; Mheshimiwa Leuu Omary Abadalla - Kaimu Mkurugenzi Mambo ya Nje Zanzibar; na Balozi Yusuph Mndolwa - *Chief of Protocol,* karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, tuna Wakuu wa Idara na Vitengo wa Taasisi zilizopo chini ya Wizara, wote kwa pamoja karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Stergomena Tax, Waziri, ambao ni familia yake wakiongozwa na Bi. Elma Tax, karibu sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Kuna Wanafunzi 15 kutoka Chuo cha Diplomasia kurasini Dar es Salaam, karibuni sana wanafunzi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambao ni Balozi Luteni Jenerali Mstaafu Abdulrahman Shimbo - *Board Member* - Tanzania *China Friendship Association,* pia tunaye Meja Jenerali Mstaafu Khamis Semfuko ambaye ni *Board Member,* Tanzania *China Friendship Association*, pia tuna Ndugu Joseph Kulwa Kahama, Katibu Mkuu wa Tanzania *China Friendship Association*, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tuna Wawakilishi wa Jumuiya ya Kimataifa kutoka Ofisi za Kibalozi na Mashirika ya Kimataifa yaliyopo chini ya Wizara ambao ni *Honorable* Lebbius Tangeni Tobias - *High Commissioner Republic of* Namibia, *you are most welcome*. Honorable Ricardo Mtumbuida - *Ambassador Republic of Mozambique, you are welcome*. *Honorable* Yordenis Despaigne Vera - *Ambassador Republic of Cuba, you are welcome*. *Honorable* Chris Masocha - *Counsellor Republic of* Zimbabwe, you are *welcome*. *Miss* Epiphanie Buzizi - *Charge d'affaires, Republic of* Rwanda, you are *welcome*. *(Applause)*

*Mr.* Oguzhan Balci - *Deputy Head of Mission*, Turkiye *you are most welcome; Mr.* Bacar Salim - *Deputy Ambassador, Republic of Comoros, you are most welcome; Mr.* Wu Yuan - *Director of Political Affairs Unit, The People's Republic of China, you are most welcome. Mr.* Johnny Wang - *First Secretary, The People's Republic of China, you are most welcome; Mr.* Ryan Mitchell - *Political Officer of British High Commission, you are most welcome. Mr.* Ziyad Al-Atmi - *Deputy Charge'd'affaires, Republic of* Saudi Arabia, *you are most*

*welcome.* *Mr.* Meshari Almasoud - *Consul, Republic of* Saudi Arabia, *you are warmly welcomed. (Applause)*

Mr. Jealous Chiroye, *Representative – ILO, welcome. Mr.* Moses Ole Neselle, *Representantive - ECTAD Programme Analyst, – FAO, you are most welcome.* Dkt. Majaliwa Marwa, *Assistant Representative - UNFPA, you are most welcome. Mr.* Juvenali Ndimurirwo - *Director of Finance, EAC (East African Community).* Ms. Suma Mwakyusa, *Principal International Relations Officer, East African Community. Mr.* Musa Ngwegwe, *Liaison Officer - Southern African Development Community, Regional Counter Terrorism Center, you are most welcome. (Applause)*

Mr. Richard Mrema, *Finance & Administration Officer - Southern African Development Community, Regional Counter Terrorism Center, you are most welcome. Mr.* Eben Mnzava - *EAC Youth Ambassador to* Tanzania, *you are most welcome. Ms.* Diana Paul Chando, *AU Youth Ambassador for Peace, you are most welcome. Ms.* Kaneni Mushi - *Founder of Women in Diplomacy, you are most welcome. (Applause)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tunao wageni 33 wa Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao ni Kwaya ya Upendo kutoka Kanisa la Anglikana Kijiji cha Mlunduzi Jimbo la Kibakwe, wale pale juu karibuni sana. *(Makofi)*

kuna Mgeni wa Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Ndugu Mju Silima Makame, Mjumbe wa Kamati ya Siasa kutoka Jimbo la Uzini Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja, karibu sana mgeni wa Naibu Waziri, yule pale. *(Makofi)*

Tuna wageni watano wa Mheshimiwa Hussein Amar, Makatibu wa Siasa na Wenezi kutoka Wilaya Tano za Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Wageni 11 wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo ambao ni Watumishi wa Taasisi za Wizara na Wadau kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Doreen Sinare, Afisa Mtendaji Mkuu *COSOTA;* Ndugu Flora Mpanju, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Miliki Bunifu Afrika; Ndugu Wasiti Badi Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Azam Media, karibuni sana nyote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia Ndugu Johnson Mshana, Mwakilishi wa Mtendaji Mkuu *DSTV* na Ndugu Camila Owora – Mwakilishi *ZIIKI* Media, karibuni sana nyote. *(Makofi)*

Kuna wageni wawili wa Mheshimiwa David Kihenzile kutoka Mafinga Mkoa wa Iringa, karibu wageni wetu kutoka Mafinga. *(Makofi)*

Tunae mgeni wa Mheshimiwa Tumaini Magessa ambae ni Mwenyekiti Kata ya Butundwe kutoka Mkoa wa Geita, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo Katibu *UVCC* Kata Magata kutoka Muleba Mkoa wa Kagera, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 85 wa Mheshimiwa Anna Lupembe, Wanamaombi kutoka Dodoma na Kwaya Kuu kutoka Kanisa la *KKKT,* Usharika wa Segerea Jijini Dar es Salaam, karibuni sana wanakwaya. *(Makofi)*

Wageni 49 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Kwaya Kuu kutoka *Arusha Road* Jimbo la Makao Mkuu Dayosisi ya Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Magreth Sitta kutoka Urambo Mkoa wa Tabora, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili Mheshimiwa Josephine Genzabuke ambao ni watoto wake kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana wageni wote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tuna wageni pia waliotutembelea Bunge kwa ahili ya mafunzo ajili ya mafunzo wanafunzi na walimu 100 kutoka Shule ya Sekondari Itega, karibuni wanafunzi wetu katika Bunge letu, karibuni sana wageni wote ambao mmehudhuria leo katika Ukumbi wetu wa Bunge. *(Makofi)*

Katibu tunaendelea

**NDG. MONICA MWAGA-KATIBU MEZANI**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nitaanza kumuita Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili aweze kuwasilisha hotuba yake, karibu sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Stergomena Tax kwa ajili ya kuwasilisha.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge na Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji na Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2022/2023, na lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa unyenyekevu mkubwa nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ninaahidi kuwa nitaendelea kutimiza majukumu yangu kwa weledi, kujituma, kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

na kuimarisha Mahusiano ya Kimataifa na kulinda maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutimiza miaka miwili ya kuiongoza Taifa letu kwa ujasiri, maono mapana na mafanikio makubwa. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kama Mwanadiplomasia Namba moja, ameimarisha uhusiano baina ya nchi yetu na nchi mbalimbali, Taasisi za Kikanda na Kimataifa na kuliletea heshima kubwa Taifa letu. Ametekeleza Diplomasia ya Uchumi kwa vitendo na kwa umahiri wa hali ya juu kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utendaji mahiri na wa kizalendo. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri iliyotoa dira na mwangozo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia Ackson Mwansasu, pamoja na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu Mbunge - Naibu Spika wa Bunge, kwa kuendelea kuliongoza vema Bunge letu Tukufu. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, Mheshimiwa David Kihenzile Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kusini na wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Najma Giga ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge hili Tukufu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje,

Ulinzi na Usalama na Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini kwa kuchaguliwa tena kuendelea kuwa viongozi wa Kamati hii. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa ushirikiano mkubwa wanaotupatia, na kazi kubwa ya kuishauri Wizara, na Serikali kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nimshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kumuamini Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kumteua, Balozi Dkt. Samwel William Shelukindo kuwa Katibu Mkuu, na kuendelea kumuamini Balozi Fatma Mohamed Rajab, kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Dkt. Tulia Ackson Mwansasu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa na Serikali ya Tanzania ili kugombea nafasi ya Rais wa Bunge la Dunia kwa kipindi cha mwaka 2023/2026 *(The President of the Inter-parliamentary Union)* na Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula kugombea nafasi ya Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola, tunawaombea ushindi katika kugombea nafasi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Bonaventure au tunavyomwita zaidi Bonaventura Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Magu kwa kazi kubwa anayoifanya kutatua changamoto za wananchi wa Magu na katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi Wanamagu tutaendelea kukupa ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru pia familia yangu kwa upendo na kuendelea kunipa moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Septemba 2022, Tanzania na Jumuiya ya Kimataifa ilipokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Malkia Elizabeth II ambaye aliliongoza Taifa la Uingereza kwa

kipindi cha zaidi ya miaka sabini. Naomba kwa niaba ya Serikali kurudia tena kutoa salamu za pole kwa familia ya Mfalme na wananchi wa Uingereza kwa kifo cha kiongozi huyo. Aidha, nampongeza Mfalme Charles III kwa kutawazwa kuwa Mfalme wa Taifa la Uingereza. Serikali ya Tanzania itaendelea kushirikiana na Serikali ya Uingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwezi Machi, 2023 Mkutano wa 14 wa Bunge la Jamhuri ya Watu wa China ulimchagua Mheshimiwa Xi Jinping kuwa Rais wa nchi hiyo kwa muhula wa tatu, napenda kutumia nafasi hii kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mara nyingine tena kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Xi Jinping kwa kuchaguliwa kwake na kuihakikishia Jamhuri ya Watu wa China kuwa Tanzania itaendelea kuimarisha ushirikiano wa kirafiki, kihistoria kati ya nchi hizi mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, nchi za Angola, Senegal, Kenya, Lesotho, Tunisia na Nigeria zilifanya chaguzi. Nawapongeza wananchi wa nchi hizo kwa kukamilisha chaguzi kwa amani na kwa njia za kidemokrasia. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendelea kushirikiana na Viongozi waliochaguliwa na Serikali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashukuru kwa salamu za rambirambi tulizozipokea kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, Viongozi mbalimbali, Jumuiya ya Wanadiplomasia na Washirika wa Maendeleo kufuatia kifo cha Bernard Kamilius Membe Mwanadiplomasia mahiri aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, pia kifo cha Celestine Joseph Mushy, aliyekuwa Balozi wa Tanzania nchini Austria na Mwakilishi wa Kudumu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa Vienna - Austria, tunautambua na tutauenzi daima mchango wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nitumie nafasi hii, kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kutoa salaam za pole kwa Viongozi

Wakuu wa Nchi na Serikali na wananchi wa Mataifa ya Brazil, Indonesia, Jamhuri ya Korea, Madagascar, Malawi, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Marekani, Mauritius, Msumbiji, Pakistan, Syria na Uturuki kufuatia maafa yaliyosababishwa na ajali, na majanga ya asili ikiwemo vimbunga, matetemeko ya ardhi na mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu ni kama inavyoonekana katika kitabu cha hotuba ya bajeti kilichowasilishwa kwako nitatoa muhtasari na naomba hotuba kamili iingizwe kwenye Kumbukumbu za Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania na Uhusiano wa Kimataifa. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuzingatia misingi madhubuti iliyowekwa na Waasisi wa Taifa letu katika kusimamia uhusiano wa kimataifa, kama ilivyoainishwa katika aya ya 21 ya hotuba yangu, misingi hii imeifanya nchi yetu kuendelea kupaza sauti katika jukwaa la Kimataifa kushawishi mabadiliko ya kisiasa na kiuchumi ulimwenguni na kuweka mazingira yanayowezesha ustawi wa nchi zinazoendelea. Aidha, utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi utaendelea kuwa kpaumbele cha Serikali ili kunufaika na fursa za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya siasa na ulinzi na usalama duniani, baadhi ya nchi Barani Afrika na ulimwenguni zimeendelea kukabiliwa na migogoro inayochagizwa na tofauti za kiitikadi, kudorola kwa uchumi ugaidi na machafuko ya kisiasa. Hali ya ukosefu wa amani usalama na umaskini vimeendele kuwa chanzo cha maelfu ya watu kuyakimbia mataifa yao na hivyo kusababisha ongezeko la wakimbizi na wahamiaji haramu na ongezeko la uhalifu unaovuka mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu hali ya Siasa, Ulinzi na Usalama Kimataifa ni kama inavyoonekana katika aya ya 22 hadi aya ya 42 ya hotuba yangu na haya yana madhara pia kwa nchi yetu, ndiyo maana sisi tunaendelea kuwa sehemu ya Jumuiya ya Mataifa kusaidiana na chi nyingine

kukabilianaa na baadhi ya majanga ili kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na amani na kustahimili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Muundo wa Wizara, Toleo Na. Nne la Februari 2022 na kuongozwa na sera na miongozo mbalimbali ya Kitaifa kikanda na Kimataifa kama inavyoonekana katika aya ya 43 hadi ya 44 ya hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapato na Matumizi. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ilipanga kukusanya shilingi 1,559,879,000 katika kipindi cha mwezi Julai 2022 hadi Aprili 2023, Wizara imekusanya kiasi cha shilingi 704,417,870.67, ikiwa ni sawa na asilimia 60.2 ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, kiasi cha Shilingi 208,366,964,000 kiliidhinishwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi 203,666,964,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 4,700,000,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili mwaka 2023 Wizara ilipokea kiasi cha shilingi192,347,150,163.88 sawa na asilimia 92.3 ya kiasi kilichopangwa. Mchanganuo ni kama unavyoonekana katika jedwali Namba Moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 Wizara ilitumia kiasi cha Shilingi 187,238,392,736.97 sawa na asilimia 97.34 ya fedha zilizopokelewa. Mchanganuo ni kama inavyoonekana katika jedwali Namba Mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu. Nikianza na kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje. Ili kuendana na mabadiliko katika uhusianowa Kimataifa na Mambo ya Nje, Wizara imefanya tathmini ya Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2021, tathmini hiyo pia ni utekelezaji wa ushauri wa Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini imebainisha kuwa misingi ya sera iliyopo bado inakidhi matakwa ya sasa, hata hivyo tathmini hiyo imebaini kuwa yapo maeneo mapya yanayohitaji kujumuishwa katika sera aidha tathmini imebainisha kuwa yamekuwepo mafanikio makubwa katika utekelezaji wa sera ya mambo ya nje ikiwa ni pamoja na kuimarika kwa ujirani mwema na uwili, kuimarika kwa ushirikiano wa kikanda na kimataifa, kisiasa, kijamii na kiuchumi. Kushiriki na kufanikisha usuluhishi wa migogoro kuchangia katika misheni za kulinda amani Kikanda na Kimataifa na kuwa mwenyeji wa Taasisi za Kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, marejeo ya sera yameendelea kuweka msisitizo katika Diplomasia ya Uchumi. Maeneo mapya yatakayojumuishwa katika sera mpya ambayo tunaendelea kuiandaa ni pamoja na *diaspora*, Uchumi wa Buluu, uratibu wa mikataba na itifaki za kikanda na kimataifa, mazingira na mabadiliko ya tabia nchi, haki za binadamu hususan kuzingatia mila na desturi za Taifa letu na kukuza na kubidhaisha lugha ya Kiswahili. Kufuatia tathmini hiyo inayoendelea ya marejeo ya sera, marejeo hayo yamejumisha pia mkakati wa mpango wa utekelezaji na mfumo wa kufuatilia utekelezaji na kufanya tathmini. Lengo ni kuwezesha sera hii kutekelezwa kwa ufanisi na kupima matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Diaspora ya Uchumi ni dhana kuu katika kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje, ambayo dhamira yake ni kuwa na ushirikiano na uhusiano wa Kimataifa wenye manufaa ya kiuchumi. Aidha, utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi unahusisha sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii katika sekta ya Umma na sekta binafsi. Kwa kutambua kuwa utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi ni suala mtambuka na ili kuongeza tija katika utekelezaji wake, Wizara inaendelea kuandaa Mpango na Mkakati wa Kitaifa wa utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi. Mpango huo utawezesha kutoa tafsiri ya Diplomasia ya Uchumi utaainisha wadau kutoka sekta zote husika; Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na wajibu na malengo kwa kila sekta, wajibu wao na jinsi ya kushiriki ili kuhakikisha kwamba utekelezaji huu unakuwa ni wa tija zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi katika mwaka 2022/2023 ni kama yanavyoonekana kwa kina katika aya 58 hadi aya ya 75 katika maeneo ya uhusiano baina ya Tanzania na nchi nyingine, ziara za Viongozi Wakuu, ushirikiano wa Tanzania na nchi nyingine na ushirikiano wa kikanda na Kimataifa katika hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kwa kifupi, uhusiano baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nchi nyingine. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 Wizara iliratibu ziara za safari za viongozi wakuu 19 nje ya nchi, ambapo Mheshimiwa Rais alifanya ziara nane, Mheshimiwa Makamu wa Rais alifanya ziara tatu, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar ziara nne na Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara nne pia. Ziara hizi ni kama zinavyoainishwa katika aya ya 59 ya hotuba yangu.

(1) Ziara za Viongozi wetu wa Kitaifa zimeliletea Taifa letu mafanikio makubwa ya kiuchumi, nitayataja kwa uchache, kama yafuatavyo:-

(2) Tanzania na China zimesaini Hati ya Makubaliano kuruhusu zao la parachichi na mauzo ya uvuvi yakiwemo mabondo ya samaki kutoka Tanzania kuingia katika Soko la China na kuongeza wigo wa soko la bidhaa za Tanzania nje ya nchi. *(Makofi)*

Serikali ya Watu wa China imekubali kuipatia Tanzania mkopo wa masharti nafuu wa Dola za Marekani milioni 297.64 kwa ajili ya mradi wa mawasiliano vijijini; msaada wa Dola za Marekani milioni 24.86 kwa ajili ya upanuzi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete na mkopo wa Dola za Marekani milioni 58.3 kwa ajili ya kugharamia upanuzi wa jengo la tatu la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Karume Zanzibar; kutekeleza mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa *KVA* 400 *North East Transmission Line;* na kuendelea kutoa msaada wa ujenzi wa vyuo vya ufundi *(VETA)* nchini.

(3) Tanzania ilichaguliwa na Jukwaa la Uchumi Duniani kuwa miongoni mwa nchi 20 zitakazokuwa na vituo vya mapinduzi ya nne ya viwanda duniani. Hatua hiyo itawezesha kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja katika ujenzi wa viwanda na kuongeza ajira kwa Watanzania. *(Makofi)*

(4) Tanzania kunufaika kupitia Dola za Kimarekani 550 zilizotengwa ili kuimarisha usalama wa chakula Barani Afrika na Tanzania kuwa mwenyeji wa Jukwaa la Mapinduzi ya Kilimo Afrika unaotarajiwa kufanyika mwezi Septemba na uzinduzi wake ulifanyika na Mheshimiwa Rais wiki iliyopita. *(Makofi)*

(5) Serikali ya Jamhuri ya Korea imeahidi kushirikiana na Tanzania kujenga Chuo cha Teknolojia cha Kidijitali ambacho kitakuwa ni cha kipekee Afrika Mashariki na Kati na kuipatia Tanzania mkopo wa masharti nafuu wa Dola za Marekani milioni 70 kwa ajili ya mradi wa upanuzi wa Mfumo wa Vitambulisho vya Taifa; Dola za Marekani milioni 65 kwa ajili ya mradi wa uboreshaji wa miundombinu na upimaji na ramani na kusainiwa kwa Hati ya Makubaliano kati ya kampuni ya uzalishaji dawa na vifaa tiba za Korea na Bohari ya Dawa Tanzania.

(6) Dola ya *Qatar* kutoa ufadhili kwa wanafunzi wa masomo ya afya; kujenga jengo la mama na mtoto na kuleta wataalamu wa afya nchini na ujenzi wa vyumba vya madarasa ya sekondari na kusaidia miradi mingine ya kimkakati ya maendeleo.

(7) Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zinazotarajiwa kunufaika na ufadhili wa Benki ya Dunia kwa ajili ya kutekeleza Mradi ya Nishati Jadidifu kupitia Mfuko wa Teknolojia ya Nishati Salama uliotengewa Dola za Marekani bilioni 1.2 na Benki hiyo.

(8) Tanzania na Oman zimesaini hati za makubaliano ya ushirikiano katika Sekta za Elimu ya Juu na mafunzo ya ufundi; utunzaji wa nyaraka; na ujenzi wa kituo cha uhifadhi wa taarifa. Hati hizo zitawezesha kupata ufadhili wa masomo nchini Oman na kuziwezesha nchi hizi mbili kubadilishana uzoefu na ujuzi.

(9) Tanzania na Afrika ya Kusini kuendelea kufanya tafiti za pamoja, kukuza masoko na biashara na kurejea Mkataba wa ushirikiano katika Sekta ya Sanaa na utamaduni ili kukuza lugha ya Kiswahili; na

(10) Mashirika mbalimbali ya ndege ikiwa ni pamoja na *Air France* na *Oman Air* wameanza safari za moja kwa moja za ndege kuja Tanzania. Haya ni baadhi tu ya mafaniko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara za kikazi nchini Afrika ya Kusini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitunukiwa tuzo ya juu ya heshima ijulikanayo kama *Order of South Africa* iliyotolewa na Rais wa Afrika Kusini. Tuzo hiyo ni ishara ya kumpongeza kwa kuwa Rais wa kwanza mwanamke wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini kwa kuthamini mchango wake mkubwa katika kudumisha udugu wa kihistoria kati ya mataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla ziara hizi za Rais huyu wa Awamu ya Sita na viongozi wengine wakuu, zimeimarisha uhusiano wa Kimataifa baina ya nchi yetu na nchi rafiki, Jumuiya za Kikanda na Jumuiya za Kimataifa na kuleta mafanikio makubwa kiuchumi na kijamii ikiwa ni pamoja na ongezeko la uwekezaji, kufungua masoko ya bidhaa na huduma mbalimbali, ongezeko la watalii, upatikanaji wa misaada na mikopo yenye masharti nafuu kwa miradi mbalimbali. Mafanikio ni mengi, nimeeleza kwa kifupi. Mafanikio haya pia yameelezwa kwa kina katika hotuba za bajeti za kisekta kwa kutambua kuwa utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi ni suala mtambuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako Tukufu, naomba kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na mafanikio ambayo ameliletea Taifa letu katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wake. Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya, nguvu na maono zaidi. Napenda pia kuwashukuru wadau wote kutoka Sekta ya Umma na Binafsi kwa ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara za kikazi na kitaifa za viongozi wakuu kutoka mataifa mengine hapa nchini ikiwa ni pamoja na ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Kamala Harris, Makamu wa Rais wa Marekani; ziara ya Kitaifa ya Mheshimiwa Hakainde Hichilema, Rais wa Jamhuri ya Zambia; ziara ya Kitaifa ya Mheshimiwa Felix Antoine Tshisekedi Tshilombo, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Paul Kagame, Rais wa Jamhuri ya Rwanda. Ziara hizo zimekuwa na mafanikio mengi kama inavyoonekana katika aya ya 65 hadi aya ya 66 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kushirikiana na Nchi za Afrika ikiwa ni pamoja na kupitia katika Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano. Mikutano ya Tume za pamoja nane ilifanyika katika kipindi hiki na ilikuwa na mafaniko mengi kama inavyoonekana katika aya ya 67 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kushirikiana na Nchi za Asia na Australasia katika maeneo mbalimbali. Pamoja na mambo mengine, mwezi Agosti 2022, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano Mkuu wa Nane wa Kimataifa wa Tokyo kuhusu Maendeleo ya Afrika *(TICAD VIII)* uliofanyika nchini Tunisia. Wakati wa Mkutano huo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliwasilisha miradi nane ya kipaumbele katika sekta za miundombinu, nishati, kilimo, maji, mifugo, uvuvi na Uchumi wa Bluu yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 1.18. Majadiliano kuhusu upatikanaji wa fedha kwa miradi hiyo yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, wakati wa Mkutano huo, Tanzania na Japan zilikubaliana kuanza utekelezaji wa miradi

mitatu iliyojadiliwa katika *TICAD VI*. Miradi hiyo ni ujenzi wa Barabara ya Arusha – Holili; mradi wa maji Zanzibar na mradi wa ukarabati wa Barabara ya Kigoma. Maelezo ya kina yapo katika aya ya 66 mpaka 73.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano wa Tanzania na nchi za Afrika ya Kati. Serikali imeendelea kuimarisha mahusiano na Nchi za Mashariki ya Kati kama inavyoonekana katika aya ya 74 ya hotuba

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano wa Tanzania na Nchi za Ulaya na Amerika, pia uhusiano kati ya Tanzania na Nchi za Ulaya na Amerika umeendelea kuimarika, kama inavyoonekana katika aya ya 75 ya hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuimarisha uhusiano na Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika. Mwezi Februari, 2023 Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 36 wa Wakuu wa Nchi na Serikali. Mkutano huo ulipokea tathmini ya utekelezaji wa Ajenda 2023 na kupitisha mpango wa miaka 10 wa utekelezaji wa Ajenda hiyo. Mpango huo wa miaka 10 uliopitishwa umezingatia maslahi ya Tanzania. Aidha, katika mkutano huo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitunukiwa tuzo ya *African Leaders Malaria Alliance* kutokana na mchango wake mkubwa na juhudi za Serikali ya Tanzania katika kutokomeza ugonjwa wa Malaria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika utekelezaji wa hatua za Mtangamano za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuzingatia Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka 1999 na itifaki zake na hivyo kusimamia maslahi ya Tanzania katika mtangamano huo kupitia Umoja wa Forodha na Soko la Pamoja. Mwezi Novemba, 2022 jumuiya ilipokea tathmini ya utekelezaji wa Mpangokazi wa Miaka Kumi (2014 – 2024) wa kufikia Sarafu Moja katika Umoja wa Fedha. Tathmini hiyo imebainisha kuwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki hazijakidhi baadhi ya vigezo vilivyoainishwa katika Itifaki ya Umoja wa Fedha.

Ni Tanzania na Uganda tu ndizo pekee zilifanikiwa kukidhi vigezo vitatu kati ya vinne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na matokeo ya tathmini hiyo, jumuiya ilihuisha mpango wa kazi wa kufikia sarafu moja na kuongeza muda wa utekelezaji wake kutoka kutoka mwaka 2024 mpaka 2031. Aidha, chini ya ushirikiano wa Afrika Mashariki Tanzania imeendelea kushirikiana na Nchi Wanachama na kunufaika kupitia utekelezaji wa miradi ya kikanda katika sekta mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Sekta ya Biashara, Viwanda, Kilimo, uendelezaji miundombinu, Afya, Ulinzi na Usalama. Maelezo ya kina yapo katika aya ya 87 hadi aya ya 95 ya hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika, Bunge la Afrika Mashariki lilipitisha miswada miwili ya sheria ambayo ni Muswada wa Sheria ya Kamisheni ya Huduma za Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 2022 na Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 2022. Kutungwa kwa sheria hizo kunatoa nafasi ya kuanzishwa kwa Kamisheni ya Huduma za Fedha ya Afrika Mashariki kama Taasisi ya Jumuiya ya kuboresha usimamizi wa forodha na taratibu zake katika jumuiya. Maelezo ya kina yapo katika aya ya 97 hadi ya 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mtangamano wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kwa lengo la kusimamia maslahi ya Taifa na kuzitumia fursa za kiuchumi na kijamii katika Jumuiya hiyo. Mwezi Agosti, 2022, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 42 wa Wakuu wa Nchi na Serikali. Katika Mkutano huo, Nchi Wanachama ziliridhia na kusaini Itifaki ya *SADC* ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu. Kusainiwa kwa Itifaki hiyo kutaiwezesha Tanzania kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine za *SADC* katika mapambano dhidi ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu pamoja na uhalifu mwingine unaovuka mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Mawaziri katika Mkutano wake wa Machi, 2023 liliridhia pia Mpango wa Utekelezaji wa

Miradi ya Jumuiya ambao umejumuisha miradi 11 ambayo inayojumuisha Tanzania. Miradi hiyo ipo katika Sekta ya Maji, Miundombinu, Nishati, Masoko, na Viwanda. Nchi wanachama wa *SADC* zimeendelea pia kufuatilia na kushirikiana katika ulinzi na usalama na kuweka mikakati ya pamoja ya kuimarisha usalama na kudhibiti ugaidi na uhalifu unaovuka mipaka. Maelezo ya kina yako katika aya ya 101 mpaka 107.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutengeneza mazingira wezeshi ili kuhakikisha na kuwezesha ushiriki wa Watanzania wanaoishi nje ya nchi *(Diaspora)* kushiriki na kuchangia katika maendeleo ya Taifa lao na kuwatatulia changamoto walizonazo lakini kuwawezesha kunufaika na fursa mbalimbali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, mwamko wa *Diaspora* kutuma fedha *(remittances)* na kuwekeza katika sekta ya kiuchumi na kijamii hapa nchini umeendelea kuongezeka. *Diaspora* wameendelea kutuma fedha nchini, ambapo katika kipindi cha kuanzia Januari mpaka Desemba, 2022 walituma takribani Dola za Marekani bilioni 1.1 kupitia vyanzo rasmi. Fedha hizo ni takribani mara mbili ya kiasi kilichotumwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Aidha, uwekezaji katika mifuko ya uwekezaji na ununuzi wa nyumba na viwanja umeendelea kuongezeka kutoka kwa *diaspora*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara imekamilisha maandalizi ya Mfumo wa Kidigitali wa Kukusanya na Kutunza Taarifa za *Diaspora (Diaspora Digital Hub)*. Mfumo huo ulizinduliwa tarehe 22 Mei, 2023, na utaiwezesha Serikali kupata takwimu sahihi za idadi ya *diaspora*, mahali walipo, ujuzi na uzoefu walionao. Mfumo huo pia utawawezesha *diaspora* kupata taarifa kuhusu fursa na huduma mbalimbali zinazotolewa na sekta za Umma na binafsi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kutambua umuhimu wa *diaspora* na ili kutoa fursa zaidi, Wizara iko katika hatua za mwisho za maandalizi ya kuwapatia hadhi maalum *diaspora* wenye asili ya Tanzania na *diaspora* wenye uraia wa nchi nyingine. Wizara ilikusanya maoni

kutoka ndani na nje ya nchi na hususan kutoka kwa *diaspora*. Hadhi maalum ambayo inaandaliwa imezingatia mapendekezo yote yaliyotolewa na *diaspora*. Nia ya Serikali ni kuhakikisha kuwa *diaspora* hawa wa Kitanzania wanapata fursa na huduma mbalimbali nchini. Maoni hayo yameainisha maeneo yaliyopendekezwa kuwa sehemu ya hadhi maalum ambayo tayari yameshafanyiwa kazi. Tuna imani kwamba kufika mwisho wa mwaka huu wa fedha, hadhi maaulum hii itakuwa tayari na imeshatolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii, kuwapongeza na kuwashukuru kwa dhati *diaspora* wote kwa kuendelea kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya Taifa letu. Aidha, nawahamasisha *diaspora* kujiandikisha katika mfumo wa kidijitali wa kukusanya na kutunza taarifa ili watambuliwe na kunufaika na fursa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki, Wizara iliratibu na kufanikisha kusainiwa kwa Mikataba 13 na Hati za Makubaliano 37. Mikataba na hati hizo zinahusu sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii ikiwemo ulinzi na usalama; kilimo na uvuvi; viwanda, biashara, uwekezaji; TEHAMA; utalii; afya; elimu; mawasiliano; utamaduni; sanaa na michezo; mazingira; Uchumi wa Bluu; uchukuzi; na sayansi na teknolojia. Kupitia mikataba hiyo ya makubaliano hayo, nchi yetu itanufaika na fursa mbalimbali kisekta. Orodha ya Mikataba na Hati za Makubaliano zilizoingiwa inaonekana katika Kiambatisho Na. 1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kusimamia masuala ya utawala na maendeleo ya rasilimaliwatu kwa lengo la kuimarisha utendaji wa kazi. Katika kipindi hiki, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya uteuzi wa mabalozi 11 kuiwakilisha Tanzania katika nchi za Austria, Cuba, Ethiopia, Malawi, Indonesia, Uholanzi, Umoja wa Falme za Kiarabu, Umoja wa Mataifa - Marekani, Uturuki, Zambia, na Zimbabwe. Vilevile, katika kipindi hicho, Wizara imeajiri jumla ya watumishi 14. Pia, Wizara imepata kibali cha kuajiri watumishi

wapya 17. Aidha, watumishi 19 wamepandishwa vyeo, kati yao ikiwa ni Wakurugenzi wasaidizi 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara; katika mwaka wa fedha 2022/2023, wizara ilitengewa kiasi cha shilingi 4,700,000,000 kwa ajili ya bajeti ya maendeleo ambapo ni ukarabati wa majengo manne katika Ubalozi wa Tanzania Pretoria, Afrika Kusini na ujenzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Maelezo ya kina yanaonekana katika aya ya 41 ya hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza dhamira ya Serikali ya kujenga majengo na Ofisi za Balozi na vitega uchumi na ukarabati wa Balozi zetu kwa kasi zaidi na kuimarisha taswira ya Taifa letu, Wizara imefanya tathmini ya kina na kuainisha miradi ya kipaumbele na kuandaa mpango wa muda mrefu na wa kati kuainisha changamoto zilizopo na jinsi ya kukabiliana nazo hususan ili kuwezesha ubia na ushiriki wa sekta binafsi katika uendelezaji wa miradi hii. Miradi 15 imeainishwa kama miradi ya kiapumbele kama inavyoonekana katika kiambatanisho namba tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kiambatanisho namba tatu hiki Waheshimiwa Wabunge imeainishwa miradi 14. Mradi mmoja haupo pale, naomba niutaje kwamba ni Mradi wa Ubalozi wa Nairobi, huo ndio unafanya hiyo miradi iwe 15 na si 14 kama ilivyooneshwa hapo. Taratibu za ubia zinaendelea ambapo tayari taratibu za kushirikiana na *NSSF* kuendeleza majengo katika Balozi ya Nairobi na Kinshansa zimekamilika. Changamoto zilizobainishwa na jinsi ya kuzitatua ni kama inavyoonekana katika kiambatanisho namba tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru sana wadau wote waliojitokeza kushirikiana na Wizara na utayari wao. Nafikiri huu utakuwa ni mwanzo sasa na mwarobaini wa kutatua tatizo au changamoto ya uendelezaji wa majengo na vitega uchumi katika balozi zetu. Fedha za Serikali ni chache, hatuwezi kuweza kutoa fedha kufanya miradi yote hii; lakini sasa maadam

tumeshakubaliana na sekta binafsi na tumeweka utaratibu tuna imani hadhi ya balozi itainuka na majengo mengi yatajengwa kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha Wizara imeanza kutekeleza mradi wa kuendeleza viwanja vya Serikali Jijini Lusaka Zambia. Mradi huu unahusisha majengo 10 kama yanavyoonekana katika kiambatanisho namba mbili cha hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi zilizo chini ya Wizara. Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa taasisi tatu zilizo chini ya Wizara ambazo ni Kituo cha Kimataifa cha Arusha, Chuo cha Diplomasia na Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini Katika Masuala ya Utawala Bora. Kiasi cha fedha kilichoidhinishwa kwa taasisi hizi na utekelezaji wa majukumu ni kama inavyoonekana katika aya ya 148 hadi aya ya 169 ya hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto na hatua zilizochukuliwa; pamoja na kuwepo mafanikio, Wizara imekabiliwa au inakabiliwa na changamoto kadhaa. Changamoto hizo pamoja na mipango ya kukabliana nazo vimeainishwa katika aya ya 170 hadi aya ya 171.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani. Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa kimataifa na diplomasia na kupata ushirikiano mkubwa kutoka kwa wadau na washirika wa maendeleo, jumuiya za kikanda na kimataifa katika kufanikisha utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo napenda kuzishukuru nchi zote, mashirika yote ya kikanda na kimataifa. Tumeendelea kushirikiana nao kama inavyoonekana katika aya ya 173 hadi ya 176 ya hotuba yangu na kama walivyoshiriki leo na kutambulishwa na wewe kabla ya kuanza kuwasilisha hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *to the international communities, friends and partners; thank you so much for continued cooperation and partnership and I thank you for being here with us this morning. We greatly value your support Tanzania under the firm leadership of Her Excellency Doctor Samia Suluhu Hassan remains committed to continue cooperating with you all.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa ushirikiano wao umekuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha malengo ya Wizara na Serikali kwa ujumla, nawashukuru sana sana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru watendaji na watumishi wa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara kwa utendaji wao mahiri unaowezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi na kulinda na kutetea maslahi ya Taifa letu ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee napenda kumshukuru Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk (Mb), Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, aliyekuwa Waziri kabla yangu Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula, Balozi Dkt. Samwel Shelukindo (Katibu Mkuu) na Balozi Joseph Edward Sokoine aliyekuwa Katibu Mkuu, Balozi Fatma Mohammed Rajab (Naibu Katibu Mkuu), Bwana Ephrahim Mafuru (Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Mikutano ya Kimataifa Arusha), Bwana Lamau Mpodo (Mtendaji Mkuu wa Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini Katika Masuala ya Kidemokrasia na Utawala Bora) na Bwana Felix Wandwe (Kaimu Mkurugenzi wa Chuo cha Diplomasia), Wakuu wa Idara, Waheshimiwa Mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania nje ya nchi, wakuu wa vitengo, watumishi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha napenda kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote na wadau kutoka sekta ya umma na sekta binafsi kwa ushirikiano mkubwa wanaotupatia katika kutekeleza Diplomasia ya Uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha ni pamoja na kuratibu na kutekeleza Diplomasia ya Uchumi ikiwa ni pamoja na: -

a) Kuratibu ziara za kikazi za viongozi wakuu na kukamilisha maandalizi ya mpango wa kitaifa wa utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi;

b) Kukamilisha maboresho ya Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2021 nadhani sasa itakuwa 2023;

c) Kuratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika majadiliano ya kimataifa na jumuiya za kikanda;

d) Kutekeleza mpango mkakati wa uendelezaji wa viwanda vinavyomilikiwa na Serikali nje ya nchi na kukarabati majengo ya balozi;

e) Kuimarisha ushiriki na mchango wa *diaspora* katika maendeleo ya Taifa ikiwa ni pamoja na kukamilisha mfumo na taratibu za kutoa hadhi maalum kwa *diaspora;*

f) Kuimarisha utendaji kazi wa Wizara na balozi na konseli kuu kwa kuzipatia rasilimali watu, fedha na vitendea kazi stahiki, na

g) Kuimarisha Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini. Nimeeleza kwa baadhi lakini yote yanaonekana katika hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024; katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 1,559,879,000 ikiwa ni mapato ya Serikali yatakayopatikana kutokana na vyanzo mbalimbali vilivyopo Makao Makuu ya Wizara na katika Balozi za Tanzania. Aidha Wizara imetengewa kiasi cha shilingi 247,971,524,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 230,083,919,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida yakijumuisha shilingi

213,304,516,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 16,779,400,000 kwa ajili ya mishahara. Aidha, kiasi cha shilingi 17,887,608,000 kimetengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha za bajeti za matumizi mengineyo, shilingi 1,534,857,886 ni kwa ajili ya Mpango wa Hiari wa Kujitathmini Katika Masuala ya Utawala Bora na Demokrasia *(APRM),* shilingi 1,200,000,000 ni kwa ajili ya Chuo cha Diplomasia na shilingi 1,000,400,000 ni kwa ajili ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, na shilingi 880,000,000 ni kwa ajili ya Bodi ya Ushauri wa Masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika. Aidha, kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara, shilingi 3,169,255,819 ni kwa ajili ya mishahara ya Chuo cha Diplomasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kiasi cha shilingi 17,887,608,000 kilichotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, shilingi 17,700,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 187,608,000 ni fedha za nje. Aidha katika fedha hizo, shilingi 5,400,000,000 ni kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika na Haki za Binadamu ambao uko Arusha ambao umeanza mwaka huu wa fedha, na shilingi 3,900,000,000 ni kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa vyumba tisa vya mihadhara katika Chuo cha Diplomasia na shilingi 2,000,000,000 ni kwa ajili ya kufanya chambuzi yakinifu kwa ajili ya miradi 13 ya kipaumbele katika Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Majengo Balozini. Hii ni muhimu sana kwa sababu chambuzi hizi ndizo zinatuwezesha kuvutia wabia ambao wamejitokeza. Shilingi 6,400,000,000 ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya Serikali katika balozi za Tanzania na shilingi 187,608,000 ni kwa ajili ya kuboresha mifumo ya utendaji kazi. Katika ujenzi wa vitega uchumi katika balozi zetu nje ya nchi Wizara itashirikiana na sekta binafsi kupitia ubia *(PPP)* na pia Mikopo ya Kiserikali kupitia Hazina kama nilivyokwisha eleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Ili kuweza kutekeleza kwa kikamilifu majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 247,971,524,000. Kati ya fedha hizo shilingi 230,083,916,000 ni kwa

ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 17,887,608,000 ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuhitimisha kwa kukushukuru tena wewe binafsi kwa jinsi unavyoendesha vikao vya Bunge kwa umahiri wa hali ya juu na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. STERGOMENA L. TAX (MB.), WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

***1. Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, na lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

***2. Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na makadirio ya mapato na matumizi.

***3. Mheshimiwa Spika,*** kabla sijaendelea na uwasilishaji naomba kwa unyenyekevu nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini na kuniteuwa kuwa Waziri wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Ninaahidi kuwa nitaendelea kutimiza majukumu yangu kwa weledi, kujituma, na kuzingatia Katiba ya

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kuimarisha mahusiano ya Kimataifa na kulinda maslahi ya Taifa letu.

***4. Mheshimiwa Spika,*** aidha, naomba kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka miwili ya kuiongoza nchi yetu kwa ujasiri, maono mapana, na mafanikio makubwa. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kama Mwanadiplomasia Namba 1, ameimarisha uhusiano baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nchi mbalimbali, Taasisi za Kikanda na Kimataifa na kuliletea heshima kubwa Taifa letu. Ametekeleza Diplomasia ya Uchumi kwa vitendo, ambapo ametumia diplomasia kwa umahiri wa hali ya juu kutimiza malengo ya kiuchumi kwa maslahi ya Taifa letu kama inavyoonekana katika maeneo mbalimbali katika Hotuba hii.

***5. Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utendaji mahiri na wa kizalendo.

***6. Mheshimiwa Spika,*** naungana na Waheshimiwa Mawaziri, Wabunge na Watanzania wenzangu kuendelea kuwaombea Viongozi wetu Wakuu kwa Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa afya njema, na mafanikio katika kutekeleza majukumu ya kuliongoza Taifa, ikiwemo kukuza na kuimarisha diplomasia na uhusiano wa kimataifa. Kazi iendelee!

***7. Mheshimiwa Spika,*** nakupongeza kwa dhati wewe binafsi, pamoja na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika wa Bunge kwa kuendelea kuliongoza vema Bunge hili Tukufu. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti; Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kusini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo; na Mheshimiwa Najma

Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. Nina imani kubwa kuwa wataendelea kukusaidia katika utekelezaji wa majukumu ya kuliongoza Bunge hili Tukufu.

***8. Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, na Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini kwa kuchaguliwa tena kuendelea kuwa viongozi wa Kamati hii. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa na wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa ushirikiano mkubwa wanaotupatia, na kwa kazi kubwa ya kuishauri Wizara, na Serikali kwa ujumla. Miongozo na ushauri wao katika masuala mbalimbali umekuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Kwa muktadha huo, nawapongeza pia Wenyeviti wa Kamati nyingine za Kudumu za Bunge kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kikamilifu ya kuishauri Serikali.

***9. Mheshimiwa Spika,*** namshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kumuamini Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk (Mb.) kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Vilevile, namshukuru kwa kumteua, Balozi Dkt. Samwel William Shelukindo kuwa Katibu Mkuu, na kuendelea kumwamini Balozi Fatma Mohamed Rajab, Naibu Katibu Mkuu kwa kuendelea kuhudumu katika wadhifa huo. Napenda kuwashukuru Viongozi hao kwa ushirikiano wa dhati wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

***10. Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kumshukuru mtangulizi wangu Mhe. Balozi Liberata Mulamula (Mb.), kwa kazi nzuri aliyoifanya na kuweka misingi inayoniwezesha kuendelea na utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

***11. Mheshimiwa Spika,*** kipekee napenda kuishukuru familia yangu kwa uvumilivu upendo, maombi, na kwa kuendelea kunipa moyo katika kutekeleza majukumu yangu.

***12. Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri aliyowasilisha hapa Bungeni ambayo imetoa dira na mwongozo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Nawapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri wenzangu walionitangulia kuwasilisha hotuba zao katika Bunge hili la Bajeti, na kwa kuendelea kushirikiana na Wizara yangu katika kutekeleza diplomasia ya uchumi.

***13. Mheshimiwa Spika,*** mwezi Septemba 2022, Tanzania na Jumuiya ya Kimataifa ilipokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Malkia Elizabeth II ambaye aliliongoza Taifa la Uingereza kwa kipindi cha zaidi ya miaka sabini. Naomba kwa niaba ya Serikali kurudia kutoa salamu za pole kwa Mfalme Charles III, Mkuu wa Falme ya Uingereza na Jumuiya ya Madola; familia ya Mfalme na wananchi wa Uingereza kwa kifo cha kiongozi huyo mashuhuri aliyekuwa nguzo kuu kwa Taifa hilo na Jumuiya ya Madola. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahala pema peponi. Aidha, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mfalme Charles III kwa kutawazwa kuwa Mfalme wa Taifa la Uingereza. Serikali ya Tanzania itaendelea kushirikiana na Serikali ya Uingereza katika kudumisha uhusiano kati ya nchi hizi mbili.

***14. Mheshimiwa Spika,*** Mwezi Machi 2023, Mkutano wa 14 wa Bunge la Jamhuri ya Watu wa China ulimchagua Xi Jinping kuwa Rais wa nchi hiyo kwa muhula wa tatu wa miaka mitano. Napenda kutumia nafasi hii, kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumpongeza tena Mheshimiwa Xi Jinping kwa kuchaguliwa kwake, na kuihakikishia Jamhuri ya Watu wa China kuwa Tanzania itaendelea kuimarisha ushirikiano wa kidiplomasia na kirafiki, na wa kihistoria uliopo kati ya nchi hizi mbili.

***15. Mheshimiwa Spika,*** aidha, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, nchi za Angola, Senegal, Kenya, Lesotho, Tunisia na Nigeria zilifanya chaguzi za viongozi katika hali ya amani na utulivu. Nawapongeza wananchi wa nchi hizo kwa kukamilisha chaguzi kwa amani na kwa njia za kidemokrasia. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendelea kushirikiana na Viongozi waliochaguliwa na Serikali zao. Aidha, natumia nafasi hii kuzitakia heri nchi zinazotarajia kufanya uchaguzi katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 ambazo ni Afrika Kusini, Gabon, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Liberia, Madagascar, Mali, Sudan, Sudan Kusini, na Zimbabwe.

***16. Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu kwa nyakati tofauti imekumbwa na maafa na matukio mbalimbali yaliyosababisha athari mbalimbali zikiwemo vifo, majeruhi, na uharibifu wa mali na mazingira. Nitumie fursa hii kuwapa pole Watanzania wote waliopoteza ndugu, jamaa na mali zao katika maafa. Aidha, ninamwomba Mwenyezi Mungu awajalie majeruhi wote uponyaji wa haraka na aendelee kuwapumzisha kwa amani wale waliopoteza maisha.

***17. Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa pole kwako wewe mwenyewe, Bunge lako Tukufu, familia ya marehemu, ndugu, jamaa na watanzania wote kwa msiba uliotupata kwa kuondokewa na aliyekuwa **Mbunge wa Jimbo la Amani, Mheshimiwa Hassan Mussa** uliotokea tarehe 13 Oktoba, 2022 huko Zanzibar. Mchango wa Mbunge huyo katika shughuli za maendeleo ya Taifa letu utakumbukwa daima. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

***18. Mheshimiwa Spika,*** pia nashukuru kwa salamu za rambirambi tulizozipokea kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, Viongozi wa Serikali, Jumuiya ya Wanadiplomasia na Washirika wa Maendeleo kufuatia kifo cha **Bernard Kamilius Membe mwanadiplomasia mahiri** aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa; na kifo cha **Celestine Joseph Mushy**, aliyekuwa Balozi wa Tanzania nchini Austria na Mwakilishi wa Kudumu wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa Vienna, Austria. Tunatambua na kuthamini upendo wenu na faraja mliyotupatia katika kipindi hicho kigumu. Aidha, tunautambua, na tutauenzi daima mchango wao katika Taifa, hususan, katika diplomasia na mahusiano ya kimataifa.

***19. Mheshimiwa Spika,*** napenda pia, nitumie nafasi hii, kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kutoa salaam za pole kwa Viongozi Wakuu wa Nchi na Serikali na wananchi wa mataifa ya Brazil, Indonesia, Jamhuri ya Korea, Madagascar, Malawi, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Marekani, Mauritius, Msumbiji, Pakistan, Syria na Uturuki kufuatia maafa yaliyosababishwa na ajali, na majanga ya asili ikiwemo vimbunga, matetemeko ya ardhi na mafuriko.

***20. Mheshimiwa Spika,*** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaungana na mataifa hayo katika kipindi hiki kigumu, na tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze mahala pema roho za marehemu. Aidha, tunawaombea majeruhi wote wapone kwa haraka na kurejea katika utekelezaji wa shughuli za kujenga mataifa yao.

## 2.0 TANZANIA NA UHUSIANO WA KIMATAIFA

***21. Mheshimiwa Spika,*** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuzingatia misingi madhubuti iliyowekwa na Waasisi wa Taifa letu katika kusimamia uhusiano wa kimataifa. Misingi hiyo inapinga na kulaani vitendo vya uonevu na ukandamizaji popote duniani, kulinda uhuru wa kujiamulia mambo yetu wenyewe; kulinda mipaka ya nchi yetu; kutetea haki; kuimarisha ujirani mwema; na kutekeleza sera ya kutofungamana na upande wowote. Misingi hii ndio dira na msimamo wetu kwenye uhusiano na nchi nyingine katika Jumuiya za Kikanda na Kimataifa. Misingi hii imeifanya nchi yetu kuendelea kupaza sauti katika majukwaa ya kimataifa, kushawishi mabadiliko ya kisiasa na kiuchumi ulimwenguni, na kuweka mazingira yanayowezesha ustawi wa nchi

zinazoendelea. Azma ya Tanzania ni kuwa na dunia yenye usawa, haki na amani, hali itakayochangia kuwepo kwa ukuaji wa uchumi shirikishi na maendeleo endelevu katika mataifa yanayoendelea, na yaliyoendelea kwa ustawi wa wananchi.

***22. Mheshimiwa Spika,*** napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu na Jumuiya ya Kimataifa kuwa, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendelea kuunga mkono jitihada za kikanda na kimataifa katika kutatua na kutafuta suluhu ya changamoto zinazoikabili dunia ikiwemo, umaskini, magonjwa ya mlipuko, mabadiliko ya tabianchi, migogoro, ugaidi na uhalifu unaovuka mipaka. Utekelezaji wa diplomasia ya uchumi utaendelea kuwa kipaumbele cha Serikali ili kunufaika na fursa za kiuchumi na kijamii ikiwemo masoko ya nje kwa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini; kuvutia uwekezaji; kukuza utalii; na kuendeleza miradi katika sekta mbalimbali.

***23. Mheshimiwa Spika,*** baada ya kuainisha misingi na mwelekeo wa Sera ya Mambo ya Nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nitumie fursa hii kueleza kwa kifupi hali ya siasa, ulinzi na usalama duniani katika kipindi hiki.

**AFRIKA**

***24. Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya nchi zimeendelea kukabiliwa na migogoro inayochagizwa kwa kiasi kikubwa na tofauti za kiitikadi, kudorora kwa uchumi, ugaidi na machafuko ya kisiasa. Hali ya ukosefu wa amani, usalama na umaskini wa kipato vimeendelea kuwa chanzo cha maelfu ya watu kuyakimbia mataifa yao, na hivyo kusababisha ongezeko la wakimbizi na wahamiaji haramu. Hali hiyo imesababisha ongezeko la uhalifu unaovuka mipaka, hususan biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.

**Jamhuri ya Burkina Faso na Jamhuri ya Guinea**

***25. Mheshimiwa Spika,*** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama mwanachama wa Umoja wa Afrika (AU) inaendelea kulaani mapinduzi ya kijeshi yanayoendelea na michakato yote ya

kubadilisha Serikali kinyume na Katiba na kuzisihi nchi hizo kurejesha utawala wa kiraia na kidemokrasia. Nchi zilizokumbwa na mapinduzi hayo ni pamoja na Jamhuri ya Burkina Faso na Jamhuri ya Guinea.

**Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia**

***26. Mheshimiwa Spika,*** hali ya ulinzi na usalama nchini Ethiopia imeendelea kuimarika kufuatia kukamilika kwa mazungumzo na kusainiwa Mkataba wa kusitisha mapigano baina ya Serikali ya nchi ya Ethiopia na Kikundi cha wapiganaji cha Jimbo la Tigray mwezi Novemba, 2022. Tanzania inaunga mkono utekelezaji wa Mkataba wa kuanzisha Serikali ya mpito katika Jimbo la Trigay, na kuruhusu misaada ya kibinadamu na huduma za jamii katika Jimbo hilo.

**Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo**

***27. Mheshimiwa Spika,*** maeneo ya mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), hususan majimbo ya Ituri, Kivu Kaskazini na Kusini yameendelea kukabiliwa na changamoto ya kiusalama kutokana na kuendelea kuwepo wa vikundi vya waasi vinavyofanya mashambulizi ya mara kwa mara dhidi ya raia, jeshi la DRC, (*Armed Forces of the Democratic Republic of the Congo* - FARDC), na vikosi vya kulinda amani vya Umoja wa Mataifa. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaunga mkono jitihada za kikanda, na kimataifa za kutafuta suluhu ya mgogoro huo kwa njia za amani, ikiwa ni pamoja na kuchangia walinda amani kupitia Misheni ya Umoja wa Mataifa (MONUSCO).

**Jamhuri ya Libya**

***28. Mheshimiwa Spika,*** hali ya ulinzi na usalama nchini Libya imeendelea kudorora licha ya juhudi zinazoendelea kufanyika ili kurejesha hali ya amani. Hali hii imesababishwa na uwepo wa Serikali mbili ambazo ni Serikali inayoungwa mkono na Umoja wa Mataifa, na Serikali inayoungwa mkono na Bunge la nchi hiyo. Tanzania inaunga mkono msimamo wa Afrika kuhusu nchi ya Libya kuheshimu mkataba uliosainiwa mwaka 2022 wa kurejesha amani,

na kufanya uchaguzi kama ilivyopangwa hapo mwezi Oktoba, 2023, ili kurejesha uongozi wa Kidemokrasia.

**Jamhuri ya Mali**

***29. Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama katika Jamhuri ya Mali inaendelea kuimarika kufuatia nchi hiyo kupanga kufanya uchaguzi mkuu mwezi Juni, 2023 kwa lengo la kurejesha mamlaka ya kiraia baada ya mapinduzi ya kijeshi yaliyomwondoa madarakani Rais Ibrahim Boubacar Keita mwaka 2020. Tanzania inaunga mkono jitihada hizo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa misingi iliyoainishwa katika Mkataba wa kuanzisha Umoja wa Afrika.

**Jamhuri ya Morocco na Saharawi**

***30. Mheshimiwa Spika,*** mgogoro kati ya Saharawi na Morocco bado unaendelea, kufuatia Morocco kuendelea kutambua eneo la Sahara Magharibi kama sehemu ya nchi yao. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kuunga mkono mapendekezo yaliyotolewa na Umoja wa Afrika, kuwa pande mbili kurejea kwenye meza ya mazungumzo ili kutafuta suluhu kwa njia ya amani.

**Jamhuri ya Msumbiji**

***31. Mheshimiwa Spika,*** hali ya ulinzi na usalama nchini Msumbiji imeendelea kuimarika, isipokuwa katika maeneo ambayo yameendelea kukabiliwa na mashambulizi kutoka katika kikundi cha kigaidi cha Al-Sunna Wal-Jamaa. Mashambulizi hayo yamesababisha vifo na watu kuyakimbia makazi yao, hususan wanawake, wazee na watoto na uharibifu wa miundombinu. Maeneo hayo ni pamoja na wilaya za Mocimboa da Praia, na Niassa. Tanzania imeendelea kushiriki katika juhudi za kutafuta amani na usalama katika maeneo hayo kupitia Misheni ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC Mission in Mozambique-SAMIM*).

***32. Mheshimiwa Spika,*** Tanzania kwa kushirikiana na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha uwezo wa kukabiliana na matishio ya kigaidi, ikiwemo utekelezaji wa Mkakati wa Kikanda wa Kupambana na Ugaidi. Aidha, Kituo cha Kupambana na Ugaidi cha SADC (SADC-RCTC) kilichopo Dar es Salaam kimeendelea kuimarishwa.

**Jamhuri ya Sudan**

***33. Mheshimiwa Spika,*** Sudan imeendelea kukabiliana na changamoto za kiusalama ambapo mwezi Aprili 2023 yamezuka mapigano ya kivita kati ya Jeshi la Sudan (*Sudan Armed Forces - SAF*), na kikosi cha Msaada wa Haraka (*Rapid Support Forces*-RSF) ambayo yametokana na mvutano wa kisiasa kuelekea hatua ya kurejesha utawala wa kiraia katika nchi hiyo. Tanzania inaendelea kuzisihi pande hizo mbili za mgogoro kusitisha mapigano na kurejea kwenye meza ya mazungumzo kwa kuzingatia Tamko la Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika la tarehe 16 Aprili, 2023.

***34. Mheshimiwa Spika,*** kufuatia mapigano hayo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifanikiwa kuwarejesha nchini raia 206 ikiwemo wafanyakazi wa ubalozi, Wanafunzi na raia wa Tanzania waliokuwa wanaishi nchini Sudan. Raia hao walirejea nchini salama hapo tarehe 27 Aprili 2023. Natumia nafasi hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwajali raia wake, na kuwezesha kuwarejesha nchini watanzania waliokuwa wanaishi Jamhuri ya Sudan, na kuhakikisha kuwa zoezi hilo limefanyika kwa wakati na mafanikio.

**ULAYA NA AMERIKA**

***35. Mheshimiwa Spika,*** kiujumla hali ya siasa, ulinzi na usalama katika ukanda wa Ulaya na Amerika imeendelea kuwa ya amani isipokuwa mgogoro unaondelea kati ya Shirikisho la Urusi, na Jamhuri ya Ukraine. Hali hiyo imechangia kuzorota kwa hali ya usalama katika eneo la mashariki ya Ulaya. Aidha, mgogoro huo

umesababisha kudorora kwa uchumi wa dunia, ambapo nchi nyingi, ikiwemo Tanzania zimeendelea kushuhudia kuongezeka kwa mfumuko wa bei za bidhaa na huduma hasa vyakula, nishati, na mbolea. Tanzania inaendelea kuunga mkono jitihada za Jumuiya ya Kimataifa ikiwa ni pamoja na Umoja wa Mataifa, katika kutafuta suluhu ya mgogoro huo kwa njia ya majadiliano, ili kurejesha amani na usalama.

**MASHARIKI YA KATI**

***36. Mheshimiwa Spika,*** hali ya siasa, ulinzi na usalama katika ukanda wa Mashariki ya Kati imeendelea kuimarika isipokuwa kwa baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:

**Israel na Palestina**

***37. Mheshimiwa Spika,*** mgogoro kati ya Israel na Palestina umeendelea kuleta changamoto za kiusalama katika ukanda wa Mashariki ya Kati, ambapo kila upande unaushutumu mwenzake kwa kuanzisha vurugu na mapigano. Kuendelea kwa vurugu na mapigano hayo kunakwamisha juhudi za kimataifa katika kufikia amani ya kudumu. Tanzania inaendelea kuunga mkono juhudi za Umoja wa Mataifa, na msimamo wa Umoja wa Afrika unaozitaka pande husika kuheshimu makubaliano ya kuwepo kwa mataifa mawili huru ya Palestina na Israel, na yanayoishi kwa amani.

**Lebanon**

***38. Mheshimiwa Spika,*** Lebanon imeendelea kukabiliwa na changamoto ya uwepo wa makundi yenye itikadi kali zinazokinzana. Hali hii imechangia kudorora kwa uchumi na kusababisha maandamano na vurugu za mara kwa mara. Tanzania imeendelea kuunga mkono juhudi za Jumuiya za Kimataifa katika kurudisha amani na usalama nchini humo. Aidha, Tanzania inaendelea kushiriki katika juhudi za kulinda amani nchini Lebanon kwa kuchangia Walinda Amani kupitia Misheni ya Umoja wa Mataifa (UNIFIL).

**Yemen**

***39. Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama nchini Yemen imeendelea kuwa ya mapigano yanayojitokeza mara kwa mara kati ya jeshi la Serikali na kundi la wanamgambo wa Houthi. Mapigano hayo yamekuwa na athari kwa ustawi wa nchi hiyo ambapo zaidi ya watu milioni 4 wamekimbia makazi yao, na kusababisha uhitaji mkubwa wa huduma za kibinadamu. Tanzania inaunga mkono juhudi za Umoja wa Mataifa za kutafuta suluhu ya mgogoro huo, unaozitaka pande mbili kumaliza mgogoro huo kwa njia ya amani.

**ASIA NA AUSTRALASIA**

***40. Mheshimiwa Spika,*** hali ya siasa, ulinzi na usalama katika ukanda wa Asia na Australasia imeendelea kuimarika isipokuwa kwa baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:

**Rasi ya Korea**

***41. Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama katika Rasi ya Korea imeendelea kuwa ya mashaka kutokana na mvutano uliopo baina ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea (DPRK) na Jamhuri ya Korea na washirika wake. Tanzania inaendelea kuunga mkono juhudi za Umoja wa Mataifa za usuluhishi wa migogoro hiyo kwa njia ya amani.

**Sri Lanka**

***42. Mheshimiwa Spika,*** hivi karibuni nchi ya Sri Lanka imekumbwa na maandamano makubwa ambayo yamesababisha mabadiliko ya kiutawala. Maandamano hayo yamesababishwa na kuzorota kwa hali ya uchumi wa nchi hiyo. Kwa sasa serikali ya Sri Lanka inafanya juhudi za kuleta mageuzi ya kiuchumi ikiwemo kushirikiana na taasisi za kifedha duniani kwa lengo la kupata misaada ya kifedha kwa ajili ya kutekeleza programu za kufufua uchumi wa nchi hiyo.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

***43. Mheshimiwa Spika,*** kabla ya kueleza utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, naomba nitaje majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kama yalivyoainishwa katika Muundo wa Wizara Toleo la tarehe 4 Februari 2022, ambayo ni yafuatayo:

a) Kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje;

b) Kusimamia na kuratibu masuala ya uhusiano baina ya Tanzania na nchi nyingine;

c) Kusimamia na kuratibu masuala ya mikataba na makubaliano ya kimataifa;

d) Kusimamia masuala yanayohusu kinga na haki za wanadiplomasia waliopo nchini;

e) Kusimamia na kuratibu masuala ya itifaki na uwakilishi;

f) Kuanzisha na kusimamia huduma za kikonseli;

g) Kuratibu masuala ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa;

h) Kuratibu na kusimamia masuala ya Watanzania wananoishi ughaibuni;

i) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

j) Kuratibu biashara ya kimataifa na diplomasia uchumi;

k) Kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo ya Taasisi zilizo chini ya Wizara; na

l) Kusimamia utawala na maendeleo ya watumishi Wizarani na katika Balozi za Tanzania.

***44. Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa majukumu ya Wizara umeendelea kuongozwa na sera, sheria na miongozo mbalimbali ya kitaifa, kikanda, na kimataifa, ikiwemo Dira ya Taifa ya mwaka 2025; Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26); Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (2021 - 2026); Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025; Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001; Mpango Mkakati wa Wizara wa mwaka 2021/2022 – 2025/2026; Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; Ajenda ya 2030 ya Umoja wa Mataifa ya Malengo ya Maendeleo Endelevu; Ajenda ya 2063 ya Umoja wa Afrika; Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 1999 na Itifaki zake; Mkakati wa Sita wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki 2021/2022 - 2025/2026; Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika wa mwaka 1992 na Itifaki zake; Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2050; Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ya mwaka 2050; na Mpango Mkakati Elekezi wa Maendeleo wa SADC 2020 – 2030.

***45. Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa majukumu ya wizara ulizingatia pia maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wakati wa kujadili Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; na maagizo yaliyotolewa kwa nyakati tofauti kwa Wizara na Viongozi wa Kitaifa, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali.

### 3.1 Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

### 3.1.1 Mapato

***46. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ilipanga kukusanya **Shilingi 1,559,879,000**. Kati ya kiasi hicho, **Shilingi 116,069,000** ni makadirio ya makusanyo kutoka Makao Makuu ya Wizara na **Shilingi 1,443,810,000** ni makadirio ya makusanyo kutoka Balozi za Tanzania. Vyanzo vya mapato hayo ni uhakiki wa nyaraka, na pango la majengo ya Serikali nje ya nchi.

***47. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwezi Julai 2022 hadi Aprili 2023 Wizara imekusanya jumla ya Shilingi 704,417,870.67, sawa na asilimia 60.21 ya lengo. Kati ya kiasi hicho Shilingi 148,802,000 ni makusanyo kutoka Makao Makuu ya Wizara sawa na asilimia 128.20 ya kiasi kilichotarajiwa katika makusanyo toka Makao Makuu, na Shilingi 555,615,870.67 ni kutoka Balozi za Tanzania, sawa na asilimia 38.48 ya kiasi kilichopangwa kukusanywa kutoka Balozini. Kutokufikiwa kwa malengo kumetokana na kukosekana kwa wapangaji katika baadhi ya majengo ya Serikali kwenye Balozi za Tanzania nje ya nchi. Hali hii imesababishwa na uchakavu wa majengo katika balozi zetu na uwepo wa janga la UVIKO-19 uliosababisha biashara katika nchi mbalimbali kufungwa. Fedha zote za maduhuli zilizokusanywa na Wizara ziliingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa taratibu.

### 3.1.2 Fedha Zilizoidhinishwa

***48. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, kiasi cha **Shilingi 208,366,964,000** kiliidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 203,666,964,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na Shilingi 4,700,000,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika fedha zilizotengwa kwa Matumizi ya Kawaida, **Shilingi 188,937,219,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 14,729,745,000** ni kwa ajili ya Mishahara.

### 3.1.3 Mapato na Matumizi

***49. Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 Wizara ilipokea kiasi cha **Shilingi 192,347,150,163.88** sawa na asilimia **92.31** ya kiasi kilichopangwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 177,629,148,103.89** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, sawa na

asilimia 94.01 ya kiasi kilichopangwa kwa matumizi mengineyo; **Shilingi 12,685,955,342.94** ni kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 86.12 ya kiasi kilichopangwa kwa ajili ya mishahara; na **Shilingi 2,032,046,717.05** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na asilimia 43.24 ya kiasi kilichopangwa kwa miradi ya maendeleo.

***Jedwali Na. 1 Mchanganuo wa fedha zilizopangwa na kupokelewa***

| Na. | Aina ya Bajeti | Kiasi kilichopitishwa | Kiasi kilichopokelewa kufikia Aprili 2023 | Kiwango cha Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mishahara | 14,729,745,000.00 | 12,685,955,342.94 | 86.12 |
| 2 | Matumizi Mengineyo | 188,937,219,000.00 | 177,629,148,103.89 | 94.01 |
| | **Jumla Matumizi ya Kawaida** | **203,666,964,000.00** | **190,315,103,446.83** | **93.44** |
| 3 | Matumizi ya Maendeleo | 4,700,000,000.00 | 2,032,046,717.05 | 43.24 |
| | **Jumla Matumizi ya Maendeleo** | **4,700,000,000.00** | **2,032,046,717.05** | 43.24 |
| | | **208,366,964,000.00** | **192,347,150,163.88** | **92.31** |

***50. Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 Wizara ilitumia kiasi cha **Shilingi 187,238,392,736.97** sawa na asilimia 97.34 ya fedha zilizopokelewa. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 175,130,466,231.97** sawa na asilimia 98.59 ya kiasi kilichopokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, na kiasi cha **Shilingi 11,183,969,544.00** sawa na asilimia 88.16 kilitumika kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 923,956,961.00** sawa na asilimia 45.47 kilitumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

***Jedwali 2: Mchanganuo wa fedha zilizopokelewa na kutumika***

| Na. | Aina ya Bajeti | Kiasi kilichopokelewa kufikia Aprili 2023 | Kiasi kilichotumika kufikia Aprili 2023 | Kiwango cha Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mishahara | 12,685,955,342.94 | 11,183,969,544.00 | 88.16 |
| 2 | Matumizi Mengineyo | 177,629,148,103.89 | 175,130,466,231.97 | 98.59 |
| | **Jumla Matumizi ya Kawaida** | **190,315,103,446.83** | **186,314,435,775.97** | **97.90** |
| 3 | Matumizi ya Maendeleo | 2,032,046,717.05 | 923,956,961.00 | 45.47 |
| | **Jumla Matumizi ya Maendeleo** | **2,032,046,717.05** | **923,956,961.00** | **45.47** |
| | **Jumla ya Fedha** | **192,347,150,163.88** | **187,238,392,736.97** | **97.34** |

**UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU**

**3.2 Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje**

***51. Mheshimiwa Spika,*** napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuongozwa na Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001. Ili kuendana na mabadiliko katika uhusiano wa kimataifa na mambo ya nje, Wizara imefanya marejeo ya sera hiyo. Katika marejeo hayo Wizara imefanya tathmini kupima iwapo misingi na malengo ya Sera ya Mambo ya Nje vinakidhi mahitaji ya sasa baada ya zaidi ya miaka 20. Aidha, tathmini hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa ushauri wa Bunge hili.

***52. Mheshimiwa Spika,*** napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, tathmini hiyo imebainisha kuwa misingi ya Sera iliyopo bado inakidhi matakwa ya sasa na ya baadaye. Aidha, yapo maeneo mapya yanayohitaji kujumuishwa katika Sera hii. Misingi hiyo ni

kulinda uhuru wa kujiamulia mambo yetu wenyewe; kuheshimu mipaka ya nchi na uhuru wa kisiasa; kulinda uhuru, haki za binadamu, usawa na demokrasia; kukuza ujirani mwema; kuendeleza Umoja wa Afrika; kukuza ushirikiano wa kiuchumi na wabia wa maendeleo; kuunga mkono utekelezaji wa sera ya kutofungamana na upande wowote; kuimarisha ushirikiano wa nchi zinazoendelea; na kuunga mkono Umoja wa Mataifa katika jitihada zake za kuimarisha maendeleo ya uchumi wa kimataifa, amani na usalama. Tathmini hiyo imeainisha pia maeneo mapya yanayohitaji kujumuishwa katika Sera ya Mambo ya Nje, na imeibua mikakati mipya ya utekelezaji wa sera hiyo, ili kuendana na mazingira ya sasa na ya baadaye.

***53. Mheshimiwa Spika,*** kwa muktadha huo, Wizara kwa kushirikiana na wadau muhimu ndani na nje ya Serikali imekamilisha maandalizi ya marekebisho ya Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 Toleo la Mwaka 2023 na Mkakati wa utekelezaji. Marekebisho ya Sera yameendelea kuweka msisitizo katika diplomasia ya uchumi. Aidha, maeneo mapya yaliyojumuishwa ni pamoja na masuala ya diaspora; uchumi wa buluu; mazingira na mabadiliko ya tabianchi; na kukuza na kubidhaisha lugha ya Kiswahili. Taratibu za kukamilisha Sera hii zinaendelea kwenye ngazi za maamuzi baada ya ngazi za wataalam kukamilika.

### 3.3 Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi

***54. Mheshimiwa Spika,*** Diplomasia ya Uchumi ni dhana kuu katika utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje, ambayo dhamira yake ni kuwa na ushirikiano na uhusiano wa Kimataifa wenye manufaa ya kiuchumi. Dhana hii inazingatiwa katika malengo yote ya sera ya mambo ya nje ambapo hata malengo yanayoonekana ya kisiasa yanachukuliwa kuwa ni sehemu ya kutoa fursa ya kuelekea mahusiano yenye manufaa ya kiuchumi.

***55. Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi unahusisha sekta mbalimbali za kiuchumi na jamii, zilizopo katika sekta ya Umma na sekta Binafsi. Masuala yanayozingatiwa ni pamoja na kutafuta masoko ya bidhaa zetu, kutafuta fursa za

kiuchumi katika sekta mbalimbali, mikopo na misaada yenye masharti nafuu; kuvutia uwekezaji na mitaji; kuvutia watalii, kubidhaisha lugha ya Kiswahili, fursa za elimu, utaalamu na ujuzi na ajira nje ya nchi.

***56. Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua kuwa utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi ni suala mtambuka, na ili kuongeza tija katika utekelezaji wake, Wizara inaendelea na maandalizi ya Mpango na Mkakati wa Kitaifa wa utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi. Mpango Mkakati utawezesha wadau kutoka sekta zote husika, sekta ya umma na sekta binafsi kushiriki kikamilifu na kwa tija zaidi.

***57. Mheshimiwa Spika,*** mafanikio yaliyotokana na utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi katika mwaka 2022/23 ni kama yanavyoonekana katika sehemu 3.4(3.4.1 – 3.4.5) hapo chini, hususan uhusiano baina ya Tanzania na nchi nyingine, ziara za Viongozi Wakuu, ushirikiano wa Tanzania na nchi nyingine.

## 3.4 Kusimamia na Kuratibu Masuala ya Uhusiano Baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Nchi Nyingine

***58. Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu ushirikiano na uhusiano baina ya Tanzania na nchi nyingine duniani katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii ifuatavyo:

### 3.4.1 Ziara za Kikazi za Viongozi Wakuu

***59. Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu na kufanikisha ziara za kikazi za kimataifa za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika nchi mbalimbali ifuatavyo:

a) Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jijini Nairobi, Kenya mwezi Septemba 2022 kuhudhuria Sherehe za Uapisho wa Mheshimiwa Dkt. William Ruto, Rais wa Jamhuri ya Kenya;

b) Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jijini Doha, Qatar mwezi Oktoba 2022 kushiriki Mkutano Mkuu wa Dunia wa Ubunifu katika Masuala ya Afya;

c) Ziara ya Kitaifa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jijini Beijing, China mwezi Novemba 2022 kwa mwaliko wa Mheshimiwa Xi Jinping, Rais wa Jamhuri ya Watu wa China;

d) Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jijini Sharm el Sheikh, Misri mwezi Novemba 2022 kushiriki Mkutano wa 27 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi;

e) Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jijini Washington D.C, Marekani mwezi Desemba 2022 kushiriki katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika na Marekani;

f) Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jijini Davos, Uswisi mwezi Januari 2023 kushiriki Mkutano wa Jukwaa la Uchumi Duniani;

g) Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jijini Bujumbura, Burundi mwezi Februari 2023 kushiriki Mkutano wa 20 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

h) Ziara ya Kitaifa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jijini Pretoria, Afrika Kusini mwezi Machi 2023 ambapo alishiriki pia Mkutano wa Pili

wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Afrika Kusini na kongamano la kibiashara kati ya nchi hizi;

i) Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jijini New York, Marekani mwezi Septemba 2022 kushiriki katika Kikao cha 77 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa;

j) Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jijini Kigali, Rwanda mwezi Septemba 2022, kushiriki Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu Maendeleo ya Kilimo ulioratibiwa na Jukwaa la Mapinduzi ya Kilimo Afrika (AGRF);

k) Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jijini Baku, Azerbaijan mwezi Machi 2023 kushiriki katika Mkutano wa Ngazi ya Juu wa Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote;

l) Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi jijini Bujumbura, Burundi mwezi Julai 2022 kuhudhuria Sherehe za Uhuru wa Jamhuri ya Burundi;

m) Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi jijini Muscat, Oman mwezi Oktoba 2022;

n) Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi jijini Kampala, Uganda mwezi Oktoba 2022 kuhudhuria sherehe za uhuru wa Jamhuri ya Uganda;

o) Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi jijini Riyadh, Saudi Arabia mwezi Desemba 2022 kushiriki katika Mkutano wa 22 wa Baraza la Kimataifa la Safari na Utalii;

p) Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Jamhuri ya Korea mwezi Oktoba 2022, kufuatia mwaliko wa Mheshimiwa Han Duck-soo, Waziri Mkuu wa nchi hiyo;

q) Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Tunisia, mwezi Oktoba, 2022 kushiriki Mkutano Mkuu wa Nane wa Kimataifa wa Tokyo kuhusu Maendeleo ya Afrika;

r) Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jijini Kampala, Uganda mwezi Desemba 2022, kuhudhuria sherehe za miaka 75 ya Msikiti wa Chuo Kikuu cha Makerere; na Ziara ya Kikazi Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jijini Luanda, Angola mwezi Desemba, 2022 kushiriki Mkutano wa 10 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Nchi za Afrika, Karibiani na Pasifiki.

***60. Mheshimiwa Spika,*** ziara za viongozi wetu wa kitaifa nje ya nchi zimeliletea taifa letu mafanikio makubwa ya kiuchumi na kijamii ikiwemo yafuatayo:

a) Mheshimiwa Sheikh Tamim Bin Hamad Al Thani, Amiri na Mtawala wa Dola ya Qatar ameahidi kutoa ufadhili kwa wanafunzi wa masomo ya afya; kujenga jengo la mama na mtoto; na kuleta wataalamu wa afya nchini kwa lengo la kubadilishana ujuzi; ujenzi wa vyumba vya madarasa ya sekondari; na kusaidia baadhi ya miradi ya kimkakati ya

maendeleo ya Tanzania kupitia mfuko wa Maendeleo wa Qatar;

b) Tanzania na Oman zilisaini hati za makubaliano ya ushirikiano katika sekta za elimu ya juu na mafunzo ya ufundi; utunzaji wa nyaraka; na ujenzi wa kituo cha uhifadhi wa taarifa. Kusainiwa kwa hati hizo kutawezesha watanzania kupata ufadhili wa masomo nchini Oman, na kuziwezesha nchi hizi mbili kubadilishana uzoefu na ujuzi katika masuala ya utunzaji na uhifadhi wa nyaraka;

c) Tanzania na China zimesaini Hati ya Makubaliano kuruhusu zao la parachichi kuingia katika soko la China, na Hati ya Makubaliano kuruhusu mazao ya uvuvi (*wild aquatic products*) yakiwemo mabondo ya samaki kutoka Tanzania kuingia katika soko la China. Kusainiwa kwa hati hizo kumeongeza wigo wa soko la bidhaa za Tanzania nje ya nchi;

d) Serikali ya Watu wa China kuipatia Tanzania mkopo wa masharti nafuu wa Dola za Marekani milioni 297.64 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa mawasiliano vijijini; msaada wa Dola za Marekani milioni 24.86 kwa ajili ya upanuzi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, na mkopo wa Dola za Marekani milioni 58.3 kwa ajili ya kugharamia upanuzi wa Jengo la 3 la Abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Amani Abeid Karume Zanzibar; Serikali ya China kutekeleza mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa 400 KVA North East Transmission Line; na kuendelea kutoa msaada wa ujenzi wa vyuo vya ufundi (VETA) nchini Tanzania.

e) Tanzania ilichaguliwa na Jukwaa la Uchumi Duniani kuwa miongoni mwa nchi 20 zitakazokuwa vituo vya mapinduzi ya nne ya viwanda duniani. Hatua hiyo itawezesha nchi yetu kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja katika ujenzi wa viwanda na kuongeza ajira kwa watanzania;

f) Kutengwa kwa Dola za Marekani milioni 550 ili kuimarisha usalama wa chakula barani Afrika na kuandaa Mpango wa Miaka Mitano (2023 – 2027) na kuridhiwa kwa ombi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Jukwaa la Mapinduzi ya Kilimo Afrika (*AGRF*) unaotarajiwa kufanyika mwezi Septemba 2023;

g) Serikali ya Jamhuri ya Korea imeahidi kushirikiana na Tanzania kujenga Chuo cha Teknolojia ya Kidijitali ambacho kitakuwa cha kipekee Afrika Mashariki na Kati; kuipatia Tanzania mkopo wa masharti nafuu wa Dola za Marekani milioni 70 kwa ajili ya mradi wa upanuzi wa mfumo wa vitambulisho vya Taifa; Dola za Marekani milioni 65 kwa ajili ya mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya upimaji na ramani; na kusainiwa kwa Hati ya Makubaliano kati ya kampuni za uzalishaji dawa na vifaa tiba za Korea na Bohari ya Dawa Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Tanzania; na

h) Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zinazotarajiwa kunufaika na ufadhili wa Benki ya Dunia kwa ajili ya kutekeleza miradi ya nishati jadidifu kupitia Mfuko wa Teknolojia ya Nishati Salama (*Clean Energy Technology Fund - CTF*) uliotengewa Dola za Marekani bilioni 1.2 na Benki hiyo.

***61. Mheshimiwa Spika,*** Tanzania na Afrika ya Kusini zitaendelea kufanya tafiti za pamoja, kukuza masoko na biashara; na kurejea Mkataba wa ushirikiano katika sekta ya sanaa na utamaduni ili kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili, kubadilishana wataalam, tafiti, tafsiri na ukalimani, na kuimarisha masuala ya udhibiti ubora wa elimu ya juu. Aidha, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitunukiwa tuzo ya juu ya heshima ijulikanayo kama *Order of South Africa* inayotolewa na Rais wa Afrika Kusini. Tuzo hiyo ni ishara ya kumpongeza kwa kuwa Rais wa kwanza mwanamke wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuthamini mchango wake katika kudumisha udugu wa kihistoria kati ya mataifa haya mawili.

***62. Mheshimiwa Spika,*** kwa ujumla ziara hizi za Rais wa Awamu ya Sita (6) Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, na Viongozi wengine Wakuu zimeimarisha uhusiano wa Kimataifa baina ya nchi yetu na nchi rafiki, Jumuiya za Kikanda, na Jumuiya za Kimataifa na kuleta mafanikio makubwa kiuchumi na kijamii. Mafanikio hayo ni pamoja na ongezeko la uwekezaji, kufungua masoko ya bidhaa mbalimbali, ongezeko la watalii, upatikanaji wa misaada na mikopo yenye masharti nafuu kwa miradi mbalimbali katika sekta za kijamii na kiuchumi. Mafanikio haya yameelezwa kwa kina katika Hotuba za Bajeti za Kisekta.

***63. Mheshimiwa Spika,*** kupitia Bunge lako Tukufu, naomba kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na mafanikio ambayo ameiletea taifa letu katika kipindi cha miaka miwili (2) ya uongozi wake. Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya, nguvu na maono zaidi. Napenda pia kuwashukuru wadau wote toka sekta ya Umma na Binafsi kwa kuendelea kushirikiana na Wizara yangu katika utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje.

### 3.4.2 Ziara za Kikazi za Kitaifa za Viongozi Wakuu toka Mataifa ya Nje

***64. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara za kikazi na kitaifa za viongozi wakuu kutoka mataifa mengine hapa nchini kama ifuatavyo:

a) Ziara ya Kitaifa ya Mheshimiwa Hakainde Hichilema, Rais wa Jamhuri ya Zambia hapa nchini mwezi Agosti, 2022 kwa mwaliko wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

b) Ziara ya Kitaifa ya Mheshimiwa Felix Antoine Tshisekedi Tshilombo, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) hapa nchini mwezi Oktoba 2022 kwa mwaliko wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

c) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Paul Kagame, Rais wa Jamhuri ya Rwanda iliyofanyika mwezi Aprili 2023 kwa mwaliko wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

d) Ziara ya kikazi Mheshimiwa Kamala Harris, Makamu wa Rais wa Marekani nchini Tanzania mwezi Machi 2023 kwa mwaliko wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

e) Ziara ya Mhe. Sheikh Shakhboot Bin Nahyan Al Nahyan, Waziri wa Nchi anayeshughulikia Mambo ya Nje wa Umoja wa Falme za Kiarabu iliyofanyika Zanzibar mwezi Februari 2023; na

f) Ziara ya kikazi ya Mhe. Helen Budriger Artieda, Waziri wa Mambo ya Nje wa Uswisi ambaye aliambatana na wafanyabiashara kutoka Uswisi mwezi Februari 2023.

***65. Mheshimiwa Spika,*** ziara hizo zimekuwa na mafanikio mengi kwa nchi yetu yakiwemo yafuatayo:

a) Tanzania na Zambia zilikubaliana kuimarisha utekelezaji wa mikataba ya TAZARA na TAZAMA; Mkataba wa Usafiri wa Anga (BASA); Tanzania kuiuzia gesi asilia nchi ya Zambia kutoka Mtwara; kusainiwa kwa mikataba ya makubaliano ya ushirikiano katika sekta za ulinzi, sanaa na utamaduni;

b) Marekani imeahidi kujenga kiwanda kikubwa nchini cha kuchakata madini yanayotumika kutengeneza betri za magari ya umeme kwa ajili ya soko la Marekani na dunia kinachotarajiwa kukamilika ifikapo mwaka 2026. Kiwanda hiki kinatarajiwa kuongeza mauzo ya Tanzania nje ya nchi na kuzalisha ajira kwa watanzania; Marekani kutoa msaada wa nyongeza wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 1.3 kupitia Shirika lake la misaada la USAID kwa ajili ya kukabiliana na magonjwa ya mlipuko; Tanzania na Marekani zilisaini

mkataba wa msaada wa wenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 1.1 kwa ajili ya kufadhili miradi ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini, na Hati ya Makubaliano ya kubadilishana ushauri wa kitaalam na kujenga uwezo wa Tanzania kusimamia bandari, hususan katika maeneo ya upanuzi wa bandari, vifaa vya kisasa na uendelezaji wa bandari, Hati ya Makubaliano ya kuanzisha ushirikiano katika masuala ya mawasiliano na teknolojia ya mawasiliano ya kisasa yenye kasi ya 5G, mapambano dhidi ya uhalifu wa kimtandao na usalama wa kimtandao, na Hati ya Makubaliano ya msaada wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 500 kwa ajili ya kuimarisha mazingira ya biashara kati ya Tanzania na Marekani; na Tanzania na Marekani kutekeleza mradi wa kulinda mazingira ya bahari na kuongeza tija kwenye mfumo wa ikolojia ya bahari utakaotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (5) kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 8.4;

c) Umoja wa Falme za Kiarabu umefungua Konseli Kuu yake Zanzibar itakayorahisisha upatikanaji wa huduma za kikonseli, viza na kuchagiza ukuaji wa biashara, utalii na uwekezaji kati ya Tanzania na Umoja huo;

d) Tanzania na Uswisi zimekubaliana kuanzisha ushirikiano katika sekta ya nishati hususan, uendelezaji wa nishati jadidifu; mafuta na gesi; viwanda vya dawa na vifaa tiba; na

e) Tanzania na Rwanda zimekubaliana kuendelea kuimarisha ushirikiano wa kibiashara; kuimarisha ushirikiano katika sekta ya miundombinu na TEHAMA na kukamilisha mradi wa pamoja wa Kufua Umeme wa Rusumo unaozijumuisha Burundi, Tanzania na Rwanda.

***66. Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio yaliyoainishwa, ziara hizo zimeendelea kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na nchi nyingine. Wizara itaendelea kuratibu ziara za kimkakati za Viongozi Wakuu wa Kitaifa nje ya nchi, na Viongozi

Wakuu wa nchi nyingine wanaozuru Tanzania, ili nchi yetu iendelee kunufaika na fursa za kiuchumi na kijamii, na kung'ara Kikanda na Kimataifa.

### 3.4.2 Ushirikiano wa Tanzania na Nchi za Afrika

***67. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushirikiana na Nchi za Afrika ikiwa ni pamoja na kupitia katika Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano ifuatavyo:

a) Mwezi Agosti 2022, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 15 wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Msumbiji uliofanyika jijini Dar es Salaam. Kupitia Mkutano huo, Tanzania na Msumbiji zimeendelea kuimarisha ushirikiano katika maeneo ya biashara, uwekezaji, diplomasia, nishati na kilimo. Vilevile, nchi hizi zilisaini Hati ya Makubaliano ya ushirikiano katika masuala ya ulinzi na usalama. Kusainiwa kwa hati hii kutachangia kuimarisha ulinzi na usalama kwa nchi hizi, ikiwemo maeneo ya mipakani.

b) Mwezi Septemba 2022, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, uliofanyika jijini Dar es Salaam. Mkutano huo uliwezesha kufikiwa kwa makubaliano ya ushirikiano katika masuala ya diplomasia, biashara, uwekezaji, kilimo, nishati, ujenzi, uchukuzi na fedha. Vilevile, nchi hizi zilisaini Hati ya Makubaliano ya ushirikiano katika sekta ya ulinzi kwa lengo la kuimarisha masuala ya ulinzi na usalama.

c) Mwezi Oktoba 2022, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Tano (5) wa Tume ya Kudumu ya Pamoja ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Malawi uliofanyika jijini Dar es Salaam. Katika Mkutano huo pande mbili zilisaini Hati za Makubaliano ya ushirikiano katika maeneo ya usalama wa raia na uhamiaji. Kusainiwa kwa hati hizi kutaimarisha usalama wa raia na biashara mpakani, na kurahisisha uingiaji na utokaji wa raia wa nchi hizi.

d) Mwezi Oktoba 2022, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 10 wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Zambia uliofanyika jijini Lusaka, Zambia. Kupitia Mkutano huo, pamoja na masuala mengine pande mbili zilijadiliana kuhusu namna ya kuhuisha utendaji wa TAZARA na TAZAMA; namna ya kukubaliana na changamoto zinazowakabili madereva, wamiliki wa malori na wasafirishaji wa mizigo kwenda Zambia na DRC; na kuendeleza ushirikiano katika sekta za kilimo, biashara, uwekezaji, nishati na sekta ya fedha. Vilevile, nchi hizi zilisaini Mkataba wa kubadilishana wafungwa ambao utawezesha wafungwa wa Tanzania kutumikia vifungo nchini mwao.

e) Mwezi Februari 2023, Tanzania na Angola zilisaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Chuo cha Diplomasia cha Tanzania na Chuo cha Diplomasia cha Angola. Tanzania imekuwa na ushirikiano wa kihistoria wa muda mrefu na Angola ambao umewezesha wanadiplomasia wengi kutoka Angola kupata mafunzo kwenye Chuo cha Diplomasia Tanzania. Hivyo, kusainiwa kwa hati hiyo kunatoa nafasi kwa vyuo hivyo kubadilishana wataalam, ujuzi na uzoefu katika maeneo ya ufundishaji, machapisho, mitaala na tafiti za masuala ya kimataifa na makongamano ya kitaaluma.

f) Mwezi Februari 2023, Wizara ilisaini Hati mbili za Makubaliano za kuanzisha Tume za Kudumu za Pamoja za Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Muungano wa Visiwa vya Comoro; na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Angola. Kuanzishwa kwa Tume hizo kunaweka mfumo rasmi wa ushirikiano ambao utawezesha nchi hizi kuainisha maeneo ya ushirikiano na kuwezesha wataalam wa pande husika kukutana mara kwa mara kwa ajili ya kujadiliana namna ya kuyatekeleza maeneo husika kwa maslahi ya pande zote.

g) Mwezi Machi 2023, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Tatu wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya

Tanzania na Namibia uliofanyika jijini Windhoek, Namibia. Kupitia Mkutano huo, nchi hizi mbili zilikubaliana kuimarisha ushirikiano katika sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na nishati. Vilevile, zilisaini Hati za Makubaliano ya Ushirikiano tatu (3) katika maeneo ya nishati; usalama wa raia; na mashauriano ya kisiasa na kidiplomasia. Kufuatia makubaliano hayo pamoja na Hati zilizosainiwa Tanzania na Namibia zitashirikiana katika kubadilishana uzoefu na ujuzi; uhawilishaji wa teknolojia; utafiti; kukuza biashara miongoni mwao, na kuvutia uwekezaji katika sekta hizo.

h) Mwezi Machi 2023, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Pili wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Afrika Kusini uliofanyika jijini Pretoria, Afrika Kusini. Katika Mkutano huo, nchi hizi mbili zilisaini Hati tatu (3) za Makubaliano ya Ushirikiano katika maeneo ya biashara, mashauriano ya kisiasa na kidiplomasia na ushirikiano kati ya Vyuo vya Diplomasia. Aidha, Kupitia Mkutano huo, nchi hizi mbili zilifanya Kongamano la kibiashara lililozikutanisha kampuni kutoka Tanzania na Afrika Kusini, pamoja na wadau wengine wa biashara na uwekezaji.

### 3.4.3 Ushirikiano wa Tanzania na Nchi za Asia na Australasia

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushirikiana na Nchi za Asia na Australasia ifuatavyo:

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Agosti 2022, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano Mkuu wa Nane wa Kimataifa wa Tokyo kuhusu Maendeleo ya Afrika (TICAD VIII) uliofanyika nchini Tunisia. Wakati wa Mkutano huo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliwasilisha miradi nane ya kipaumbele katika sekta za miundombinu, nishati, kilimo, maji, mifugo, uvuvi na uchumi wa buluu yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 1.18 kwa ajili ya kupata ufadhili kutoka Serikali ya Japan. Majadiliano kuhusu upatikanaji wa fedha hizo yanaendelea kati ya Serikali za nchi hizi mbili.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** wakati wa Mkutano huo, Tanzania na Japan zilikubaliana kuanza utekelezaji wa miradi mitatu ya TICAD VI iliyokuwa imekwama kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kuongezeka kwa gharama za malighafi na kushuka thamani kwa fedha ya Japan. Miradi hiyo ni ujenzi wa barabara ya Arusha – Holili inayojengwa kwa mkopo wa masharti nafuu wa Yen bilioni 24.31; mradi wa maji Zanzibar unaojengwa kwa mkopo wa masharti nafuu wa Yen bilioni 10.864; na mradi wa ukarabati wa Bandari ya Kigoma unaotekelezwa kwa msaada wa Yen bilioni 2.726.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba 2022 Wizara iliratibu ziara ya wawakilishi wa Kampuni ya DHD Fracon PVT Ltd toka India yenye lengo la kuwekeza katika kilimo cha miwa na kujenga kiwanda cha sukari mkoani Simiyu. Ujumbe huo ulikutana na kufanya mazungumzo na Uongozi wa Mkoa wa Simiyu ili kupatiwa eneo kwa ajili ya uwekezaji huo. Mradi huo unakadiriwa kuwa na thamani ya Dola za Marekani milioni 50 na utatoa ajira 550 za moja kwa moja na ajira 3,000 zisizo za moja kwa moja.

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Jamhuri ya Korea imewezesha Kampuni ya Green Mirae toka Korea kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha kukamua mafuta ya maganda ya Korosho mkoani Pwani. Kiwanda hicho kinatarajiwa kuzinduliwa na kuanza uzalishaji mwezi Juni 2023. Aidha, kampuni hiyo imeonesha nia ya kujenga kiwanda cha kubangua korosho ili kujihakikishia upatikanaji wa malighafi ya kiwanda cha kukamua mafuta ya maganda ya korosho.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Jamhuri ya Korea, imewezesha Kampuni ya GF OIL toka Korea kuingia makubaliano na Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) ya kuwekeza kwenye mashamba ya kilimo cha michikichi pamoja na kujenga viwanda vya kukamua mafuta ya michikichi mkoani Kigoma. Mazungumzo yanaendelea kupitia Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

**3.4.4 Ushirikiano wa Tanzania na Nchi za Mashariki ya Kati**

***74. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha mahusiano na Nchi za Mashariki ya Kati ifuatavyo:

a) Mwezi Julai 2022, Wizara iliratibu ziara ya Mamlaka ya Uwekezaji na Maendeleo ya Kilimo (*the Arab Authority for Agricultural Investment and Development - AAAID*), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Uchumi Afrika (BADEA) na kampuni ya Al-bashyer kutoka Oman. Lengo la ziara hiyo lilikuwa ni kutembelea maeneo mbalimbali na kufanya mazungumzo na taasisi za umma na binafsi kwa ajili ya kufanya biashara na uwekezaji. Miongoni mwa taasisi zilizotembelewa ni Benki ya Maendeleo ya Kilimo nchini (TADB), Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), kiwanda cha nyama cha TANCHOICE, kampuni ya Masenga inayojishughulisha na uwekezaji kwenye kilimo na ufugaji pamoja na eneo la uwekezaji la Ranchi ya Zanzibar Bagamoyo (RAZABA). Ziara hii iliwezesha kusainiwa kwa Mkataba wa Makubaliano ya Ushirikiano kati ya NARCO na *The Arab Authority for Agricultural Investment and Development (AAAID)*. Mkataba huo una lengo la kuwezesha uwekezaji katika sekta ya mifugo. Vilevile, Benki ya BADEA iliingia makubaliano ya kuikopesha Benki ya Kilimo Tanzania (TADB) kiasi cha Dola za Marekani milioni 40 kwa ajili ya kutoa mikopo ya masharti nafuu kwenye sekta ya kilimo. Aidha, Kampuni ya Al-Bashyer iliingia makubaliano na kiwanda cha TANCHOICE ya kusafirisha nyama kwenda nchini Oman. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, kiwanda cha TANCHOICE kinaendelea kusafirisha nyama kwenda nchini Oman.

b) Mwezi Agosti 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha kusainiwa kwa Hati ya Makubaliano kati ya Hospitali ya Benjamin Mkapa na Hospitali ya Sheba ya nchini Israel. Makubaliano hayo yanatoa fursa kwa madaktari wa Hospitali ya Benjamin Mkapa kujengewa uwezo katika tiba ya magonjwa ya moyo, kufanya ziara za kitabibu na ufadhili katika shahada ya mfumo wa mmeng'enyo wa chakula (*Gastroenterology*) nchini Israel.

c) Mwezi Septemba 2022, Wizara iliratibu na kufanikiwa kupeleka wanafunzi 250 nchini Israel kupata mafunzo ya vitendo na ujuzi kuhusu kilimo na ufugaji kwa muda wa miezi 11. Wanafunzi hao walitoka kwenye vyuo vya kilimo na mifugo hapa nchini. Aidha, katika kipindi hiki maandalizi ya kupeleka wanafunzi wengine 260 mwezi Agosti, 2023 nchini Israel yanaendelea. Ni matarajio ya Serikali kuwa, wanafunzi hao watakaporejea watajiajiri, watatoa ajira kwa wengine, na kukuza sekta za kilimo na mifugo.

d) Mwezi Desemba 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha Mkutano wa Pili wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Falme ya Oman uliofanyika jijini Muscat, Oman. Katika Mkutano huo pande hizi mbili zilikubaliana kuimarisha na kukuza ushirikiano katika sekta mbalimbali za uchumi, ikiwemo biashara, utalii, uchukuzi na uchumi wa buluu. Manufaa ya Makubaliano hayo, ni pamoja na kuanzishwa kwa mfuko wa pamoja wa uwekezaji, na kuanzishwa kwa safari za meli kati ya nchi hizi mbili, kuongezeka kwa watalii kutoka Oman, na kukuza soko la bidhaa za Tanzania nchini Oman, hususan nyama, mchele, na mbogamboga.

e) Mwezi Januari 2023, Wizara iliratibu na kufanikisha ujio wa timu ya Madaktari bobezi wa magonjwa ya moyo kutoka Taasisi ya Watoto ya Moyo (*Children Heart Association*) ya nchini Kuwait. Madaktari hao walitoa matibabu kwa wagonjwa 86 katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dodoma na Hospitali ya Mnazi Mmoja, Zanzibar. Katika ziara hiyo madaktari hao walitoa msaada wa vifaa tiba vya kisasa katika Hospitali ya Benjamin Mkapa. Ujio wa madaktari hao, umesaidia kupunguza gharama za matibabu na kubadilishana uzoefu na ujuzi.

### 3.4.5 Ushirikiano wa Tanzania na Nchi za Ulaya na Amerika

***75. Mheshimiwa Spika,*** Uhusiano kati ya Tanzania na Nchi za Ulaya na Amerika umeendelea kuimarika, na katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 shughuli zifuatazo zilifanyika:

a) Mwezi Oktoba 2022, Wizara ilifanya ziara ya kikazi katika nchi za Poland na Ureno. Katika ziara hiyo, pamoja na mambo mengine, Serikali ya Poland ilieleza utayari wa kuendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika kuboresha sekta ya kilimo nchini. Aidha, ziara hiyo ililenga kuhakikisha miradi ya kuunganisha matrekta, na ujenzi wa vihenge na maghala ya kisasa nchini inayotekelezwa kwa fedha za mkopo kiasi cha Dola za Marekani milioni 110 kutoka Serikali ya Poland inakamilika. Kupitia ziara hiyo pande mbili zilikubaliana kuhuisha Mkataba wa mkopo uliofikia ukomo mwezi Desemba, 2022. Mkataba huo umeongezewa muda na sasa utafikia tamati mwezi Desemba, 2025. Kuhuishwa kwa Mkataba huo kutasaidia kukamilisha miradi hiyo ambayo ni muhimu kwa sekta ya kilimo.

b) Katika ziara hii nchini Poland Wizara ilitembelea Chuo Kikuu cha Warsaw; Kituo cha Maji cha Chuo Kikuu cha Warsaw cha Sayansi ya Maisha, na kukutana na watoa huduma za kiusalama mijini. Kufuatia ziara hiyo, Vyuo Vikuu vya Dodoma, Dar es Salaam, Ardhi, na Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela vimeanza majadiliano na Chuo Kikuu cha Warsaw kuhusu ushirikiano katika utoaji wa taaluma za maji. Vilevile, pande mbili zilikubaliana kufufua mazungumzo kuhusu ushirikiano wa kutekeleza mradi wa kuboresha mifumo ya maji safi na maji taka katika jiji la Dar es Salaam na Dodoma; kukamilisha mchakato wa kusaini Hati ya Makubaliano ya ushirikiano kwenye sekta ya elimu; na ushirikiano katika huduma za mtandao wa kidigitali kwa ajili ya usalama mijini. Sekta husika zinaendelea na hatua za majadiliano.

c) Katika kuimarisha uhusiano wa Tanzania na Ureno, mwezi Oktoba 2022 wakati wa ziara nchini Ureno, Tanzania na Ureno zilisaini Hati ya Makubaliano ya kuanzisha majadiliano ya kidiplomasia na mashauriano ya kisiasa. Makubaliano hayo yataimarisha uhusiano wa kisiasa na kidiplomasia, na hivyo kufungua milango ya ushirikiano wa kiuchumi, ikiwa ni pamoja

na uchumi wa buluu; na biashara kwa bidhaa za kahawa, chai, samaki, viungo vya chakula na mbao. Aidha, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) zilikubaliana na Kituo cha Kukuza Uwekezaji cha Ureno (AICEP) kukamilisha Hati za Makubaliano (MoU), ili kukuza mahusiano na kuchochea uwekezaji na biashara.

d) Mwezi Desemba 2022, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 10 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Nchi za Afrika, Karibiani na Pasifiki (OACPS) uliofanyika jijini Luanda, Angola. Mkutano huo ulipitisha Tamko la Luanda (*Luanda Declaration*) linalolenga pamoja na mambo mengine, kuimarisha ushirikiano ndani ya Jumuiya kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; usalama wa chakula; changamoto ya usalama barabarani; upanuzi wa shughuli za kiuchumi (*economic diversification*); na kudumisha na kuimarisha amani na usalama baina ya Nchi Wanachama wa *OACPS*.

e) Mwezi Desemba 2022, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika na Marekani uliofanyika nchini Marekani. Mkutano huo ulijadili dhana ya kuimarisha ushirikiano baina ya nchi za Afrika na Marekani katika uchumi; biashara, uwekezaji; maendeleo ya vijana; diaspora; afya; usalama wa chakula; amani na usalama; demokrasia, haki za binadamu na utawala bora; TEHAMA; na utunzaji wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Tanzania inatarajia kunufaika ifuatavyo:

i. Mkakati uliotangazwa na Marekani wa kuzipatia nchi za Afrika jumla ya Dola za Marekani milioni 150 kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kupitia matumizi bora ya nishati. Aidha ufadhili huo utaimarisha utekelezaji wa Mpango wa Lishe Bora wa "*Feed the Future*";

ii. Kiasi cha Dola za Marekani bilioni 1.2 kupitia Mpango wa *Millennium Challenge Corporation* (MCC) kwa ajili ya kuendeleza miundombinu;

iii. Dola za Marekani bilioni 600 kwa kipindi cha miaka mitano kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa *Partnership for Global Infrastructure and Investment* (PGII) ulio chini ya Mataifa ya G7 kuendeleza miundombinu katika Bara la Afrika;

iv. Dola za Marekani milioni 20 kwa ajili ya kuwapatia mbolea wakulima wadogo hususan wanawake;

v. Dola za Marekani milioni 10 kusaidia kampuni ndogo na za kati zinazohusika na utoaji wa huduma za maji safi;

vi. Kuanzisha Mpango wa Mageuzi ya Kidijitali Barani Afrika (*Digital Transformation with Africa*); na

vii. Dola za Marekani milioni 350 kuendeleza tasnia ya uchumi wa kidijitali Barani Afrika. Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara za Kisekta, Taasisi za Umma na Binafsi ili kuhakikisha Tanzania inakuwa miongoni mwa mataifa yatakayonufaika na ufadhili huo kupitia uwasilishaji wa mapendekezo ya miradi ya maendeleo.

f) Mwezi Februari 2023, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara iliratibu Kongamano la Kwanza la Biashara na Uwekezaji kati ya Tanzania na Umoja wa Ulaya. Kongamano hilo lilifanyika jijini Dar es Salaam na kushirikisha zaidi ya wafanyabiashara 1000 kutoka Tanzania, na nchi za Umoja wa Ulaya. Kupitia kongamano hilo yafuatayo yalifanyika:

i. Tanzania na Ufaransa zilisaini Mkataba wa Uwili wa Ushirikiano katika Huduma za Usafiri wa Anga. Kusainiwa kwa mkataba

huo kutawezesha kuanzishwa kwa safari za anga za moja kwa moja kati ya nchi hizi, na kukuza sekta ya utalii na Biashara;

ii. Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ya Tanzania (TPA) na Bandari ya *Antwerp Burges International* zilisaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano katika usimamizi wa bandari. Kusainiwa kwa Hati hiyo kutaiwezesha TPA kujengewa uwezo katika maeneo ya usimamizi na uendelezaji wa bandari, na hivyo kuongeza mchango wa bandari zetu katika uchumi wa taifa;

iii. Kusainiwa kwa Mkataba baina ya Serikali, Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Umoja wa Ulaya (EU) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kufua umeme katika maporomoko ya maji Kakono, mkoani Kagera (MW 88). Kupitia Mkataba huo, AFD itatoa mkopo wa masharti nafuu kiasi cha Euro milioni 110 sawa na shilingi bilioni 272.6, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) itatoa kiasi cha Dola za Marekani Milioni 161.47 sawa na shilingi bilioni 374.9, na Umoja wa Ulaya utatoa msaada wa kiasi cha Euro milioni 35 sawa na shilingi bilioni 86.7. Kutekelezwa kwa mradi huo kutasaidia wakazi wa mkoa wa Kagera kuondokana na changamoto ya kukosa umeme wa uhakika, na kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii; na

iv. Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) ilisaini makubaliano na benki za CRDB, NMB na KCB ya kiasi cha Euro milioni 350 kwa ajili ya mikopo kwa wajasiriamali nchini. Vilevile, benki ya FMO ya Uholanzi na benki ya PROPARCO ya Ufaransa zilisaini makubaliano na benki za NMB ya kiasi cha Euro milioni 115 kwa ajili ya mikopo kwa sekta binafsi nchini. Halikadhalika, benki ya FMO ilisaini makubaliano na benki ya NMB ya kiasi cha Euro milioni 10 kwa ajili ya mikopo kwa wanawake na vijana nchini. Kusainiwa kwa mikataba hiyo kutachochea ukuaji wa sekta binafsi na biashara nchini.

i. Mwezi Februari 2023, Wizara iliratibu Majadiliano ya Kisiasa kati ya Tanzania na Umoja wa Ulaya yaliyofanyika jijini Dar es Salaam. Majadiliano hayo yalifanyika kwa mujibu wa Ibara ya 8 ya Makubaliano ya Mkataba wa Cotonou (*Cotonou Partnership Agreement*) uliosainiwa mwaka 2000. Kupitia majadiliano hayo, Tanzania na Umoja wa Ulaya zilikubaliana kukuza ushirikiano kwenye maeneo ya biashara na uwekezaji; uchumi wa buluu; mabadiliko ya tabianchi; haki za binadamu na demokrasia; na Mpango wa Umoja wa Ulaya wa *Global Gateway Investment Package* uliotengewa Euro milioni 150. Maeneo mengine ni kuimarisha ushirikiano katika ulinzi na amani hususan kupitia Jumuiya za Kikanda, ikiwemo Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Jumuiya ya Ukanda wa Maziwa Makuu (ICGLR), na ushirikiano wa kimataifa.

ii. Mwezi Februari 2023, Wizara iliratibu ziara ya ujumbe wa Hospitali ya Benjamin Mkapa jijini Vienna, Austria. Kupitia ziara hiyo, Hospitali ya Benjamin Mkapa ilisaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano na Hospitali Kuu ya Vienna *(Vienna General Hospital),* pamoja na Chuo Kikuu cha Tiba cha Vienna. Makubaliano hayo yanalenga kuwapatia mafunzo ya kuwajengea uwezo madaktari wa Hospitali ya Benjamin Mkapa katika utoaji wa huduma za tiba za kibingwa ikiwemo tiba za magonjwa ya mfumo wa mkojo na saratani ya kibofu, tiba ya magonjwa ya mifupa, na patholojia.

iii. Mwezi Machi 2023, Wizara iliratibu na kushiriki katika majadiliano ya ushirikiano baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Latvia. Kupitia majadiliano hayo, pande mbili zilikubaliana kuimarisha ushirikiano kwenye sekta za kilimo, TEHAMA, usafiri wa anga, biashara na uwekezaji. Hatua hiyo itainufaisha Tanzania kupitia uwekezaji wa moja kwa moja, upatikanaji wa masoko, na uhawilishaji wa ujuzi na teknolojia kutoka nchi ya Latvia.

### 3.5 Kuratibu Masuala ya Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

### 3.5.1 Umoja wa Afrika

***76. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha uhusiano na Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika (AU) kupitia ushiriki wake katika vikao vya Umoja huo na kulinda maslahi ya taifa. Mwezi Februari 2023 Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 36 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika jijini Addis Ababa, Ethiopia. Pamoja na mambo mengine, mkutano ulitoa tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Miaka 10 ya Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Afrika (*Agenda 2063: The Africa We Want*), na kuainisha maeneo ya kipaumbele yanayopaswa kujumuishwa katika Mpango wa Pili wa Miaka 10 wa Utekelezaji wa Agenda 2063 kuanzia mwaka 2023 hadi 2033. Maeneo hayo yamezingatia vipaumbele vya Tanzania, ambayo ni pamoja na:

i. Kila nchi mwanachama kufikia kipato cha kati;

ii. Bara la Afrika kuunganika zaidi kupitia soko la pamoja la huduma za kidijitali, soko la usafiri wa anga, na miundombinu mingine ya kiuchumi;

iii. Kuimarisha taasisi za kidemokrasia zinazozingatia mahitaji ya wananchi;

iv. Afrika kutatua migogoro kwa njia ya amani; na

v. Kuimarisha na kukuza maadili na tamaduni za kiafrika.

***77. Mheshimiwa Spika,*** katika Mkutano huo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitunukiwa tuzo ya *African Leaders Malaria Alliance (ALMA)* kutokana na mchango wake wa kuongoza juhudi za Serikali ya Tanzania katika kutokomeza ugonjwa wa malaria. Baadhi ya juhudi hizo ni pamoja na kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na uimarishaji wa miundombinu ya vituo vya afya.

***78. Mheshimiwa Spika,*** pembezoni mwa mkutano huo, Mheshimiwa Rais alishiriki Mkutano wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kuhusu juhudi za upatikanaji wa amani mashariki mwa DRC kama sehemu ya kuimarisha amani na usalama katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, na ukanda wa Maziwa Makuu.

***79. Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba, 2022 Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 17 wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika kuhusu Maendeleo ya Viwanda barani Afrika na Uanuai wa Uchumi (*Industrialization and Economic Diversification*) na Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA) uliofanyika jijini Niamey, Niger. Mkutano huo uliazimia mambo mbalimbali yenye manufaa kwa nchi yetu ifuatavyo:

i. Kuongeza kasi ya uendelezaji wa viwanda vya uzalishaji bidhaa ili kukuza uchumi kwa kuongeza mnyororo wa thamani kwenye rasilimali za bara la Afrika katika sekta za kipaumbele za afya na dawa za binadamu, madini, chakula, lishe na mavazi ili kupunguza utegemezi; na

ii. Kuanzisha Programu unganishi kati ya Mifumo ya Elimu na Soko la Afrika kwa lengo la kuongeza ushindani wa Sekta Binafsi kwa kujenga uwezo na ujuzi unaohitajika kwenye maendeleo ya viwanda.

### 3.5.2 Jumuiya ya Afrika Mashariki

***80. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika utekelezaji wa hatua za Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuzingatia Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 1999 na itifaki zake, na hivyo kusimamia maslahi ya Tanzania katika mtangamano huo.

#### 3.5.2.1 Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki

***81. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inayolenga kukuza biashara, kuongeza ufanisi katika uzalishaji,

kukuza uwekezaji wa ndani baina ya nchi wanachama na kuendeleza viwanda. Kwa mwaka 2022 thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania ndani ya Jumuiya iliongezeka kwa asilimia 21.8 kufikia Dola za Marekani bilioni 1.4 ikilinganisha na Dola za Marekani bilioni 1.2 mwaka 2021. Ongezeko hilo linatokana na uwepo wa mazingira bora ya uwekezaji na biashara kwa kuondoa vikwazo visivyo vya kiforodha miongoni mwa nchi wanachama. Aidha, Wizara inaendelea kuhamasisha wafanyabiashara wa Tanzania kutoa taarifa mapema kuhusu vikwazo visivyo vya kiforodha wanavyokumbana navyo ili vipatiwe ufumbuzi wa haraka.

**3.5.2.2 Soko la Pamoja**

***82. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo ni hatua ya pili ya Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Maeneo ya msingi yanayotekelezwa katika Itifaki hii ni pamoja na soko huru la bidhaa; uhuru wa raia wa Afrika Mashariki kutoka na kuingia ndani ya Jumuiya; uhuru wa raia wa Afrika Mashariki kupata ajira ndani ya Jumuiya; uhuru wa kufanya biashara ya huduma; uhuru wa kuwekeza mitaji; haki ya raia wa Afrika Mashariki kuanzisha na kuendesha shughuli za kiuchumi na biashara ndani ya Jumuiya; na haki ya ukaazi kwa raia wa Afrika Mashariki.

***83. Mheshimiwa Spika,*** mwezi Julai 2022, Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki walikuwa na Mkutano Maalum wa Kilele kuhusu utekelezaji wa Soko la Pamoja *(The High-Level Summit Retreat on the EAC Common Market*). Mkutano huo ulipokea taarifa na kujadili mafanikio, fursa, na changamoto katika miaka 11 ya utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja. Mkutano uliazimia namna ya kuongeza kasi ya utekelezaji kwa ajili ya ustawi wa Nchi na wananchi wa Afrika Mashariki. Miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa katika Mkutano huo ni pamoja na: kuchochea biashara ili kuongeza kiwango cha biashara miongoni mwa Nchi Wanachama; kuongeza uzalishaji na kiwango cha matumizi ya bidhaa zinazozalishwa ndani ya Jumuiya; na kuwezesha uhamishaji wa matumizi ya bima za afya za umma ndani ya Nchi Wanachama.

### 3.5.2.3 Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki

***84. Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba 2022, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Fedha na Masuala ya Uchumi uliofanyika jijini Arusha. Mkutano huo, pamoja na masuala mengine ulijadili tathmini ya utekelezaji wa Mpangokazi wa Miaka Kumi (2014 – 2024) wa Kufikia Sarafu Moja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa mujibu wa ibara ya 5 (3) ya Itifaki ya Umoja wa Fedha, nchi wanachama zilitakiwa kufikia vigezo vya uchumi mpana mwaka 2021 na kuvidumisha kwa muda wa miaka mitatu (3) mfululizo kabla ya kuingia kwenye sarafu moja mwaka 2024.

***85. Mheshimiwa Spika,*** vigezo hivyo ni kiwango cha juu cha mfumuko wa bei kisichozidi asilimia 8; kiwango cha juu cha deni la taifa kisichozidi asilimia 50 ya pato la Taifa; akiba ya fedha za kigeni ya kutosheleza mahitaji ya miezi minne na nusu; na kiwango cha juu cha nakisi ya bajeti, ikijumuisha misaada kisichozidi asilimia 3 ya pato la Taifa. Tathmini hiyo imebainisha kuwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki hazijakidhi baadhi ya vigezo vilivyoainishwa katika Itifaki ya Umoja wa Fedha. Aidha, Tanzania na Uganda ndizo nchi pekee zilizofanikiwa kukidhi vigezo vitatu (3) kati ya vinne (4). Hakuna Nchi Mwanachama iliyoweza kukidhi kigezo cha nakisi ya bajeti, ikijumuisha misaada kutozidi asilimia 3 ya pato la Taifa.

***86. Mheshimiwa Spika,*** kutokana na matokeo ya tathmini hiyo, Mkutano wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Fedha na Mipango ulihuisha Mpango Kazi wa kufikia Sarafu Moja na kuongeza muda wa utekelezaji wake kutoka mwaka 2024 hadi 2031. Mpango Kazi uliohuishwa umeainisha shughuli zitakazotekelezwa, ikiwa ni pamoja na kuanzisha Taasisi zitakazosimamia utekelezaji wa Umoja wa Fedha; na uoanishaji wa Sera za Kodi, Sera za Fedha na Sera za Viwango vya Kubadilisha Fedha za Kigeni.

### 3.5.2.4 Utekelezaji wa Programu za Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Sekta za Uzalishaji

#### Sekta ya Viwanda

***87. Mheshimiwa Spika,*** mwezi Desemba 2022, Wizara iliratibu na kushiriki katika Maonesho ya 22 ya Wajasiriamali Wadogo na wa Kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yajulikanayo kama Juakali/Nguvukazi yaliyofanyika jijini Kampala, Uganda. Maonesho hayo yalikuwa na kaulimbiu isemayo '*Buy East Africa for Resilience and Sustainable Development*' yalijumuisha wajasiriamali takribani 1,500 kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wajasiriamali 250 kutoka Tanzania walishiriki maonesho hayo ambapo kati yao 198 walitoka Tanzania Bara na 52 walitoka Zanzibar. Katika maonesho hayo Tanzania ilipata tuzo katika eneo la ubunifu wa mashine za kubangulia korosho na kujaza hewa ya *oxygen* migodini. Aidha, kampuni ya Tanzania ya Woiso *Leather Products* inayojishughulisha na utengenezaji wa viatu vya ngozi ilikuwa mshindi wa pili, na kampuni ya Tanzania ya *Urban Vintage* inayojishughulisha na uzalishaji wa mvinyo kwa kutumia zabibu ilikuwa mshindi wa tatu.

***88. Mheshimiwa Spika,*** mwezi Desemba 2022, Wizara iliratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa 41 wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Biashara, Viwanda, Fedha na Uwekezaji uliofanyika jijini Arusha. Pamoja na mambo mengine, Mkutano huo ulipitisha Kanuni za Jumuiya ya Afrika Mashariki za kuunganisha (*assembling*) magari na pikipiki katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kanuni hizi zinalenga kukuza na kusimamia uzalishaji wa baadhi ya vipuri vya magari na pikipiki ili kuchangia katika mnyororo wa thamani katika sekta ya uunganishaji wa magari katika Nchi Wanachama. Wizara inahamasisha wawekezaji kuchangamkia fursa za uwekezaji nchini Tanzania katika kutengeneza na kuzalisha vipuri vya magari na pikipiki kwa ajili ya soko la Afrika Mashariki.

***89. Mheshimiwa Spika,*** mwezi Februari 2023, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye Mkutano wa 43 wa Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki uliofanyika jijini Bujumbura, Burundi. Pamoja na mambo mengine, mkutano huo uliidhinisha na kupitisha Sera ya Kanda Maalum za Kiuchumi ya Afrika Mashariki. Utekelezaji wa Sera hiyo utawezesha Nchi Wanachama kuanzisha au kuendeleza Kanda na Maeneo Maalum ya Kiuchumi, na hivyo kuimarisha ukuaji wa viwanda na mauzo ya nje.

**Sekta ya Kilimo**

***90. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara inaendelea kuratibu mradi wa ushirikiano kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya (*MARKUP EU-EAC*) unaolenga kuwezesha bidhaa za kilimo kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki kukidhi viwango vya soko la Umoja wa Ulaya. Bidhaa zilizopewa kipaumbele katika mradi huo ni kahawa, chai, parachichi, viungo na mbogamboga. Mradi huo unatekelezwa katika mikoa ya Tanga, Morogoro, Njombe, Ruvuma, Mbeya, Songwe na visiwa vya Pemba na Unguja. Mradi umewezesha wakulima kuzalisha mazao ya kilimo kwa kutumia mbegu bora na kuzingatia utunzaji wa mazingira, ambapo vyama vya ushirika 26 kutoka mikoa ya Njombe na Ruvuma vimepata hati za ubora na hivyo kukidhi vigezo vya kuuza mazao katika soko la Ulaya.

**3.5.2.5 Utekelezaji wa Miradi na Programu za Miundombinu ya Uchumi na Huduma za Jamii**

**Sekta ya Barabara**

***91. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango iliratibu ushiriki wa Tanzania katika majadiliano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi ya ujenzi ya barabara za kikanda. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa barabara ya Lusahunga – Rusumo/Kayonza - Kigali yenye urefu wa km 162. Juhudi hizi ziliwezesha upatikanaji wa mkopo wa masharti nafuu wa shilingi bilioni 153.6 kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya ujenzi wa kipande cha kuanzia Lusahunga - Rusumo (km 92) kwa kiwango cha lami. Utekelezaji wa mradi huo umeanza mwezi Februari, 2023. Barabara hiyo itakapokamilika

itarahisisha usafiri wa abiria na usafirishaji wa mizigo kati ya Tanzania, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, na hivyo kukuza biashara na shughuli nyingine za kiuchumi miongoni mwa nchi hizi.

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi mwingine wa kikanda ulioendelea katika mwaka 2022/23 ni ujenzi wa barabara ya kikanda ya Kabingo - Kasulu - Manyovu - Rumonge hadi Gitaza yenye urefu wa km 305 unaozijumuisha nchi za Tanzania na Burundi. Kwa upande wa Tanzania mradi huu unahusisha kipande chenye urefu wa km 260.6 kutoka Kabingo – Kasulu hadi Manyovu. Ushirikiano wa kikanda umewezesha upatikanaji wa fedha kiasi cha shilingi bilioni 325.64 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika. Utekelezaji wa mradi huo unafanyika katika sehemu nne ambazo ni Manyovu - Kasulu (km 68.25), Kanyani-Mvugwe (km 70.50), MvugweNduta (km 59.35) na Nduta-Kibondo-Kabingo (km 62.50). Ujenzi wa sehemu zote nne umeanza na upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ushiriki wa Tanzania katika kuendeleza programu za miundombinu za Jumuiya ya Afrika Mashariki umechangia pia upatikanaji wa mkopo wa shilingi bilioni 176.72 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa ajili ya ujenzi wa kipande cha barabara cha Pangani - Tungamaa (km 25.6), na ujenzi wa Daraja la Pangani (mita 525) katika Barabara ya kikanda kati ya Tanzania na Kenya kutoka Bagamoyo - Tanga/Malindi - Lungalunga yenye urefu wa km 400 kwa kiwango cha lami. Kukamilika kwa barabara hiyo kutarahisisha usafirishaji na kukuza biashara na uchumi wa nchi hizi.

**Sekta ya Reli**

***94. Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu majadiliano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Burundi kuhusu kushirikiana katika ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kutoka Uvinza (Tanzania) hadi Gitega (Burundi). Mradi huo unatarajiwa kutekelezwa kupitia ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Kukamilika kwa ujenzi wa reli hiyo, kutaiunganisha nchi yetu na nchi jirani za Burundi, Rwanda na DRC.

**Sekta ya Afya**

***95. Mheshimiwa Spika,*** mwezi Machi 2023, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 23 wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la Afya la Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika jijini Bujumbura, Burundi. Katika mkutano huo, Tanzania ilifanikiwa kuzishawishi nchi nyingine kuanzisha Kituo cha Umahiri cha Kikanda cha Jumuiya ya Afrika Mashariki cha Sayansi ya Afya ya Kinywa kitakachosimamiwa na Chuo Kikuu cha Sayansi ya Afya Muhimbili (MUHAS). Kuanzishwa kwa Kituo hicho kutawanufaisha wananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, na hususan Tanzania katika, kudhibiti na kutibu magonjwa ya afya ya kinywa ambayo ni sehemu ya magonjwa yasiyoambukiza.

**3.5.2.6 Ushirikiano katika Siasa, Ulinzi na Usalama**

***96. Mheshimiwa Spika,*** hali ya ushirikiano katika sekta ya ulinzi na usalama katika Jumuiya ya Afrika Mashariki imeendelea kuwa imara. Hata hivyo zimekuwepo changamoto za kiusalama mashariki mwa DRC ambazo zimehitaji juhudi za pamoja kama Jumuiya. Kwa nyakati mbalimbali, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mikutano ya Wakuu Nchi ikiwa ni pamoja na Mkutano wa 20 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Julai 2022 jijini Arusha, na Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ajili ya kutathmini hali ya usalama katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) uliyofanyika mwezi Februari 2023, jijini Bujumbura, Burundi. Katika Mikutano hiyo, Nchi Wanachama zilipata fursa ya kujadiliana kuhusu changamoto za kiusalama katika eneo hilo na kukubaliana jinsi ya kukabiliana nazo, ikiwa ni pamoja na:

a) Kutafuta amani ya kudumu mashariki ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa njia mbili, mazungumzo ya kisiasa na njia za kijeshi. Katika njia hizi Jumuiya ya Afrika Mashariki ilimteua Mheshimiwa Uhuru Muigai Kenyatta, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Kenya kuwa mwezeshaji wa mazungumzo ya kisiasa, na kuidhinisha kikosi cha Pamoja cha Kulinda Amani cha Jumuiya ya Afrika Mashariki (*East African Community Regional Forces for the Restoration of Peace and Stability in Eastern DRC – EACRF DRC)*, na

b) Kuhuisha juhudi za kurejesha amani mashariki mwa DRC kati ya Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu, na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**3.5.2.7 Bunge la Afrika Mashariki**

***97. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki. Katika kipindi hiki, Wabunge 63 kutoka Nchi Wanachama waliapishwa kutumikia Bunge la Tano kwa kipindi cha miaka mitano. Idadi hiyo ya Wabunge imeongezeka kutokana na DRC kujiunga katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vilevile, Bunge lilimchagua Mheshimiwa Joseph Ntakirutimana kutoka Jamhuri ya Burundi kuwa Spika wa Bunge hilo kwa kipindi cha miaka mitano.

***98. Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, Bunge la Afrika Mashariki lilipitisha miswada miwili (2) ya sheria ambayo ni muswada wa Sheria ya Kamisheni ya Huduma za Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 2022 na muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 2022.

***99. Mheshimiwa Spika,*** kutungwa kwa sheria hizo kunatoa nafasi ya kuanzishwa kwa Kamisheni ya Huduma za Fedha ya Afrika Mashariki kama Taasisi ya Jumuiya yenye majukumu ya kusimamia utekelezaji wa sera, sheria na taratibu za Jumuiya katika sekta ya fedha. Uanzishwaji wa Taasisi hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa Ibara ya 21 ya Itifaki ya Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki.

***100. Mheshimiwa Spika,*** muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Forodha unalenga kuboresha usimamizi wa forodha na taratibu zake katika Jumuiya. Marekebisho ya Sheria hiyo, yatarahisisha shughuli za biashara na kukuza uwekezaji baina ya Tanzania na nchi nyingine wanachama kupitia maboresho ya viwango vya ushuru wa bidhaa.

### 3.5.3 Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

***101. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mtangamano wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kwa lengo la kusimamia maslahi ya taifa, na kuzitumia fursa za kiuchumi na kijamii katika Jumuiya hiyo.

***102. Mheshimiwa Spika,*** mwezi Agosti 2022, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 42 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika jijini Kinshasa, DRC. Katika Mkutano huo, Nchi Wanachama ziliridhia na kusaini Itifaki ya SADC ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu. Kusainiwa kwa Itifaki hiyo kutaiwezesha Tanzania kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine za SADC katika mapambano dhidi ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu pamoja na uhalifu mwingine unaovuka mpaka.

***103. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, katika mkutano huo, Nchi Wanachama ziliridhia Marekebisho ya Ibara ya 9 (1) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa SADC wa mwaka 1992 kuwezesha uanzishwaji wa Bunge la SADC ikiwa ni mojawapo ya Taasisi za SADC. Kuanzishwa kwa Bunge hilo kutaongeza wigo wa ushiriki wa wananchi wa Jumuiya katika hatua za mtangamano wa SADC kupitia wawakilishi wao katika chombo hicho kitakachokuwa na majukumu ya kutoa ushauri kuhusu masuala ya mtangamano. Kadhalika, katika Mkutano wa 42 Nchi Wanachama ziliridhia Marekebisho ya Itifaki ya Maendeleo ya Utalii ya SADC ya mwaka 1998. Kusainiwa kwa marekebisho hayo kutaiwezesha Tanzania kuimarisha ushirikiano na Nchi Wanachama wa SADC katika kukuza sekta ya utalii kupitia kuvutia uwekezaji katika sekta hiyo, kutangaza vivutio vya utalii, na kubadilishana ujuzi na uzoefu katika usimamizi wa sekta hiyo.

***104. Mheshimiwa Spika,*** aidha, mwezi Machi 2023, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Baraza la Mawaziri la SADC uliofanyika jijini Kinshasa, DRC. Pamoja na mambo mengine, Baraza lilipitisha Kanuni za Fidia na Stahiki kwa Operesheni za

Amani na Mazoezi ya Kijeshi ya SADC. Kupitishwa kwa Kanuni hizo, kutawezesha familia za walinda amani kutoka Nchi Wanachama waliopoteza maisha au kupata ulemavu katika operesheni za ulinzi wa amani au mazoezi ya kijeshi ya SADC kulipwa fidia. Kanuni hizo ni muhimu kwa Tanzania kwa kuwa nchi yetu ni miongoni mwa Nchi Wanachama zinazochangia walinda amani katika misheni za ulinzi wa amani za Jumuiya.

***105. Mheshimiwa Spika,*** Aidha, mkutano huo wa Baraza la Mawaziri wa Machi 2023 uliidhinisha pia Mpango wa Utekelezaji wa Miradi ya Jumuiya wenye miradi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na miradi 11 inayojumuisha Tanzania. Miradi hiyo ipo katika sekta za maji, miundombinu, nishati, masoko, na viwanda, na kusisitiza ukamilishwaji wa ujenzi wa Sanamu ya Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika Kituo cha Amani na Usalama cha Umoja wa Afrika (AU). Vilevile, katika mkutano huu, Nchi Wanachama zilikubaliana kuwa nchi zenye uwezo na malighafi, ikiwa ni pamoja na Tanzania, zizalishe mbolea na kusambaza katika kanda, ili kupunguza utegemezi kwa mbolea kutoka nje.

***106. Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba 2022 na Machi 2023, Wizara iliratibu na kushiriki Mikutano ya Dharura ya Kamati ya Mawaziri wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya SADC. Mikutano hii ilijadili hatua za kuimarisha hali ya ulinzi na usalama Mashariki mwa DRC, na Kaskazini mwa nchi ya Msumbiji na kupendekeza namna bora ya kuboresha utendaji kazi wa Misheni ya Ulinzi wa Amani ya SADC nchini Msumbiji (SAMIM). Aidha, Kamati ilijadili kuhusu utendaji wa kikosi cha *Force Intervention Brigade (*FIB*)* ndani ya Misheni ya Kulinda Amani ya Umoja wa Mataifa (MONUSCO) na kukubaliana hatua za kuchukua kwa maslahi ya Jumuiya, na Nchi Wanachama.

***107. Mheshimiwa Spika,*** kufanikiwa kwa malengo ya SAMIM na MONUSCO kutasaidia kuimarisha usalama katika kanda, na nchi yetu, na kudhibiti ugaidi na uhalifu unaovuka mipaka. Aidha,

uwepo wa amani na usalama ni kichocheo cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii baina ya nchi zinazopakana.

### 3.5.4 Jumuiya ya Nchi zilizo kwenye Mwambao wa Bahari ya Hindi

***108. Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba 2022, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 22 wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Nchi zilizo kwenye Mwambao wa Bahari ya Hindi (IORA) uliofanyika jijini Dhaka, Bangladesh. Lengo la mkutano huo lilikuwa ni kupokea na kujadili taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa masuala mbalimbali ya IORA.

Pamoja na mambo mengine, Mkutano huo uliridhia Tanzania kuwa mwenyeji wa Mdahalo wa Tisa wa IORA unaotarajiwa kufanyika mwezi Mei 2023 huko Zanzibar. Kufanyika kwa Mdahalo huo hapa nchini kutatoa fursa kwa wataalam kubadilishana uzoefu, kutangaza utalii na fursa nyingine za uwekezaji, hususan katika uchumi wa buluu. Aidha, Mdahalo huo utakuwa na tija kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa utaimarisha mahusiano ya kikanda baina ya Tanzania na Nchi Wanachama wa IORA.

***109. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, katika Mkutano wa 22 Tanzania ilifanikiwa kuzishawishi Nchi Wanachama wa IORA kuanzisha utaratibu wa kufanya ukaguzi wa hesabu za Jumuiya hiyo kwa mzunguko (*rotational basis*). Kukubalika kwa pendekezo hilo kutaongeza uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali za IORA ikilinganishwa na utaratibu wa sasa ambapo ukaguzi unafanywa na nchi ya Mauritius pekee yalipo Makao Makuu. Aidha, utaratibu huo utatoa fursa kwa wakaguzi wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuimarisha uwezo wa kufanya kaguzi katika Jumuiya za Kikanda na Kimataifa.

***110. Mheshimiwa Spika,*** aidha, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa mara ya kwanza Tanzania imepata nafasi ya Mkurugenzi wa Huduma za Mashirika ya Jumuiya ya IORA aliyeanza kazi mwezi Oktoba, 2022. Kupatikana kwa nafasi hiyo kumetoa fursa kwa Tanzania kuwa sehemu ya Sekretariati ya IORA,

na hivyo kuhamasisha Watanzania wengine wenye sifa kuomba nafasi za kazi katika Jumuiya ya IORA na Jumuiya nyingine za Kimataifa kwa manufaa yao na taifa kwa ujumla.

**3.5.5 Ushirikiano wa Kimataifa**

***111. Mheshimiwa Spika,*** Katika ushirikiano wa kimataifa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilishiriki katika shughuli mbalimbali za kimataifa. Mwezi Julai 2022, Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika maadhimisho ya kwanza ya Siku ya Lugha ya Kiswahili Duniani yaliyofanyika jijini Paris, Ufaransa. Bunge lako Tukufu litakumbuka kuwa Mkutano wa 41 wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) ulipitisha tarehe 7 Julai ya kila mwaka kuwa Siku ya Kimataifa ya Kiswahili. Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ilikuwa Kiswahili kwa Amani na Ustawi ikiwa na lengo la kuhamasisha matumizi ya lugha hiyo katika kufanikisha juhudi za kutafuta amani duniani na kuchochea shughuli za maendeleo kwa ustawi. Kufanyika kwa maadhimisho hayo kunatoa nafasi kwa nchi yetu kutangaza utamaduni wake, na kueneza matumizi ya Kiswahili duniani na kufungua fursa za kiuchumi na kijamii kwa watanzania.

***112. Mheshimiwa Spika,*** mwezi Septemba 2022, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 77 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa uliofanyika jijini New York, Marekani. Kupitia Mkutano huo, Tanzania ilipata nafasi ya kuieleza Jumuiya ya Kimataifa kuhusu hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita katika kuimarisha demokrasia, haki za binadamu, utawala bora na utawala wa sheria. Vilevile, ilieleza kuhusu utekelezaji wa programu na mipango ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, kuendeleza miundombinu ya kiuchumi na kijamii ambazo zimesaidia kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya taifa.

***113. Mheshimiwa Spika,*** katika Mkutano huo, Tanzania iliainisha jitihada za Serikali katika kupambana na UVIKO-19 na kusisitiza azma yake ya kuwekeza katika uzalishaji wa chanjo za magonjwa ya mlipuko na vifaa tiba, na kuiomba Jumuiya ya Kimataifa kuunga

mkono juhudi hizo. Pia, Tanzania ilieleza jitihada zake katika kutunza mazingira na kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa maendeleo endelevu yatakayohakikisha ustawi wa vizazi vya sasa, na baadaye.

***114. Mheshimiwa Spika,*** Mwezi Oktoba 2022, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano Mkuu wa Shirika la Kimataifa la Umoja wa Mawasiliano (ITU) uliofanyika jijini Bucharest, Romania. Tanzania ilichaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Utendaji la Shirika hilo kwa kipindi cha 2023 hadi 2026. Mafanikio hayo ni muhimu kwa nchi yetu kwa kuwa yataiwezesha Tanzania kuchangia ajenda zake kupitia Shirika hilo. Vilevile, ujumbe wa Tanzania ndani ya ITU utaiwezesha nchi yetu kunufaika na programu na miradi ya Shirika hilo inayolenga kujenga uwezo, na kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya mawasiliano kwa Nchi Wanachama wa ITU.

***115. Mheshimiwa Spika,*** mwezi Machi 2023, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye Mkutano wa 67 wa Kamisheni ya Umoja wa Mataifa ya Hali ya Wanawake Duniani uliofanyika jijini New York, Marekani. Kupitia mkutano huo, Tanzania ilieleza dunia kuhusu hatua zinazochukuliwa na Serikali ili kuongeza uwezeshaji wa wanawake kiuchumi na kjamii hapa nchini. Vilevile, ilitumia nafasi hiyo kutoa rai kwa jumuiya ya kimataifa kuchangia katika juhudi hizo za Serikali kwa kuwekeza katika miradi inayolenga kuongeza ushiriki wa wanawake katika shughuli za kiuchumi.

***116. Mheshimiwa Spika,*** mwezi Machi 2023, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Ngazi ya Juu wa Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote (NAM) uliofanyika Baku, Azerbaijan. Kupitia Mkutano huo, Tanzania iliungana na nchi nyingine wanachama wa NAM kuendelea kuhimiza ushirikiano wa jumuiya ya kimataifa katika kulinda na kudumisha amani na usalama ulimwenguni, na kukabiliana na athari za kiuchumi na kijamii. Pembezoni mwa Mkutano huo, Tanzania na Azerbaijan zilifanya mazungumzo ya uwili kuhusu kuanzisha ushirikiano katika sekta ya nishati hususan mafuta na gesi. Kupitia ushirikiano huo Tanzania itanufaika na ujuzi

na uzoefu wa nchi ya Azerbaijan katika sekta hiyo. Vilevile, utafungua milango kwa ushirikiano wa kibiashara na uwekezaji kati ya nchi hizi mbili.

***117. Mheshimiwa Spika,*** mwezi Machi 2023, Wizara iliratibu na kushiriki katika Kikao cha 52 cha Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu uliofanyika Ofisi za Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa jijini Geneva, Uswisi. Katika kikao hicho, Tanzania iliieleza jumuiya ya kimataifa kuhusu mafanikio yake katika kuboresha demokrasia, kusimamia haki za binadamu, utawala bora na utawala wa sheria nchini, chini ya Serikali ya Awamu ya Sita.

**3.6 Uratibu wa Watanzania Wanaoishi Nje ya Nchi (*Diaspora*)**

***118. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutengeneza mazingira wezeshi ili kuhamasisha na kuwezesha ushiriki wa Watanzania wanaoishi nje ya nchi (*Diaspora*) kuchangia maendeleo ya Tanzania.

***119. Mheshimiwa Spika,*** napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, mwamko wa *Diaspora* kutuma fedha (*remittances*), na kuwekeza katika sekta za kiuchumi na kijamii hapa nchini umeendelea kuongezeka. Katika kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba 2022 *Diaspora* waliwekeza takriban shilingi bilioni 4.4 katika ununuzi wa nyumba na viwanja kupitia Shirika la Nyumba la Taifa, Kampuni ya *Orange Tanzania Ltd* (*Hamidu City Park*), na Kampuni ya *KC Land Development Plan Consultant Ltd*. Uwekezaji huo ni sawa na ongezeko la shilingi bilioni 2.2 zilizowekezwa katika kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba 2021. Vilevile, katika kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba 2022 *Diaspora* waliwekeza katika hisa za Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja (*UTT - AMIS*) zenye thamani ya takribani shilingi bilioni 2.5.

***120. Mheshimiwa Spika,*** pia, *Diaspora* wameendelea kutuma fedha nchini (*remittances*), ambapo katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2022 walituma takribani Dola za Marekani bilioni 1.1 kupitia vyanzo rasmi (yaani miamala ya kampuni za simu, benki na taasisi nyingine za fedha). Fedha hizo ni

takribani mara mbili ya kiasi kilichotumwa na *Diaspora* katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2021, ambapo Dola za Marekani milioni 569.3 zilitumwa.

***121. Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara imekamilisha maandalizi ya Mfumo wa Kidigitali wa Kukusanya na Kutunza Taarifa za *Diaspora* (*Diaspora Digital Hub*). Mfumo huo ulizinduliwa tarehe 22 Mei 2023, na utaiwezesha Serikali kupata takwimu sahihi za idadi ya *Diaspora*, mahali walipo, ujuzi na uzoefu walionao, Mfumo utawawezesha pia *Diaspora* kupata taarifa kuhusu fursa na huduma mbalimbali zinazotolewa na sekta za umma na binafsi nchini. Napenda kuzishukuru Benki ya CRDB, Benki ya NMB na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwa kushirikiana na Wizara katika maandalizi ya Mfumo huu muhimu. Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha Taasisi za umma na binafsi kuanzisha madawati ya *Diaspora*, ili kuongeza wigo wa huduma kwa *Diaspora*. Hadi sasa Taasisi za Serikali zilizoanzisha madawati ya huduma kwa *Diaspora* ni pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa; Idara ya Uhamiaji Tanzania; Kituo cha Uwekezaji Tanzania; na Shirika la Nyumba la Taifa. Madawati hayo yameanzishwa pia katika kampuni za simu za Vodacom, Tigo, Airtel na TTCL pamoja na benki za CRDB, NMB, PBZ, TCB, NBC, Stanbic, EXIM, Equity, Azania na BOA.

***122. Mheshimiwa Spika,*** napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kutambua umuhimu wa *Diaspora*, Wizara ipo katika hatua za mwisho za maandalizi ya kuwapatia Hadhi Maalum *Diaspora* wenye asili ya Tanzania na Uraia wa nchi nyingine (*Tanzania Non-Citizen Diaspora*). Wizara ilikusanya maoni toka kwa wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi, ikiwa ni pamoja na kutoka kwa *Diaspora*. Maoni yameainisha maeneo/masuala yanayopendekezwa kujumuishwa katika Hadhi Maalum.

***123. Mheshimiwa Spika,*** aidha, mwezi Machi 2023, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania ilitoa maelekezo kwa benki na taasisi za fedha nchini kuruhusu raia wa kigeni wakiwemo *Diaspora*

wenye asili ya Tanzania na uraia wa nchi nyingine kufungua akaunti za fedha za kigeni kwa kutumia vitambulisho mbadala vya utambuzi tofauti na hati ya kusafiria ya Tanzania na kitambulisho cha NIDA. Nyaraka hizo mbadala za utambuzi ni pamoja na hati ya kusafiria za nchi ya kigeni; leseni za udereva za nchi ya kigeni; kitambulisho cha kupigia kura cha nchi ya kigeni; na kitambulisho cha kazi cha nchi ya kigeni au kitambulisho cha mwanafunzi cha nchi ya kigeni. Hatua hiyo itawawezesha *diaspora* kuweka fedha zao za kigeni katika benki za hapa nchini.

***124. Mheshimiwa Spika,*** Diaspora wameendela kuitangaza vyema nchi yetu na kuwekeza katika sekta za kiuchumi. Napenda kutumia fursa hii, kuwapongeza na kuwashukuru kwa dhati *Diaspora* wote kwa kuendelea kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya Taifa letu.

**3.7 Kuratibu Masuala ya Itifaki, Uwakilishi na Huduma za Kikonseli**

***125. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu masuala ya haki na kinga kwa Jumuiya ya Wanadiplomasia hapa nchini kama ilivyoainishwa katika sheria za kimataifa hususan, Mkataba wa Vienna kuhusu Uhusiano wa Kidiplomasia wa mwaka 1961 na Waraka Na. 2 wa Rais wa mwaka 1964 kuhusu Mawasiliano baina ya Taasisi za Serikali na Jumuiya ya Wanadiplomasia.

***126. Mheshimiwa Spika,*** Katika kuimarisha uhusiano na Jumuiya ya Wanadiplomasia hapa nchini, Wizara imeendelea kuimarisha utaratibu wa mashauriano kuhusu utekelezaji wa sera, mikakati na mipango ya maendeleo. Katika kipindi hiki, Wizara iliratibu uwasilishaji wa Hati za Utambulisho kwa mabalozi wa nchi za Australia, Belgium, Brazil, Canada, Chile, China, Colombia, Cuba, Finland, Ghana, Hungary, Holy See (Vatican), India, Indonesia, Iran, Israel, Jamhuri ya Czech, Jamhuri ya Korea, Malawi, Marekani, Mexico, Misri, Romania, Saudi Arabia, Slovak, Spain, Sweden, Ureno, Ukraine na Zambia.

***127. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa huduma za kiitifaki na kikonseli ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa viza kwa

maafisa na watendaji wa Serikali, viongozi wa vyama vya siasa na waheshimiwa wabunge. Aidha, Wizara imeendelea kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali zinazowakabili watanzania nje ya nchi kwa kushirikiana na wadau wengine, na kulinda maslahi ya watanzania wanaofanya kazi kwenye Balozi na Mashirika ya Kimataifa hapa nchini.

***128. Mheshimiwa Spika,*** kipekee napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa kuitisha mkutano wa mabalozi wanaoiwakilisha nchi yetu katika mataifa mbalimbali duniani uliofanyika mwezi Novemba 2022 Zanzibar. Mkutano huo ulitoa fursa kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuwasikiliza Mabalozi wetu na kutoa maelekezo, na miongozo kwa Mabalozi hao kuhusu mwelekeo katika utekelezaji wa diplomasia ya uchumi kwa manufaa ya taifa.

**3.8 Mikataba ya Kimataifa na Hati za Makubaliano**

***129. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Wizara iliratibu na kufanikisha kusainiwa kwa Mikataba 13 na Hati za Makubaliano 37. Mikataba na Hati hizo zinagusa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii ikiwemo ulinzi na usalama; kilimo na uvuvi; viwanda, biashara, uwekezaji; TEHAMA; utalii; afya; elimu; mawasiliano; utamaduni; sanaa na michezo; mazingira; uchumi wa buluu; uchukuzi; na sayansi na teknolojia.

***130. Mheshimiwa Spika,*** kupitia Mikataba na Makubaliano hayo, nchi yetu itanufaika na fursa mbalimbali kama vile fursa za masoko ya bidhaa za kilimo, mifugo na uvuvi zinazozalishwa hapa nchini; kuongeza idadi ya watalii kutoka nje; kuvutia mitaji na teknolojia; na kuwezesha watanzania kunufaika na fursa za ajira na ufadhili wa masomo ughaibuni. Orodha ya Mikataba na Hati za Makubaliano hayo ni kama inavyoonekana katika ***Kiambatisho Na. I***.

### 3.9 Elimu kwa Umma

***131. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje, diplomasia ya uchumi na fursa zitokanazo na ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya za Kikanda na Kimataifa ambazo Tanzania ni Mwanachama. Utoaji wa elimu kwa umma hufanyika kupitia vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo televisheni, redio, magazeti, na njia nyingine za mawasiliano kama vile majarida, machapisho, maonesho, semina, tovuti na mitandao ya kijamii ya Wizara ambayo inajumuisha *Twitter, Instagram, YouTube, Facebook* na blogu. Balozi zetu nje ya nchi pia zimeendelea kutoa elimu kuhusu fursa za biashara, uwekezaji na utalii kupitia ushiriki wa mabalozi katika vipindi vya televisheni na redio ndani na nje ya nchi.

***132. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa elimu kwa makundi mbalimbali katika jamii kupitia mafunzo yenye lengo la kuwajengea uwezo. Mwezi Julai 2022, Wizara kwa kushirikiana na Sekretarieti ya SADC iliendesha mafunzo kwa waandishi wa habari 50 kuhusu fursa zinazopatikana SADC. Wizara pia ilishirikiana na mabalozi wastaafu kuendesha mafunzo kwa wanahabari 20 kuhusu uandishi wa taarifa za kidiplomasia.

***133. Mheshimiwa Spika,*** halikadhalika, Wizara imeendelea kutoa taarifa kwa vyombo vya habari na kufanya mafunzo na mikutano na waandishi wa habari pamoja na wahariri kuhusu utekelezaji wa majukumu yake na kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali ya kimataifa. Kupitia taarifa hizo wananchi walihabarishwa kuhusu fursa za masomo nje ya nchi na ajira katika jumuiya za kikanda na mashirika ya kimataifa. Wizara pia ilishiriki katika maonesho ya kibiashara ya kimataifa yanayofanyika ndani na nje ya nchi na kutoa elimu kwa umma ikiwemo Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba) yaliyofanyika jijini Dar es Salaam mwezi Julai 2022, na Maonesho ya Wajasiriamali Wadogo na wa Kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (Juakali/Nguvukazi) yaliyofanyika jijini Kampala, Uganda mwezi Novemba 2022.

***134. Mheshimiwa Spika,*** ili kutoa elimu kwa umma kimkakati na kuwawezesha Watanzania wengi zaidi kuzifahamu na kuzitumia fursa zitokanazo na ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa, Wizara inakamilisha Mkakati wa kutoa Elimu kwa Umma (*Communication Strategy*).

**3.10 Utawala na Maendeleo ya Rasilimaliwatu**

***135. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia masuala ya utawala na maendeleo ya rasilimaliwatu kwa lengo la kuimarisha utendaji wa kazi. Wizara ina jumla ya watumishi 546 wa kada mbalimbali. Kati yao, watumishi 208 wapo kwenye Balozi za Tanzania na watumishi 338 wapo Makao Makuu ya Wizara.

***136. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya uteuzi wa mabalozi 11 kwa ajili ya kuiwakilisha Tanzania katika nchi za Austria, Cuba, Ethiopia, Malawi, Indonesia, Uholanzi, Umoja wa Falme za Kiarabu, Umoja wa Mataifa-Marekani, Uturuki, Zambia, na Zimbabwe.

***137. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake kupitia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa lengo la kuboresha utendaji na kuongeza tija. Katika kipindi hiki, watumishi 20 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 15 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi.

***138. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, katika kipindi hicho Wizara imeajiri jumla ya watumishi 14 ambapo watumishi tisa (9) ni Maafisa Mambo ya Nje Daraja la II, watatu (3) ni Madereva Daraja la II na wawili (2) ni Wasaidizi wa Kumbukumbu. Pia, Wizara imepata kibali cha kuajiri watumishi wapya 17 wa kada ya Maafisa Mambo ya Nje Daraja la II. Taratibu za kuajiri watumishi hao zinaendelea.

***139. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho, afisa mmoja alipandishwa cheo kuwa Mkurugenzi Msaidizi na watumishi sita (6) walipandishwa vyeo. Kati ya watumishi hao, wawili ni kada ya Afisa

Mambo ya Nje na wanne ni kada ya Uhasibu. Aidha, watumishi wawili (2) walibadilishwa kada na watumishi 17 walithibitishwa vyeo.

***140. Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali za umma unaozingatia thamani ya fedha na utendaji kazi wenye tija katika balozi zetu, Wizara imefanya ukaguzi katika maeneo ya usimamizi wa fedha; ununuzi; utawala na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye balozi saba (7) za Tanzania. Balozi hizo ni Addis Ababa (Ethiopia), New Delhi (India), Tokyo (Japan), Kuwait City (Kuwait), Abu Dhabi (UAE), Khartoum (Sudan) na Cairo (Misri). Aidha, ukaguzi umefanyika katika Makao Makuu ya Wizara na kubaini kuwa matumizi ya rasilimali yanazingatia sheria, kanuni na taratibu za fedha za umma.

## 3.11 Kuratibu na Kusimamia Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara na Taasisi Zilizo Chini ya Wizara

### 3.11.1 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara

***141. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ilitengewa kiasi cha shilingi 4,700,000,000 kwa ajili ya bajeti ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 700,000,000 ni kwa ajili ya ukarabati wa majengo manne (4) katika Ubalozi wa Tanzania Pretoria, Afrika Kusini na shilingi 4,000,000,000 ni kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu eneo la Lakilaki, jijini Arusha.

***142. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na hatua za ukarabati wa majengo manne (4) katika Ubalozi wa Tanzania Pretoria ambayo ni jengo la Ofisi za Ubalozi; jengo la makazi ya Balozi; jengo la makazi ya Mkuu wa Utawala na Fedha; na jengo la makazi ya Mwambata Utawala, kwa gharama ya Dola za Marekani 523,561.43 sawa na shilingi 1,293,950,000.00 pamoja na kodi. Kiasi kilichosalia cha shilingi 593,950,000 kimetengwa katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024.

***143. Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ujenzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu utahusisha ujenzi wa jengo kuu la utawala/ofisi (ukumbi wa mikutano na vyumba vya mihadhara); zahanati; karakana na kituo cha mafuta; na kituo cha kulelea watoto. Aidha, Mkandarasi amepatikana kwa gharama ya shilingi 62,968,086,187.78 pamoja na kodi. Fedha zitaendelea kutengwa katika bajeti ya Wizara kila mwaka kulingana na mtiririko wa fedha (*cash flow*).

***144. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 imeanza kutekeleza mradi wa kuendeleza viwanja vya Serikali jijini Lusaka, Zambia kwa kiasi cha Kwacha 500,000,000 (takriban shilingi bilioni 66.1) kwa kutumia utaratibu maalumu katika ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Zambia. Mradi huu unahusisha ujenzi wa majengo 10 kama inavyoonekana kwenye ***Kiambatisho Na. II*** cha Hotuba hii. Hadi Aprili 2023 Wizara imekamilisha tathmini ya zabuni za kampuni za ushauri elekezi zilizowasilisha maombi ya kuonesha nia (*expression of interest*) ya kusanifu majengo hayo. Zabuni ya kazi ya usanifu wa majengo hayo imetangazwa mwezi Mei 2023, na tuzo ya zabuni kwa kampuni zilizoshinda inatarajiwa kutolewa mwezi Juni 2023.

***145. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekamilisha uchambuzi yakinifu wa Jengo la Ubalozi na Kitega uchumi katika Ubalozi wetu Nairobi. Aidha, Wizara imekubaliana na NSSF katika kuendeleza jengo hilo. Uendelezaji wa jengo hilo ni miongoni mwa miradi ya kipaumbele ya Wizara.

***146. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na usanifu wa mradi wa ujenzi wa majengo katika viwanja vitatu (3) vya Serikali katika ubalozi wa Tanzania Kampala Uganda. Mradi huu utatumia fedha zilizotunzwa kwenye Akaunti ya Amana ya Ubalozi kiasi cha Dola za Marekani 750,000 sawa na shilingi 1,785,000,000. Majengo hayo ni jengo Jipya la Ofisi ya Ubalozi; jengo la Kitega Uchumi kwa ajili ya matumizi ya ofisi; na jengo la kitega uchumi kwa ajili ya makazi.

***147. Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza dhamira ya Serikali ya kujenga majengo ya ofisi za Balozi, vitega uchumi na ukarabati katika Balozi zetu na kuimarisha taswira ya Taifa letu, Wizara imefanya tathmini ya kina na kuainisha miradi ya kipaumbele, mpango wa muda mfupi na wa kati, changamoto zilizopo na jinsi ya kukabiliana nazo, hususan ili kuwezesha ubia na ushiriki wa sekta binafsi katika Uendelezaji wa miradi hii. Miradi ya kipaumbele ni kama inavyoonekana katika ***Kiambatisho Na. III*** cha Hotuba hii, na mpango wa muda wa kati na mfupi ni kama inavyoonekana katika ***Kiambatisho Na. IV,*** changamoto zilizobainishwa na jinsi ya kuzitatua ni kama inavyooneshwa katika ***Kiambatisho Na. V.***

**3.11.2 Taasisi Zilizo Chini ya Wizara**

***148. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia Taasisi zilizo chini yake kwa lengo la kuhakikisha zinafikia malengo ya uanzishwaji wake. Kwa namna ya kipekee, ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumteua Bw. Ephraim Balozi Mafuru, kuwa Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Mikutano ya Kimataifa Arusha (AICC). Aidha, Bw. Lamau A. Mpodo ameteuliwa kuwa Mtendaji Mkuu wa Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora (APRM). Ninawapongeza Watendaji hawa na ni matarajio ya wizara kuwa wataendeleza mipango iliyopo na kubuni mipya kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija kwa taasisi hizo.

***149. Mheshimiwa Spika,*** naomba nitoe maelezo mafupi ya utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo katika kipindi hiki:

**Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha**

***150. Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC) ni kuendesha biashara ya mikutano na upangishaji wa nyumba na ofisi. Aidha, Kituo kinaendesha huduma ya afya kupitia hospitali, na kinajiendesha kwa faida bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini.

***151. Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia sheria iliyoanzisha Kituo, AICC inatekeleza majukumu yake kwa kuongozwa na Mpango

Mkakati wa miaka mitano (2022/23 - 2026/27). Mpango huo unaainisha dira na dhima ya Kituo, hususan katika kuitangaza nchi yetu katika nyanja ya utalii wa mikutano na matukio (*business tourism*) ambayo inajulikana kama "MICE" (*Meetings, Incentive travel, Conferences, Exhibition/Events*).

***152. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/2023 Kituo kilipanga kukusanya mapato ya Shilingi 16,737,049,856. Hadi mwezi Aprili, 2023 Kituo kilikusanya mapato ya Shilingi 12,782,629,220 sawa na asilimia 76 ya malengo. Mapato hayo yalitokana na huduma za kumbi za mikutano (*AICC na JNICC*) shilingi 6,582,450,243; upangishaji wa ofisi na nyumba za kuishi shilingi 3,255,585,561; na huduma za hospitali shilingi 3,170,304,225.

***153. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 kituo kilihudumia mikutano 399 ya kitaifa, na 21 ya kimataifa, ambayo ilileta washiriki 109,582 wa kitaifa, na 7,849 wa kimataifa; kimehudumia wagonjwa wa nje wapatao 71,220 na wagonjwa waliolazwa 1,300; kimeandaa mifumo ya kielektroniki kama, *Human Capital Management Information System* (HCMIS), *e-Office* pamoja na kununua vifaa vya kisasa kwa ajili ya shughuli za mikutano; kilifanya ukarabati wa nyumba 145 za makazi katika miliki za kituo zilizoko Arusha; ukarabati wa ofisi, kumbi na hospitali; pamoja na kukamilisha mpango wa mafunzo na zoezi la kuhuisha muundo wa utumishi.

***154. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, kituo kilikamilisha andiko la Biashara la mradi wa *Mount Kilimanjaro International Convention Centre* (MK-ICC) na kuliwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango. Kituo kimepata kibali cha kuendelea na mradi huo kwa njia ya Ubia na Sekta Binafsi. Ujenzi wa Kituo hicho kutaimarisha na kuongeza kasi ya utekelezaji wa diplomasia ya mikutano na maonesho hapa nchini, pamoja na kuongeza mapato ya fedha za kigeni.

**Chuo cha Diplomasia**

***155. Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Chuo cha Diplomasia ni kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa huduma ya ushauri elekezi katika masuala ya diplomasia, uhusiano wa kimataifa, stratejia, lugha za kigeni, ulinzi na usalama, usuluhishi wa migogoro na ujenzi wa amani. Kwa kutekeleza majukumu hayo, Chuo kimeendelea kukidhi mahitaji ya Taasisi za Serikali, Mashirika ya Umma, Sekta Binafsi na Balozi za nje hapa nchini.

***156. Mheshimiwa Spika,*** mafunzo hayo yanatolewa katika ngazi za astashahada, stashahada, shahada, stashahada ya uzamili na shahada ya uzamili. Katika mwaka wa masomo 2022/2023 Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 1,473 Miongoni mwa hao, 167 wanafanya mafunzo katika ngazi ya cheti, 232 wanafanya mafunzo katika ngazi ya stashahada, 927 wanafanya mafunzo katika ngazi ya shahada, 99 wanafanya mafunzo katika ngazi ya stashahada ya uzamili, na 48 wanafanya mafunzo katika ngazi ya shahada ya uzamili. Kwa upande wa lugha, Chuo kinafundisha jumla ya lugha saba (7) za kigeni ambazo ni Kiarabu, Kifaransa, Kihispania, Kiingereza, Kichina, Kikorea na Kireno. Kadhalika, Chuo kinaendesha kozi za muda mfupi katika masuala ya diplomasia, uhusiano wa kimataifa, stratejia, ulinzi na usalama, usuluhishi wa migogoro na ujenzi wa amani ambapo kuanzia mwezi Julai, 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya kozi fupi 13 zilitolewa kwa washiriki 301.

***157. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki Chuo kiliendesha makongamano matatu (3) ambayo ni kongamano la kidiplomasia kuhusu kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere na mahusiano ya kimataifa, kongamano kuhusu umuhimu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 katika utekelezaji wa diplomasia ya uchumi, na kongamano la maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania Bara na Maendeleo ya Mahusiano ya Kimataifa na Diplomasia. Kupitia makongamano hayo, wanafunzi, watumishi wa chuo, na wananchi walijengewa uelewa kuhusu umuhimu wa dhana ya diplomasia ya uchumi katika maendeleo ya taifa, na mchango wa Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere katika kukuza uhusiano wa Tanzania na Jumuiya ya kimataifa.

***158. Mheshimiwa Spika,*** Chuo kimekuwa na utaratibu wa kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwagharamia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu katika fani mbalimbali kulingana na uhitaji na umuhimu. Katika kipindi cha mwezi Julai 2022 hadi Aprili, 2023, watumishi wawili (2) walihitimu mafunzo ya ngazi ya shahada ya uzamivu. Kadhalika, watumishi Saba (7) wanaendelea na masomo ya shahada ya uzamivu na kumi (10) wanasoma shahada ya uzamili.

***159. Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, chuo kimeendelea na maandalizi ya ujenzi wa vyumba tisa (9) vya mihadhara Kurasini, jijini Dar es Salaam. Ujenzi huo utagharimu shilingi 4,450,359,568.80, kiasi cha shilingi 550,359,568.80 kimetengwa katika bajeti ya 2022/2023 na shilingi 3,900,000,000 zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2023/2024.

***160. Mheshimiwa Spika,*** kwa Mwaka wa fedha wa 2022/2023, Chuo kilipanga kukusanya na kutumia jumla ya Shilingi 7,528,498,095.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 2,927,288,095.00 ni ruzuku ya mishahara kutoka Serikali Kuu, Shilingi 3,601,210,000.00 ni makusanyo ya vyanzo vya ndani na Shilingi 1,000,000,000.00 ni ruzuku ya Matumizi Mengineyo kutoka Serikali Kuu.

***161. Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili 2023, Chuo kilikusanya kiasi cha shilingi 1,987,315,770.00 sawa na asilimia 55.18 ya kiasi kilichopangwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani. Aidha, Chuo kilipokea Shilingi 1,601,688,414.92 sawa na asilimia 40.78 ya kiasi kilichopangwa kama ruzuku toka Serikalini kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo.

***162. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa matumizi, hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 Chuo kilitumia jumla ya Shilingi 3,017,337,483.00, kati ya fedha hizo Shilingi 1,494,507,705.00 ni kutoka katika vyanzo vyake vya ndani, Shilingi 1,164,188,415.00 ni ruzuku ya mishahara na

Shilingi 358,641,363.00 ni ruzuku ya matumizi mengineyo kutoka Serikali Kuu. Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora

***163. Mheshimiwa Spika,*** Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora (APRM) ni Wakala Maalum wa Umoja wa Afrika ulioanzishwa mwaka 2003 kwa lengo la kufanya tathmini za mara kwa mara za utawala bora zenye nia ya kuimarisha maeneo ambayo nchi inafanya vizuri, kuibua changamoto za utawala bora, na kutoa mapendekezo ya ufumbuzi wa changamoto.

***164. Mheshimiwa Spika,*** bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya shughuli za APRM Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ni Shilingi 500,000,000. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, APRM Tanzania ilipokea jumla ya Shilingi 291,019,633.66 sawa na asilimia 58.20. Hadi kufikia mwezi Aprili 2023, APRM Tanzania ilitumia kiasi cha Shilingi 249,053,591.44 sawa na asilimia 85.58 ya kiasi kilichopokelewa.

***165. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki APRM Tanzania imekamilisha taratibu za kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Mpango Kazi wa APRM (2014 - 2029) kwenye Kikao cha Wakuu wa Nchi na Serikali za Umoja wa Afrika wanaoshiriki katika Mpango wa APRM kitakachofanyika mwanzoni mwa mwaka 2024. Ripoti imeangazia maeneo manne ya tathmini ambayo ni: Siasa na Demokrasia; Usimamizi wa Uchumi; Utendaji wa Mashirika ya Biashara; na Maendeleo ya Jamii. Ripoti hiyo ina maelezo yaliyofanyiwa utafiti kwa kipindi cha mwaka 2014 hadi 2019. Maandalizi ya Ripoti pia yamezingatia miongozo na kanuni za APRM.

***166. Mheshimiwa Spika,*** muhtasari wa maudhui ya kila eneo la tathmini ni kama ifuatavyo: Katika eneo la Siasa na Demokrasia, Ripoti inaonesha kuwa hatua zimepigwa katika kutatua changamoto kwenye maeneo yote ya tathmini ikiwa ni pamoja

na, suala la utatuzi wa migogoro; kufanyiwa kazi kwa maeneo sita ya Muungano, mageuzi makubwa katika utumishi wa umma sanjari na uimarishaji wa taasisi zilizopewa jukumu la kuzuia na kupambana na rushwa yanaifanya Tanzania kuwa nchi ya mfano. Pia, haki za makundi ya wanawake, watoto, vijana na wakimbizi zimeendelea kulindwa kwa kuwekewa sera rafiki zinazosimamia maslahi mapana ya makundi hayo.

***167. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu Usimamizi wa Uchumi; nchi yetu imeendelea kutekeleza sera za uchumi mpana zinazolenga kupata maendeleo endelevu. Pia, katika eneo la Usimamizi wa Mashirika ya Biashara Serikali imejielekeza katika kuimarisha mifumo ya udhibiti wa mashirika ya biashara utakaowezesha kupatikana kwa maendeleo endelevu. Vilevile, kwa upande wa maendeleo ya jamii Serikali imeendelea kuchukua hatua za kuimarisha ukusanyaji wa kodi kwa lengo la kuwa na uwezo wa kujitegemea na kuimarisha utoaji wa huduma mbalimbali za jamii.

***168. Mheshimiwa Spika,*** kutokana na mabadiliko makubwa yanayoendelea kutokea katika nyanja za siasa, uchumi na maendeleo ya jamii, na pia ikizingatiwa kuwa ni muda mrefu umepita tangu Tanzania ilipowasilisha ripoti ya kwanza chini ya Mpango wa APRM, Serikali imepanga kufanya awamu ya pili ya tathmini ya utawala bora ambayo itaainisha mafanikio yaliyopatikana, changamoto mpya, na kuziwekea mikakati ya kukabiliana nazo.

***169. Mheshimiwa Spika,*** mwezi Februari 2023, APRM Tanzania ilishiriki kikao cha Wakuu wa Nchi Wanachama wa Mpango wa APRM kilichofanyika kwa njia ya mtandao. Katika mkutano huo, Muungano wa Visiwa vya Comoro ilijiunga na Mpango wa APRM na kuwa mwanachama wa 42. Aidha, Jamhuri ya Niger iliwasilisha Ripoti ya Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango ya Nchi; Jamhuri ya Djibouti iliwasilisha Ripoti ya Tathmini ya Maeneo Mahsusi; na Jamhuri ya Kenya iliwasilisha Dondoo za Ripoti ya Uzinduzi ya Utawala Bora Kitaifa.

## 4.0 CHANGAMOTO NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA

***170. Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kuwepo mafanikio ya kiutendaji katika kutekeleza bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:

i. Upungufu wa watumishi katika Idara na Vitengo ukilinganisha na mahitaji na majukumu ya Wizara. Ili kuweza kutekeleza majukumu yake kikamilifu Wizara inahitaji kuwa na watumishi 783 kulingana na Mpango wa Rasilimali Watu wa Wizara kwa makadirio ya miaka mitano (2022 hadi 2027). Kwa sasa Wizara ina jumla ya watumishi 546 na katika mwaka 2023/24 itahitaji kuwa na watumishi 669 na hivyo kuwa na upungufu wa watumishi 123.
Serikali imeendelea kuziba pengo hili, na kwa mwaka 2023/2024 Wizara imepata kibali cha kuajiri na kuhamisha watumishi 74;

ii. Ufinyu wa bajeti, utaalamu usiotosheleza katika baadhi ya maeneo, hususan diplomasia ya uchumi, usimamizi wa ujenzi balozini;

iii. Baadhi ya sheria kutowezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika kuendeleza/kujenga majengo ya balozi na vitega uchumi katika balozi za Tanzania; na

iv. Uelewa hafifu miongoni mwa wadau kuhusu diplomasia ya uchumi, na fursa zitokanazo na mtangamano, na mikataba na makubaliano ambayo Tanzania imesaini na nchi nyingine.

***171. Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imechukua hatua zifuatazo:

i. Wizara imeendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kwa mwaka 2023/2024 Wizara imepata kibali cha kuajiri na kuhamishia watumishi 74. Aidha, Wizara itaendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,

kwa ajili ya kupatiwa vibali vya ajira mpya na mbadala za kujaza nafasi zilizo wazi.

ii. Wizara imekamilisha Mpango Mkakati wa Uendelezaji na Ujenzi wa Balozi na Vitega Uchumi ambao utatekelezwa kupitia bajeti ya serikali, mikopo na ubia kutoka taasisi za fedha. Mpango huo, umeainisha pia sheria zinazohitaji maboresho na utaratibu utakaotumika;

    Kufuatia majadiliano baina ya Wizara na Wizara ya Fedha na Mipango, ukomo wa bajeti ya maendeleo kwa mwaka 2023/2024 umeongezwa kutoka shilingi 4,700,000,000 kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 hadi shilingi 17,887,608,000. Kiasi hiki kitawezesha Wizara kutekeleza miradi ya Maendeleo inayoendelea, na kuandaa uchambuzi yakinifu wa miradi 14 ya kipaumbele ambayo Sekta Binafsi imeonesha nia ya kuendeleza kwa kushirikiana na Serikali, na hivyo kuziwezesha Sekta Binafsi kuendeleza miradi hii kwa ubia na Serikali ***(Kiambatisho III).***

iii. Kuendelea kushirikiana na Wizara za kisekta, sekta binafsi na vyombo vya habari katika kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa mbalimbali zitokanazo na Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika; Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika; na fursa zitokanazo na mikataba na makubaliano mbalimbali ambayo Tanzania imesaini na nchi nyingine; na

iv. Kukamilisha Mpango wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi ambao utaainisha maeneo mahsusi na fursa kwa kila sekta, wadau na majukumu yao katika mnyororo wa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi, na mpango wa elimu kwa Umma.

**5.0 SHUKRANI**

***172. Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa kimataifa, diplomasia, na kupata ushirikiano mkubwa kutoka kwa wadau na washirika wa maendeleo, Jumuiya za Kikanda na kimataifa katika kufanikisha utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

***173. Mheshimiwa Spika,*** kwa muktadha huu, naomba kutumia fursa hii kuzishukuru nchi zifuatazo Afrika Kusini, Algeria, Angola, Australia, Austria, Brazil, Botswana, Burundi, Canada, China, Comoros, Cuba, Denmark, Ethiopia, Eswatini, Finland, Hispania, Hungary, Indonesia, India, Israel, Italia, Iran, Ireland, Jamhuri ya Czech, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Korea, Japan, Kenya, Kuwait, Lesotho, Madagascar, Malawi, Malaysia, Marekani, Mauritius, Mexico, Misri, Morocco, Msumbiji, Namibia, New Zealand, Nigeria, Norway, Oman, Pakistan, Poland, Qatar, Romania, Rwanda, Singapore, Sri Lanka, Thailand, Tunisia, Ubelgiji, Saudi Arabia, Shelisheli, Slovenia, Sudan, Sudani Kusini, Sweden, Ufaransa, Ufilipino, Uganda, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Ukraine, Umoja wa Falme za Kiarabu, Ureno , Urusi, Uswisi, Uturuki, Vietnam, Zambia na Zimbabwe.

***174. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, naomba kutoa shukrani kwa *African Capacity Building Foundation (ACBF)*; Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); Benki ya Dunia (WB); *Investment Climate Facility for Africa*; Benki ya Exim ya China; Benki ya Exim ya India; Benki ya Exim ya Korea; Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD); Mfuko wa Ushirikiano wa Maendeleo ya Uchumi wa Korea (ECDF); Mfuko wa Maendeleo wa China na Afrika (CAD Fund); Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DfID); Mfuko wa Maendeleo wa Abu Dhabi (ADFD); Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF); Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait (Kuwait Fund); Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani (IAEA); Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden (SIDA); Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD); Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD); Shirika la Kimataifa la Kuzuia Matumizi ya Silaha za Kemikali (OPCW); Ofisi ya Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN RCO); Mfuko wa Kukuza Mtaji wa Umoja wa Mataifa (UNCDF); Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa

(UNDP); Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA); na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na UKIMWI (UNAIDS).

***175. Mheshimiwa Spika,*** pia, natoa shukrani kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula (FAO); Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO); Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wakimbizi (UNHCR); Shirika la Kazi Duniani (ILO); Shirika la Umoja wa Mataifa la Uhamaji (IOM); Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF); Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Israel (MASHAV); Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA); Shirika la Misaada la Marekani (USAID); Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Korea (KOICA); Shirika la Kimataifa la Ushirikiano wa Maendeleo la China (CIDCA); Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (UNIDO); na Taasisi ya Kimataifa ya Afya ya Korea (KOFIH).

***176. Mheshimiwa Spika,*** mashirika mengine ni Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Wanawake (UNWOMEN); Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP); Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (UNCTAD); Shirika la Umoja wa Mataifa Kuhusu Madawa ya Kulevya na Uhalifu (UNODC); Umoja wa Ulaya (EU); Shirika la Afya Duniani (WHO); na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP).
Vilevile, napenda kuwashukuru Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi ya Afrika (BADEA); Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB); Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (GiZ); *Global Fund; International Committee of the Red Cross; International Federation of the Red Cross and Red Crescent Societies*; Khalifa *Fund for Enterprise Development* (*Khalifa Fund); Medecins Sans Frontieres (MSF)*; Mfuko wa Dunia wa Wanyama Pori (WWF); *Aga Khan Foundation (AKDN) The Association of European Parliamentarians with Africa*; *The Bill and Melinda Gates Foundation*; *TradeMark Africa*; Umoja wa Posta Duniani (UPU); *International Telecomunication Union (ITU)* Umoja wa Posta Afrika (PAPU) pamoja na mifuko na mashirika mengine ya misaada.

***177. Mheshimiwa Spika,*** ni dhahiri kuwa, ushirikiano wao umekuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha malengo ya Wizara, na Serikali kwa ujumla.

***178. Mheshimiwa Spika,*** kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru watendaji na watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa utendaji wao mahiri unaoniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi, na kulinda na kutetea maslahi ya Taifa letu ndani na nje ya nchi. Kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Mhe. Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk (Mb), Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Balozi Dkt. Samwel William Shelukindo, Katibu Mkuu; Balozi Joseph Edward Sokoine, aliyekuwa Katibu Mkuu; Balozi Fatma Mohammed Rajab, Naibu Katibu Mkuu; Bw. Ephraim Balozi Mafuru, Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Mikutano ya Kimataifa Arusha (AICC), Bw. Lamau A. Mpodo, Mtendaji Mkuu wa Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora (APRM), na Bw. Felix Wandwe, Kaimu Mkurugenzi wa Chuo cha Diplomasia; Wakuu wa Idara, Waheshimiwa Mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania nje ya nchi; Wakuu wa Vitengo; na watumishi wote kwa kufanya kazi kwa umahiri, weledi, ufanisi, moyo wa uzalendo na kujitoa kulinda na kutetea maslahi ya Taifa letu.

## 6.0 MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

***179. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara imejiwekea malengo na vipaumbele vifuatavyo:

a) Kuratibu ziara za kikazi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa nje ya nchi, na ziara za Viongozi Wakuu wa mataifa mengine pamoja na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa hapa nchini kwa lengo la kudumisha uhusiano wa kidiplomasia na kutumia fursa za kiuchumi;

b) Kuratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika majadiliano ya kimataifa na jumuiya za kikanda ambazo nchi yetu ni mwanachama, hususan Umoja wa Mataifa, Umoja wa

Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki, na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika;

c) Kukamilisha maboresho ya Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001;

d) Kuendelea kuratibu na kutekeleza diplomasia ya uchumi ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya mpango wa kitaifa wa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi;

e) Kutekeleza Mpango Mkakati wa Uendelezaji wa viwanja vinavyomilikiwa na Serikali nje ya nchi na kukarabati majengo ya Balozi za Tanzania;

f) Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara;

g) Kuimarisha ushiriki wa Diaspora katika kuchangia maendeleo ya taifa ikiwa ni pamoja na kukamilisha mfumo na taratibu za kutoa Hadhi Maalum kwa Diaspora;

h) Kugharamia mahitaji ya msingi na ya kimkataba ya uendeshaji wa Balozi za Tanzania nje ya nchi ikiwemo pango la ofisi na makazi ya watumishi;

i) Kuimarisha utendaji kazi wa Balozi na Konseli Kuu kwa kuzipatia rasilimaliwatu, fedha na vitendea kazi stahiki;

j) Kufanikisha uendeshaji wa Makao Makuu ya Wizara kwa kulipa pango, kugharamia huduma za maji, umeme, simu; mafuta ya magari; na kulipa mikataba ya wazabuni;

k) Kuongeza matumizi ya TEHAMA katika usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Wizara;

l) Kuimarisha ukaguzi wa ndani na mifumo ya udhibiti Makao Makuu na Balozi za Tanzania; na utunzaji wa mali za Serikali;

m) Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara, makubaliano ya kikanda na kimataifa;

n) Kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora (APRM);

o) Kuwajengea uwezo watumishi kupitia mafunzo ya muda mrefu na mfupi na kuzingatia maslahi yao mahali pa kazi; na

p) Kutoa elimu kwa umma kuhusu ushirikiano wa kimataifa na fursa zinazopatikana kutokana na nchi yetu kuwa mwanachama wa jumuiya za kikanda na kimataifa pamoja na mikataba/makubaliano kati ya Tanzania na nchi nyingine.

**7.0 MALENGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

**Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC)**

***180. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kituo kimepanga kukusanya kiasi cha Shilingi 21,030,562,180 kutokana na vyanzo vya ndani. Fedha hizo zitatumika kugharamia uendeshaji wa Kituo ikiwemo mishahara; ununuzi wa samani za vyumba vya mikutano; vifaa vya TEHAMA; ununuzi wa vifaa tiba katika Hospitali ya AICC; na miradi ya maendeleo.

***181. Mheshimiwa Spika,*** Kituo kitaendelea kuvutia mikutano ya kimataifa kwa lengo la kuongeza mapato yake na kuitangaza nchi

kama kitovu cha diplomasia ya mikutano. Aidha, AICC inakamilisha taratibu za kuanza ujenzi wa kituo cha mikutano kitakachoitwa *Mount Kilimanjaro International Convention Centre* jijini Arusha. Kituo hicho kitaimarisha na kuongeza kasi ya utekelezaji wa diplomasia ya mikutano na maonesho hapa nchini.

**Chuo cha Diplomasia**

***182. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Chuo kinatarajia kuendelea kutekeleza majukumu yafuatayo:

a) Kutoa mafunzo ya uhusiano wa kimataifa, na mafunzo ya lugha mbalimbali na Lugha ya Kiswahili kwa wageni;

b) Kufanya tafiti katika eneo la uhusiano wa kimataifa;

c) Kutoa ushauri elekezi na huduma za kitaalamu kwa Serikali na taasisi zake;

d) Kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia;

e) Kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi wa Chuo; na

f) Kukitangaza chuo kitaifa na kimataifa.

***183. Mheshimiwa Spika,*** ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu yake kwa mwaka 2023/2024, Chuo kinatarajia kutumia kiasi cha Shilingi 11,341,255,819. Kati ya fedha hizo Shilingi 3,072,000,000 ni mapato kutoka vyanzo vya ndani, na Shilingi 8,269,255,819 ni ruzuku kutoka Serikali kuu. Ruzuku kutoka Serikali Kuu inajumuisha Shilingi 1,200,000,000.00 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; Shilingi 3,169,255,819 kwa ajili ya Mishahara; na Shilingi 3,900,000,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora

***184. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024, APRM Tanzania inatarajia kutekeleza majukumu yafuatayo:

a) Kuendelea kufanya tathmini katika masuala ya demokrasia na siasa, usimamizi wa uchumi, uendeshaji wa mashirika ya biashara na utoaji wa huduma za jamii;

b) Kuhuisha mbinu za utafiti kwa kupitia upya hojaji ya APRM, kuboresha viashiria vya utafiti, kuzingatia matumizi ya teknolojia katika utekelezaji wa mpango na kupanua wigo wa zana zinazotumika katika utafiti;

c) Kuratibu utekelezaji wa mpango kazi wa APRM kwa kushirikiana na wizara, idara na wakala wa Serikali katika kuandaa taarifa ya mwaka na kuweka mfumo madhubuti wa ufuatiliaji; na

d) Kuimarisha mawasiliano na utoaji taarifa kuhusu mpango wa APRM kwa kuzingatia Mpango wa Mawasiliano wa Miaka Mitano 2021/2022–2025/2026.

***185. Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Utawala Bora na Demokrasia (APRM) imetengewa kiasi cha Shilingi 1,757,857,866 ikijumuisha Mishahara na Matumizi Mengineyo.

## 8.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2023/2024

***186. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi 1,559,879,000 ikiwa ni mapato ya Serikali yatakayopatikana kutokana na vyanzo mbalimbali vilivyopo Makao Makuu ya Wizara, na katika Balozi za Tanzania. Vyanzo hivyo vya mapato vinajumuisha pango la nyumba za Serikali zilizopo nje ya nchi na uthibitishaji wa nyaraka.

***187. Mheshimiwa Spika,*** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara imetengewa bajeti ya kiasi cha Shilingi 247,971,524,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 230,083,916,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida yakijumuisha Shilingi 213,304,516,000 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; Shilingi 16,779,400,000 kwa ajili ya Mishahara; na Shilingi 17,887,608,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

***188. Mheshimiwa Spika,*** kati ya fedha za bajeti ya matumizi mengineyo ya Wizara, shilingi 1,534,857,866 ni kwa ajili ya Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Utawala Bora na Demokrasia (APRM), Shilingi 1,200,000,000 ni kwa ajili ya Chuo cha Diplomasia, Shilingi 1,400,000,000 ni kwa ajili ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (ACHPR) na Shilingi 280,000,000 ni kwa ajili ya Bodi ya Ushauri wa Masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika (AUABC). Aidha, kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mishahara, Shilingi 3,169,255,819.00 ni kwa ajili ya mishahara ya Chuo cha Diplomasia.

***189. Mheshimiwa Spika,*** kiasi cha Shilingi 17,887,608,000 kilichotengwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, Kati ya fedha hizo Shilingi 17,700,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 187,608,000 ni fedha za nje. Aidha, katika fedha hizo, Shilingi 5,400,000,000 ni kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu iliyopo jijini Arusha; Shilingi 3,900,000,000 ni kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa vyumba tisa (9) vya mihadhara katika Chuo cha Diplomasia; shilingi 2,000,000,000 kwa ajili ya kufanya Chambuzi yakinifu kwa ajili ya miradi 13 ya kipaumbele katika Mpango Mkakati wa utekelezaji wa majengo balozini ili kuwezesha sekta binafsi kushirikiana na Serikali katika uendelezaji wa miradi hii, na Shilingi 6,400,000,000 ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya Serikali katika balozi za Tanzania. Katika utaratibu huu Wizara itatekeleza miradi hii kupitia utaratibu wa kushirikiana na sekta binafsi (PPP), mikopo ya kiserikali kupitia HAZINA, pamoja na utaratibu maalumu wa kiserikali.

**9.0 HITIMISHO**

***190. Mheshimiwa Spika,*** ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 247,971,524,000. Kati ya fedha hizo shilingi 230,083,916,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 17,887,608,000 ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo.

***191. Mheshimiwa Spika,*** naomba kuhitimisha kwa kukushukuru tena wewe binafsi, Mheshimiwa Spika kwa jinsi unavyoendesha vikao vya Bunge kwa umahiri wa hali ya juu, na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

***192. Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Stergomena Tax. Hoja imeungwa mkono. Nashukuru kwa kuwasilisha hotuba.

Kabla sijamwita Mwenyekiti naomba nitoe matangazo machache.

Kuna wageni ambao hawakutambulishwa; wageni wa Mheshimiwa Judith Kapinga ambao ni viongozi wa Tuzo za Vijana za Afrika Mashariki *(East African Youth Awards)* wakiongozwa na Hellen William Mollel ambaye ni muasisi wa tuzo hizo na Spika Mstaafu wa Bunge la Vijana wa Afrika Mashariki; wapo pale. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lakini pia tuna mgeni wa Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor ambaye ni Ndugu Yusuph Said Mwahu. Ndugu Yusuph Said Mwahu karibu sana. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Kimei, timu mbili zilizoshinda kwenye michuano ya *Vunjo Cup* timu za Kaba, za Makuyuni na Njiapanda na viongozi wao pamoja na watendaji wa kata zote mbili. Timu hizo ziko wapi za Mheshimiwa Kimei, hazijaonekana. *(Makofi)*

Kuna wafadhili wa miradi mbalimbali ya kiharakati ya shule za msingi na zahanati kwa jina la *Help App.* Wageni hawa inaonekana wameshaondoka.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo ambalo lilisahaulika hapa; Katibu wa Bunge anawaomba niwakumbushe kwamba Wabunge wote Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo itaendesha semina kuhusu *COSOTA* ilipotoka, ilipo na inapoelekea pamoja na fursa zilizopo katika biashara ya ubunifu. Semina hii itafanyika leo Jumanne tarehe 30 Mei, mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa saba mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria katika semina hii muhimu sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ili aweze kuwasilisha taarifa ya Kamati. Karibu sana Mwenyekiti Mheshimiwa Vita Kawawa ili uweze kuwasilisha taarifa hiyo. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa ya kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Masahariki, Fungu 34.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuimarisha hali ya

mahusiano ya kimataifa kwa kutembelea nchi mbalimbali kwa lengo la kukuza uhusiano na diplomasia ya uchumi. Halikadhalika kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2022 hadi sasa ameteua Mabalozi 11 kwa ajili ya uwakilishi katika nchi na maeneo mbalimbali. Pia Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuridhia Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zinazogombea nafasi ya Urais wa Bunge la Duniani (*IPU)* na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola *(Common Wealth)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Kamati inalipongeza Bunge kwa kutoa wagombea wawili wa nafasi hizi nyeti za kimataifa ambao ni Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mbunge), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ni mgombea wa nafasi ya Urais wa Bunge la Duniani *(IPU)* na Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula mgombea wa nafasi ya Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola *(Common Wealth)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni Namba 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha sasa Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na maoni ya kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa Kamati kuchambua makadirio ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni masharti ya kifungu cha 6(3) kikisomwa pamoja na kifungu cha 7(1)(A) cha nyongeza ya nane ya Kanuni za Bunge. Aidha, Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Nafurahi kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa, na kwamba naliomba Bunge hili lijadili hoja ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa pamoja na taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya makadirio ya mapato na matumizi iliyochambuliwa inagusa fungu moja la kibajeti ambalo ni Fungu 34 Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Baada ya kutambulisha mawanda *(scope)* ya taarifa naomba kuisoma taarifa hii kwa muhtasari ili kuendana na muda pasipo kuathiri mtiririko wa maudhui. Hata hivyo, kwa umuhimu wa kumbukumbu kamili naomba taarifa yote kama ilivyowasilishwa mezani mapema leo asubuhi hii iinigie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua mradi mmoja wa ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu Jijini Arusha. Mradi huu ni moja ya miradi inayotekelezwa na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ina miradi miwili ya maendeleo ambayo ni ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu Jijini Arusha na ukarabati wa Ofisi za Ubalozi wa Tanzania Pretoria Afrika Kusini. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi, kamati ilifanikiwa kukagua mradi mmoja wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ambao ulitengewa kiasi cha shilingi bilioni nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Machi, 2023 wakati Kamati inatembelea mradi tajwa hapo juu, utekelezwaji wake ulikuwa bado haujaanza. Kamati ilielezwa kuwa sababu ya kuchelewa kuanza kwa mradi wa ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika Haki za Binadamu na Watu ni kutopokelewa kwa fedha za mradi wa maendeleo kutoka Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na matokeo ya ziara za ukaguzi wa mradi wa maendeleo, kamati ina maoni yafuatayo: -

a) Kutotolewa kwa fedha za maendeleo imekuwa ni moja ya sababu kubwa ya kuchelewa kwa kutokutekelezwa kabisa kwa miradi ya maendeleo. Hali hii inaathiri mipango ya maendeleo

iliyowekwa katika mradi husika wakati Bunge linaidhinisha fedha za mradi kwa niaba ya wananchi;

b) Tanzania iliingia makubaliano na Umoja wa Afrika mwaka 2007 kama *host agreement* ya kuwa mwenyeji wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Katika makubaliano hayo Tanzania ilikubali kujenga makao makuu ya mahakama hiyo. Hata hivyo, miaka 16 tangu makubaliano hayo bado Tanzania haijajenga makao makuu ya mahakama hiyo. Hali hii ni wazi inaathiri taswira ya Tanzania katika medani za diplomasia kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilihusu maeneo makuu matatu ambayo ni uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati, mapitio ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge na utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kamati ilipitia na kuchambua kwa kina maeneo yote matatu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzingatiaji wa maoni na ushauri wa kamati. Wakati wa kuchambua Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati ilishauri masuala mbalimbali. Naomba kulitaarifu Bunge lako kuwa taarifa ya mtoa hoja ilionesha kwamba Serikali imezingatia sehemu ya ushauri kama inavyoonekana kwenye kiambatisho namba moja ya taarifa yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa ushauri wa kamati uliozingatiwa ni kuhusu: -

a) Serikali kuandaa mpango mkakati utakaoshirikisha Sekta Binafsi katika uwekezaji kwenye ujenzi na upangishaji majengo ya balozi zetu nje ya nchi;

(b) Kuhusu utekelezaji wa maombi ya Watanzania *diaspora* ambao wamekuwa wakiomba kutambuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uzingatiaji wa ushauri, huo upo ushauri ambao utahitaji kufanyiwa kazi zaidi na Serikali. Mathalani, ushauri kuhusu Serikali kwa kushirikiana na mamlaka nyingine kuandaa mkakati unaotekelezeka wa kutoa elimu ya juu ya Diplomasia ya Uchumi na namna inavyotekelezwa kwa vitendo sambamba na kupeleka Wataalam wa Diplomasia ya Uchumi katika sekta muhimu kwa uwekezaji na biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla ushauri wa Kamati unaendelea kufanyiwa kazi na utekelezaji upo katika hatua mbalimbali. Kwa kuzingatia madaraka ya Bunge yaliyoidhinishwa katika Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ushauri ambao haujatekelezwa unapaswa kufanyiwa kazi na kuwa sehemu ya ratiba ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili uchambuzi wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kamati ilipitia Taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara katika Kipindi cha Julai, 2022 hadi Februari, 2023 kwa kuchambua hali ya ukusanyaji mapato pamoja na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukusanyaji wa Maduhuli; katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara hii ilikuwa na malengo ya kukusanya maduhuli kiasi cha shilingi 1,559,879,000.00. Kati ya fedha hizo shilingi 116,069,000.00 ni makusanyo ya Makao Makuu ya Wizara na shilingi 1,443,810,000.00 ni makusanyo kutoka Balozi za Nchi za Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2023, Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi 528,570,756.95, sawa na asilimia 34 ya lengo lililowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ulinganisho wa makusanyo ya Wizara kwa kipindi cha kufikia Februari, 2022 ambapo Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi 634,480,703.70 na kubaini kuwa makusanyo ya kipindi hiki yamepungua kwa shilingi 105,909,946.75, sawa na asilimia 16.7. Katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini yafuatayo:-

(i) Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ilipanga kukusanya shilingi 1,559,879,000.00 Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Februari, 2023 Wizara ilikuwa imekusanya shilingi 528,570,756.95 sawa na asilimia 34 tu ya lengo.

(ii) Wizara kukusanya asilimia 34 ya lengo lililopangwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kumesababishwa na uchakavu wa majengo ya Balozi zetu na athari za UVIKO.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na uchambuzi uliofanyika na Kamati, Kamati ina maoni kuwa mwenendo wa makusanyo ya Wizara hiyo siyo wa kuridhisha kwani kwa kipindi kilichobaki kumaliza mwaka huenda lengo lisifikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upatikanaji wa Fedha Kutoka Hazina; Kamati ilichambua Taarifa ya upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilibaini kuwa hadi kufikia mwezi Machi, 2023, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 173,680,792,367.9 sawa na asilimia 83.4 ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Wizara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha fedha kilichopokelewa ni ongezeko la shilingi 25,555,889,100.16, sawa na asilimia 17.25 ikilinganishwa na shilingi 148,125,303,276.43 zilizotolewa hadi kufikia mwezi Machi, 2022 ambazo zilikuwa ni asilimia 77 ya fedha zote za bajeti zilizoidhinishwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa ongezeko hilo limechangiwa na fedha za matumizi mengineyo zilizotolewa kwa asilimia 93.6 ya fedha zilizopokelewa. Aidha, katika fedha

zilizotolewa hadi kufikia mwezi Machi, 2023, Wizara ilipokea shilingi 923,956,961 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini pia, katika Fedha hizo zilizopokelewa katika mwaka wa fedha 2022/2023, shilingi 162,738,869,197.26 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Fedha hizo ni sawa na asilimia 86 ya shilingi 188,937,219,000 zilizotengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, shilingi 10,017,966,296.33 zilipokelewa kwa ajili ya mishahara ikiwa ni sawa na asilimia 68 zilizotengwa kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa kati ya shilingi 173,680,792,367.59 zilizopokelewa ni kwa ajili ya miradi ya na shilingi 923,956,061 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo ni sawa na asilimia 0.5 zilizopokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za miradi ya maendeleo zilizopangwa kutekeleza Miradi ya Ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika, Haki za Binadamu na Watu na Utamaduni na ukarabati wa Ofisi ya Ubalozi Pretoria; ni maoni ya Kamati kuwa kutokutolewa kwa fedha za maendeleo kwa mtiririko unaozingatia mipango ya Wizara, kunaathiri utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati. Serikali inapopanga mipango yake ni matarajio ya wananchi kuwa utekelezaji wake utakwenda kama ilivyokusudiwa ili kupeleka tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara; Taarifa iliyotolewa na Wizara ilibainisha kuwa katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara iliendelea kutekeleza majukumu yake 12 kama ilivyoainishwa katika ukarasa wa 15 na 16 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilichambua taarifa za Taasisi zilizopo chini ya Wizara hii ikiwa ni pamoja na Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha *(AICC)* na Chuo cha Diplomasia na Mpango wa Afrika wa Kujitathmini *(APRM)*. Kamati iliridhika na utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa kwa kiasi kikubwa Serikali imetekeleza majukumu yake kama ilivyopangwa licha ya kuwepo kwa changamoto mbalimbali. Miongoni mwa changamoto hizo ni upungufu wa watumishi katika Idara na Vitengo ikilinganishwa na mahitaji na majukumu ya Wizara, kushindwa kuendeleza majengo ya balozi na vitega uchumi katika Balozi zetu kutokana na ufinyu wa bajeti, sheria kutowezesha Sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika undelezaji wa majengo ya Balozi nje ya nchi na uelewa hafifu kuhusu Diplomasia ya Uchumi na fursa zitokanazo na mtangamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa changamoto zote zilizotolewa taarifa kuwa ziliathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2022/2023, ni zile ambazo Kamati imekuwa ikiishauri Serikali mara kwa mara kuhusu umuhimu wa kuzitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Mpango wa Bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; kabla ya kueleza uchambuzi wa makadirio ya matumizi ya Wizara hii, napenda kutoa taarifa kuwa, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara imepanga kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele 14 tofauti na ilivyokuwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo Wizara ilijiwekea vipaumbele 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara imeongeza vipaumbele viwili. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuongeza vipaumbele hivyo kwa kuwa Wizara hii inahusika na masuala ya kimataifa, ni imani ya Kamati kwamba imejipanga ipasavyo kutekeleza vipaumbele hivyo kwa ufanisi ili kufikia malengo na tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato; Kamati ilipitia makadirio ya ukusanyaji wa mapato yanayopendekezwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Mapitio hayo yalibaini kuwa Wizara imewekewa malengo la kukusanya shilingi 1,559,879,000.00. Kiasi hicho kinachokadiriwa kukusanywa ni

sawa na makadirio ya makusanyo yaliyowekwa katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo yaliyowasilishwa mbele ya Kamati, Kamati ilibaini kuwa shilingi 150,000,000.00 sawa na asilimia 9.6 ni fedha zinazotarajiwa kukusanywa Makao Makuu ya Wizara. Aidha, kiasi hicho kinatarajiwa cha jumla ya shilingi 1,409,879,000.00, sawa na asilimia 90.4 kinatarajiwa kukusanywa katika Balozi na Taasisi nje ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa ni Balozi tano tu za Tanzania nje ya nchi katika Majiji ya Lusaka, Maputo, New York, Paris, na Harare ndizo zinatarajiwa kukusanya mapato ya Serikali kupitia pango la nyumba za Serikali. Balozi hizo ndiyo pia zilitegemewa kukusanya mapato katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 hata hivyo hakuna Balozi mpya ambayo zinazotarajiwa kuiingizia Serikali mapato kutokana na mapango ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufanya uchambuzi wa kina ni matarajio ya Kamati kuwa lengo hilo limezingatia changamoto mbalimbali ambazo zimechangia kutofikia lengo la makusanyo katika mwaka wa fedha 2022/2023 na hivyo kuweka lengo lenye uhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi; katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi 247,971,524,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 213,304,516,000 sawa na asilimia 86 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)* na shilingi 16,779,400,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 17,000,608,000 sawa na asilimia saba ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo kama inavyoonekana katika chati Na.1 la Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa, bajeti inayoombwa kwa ajili ya mwaka 2023/2024 imeongezeka kwa asilimia 19 ikilinganishwa na bajeti ya 2022/2023. Ongezeko limechangiwa na kuongezeka kwa bajeti ya matumizi

mengineyo kwa asilimia 12.8 na Bajeti ya Mishahara asilimia 13.9 ikilinganishwa na zilizoidhinishwa kwa matumizi hayo katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sura ya uwiano wa bajeti iliyotengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo, mishahara na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na ulinganisho wake kwa mwaka wa fedha 2023/2024 inaonekana katika Jedwali Na.1 na Grafu Na.1 katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa fedha iliyotengwa kwa ajili ya maendeleo imeongezeka kwa kiasi cha shilingi 13,187,608,000 sawa na ongezeko la takribani asilimia 282 ikilinganishwa na shilingi bilioni 4.7 iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Hata hivyo, pamoja na kuwa mapendekezo ya bajeti ya maendeleo yameongezeka ikilinganishwa na shilingi bilioni 4.7 zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023, uhalisia ni kwamba fedha hizo zimetolewa kwa asilimia 0.5 tu ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara kufikia mwezi Februari, 2023. Kiasi hicho kilipangwa kutekeleza miradi miwili ambapo katika Mwaka wa Fedha 2023 bajeti inayoombwa ni kwa ajili ya kutekeleza miradi nane ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongezeka kwa fedha za miradi ya maendeleo kutakuwa na tija tu ikiwa fedha hizo zitapatikana kwa kuzingatia mipango ya utekelezaji wa miradi katika mwaka wa fedha husika. Ni rai ya Kamati kuwa katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali itatoa fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa ukamilifu na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kati ya miradi yake nane iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/2024, miradi miwili ipo katika utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Miradi hiyo inayojumuisha Ujenzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu Arusha; ukarabati wa Ubalozi wa Tanzania Pretoria - Afrika Kusini; ukarabati

wa Jengo la zamani la Ubalozi wa Washington DC; ujenzi wa makazi ya Ubalozi na Jengo la Kitega Uchumi Addis Ababa; ujenzi wa ukarabati wa majengo ya Ubalozi, Makazi ya Balozi na Majengo ya Vitega Uchumi Balozini; ujenzi wa vyumba vya mihadhara Chuo cha Diplomasia; na mradi wa kujenga uwezo Wizarani. Ni rai ya Kamati kuwa Wizara itakamilisha taratibu za awali na kuomba fedha Hazina kwa wakati ili kutekeleza miradi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati; kutokana na uchambuzi kama nilivyoeleza, Kamati inayo maoni yanayojenga msingi wa ushauri nitakaoutoa. Naomba kubainisha maoni hayo kama ifuatavyo:-

(i) Kwa muda wa miaka mitatu mfululizo Wizara hii imeshindwa kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wakati kutokana na kutopokelewa kwa fedha za miradi ya maendeleo. Hali hiyo imeathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa miradi iliyopangwa na hivyo kutofikiwa kwa malengo na tija iliyokusudiwa wakati Bunge linaidhinisha fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

(ii) Kuongezeka kwa fedha za miradi ya maendeleo kutakuwa na tija tu ikiwa Wizara itakamilisha taratibu za awali kwa wakati ili kuweza kuomba fedha Hazina na Serikali kutoa fedha hizo kwa wakati na kwa kuzingatia mipango ya utekelezaji wa miradi.

(iii) Kitendo cha kushindwa kuanza ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kwa miaka 16 tangu kuingia makubaliano husika na Umoja wa Afrika ni hali ambayo ikiendelea, huenda ikatia doa taswira ya nchi yetu kidiplomasia hasa katika Umoja wa Afrika na duniani kwa ujumla.

(iv) Baadhi ya nyumba za makazi ya watumishi katika Balozi mbalimbali zimechakaa na hivyo kuathiri hadhi ya Nchi, Balozi na Watumishi wetu katika nchi walizopo.

(v) Balozi zetu ni moja ya ofisi muhimu katika kuutangaza utalii wa nchi yetu, ni muhimu ofisi hizo kuwa na mkakati wa kutangaza utalii wa nchi yetu ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais katika kutangaza utalii na hivyo kuongeza mapato ya nchi. Ni muhimu sana balozi zetu zikawekewa malengo katika kuutangaza utalii.

(vi) Miongoni mwa vipaumbele vya Wizara ni kutekeleza Diplomasia ya Uchumi kwa kuwavutia wawekezaji na wafanyabiashara kutoka nje ya nchi. Diplomasia ya Uchumi bado haijatekelezwa kwa ufasaha kwa wananchi na hata viongozi ambao wanasimamia sekta mtambuka ambazo zinahusika na uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa. Hii inasababisha nchi kutonufaika ipasavyo na Diplomasia ya Uchumi.

(vii) Kuna umuhimu wa Serikali kuendelea kupeleka watumishi ubalozini kulingana na fani maalum zinazohusika na masuala ya uchumi, uwekezaji na utalii. Kufanya hivyo itakuwa ni sehemu ya nchi yetu kunufaika na Diplomasia ya Uchumi.

(viii) Wananchi wana haki ya kunufaika na fursa za kiuchumi na masoko zinazopatikana katika Jumuiya za Kikanda. Tathmini na ufuatiliaji unaonesha kuwa Watanzania hawajanufaika ipasavyo na fursa za kiuchumi na masoko katika Jumuiya za Kikanda.

(ix) Mpango wa ushirikiano wa sekta za umma na sekta binafsi katika ujenzi wa majengo ya ubalozi na vitega uchumi unakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo za kisheria. Hivyo, ili mpango huo uweze

kutekelezeka kuna umuhimu wa kuchukua hatua kumaliza changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa Kamati:-

(i) Ili kuhakikisha kuwa katika mwaka wa fedha 2023/2024, miradi yote ya maendeleo inatekelezwa kwa wakati. Wizara iweke mkakati maalum wa kuanza maandalizi mapema wa kukamilisha taratibu zote muhimu za awali zinazohitajika ili kuanza utekelezaji wa miradi na kuomba fedha Hazina kwa wakati.

(ii) Ili kupata tija iliyokusudiwa katika miradi ya maendeleo Serikali itoe fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kuzingatia mpango wa Wizara wa utekelezaji wa miradi husika.

(iii) Kutokana na umuhimu wa ujenzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Serikali itoe fedha zote zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama hiyo. Kufanya hivyo kutawezesha kuanza kutekelezwa kwa mradi huo na kuendelea kujenga taswira nzuri ya diplomasia iliyonayo nchi yetu katika Umoja wa Afrika na Duniani kwa ujumla.

(iv) Serikali iendelee kutekeleza mkakati maalum wa kukarabati nyumba za watumishi katika Balozi zetu kwa awamu ili nyumba hizo ziendane na hadhi ya Tanzania iliyonayo nje ya nchi.

(v) Kamati inapongeza Serikali kwa utekelezaji wa maombi ya Watanzania *(Diaspora)* ambao wamekuwa wakiomba kutambuliwa na Serikali. Mchakato huu unaendelea vizuri ikiwa ni pamoja na kuzinduliwa rasmi kwa Mfumo wa Kukusanya na Kutunza Taarifa za *Diaspora* Kidigitali *(Diaspora Digital Hub Registration)* uliozinduliwa rasmi na Mhe. Dkt. Stergomena Lawrence Tax, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika

Mashariki mwezi Mei, 2023. Kamati inampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kusimamia hili na uzinduzi na kazi nzuri waliyoifanya. Kamati inashauri mchakato huu wa Diaspora ukamilishwe mapema ili kuleta tija inayokusudiwa. *(Makofi)*

vi. Serikali izidishe juhudi katika kuzisimamia Balozi zetu nje ya nchi, kutangaza fursa za kitalii na vivutio mbalimbali vilivyopo nchini ili iende sambamba na kuhakikisha kunakuwa na mkakati unaotekelezeka utakaoainisha malengo na namna ya kutekeleza malengo hayo katika sekta ya utalii kwenye Balozi zetu.

vii. Katika kuhakikisha kuwa nchi inanufaika ipasavyo na diplomasia ya uchumi wizara ikamilishe mkakati wa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi katika mwaka wa fedha 2023/2024. Kukamilisha mkakati wa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi pamoja na faida nyingine pia utasaidia diplomasia ya uchumi kutekelezwa katika ngazi ya Mkoa na Wilaya.

viii. Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kushirikiana na Wizara iandae mkakati wa kupeleka watumishi wenye fani maalum kwa kuzingatia mahitaji, ikiwemo fani za uchumi, uwekezaji, utalii na biashara. Kufanya hivyo kutachochea kasi ya kutafuta wawekezaji na watalii katika Balozi zetu.

ix. Ikiwa ni sehemu ya kutatua changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Serikali iongeze kasi katika kukamilisha Sera ya Mambo ya Nje ambayo imekuwa ikishauriwa na Wabunge katika vipindi tofauti.

x. Serikali iendelee kuhamasisha kimkakati sekta binafsi kutumia fursa za biashara na uwekezaji zitokanazo na Mtangamano wa Afrika Mashariki pamoja na Jumuya za Kikanda.

xi. Wizara iendelee kutekeleza maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali ambayo hayajatekelezwa hususan katika bajeti za miaka mitatu iliyopita ya 2020/2021, 2021/2022 na 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Stergomena Lawrence Tax, Mbunge na Naibu Waziri Mheshimiwa Balozi Mbarouk Mbarouk Mbunge, Katibu Mkuu Balozi Samweli Wiliam Shelukindo pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, kwa kuiwezesha Kamati kuandaa na kukamilisha kazi yake kwa wakati. Aidha, nawashukuru Ndugu Michael Chikokoto, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Gerald Magili Mkurugenzi Msaidizi, Makatibu wa Kamati Ndugu Omary Magwinza na Ndugu Victoria Mizengo wakisaidiwa na Ndugu Rehema Kimbe, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA ASHARIKI (FUNGU 34) KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

***[Imetolewa chini ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]***

**SURA YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuimarisha hali ya mahusiano ya Kimataifa kwa kutembelea nchi mbalimbali kwa lengo la kukuza uhusiano na Diplomasia ya Uchumi. Halikadhalika, kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2022 hadi sasa ameteua **Mabalozi 11** kwa ajili ya uwakilishi katika Nchi na maeneo mbalimbali. Pia Kamati inampongeza Mhe. Rais kwa kuridhia Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zinazogombea nafasi ya Urais wa Bunge la Dunia *(IPU)* na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola *(Commonwealth)*.

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile Kamati inalipongeza Bunge kwa kutoa wagombea wawili wa nafasi hizi nyeti za Kimataifa ambao ni Mhe. Dkt. Tulia Ackson, (Mb), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ni mgombea wa nafasi ya Uraisi wa Bunge la Dunia *(IPU)* na Mhe. Balozi Liberata Mulamula, Mb, mgombea wa nafasi ya Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola *(Commonwealth)*.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo kama ilivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 6(3) (c) cha Nyongeza ya Nane, ya Kanuni za Bunge, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni miongoni mwa Wizara zinazosimamiwa na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Aidha, Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kimezipa jukumu Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki tarehe 23 Machi, 2023; kwa ajili ya kupokea Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama inavyoelekeza Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge; kwa lengo la kulinganisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, ili kulisaidia Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, pamoja na kuishauri vyema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Taarifa ninayoiwasilisha inatoa maelezo kuhusu:-

i) Utangulizi;

ii) Matokeo ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;

iii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

iv) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

v) Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; na

vi) Hitimisho.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la maelezo hayo ni kuliwezesha Bunge kupata taswira ya hali ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na kulinganisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ili Bunge liweze kuamua kuhusu Maombi ya Wizara hii.

## SURA YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua mradi mmoja wa Ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu Jijini Arusha. Mradi huu ni moja ya miradi inayotekelezwa na Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Taarifa hii inaeleza mambo makuu mawili: -

a) Muhtasari wa maelezo ya mradi uliotembelewa na kukaguliwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023; na

b) Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo.

**Mheshimiwa Spika**, Lengo la sehemu hii ni kuliwezesha Bunge kufuatilia hali ya utekelezaji na upatikanaji wa Fedha ilizoziidhinisha

na kupata mantiki ya uamuzi wake wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

**2.1 Muhtasari wa Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa;**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ina miradi miwili ya maendeleo ambayo ni Ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na ukarabati wa Ofisi za Ubalozi wa Tanzania Pretoria, Afrika ya Kusini. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi Kamati ilifanikiwa kukagua mradi mmoja wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Maelezo kuhusu mradi uliokaguliwa ni kama ifuatavyo;

**2.1.1 Mradi wa Ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu-Arusha**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ilitengewa kiasi cha **Shilingi 4,000,000,000.00** kwa ajili ya Ujenzi wa Makao Makuu.

**2.2 Matokeo ya Ukaguzi**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya muhtasari wa mradi wa maendeleo uliyokaguliwa, sasa naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuhusu matokeo ya uchambuzi wa miradi hiyo kuwa, hadi Mwezi Machi, 2023 wakati Kamati inatembelea Mradi tajwa hapo juu utekelezaji wake ulikuwa bado haujaanza. Kamati ilielezwa kuwa sababu ya kuchelewa kuanza kwa mradi wa Ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni kutopokelewa kwa fedha za miradi ya maendeleo kutoka Hazina.

**2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na matokeo ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ina maoni yafuatayo: -

i) Kutokutolewa kwa fedha za maendeleo imekuwa ni moja ya sababu kubwa ya kuchelewa au kutokutekelezwa kabisa kwa miradi ya maendeleo. Hali hii inaathiri mipango na malengo yaliyowekwa katika mradi husika wakati Bunge linaidhinisha fedha za mradi kwa niaba ya wananchi;

ii) Tanzania iliingia makubaliano na Umoja wa Afrika mwaka 2007 *(Host Agreement)* ya kuwa mwenyeji wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Katika makubaliano hayo Tanzania ilikubali kujenga Makamo Makuu ya Mahakama hiyo.

iii) Hata hivyo, miaka 16 tangu makubaliano hayo bado Tanzania haijajenga Makao Makuu ya Mahakama hiyo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Bunge liliidhinisha kiasi cha **Shilingi 4,000,000,000** ili kuanza ujenzi wa Mahakama hiyo, lakini hadi kufikia Mwezi Machi, 2023 fedha hizo hazikuwa zimepokelewa licha ya Wizara kukamilisha taratibu zote. Hali hiyo ni wazi inaathiri taswira ya Tanzania katika Medani za Diplomasia Kimataifa.

## SURA YA TATU

## 3.0 MAPITIO YA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ilihusu maeneo Makuu matatu. Maeneo hayo ni:-

i) Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati;
ii) Mapitio ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge; na
iii) Utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilipitia na kuchambua kwa kina maeneo yote matatu kama ifuatavyo: -

**3.1 Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati;**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati ilishauri masuala mbalimbali. Naomba kuliarifu Bunge kuwa, taarifa ya mtoa hoja ilionesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu ya ushauri kama inavyoonekana katika ***Kiambatisho Na. 1*** cha Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, Mfano wa ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni kuhusu;-

i) Serikali kuandaa Mpango Mkakati utakaoshirikisha Sekta Binafsi katika uwekezaji kwenye ujenzi na ununuzi majengo ya Balozi zetu nje ya nchi; na

ii) Kuhusu utekelezaji wa maombi ya Watanzania (Diaspora) ambao wamekuwa wakiomba kutambuliwa;

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na uzingatiaji wa ushauri, upo ushauri ambao utahitaji kufanyiwa kazi zaidi na Serikali. Mathalani, ushauri kuhusu Serikali kwa kushirikiana na mamlaka nyingine kuandaa mkakati unaotekelezeka wa kutoa elimu juu ya Diplomasia ya Uchumi na namna inavyotekelezwa kwa vitendo sambamba na kupeleka Wataalam wa Diplomasia ya uchumi katika sekta muhimu kwa uwekezaji na biashara.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla ushauri wa Kamati unaendelea kufanyiwa kazi na utekelezaji upo katika hatua mbalimbali. Kwa kuzingatia Madaraka ya Bunge yaliyoainishwa katika Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ushauri ambao haujatekelezwa unapaswa kufanyiwa kazi na kuwa sehemu ya ratiba ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

### 3.2 Uchambuzi wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipitia Taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara katika Kipindi cha Julai, 2022 hadi Februari, 2023 kwa kuchambua hali ya Ukusanyaji wa Mapato pamoja na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa kipindi hicho.

#### 3.2.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara hii ilikuwa na lengo la kukusanya Maduhuli ya kiasi cha **Shilingi 1,559,879,000.00.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 116,069,000.00** ni makusanyo ya Makao Makuu ya Wizara na **Shilingi 1,443,810,000.00** ni makusanyo kutoka Balozi za Tanzania Nje ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia Mwezi Februari, 2023 Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha **Shilingi 528,570,756.95** sawa na **asilimia 34** ya lengo lililowekwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ulinganisho wa makusanyo ya Wizara kwa kipindi cha kufikia Februari, 2022 ambapo Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha **Shilingi 634,480,703.70** na kubaini kuwa makusanyo ya kipindi hiki yamepungua kwa **Shilingi 105,909,946.75** sawa na **asilimia 16.7.** Katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini yafuatayo:-

i) Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ilipanga kukusanya **Shilingi 1,559,879,000.00** Hata hivyo, hadi kufikia Mwezi Februari, 2023 Wizara ilikuwa imekusanya **Shilingi 528,570,756.95** sawa na **asilimia 34 tu** ya lengo.

ii) Wizara kukusanya **asilimia 34** ya lengo lililopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kumesababishwa na changamoto mbali mbali ikiwemo uchakavu wa majengo katika Balozi zetu na athari za UVIKO 19.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati hairidhishwi na sababu zilizotolewa kuhusu makusanyo kuwa chini ya lengo kwa kuwa sababu zilizoainishwa zilikuwepo hata kipindi ambacho Wizara inaweka makadirio hayo.

**Mheshimiwa Spika**, kulingana na uchambuzi uliofanyika, Kamati ina maoni kuwa mwenendo wa makusanyo ya Wizara sio wa kuridhisha kwani kwa kipindi kilichobaki kumaliza mwaka wa fedha lengo haliwezi kufikiwa.

### 3.2.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipochambua Taarifa ya upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ilibaini kuwa hadi kufikia Mwezi Machi, 2023, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 173,680,792, 367.59** sawa na **asilimia 83.4** ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, kiwango cha fedha kilichopokelewa ni ongezeko la **Shilingi 25,555,489,091.16** sawa na asilimia **17.25** ikilinganishwa na S**hilingi 148,125,303,276.43** zilizotolewa hadi kufikia Mwezi Machi, 2022 ambazo zilikuwa ni **asilimia 77** ya bajeti yote iliyoidhinishwa katika Mwaka 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa ongezeko hilo limechangiwa na fedha za matumizi mengineyo zilizotolewa kwa **asilimia 93.6** ya fedha zilizopokelewa. Aidha, katika fedha zilizotolewa hadi kufikia Mwezi Machi, 2023 Wizara ilipokea **Shilingi 923,956,961** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini pia, kati ya Fedha zilizopokelewa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, **Shilingi 162,738,869,197.26** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Fedha hizo ni sawa na **asilimia 86** ya **Shilingi 188,937,219,000** zilizotengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Aidha, **Shilingi 10,017,966,209.33** zilipokelewa kwa ajili ya mishahara ikiwa ni sawa na **asilimia 68** ya **Shilingi 14,729,745,000** zilizotengwa kwa ajili hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa kati ya **Shilingi 173,680,792,367.59** zilizopokelewa **Shilingi 923,956,961** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo ni sawa na **asilimia 0.5** ya fedha zilizopokelewa.

Fedha za miradi ya maendeleo zilipangwa kutekeleza miradi ya ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na ukarabati wa Ofisi za Ubalozi wa Tanzania Pretoria, Afrika Kusini.

**Mheshimiwa Spika,** ni maoni ya Kamati kuwa kutokutolewa kwa fedha za maendeleo kwa mtiririko unaozingatia mipango ya Wizara, kunaathiri utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati. Serikali inapopanga mipango yake ni matarajio ya Kamati na wananchi kuwa utekelezaji wake utakwenda kama ilivyokusudiwa ili kuleta tija kwa Taifa.

### 3.3 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa iliyotolewa na Wizara ilibainisha kuwa katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara iliendelea kutekeleza majukumu yake ikiwemo Kuratibu Masuala ya Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa, Kuanzisha na Kusimamia Huduma za Kikonseli, Kusimamia na Kuratibu Masuala ya Itifaki, kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje, Kuratibu na Kusimamia Masuala ya Watanzania waishio ughaibuni, Kuratibu na Kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Taasisi zilizo chini ya Wizara, Kusimamia na Kuratibu Masuala ya Mikataba na Makubaliano ya Kimataifa; na kuratibu, kusimamia, kukuza biashara za kimataifa na kusimamia utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilichambua Taarifa za Taasisi zilizopo chini ya Wizara hii ikiwa ni pamoja na Kituo cha Mikutano cha

Kimataifa cha Arusha (AICC) na Chuo cha Diplomasia na Mpango wa Afrika wa Kujitathmini (APRM). Kamati iliridhika na utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa kwa kiasi kikubwa Serikali imetekeleza majukumu yake kama ilivyopangwa licha ya kuwepo kwa changamoto mbalimbali. Miongoni mwa changamoto hizo ni upungufu wa watumishi katika Idara na Vitengo ikilinganishwa na mahitaji na majukumu ya Wizara, kushindwa kuendeleza majengo ya balozi na vitega uchumi katika Balozi zetu kutokana na ufinyu wa bajeti, Sheria kutowezesha Sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika undelezaji wa majengo ya Balozi nje ya nchi, uelewa hafifu kuhusu Diplomasia ya Uchumi na fursa zitokanazo na mtangamano.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa changamoto zote zilizotolewa taarifa kuwa ziliathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara wa Mwaka 2022/2023, ni zile ambazo Kamati imekuwa ikiishauri Serikali mara kwa mara kuhusu umuhimu wa kuzitatua.

## SURA YA NNE

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA BAJETI YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### 4.1 Uchambuzi wa Malengo ya Bajeti

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya kueleza uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii, napenda kutoa Taarifa kuwa, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara imepanga kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele Kumi na Nne (14) tofauti na ilivyokuwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 ambapo Wizara ilijiwekea vipaumbele kumi na mbili (12).

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake, kamati imebaini kuwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara imeongeza vipaumbele viwili. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuongeza vipaumbele hivyo

kwa kuwa Wizara hii inahusika na masuala ya Kimataifa; ni imani ya Kamati kwamba imejipanga ipasavyo kutekeleza vipaumbele hivyo kwa ufanisi ili kufikia malengo na tija iliyokusudiwa.

**4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipitia Makadirio ya ukusanyaji wa Mapato yanayopendekezwa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Mapitio hayo yalibaini kuwa Wizara imewekewa lengo la kukusanya **Shilingi 1,559,879,000.00.** Kiasi hicho kinachokadiriwa kukusanywa ni sawa na makadirio ya makusanyo yaliyowekwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo yaliyowasilishwa mbele ya Kamati yalibainisha kuwa, **Shilingi 150,000,000.00** sawa na **asilimia 9.6** ni fedha zinazotarajiwa kukusanywa na Makao Makuu ya Wizara. Aidha kiasi kinachobaki cha Jumla ya **Shilingi 1,409,879,000.00** sawa na **asilimia 90.4** kinatarajiwa kukusanywa kutoka katika Balozi za Tanzania Nje ya nchi.

Aidha, katika Uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa ni Balozi tano (5) tu za Tanzania nje ya Nchi katika Majiji ya Lusaka, Maputo, New York, Paris, na Harare ndizo zinatarajiwa kukusanya mapato ya Serikali kupitia pango la Nyumba za Serikali. Balozi hizo ndizo pia zilitegemewa kukusanya mapato katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 hivyo hakuna Balozi mpya ambazo zinazotarajiwa kuiingizia Serikali mapato kutokana na kodi ya pango.


**Mheshimiwa Spika,** baada ya kufanya uchambuzi wa kina ni matarajio ya Kamati kuwa lengo hilo limezingatia changamoto mbalimbali ambazo zimechangia kutofikia lengo la makusanyo katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 na hivyo kuweka lengo lenye uhalisia.

**4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 247,971,524,000/=,** Kati ya

fedha hizo, **Shilingi 213,304,516,000/=** sawa na **asilimia 86** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), **Shilingi 16,779,400,000/=** sawa na **asilimia 7** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 17,887,608,000/**= sawa na **asilimia 7** ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo kama inavyoonekana katika **Chati Na. 1** ya Taarifa hii.

**Chati Na. 1: Uwiano wa Fedha zinazoombwa kwa Matumizi ya Wizara**




***Chanzo: Randama ya Wizara 2023/2024***

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa, Bajeti inayoombwa kwa ajili ya Mwaka 2023/2024 imeongezeka kwa **asilimia 19** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023. Ongezeko limechangiwa na kuongezeka kwa Bajeti ya matumizi mengineyo kwa **asilimia 12.8** na Bajeti ya Mishahara kwa **asilimia 13.9** ikilinganishwa na fedha zilizoidhinishwa kwa matumizi hayo katika Mwaka wa Fedha 2022/2023.


**Mheshimiwa Spika,** Sura ya uwiano wa Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, Mishahara na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na ulinganisho wake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 inaonekana katika **Jedwali Na. 1** na **Grafu Na. 1.**

**Jedwali Na. 1: Uwiano wa aina za Bajeti ya Matumizi na ulinganisho wake kwa Mwaka 2022/2023 na 2023/2024**

| MWAKA | 2022/2023 | | 2023/2024 | | % +/- |
|---|---|---|---|---|---|
| AINA YA MATUMIZI | KIASI | ASILIMIA | KIASI | ASILIMIA | |
| MISHAHARA (PE) | 14,729,745,000.00 | 7 | 16,779,400,000 | 7 | 13.9 |
| MENGINEYO (OC) | 188,937,219,000.00 | 90.6 | 213,304,516,000 | 86 | 12.8 |
| MAENDELEO | 4,700,000,000.00 | 2.2 | 17,887,608,000 | 7 | +280 |
| JUMLA | **208,366,964,000.00** | **100** | **247,971,524,000** | **100** | |

*Chanzo: Randama ya Wizara 2022/2023 na 2023/2024*

**Grafu Na. 1: Ulinganisho wa Uwiano wa Bajeti ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na 2023/2024**




*Chanzo: Randama ya Wizara 2022/2023 na 2023/2024*

**Mheshimiwa Spika,** vilevile katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa fedha iliyotengwa kwa ajili ya Maendeleo imeongezeka kwa kiasi cha **Shilingi 13,187,608,000** sawa na ongezeko la takribani **asilimia 280** ikilinganishwa na **Shilingi 4,700,000,000** iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Hata hivyo, pamoja na kuwa

mapendekezo ya Bajeti ya maendeleo yameongezeka ikilinganishwa na **Shilingi Bilioni 4.7** zilizoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, uhalisia ni kwamba fedha hizo zimetolewa kwa **asilimia 0.5 tu** ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara kufikia mwezi Februari, 2023. Kiasi hicho kilipangwa kutekeleza miradi miwili (2) ambapo katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Bajeti inayoombwa ni kwa ajili ya kutekeleza miradi Nane (8) ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** kuongezeka kwa fedha za miradi ya maendeleo kutakuwa na tija tu ikiwa fedha hizo zitapatikana kwa kuzingatia mipango ya utekelezaji wa miradi katika mwaka wa fedha husika. Ni rai ya Kamati kuwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali itatoa fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa ukamilifu na kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kati ya miradi Nane (8) iliyopangwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, miradi miwili ipo katika utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Miradi hiyo inayojumuisha Ujenzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Arusha), ukarabati wa Ubalozi wa Tanzania Pretoria - Afrika Kusini, ukarabati wa Jengo la zamani la Ubalozi wa Washington DC, ujenzi wa makazi ya Ubalozi na jengo la kitega uchumi Adis Ababa, ujenzi na ukarabati wa majengo ya Ubalozi, Makazi ya Balozi na Majengo ya Vitega Uchumi Balozini, ujenzi wa vyumba vya mihadhara Chuo cha Diplomasia na mradi wa kujenga uwezo Wizarani. Ni rai ya Kamati kuwa Wizara itakamilisha taratibu za awali na kuomba fedha Hazina kwa wakati ili kutekeleza miradi iliyokusudiwa.

## SURA YA TANO

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 5.1 Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi kama nilivyoeleza, Kamati inayo maoni yanayojenga msingi wa ushauri nitakaoutoa. Naomba kubainisha maoni hayo kama ifuatavyo:-

i) Kwa muda wa miaka mitatu mfululizo Wizara hii imeshindwa kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wakati kutokana na kutopokelewa kwa fedha za miradi ya maendeleo. Hali hiyo imeathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa miradi iliyopangwa na hivyo kutofikiwa kwa malengo na tija iliyokusudiwa wakati Bunge linaidhinisha Fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

ii) Kuongezeka kwa fedha za miradi ya maendeleo kutakuwa na tija tu ikiwa Wizara itakamilisha taratibu za awali kwa wakati ili kuweza kuomba fedha Hazina na Serikali kutoa fedha hizo kwa wakati na kwa kuzingatia mipango ya utekelezaji wa miradi;

iii) Kitendo cha kushindwa kuanza ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kwa miaka 16 tangu kuingia makubaliano husika na Umoja wa Afrika ni hali ambayo ikiendelea, huenda ikatia doa taswira ya nchi yetu Kidiplomasia hasa katika Umoja wa Afrika na Duniani kujumla;

iv) Baadhi ya nyumba za makazi ya watumishi katika Balozi mbalimbali zimechakaa na hivyo kuathiri hadhi ya Nchi, Balozi na watumishi wetu katika nchi walizopo;

v) Balozi zetu ni moja ya ofisi muhimu katika kuutangaza utalii wa nchi yetu. Hivyo ni muhimu ofisi hizo kuwa na mkakati wa kutangaza utalii wa nchi yetu ikiwa ni sehemu ya kuunga

mkono juhudi za Mheshimiwa Rais katika kutangaza utalii na hivyo kuongeza mapato ya nchi. Ni muhimu sana balozi zetu zikawekewa malengo katika kuutangaza utalii;

vi) Miongoni mwa vipaumbele vya Wizara ni kutekeleza Diplomasia ya Uchumi kwa kuwavutia wawekezaji na wafanyabiashara kutoka nje ya nchi. Diplomasia ya Uchumi bado haijaeleweka kwa ufasaha kwa wananchi na hata viongozi ambao wanasimamia Sekta Mtambuka ambazo zinahusika na uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa. Hili inasababisha nchi kutonufaika ipasavyo na Diplomasia ya Uchumi.

vii) Kuna umuhimu wa Serikali kuendelea kupeleka watumishi balozini kulingana na fani maalum zinazohusika na masuala ya uchumi, uwekezaji na utalii. Kufanya hivyo itakuwa ni sehemu ya nchi yetu kunufaika na Diplomasia ya Uchumi;

viii) Wananchi wana haki ya kunufaika na fursa za kiuchumi na masoko zinazopatikana katika Jumuiya za Kikanda. Tathmini na ufuatiliaji unaonesha kuwa Watanzania hawajanufaika ipasavyo na fursa za kiuchumi na Masoko katika Jumuiya za Kikanda.

ix) Mpango wa ushirikiano wa sekta za umma na sekta binafsi katika ujenzi wa majengo ya ubalozi na vitega uchumi unakabiliwa na changamoto mbalimbali; zikiwemo za kisheria. Hivyo, illi mpango huo uweze kutekelezeka kuna umuhimu wa kuchukua hatua kumaliza changamoto hizo.

### 5.2 Ushauri wa Kamati

i) Ili kuhakikisha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 miradi yote ya maendeleo inatekelezwa kwa wakati; Wizara iweke mkakati maalumu wa kuanza maandalizi mapema wa kukamilisha taratibu zote muhimu za awali zinazohitajika ili

kuanza utekelezaji wa miradi na kuomba fedha Hazina kwa wakati.

ii) Ili kupata tija iliyokusudiwa katika miradi ya maendeleo Serikali itoe fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kuzingatia mpango wa Wizara wa utekelezaji wa miradi husika.

iii) Kutokana na umuhimu wa ujenzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu Serikali itoe fedha zote zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama hiyo. Kufanya hivyo kutawezesha kuanza kutekelezwa kwa mradi huo na kuendelea kujenga taswira nzuri ya kidiplomasia iliyonayo nchi yetu katika Umoja wa Afrika na Duniani kwa ujumla.

iv) Serikali iendelee kutekeleza mkakati maalum wa kukarabati nyumba za watumishi katika Balozi zetu kwa awamu ili nyumba hizo ziendane na hadhi ya Tanzania iliyonayo nje ya nchi.

v) Kamati inapongeza Serikali kwa utekelezaji wa maombi ya Watanzania *(Diaspora)* ambao wamekuwa wakiomba kutambuliwa na Serikali; mchakato huu unaendelea vizuri ikiwa ni pamoja na kuzinduliwa rasmi kwa Mfumo wa kukusanya na kutunza taarifa za Diaspora Kidigitali *(Diaspora Digial Hub)* uliozinduliwa rasmi na Mhe. Dkt. Stergomena L. Taxi (Mb), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki mwezi Mei, 2023. Kamati inashauri mchakato huu ukamilishwe mapema iwezekanavyo ili kuleta tija inayokusudiwa.

vi) Serikali izidishe juhudi katika kuzisimamia Balozi zetu nje ya nchi kutangaza fursa za kitalii na vivutio mbalimbali vilivyopo nchini. Hii iende sambamba na kuhakikisha kunakuwa na mkakati unaotekelezeka utakaoainisha malengo na namna ya kutekeleza malengo hayo katika Sekta ya Utalii kwenye Balozi zetu.

vii) Katika kuhakikisha kuwa nchi inanufaika ipasavyo na Diplomasia ya Uchumi Wizara ikamilishe Mkakati wa Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi katika mwaka wa fedha 2023/2024. Kukamilisha mkakati wa utekelezaji wa Diplomasia ya uchumi pamoja na faida nyingine pia utasaidia Diplomasia ya Uchumi kutekelezwa katika ngazi ya Mkoa na Wilaya.

viii) Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora kwa kushirikiana na Wizara ziandae mkakati wa kupeleka watumishi wenye Fani maalum kwa kuzingatia mahitaji; ikiwemo Fani za Uchumi, Uwekezaji, Utalii na Biashara. Kufanya hivyo kutachochea kasi ya kutafuta wawekezaji na watalii katika Balozi zetu.

ix) Ikiwa ni sehemu ya kutatua changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Serikali iongeze kasi katika kukamilisha Sera ya Mambo ya Nje ambayo imekuwa ikishauriwa na Wabunge katika vipindi tofauti.

x) Serikali iendelee kuhamasisha kimkakati Sekta Binafsi kutumia fursa za biashara na uwekezaji zitokanazo na Mtangamano wa Afrika Mashariki pamoja na Jumuya za Kikanda.

xi) Wizara iendelee kutekeleza Maoni na Mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali ambayo hayajatekelezwa hususan katika Bajeti za miaka mitatu iliyopita ya 2020/2021, 2021/2022 na 2022/2023.

## SURA YA SITA

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao Maoni, Ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba

majina yao kama yalivyoorodheshwa yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard):* -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Vita Rashid Kawawa, Mb | - Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Vincent Paul Mbogo, Mb | - M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Abdi Hija Mkasha, Mb | - Mjumbe |
| 4. | Mhe. Ali Juma Mohamed, Mb | - Mjumbe |
| 5. | Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb | - Mjumbe |
| 6. | Mhe. Cosato David Chumi, Mb | - Mjumbe |
| 7. | Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb | - Mjumbe |
| 8. | Mhe. Dr. Alfred James Kimea, Mb | - Mjumbe |
| 9. | Mhe. Edwin Enosy Swalle, Mb | - Mjumbe |
| 10. | Mhe. Fakharia Shomar Khamis, Mb | - Mjumbe |
| 11. | Mhe. Felister Deogratius Njau, Mb | - Mjumbe |
| 12. | Mhe. Grace Victor Tendega, Mb | - Mjumbe |
| 13. | Mhe. Jafari Wambura Chege, Mb | - Mjumbe |
| 14. | Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb | - Mjumbe |
| 15. | Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb | - Mjumbe |
| 16. | Mhe. Maulid Saleh Ali, Mb | - Mjumbe |
| 17. | Mhe. Minza Simon Mjika, Mb | - Mjumbe |
| 18. | Mhe. Muharami Shabani Mkenge, Mb | - Mjumbe |
| 19. | Mhe. Mwinyikondo Rajab Mustafa, Mb | - Mjumbe |
| 20. | Mhe. Neema Lugangira, Mb | - Mjumbe |
| 21. | Mhe. Nicholaus G. Ngassa, Mb | - Mjumbe |
| 22. | Mhe. Zahor Mohammed Haji, Mb | - Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Dkt. Stagomena L. Tax (Mb), Naibu Waziri Mhe. Balozi Mbarouk Mbarouk (Mb), Katibu Mkuu Balozi Samweli Wiliam Shelukindo pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kuandaa na kukamilisha kazi yake kwa wakati.

Aidha, nawashukuru Ndg. Michael Chikokoto, *ndc,* Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Gerald Magili Mkurugenzi Msaidizi, Makatibu wa Kamati hii Ndugu Omary Magwinza na Bi. Victoria Mizengo wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono Hoja na naomba kuwasilisha.

Vita Rashid Kawawa, Mb
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**
30 Mei, 2023

***Kiambatisho Na. 1***

**UTEKELEZAJI WA MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilijadili Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na kutoa maagizo na ushauri. Ushauri na maagizo hayo yamezingatiwa kama ifuatavyo:-

**a) Chuo cha Diplomasia kisaidiwe kumaliza changamoto za Kimkataba zilizopo baina ya Chuo na Mkandarasi ili kiweze kutekeleza miradi iliyopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Aidha, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ishirikiane na Hazina kuona namna bora ya kupata fedha za ujenzi wa miundombinu ya Chuo hicho**

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Wizara ikishirikiana na Chuo cha Diplomasia kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi ya mwaka 2011 na Kanuni zake za Mwaka 2013 ilisitisha mkataba na Mshauri Elekezi pamoja na Mkandarasi wa awali. Kadhalika, kupitia sheria hiyo na kanuni zake Wizara ilikamilisha michakato ya ununuzi na kukiteua **Chuo Kikuu cha Ardhi** kama Mshauri Elekezi kwa gharama ya shilingi **190,000,000.00**, na kampuni ya ***Corporation Sole Works Superintendent*** kutekeleza ujenzi wa mradi wa vyumba vya mihadhara kwa gharama ya shilingi **4,450,359,568.80**. Hata hivyo kazi hii haijaanza, na majadiliano yanaendelea kati ya Wizara na Wizara ya Fedha na Mipango ili kutengewa kiasi hicho cha fedha.

**b) Ili kufanikisha utekelezaji wa Ilani ya CCM inayoelekeza uwekezaji katika ujenzi na ununuzi wa majengo nje ya nchi kwa ajili ya balozi zetu, uandaliwe Mpango mkakati wa kufanikisha jambo hilo. Mpango huo, uoneshe namna ya kuishirikisha sekta binafsi katika uwekezaji kwenye ujenzi na ununuzi wa majengo hayo. Aidha, katika ujenzi na ukarabati wa majengo kwenye balozi zetu mbalimbali Serikali ihakikishe kuwa:-**

i) Balozi zetu zinapata Hati ya kiwanja kinachohusika kabla ya kuendelea na upangaji na utekelezaji wa mradi;

ii) Ubalozi unapata ufafanuzi kuhusu mpango wa matumizi ya viwanja katika maeneo yanayohusika kabla ya kuamua kuwekeza katika kiwanja hicho; na

iii) Ubalozi unaandaa mkakati wa kimasoko kwa ajili ya kulitangaza jengo linalohusika ili mradi utakapokamilika uweze kuwa na tija;

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Wizara inao Mpango Mkakati wa Kujenga, Kununua na Kukarabati Majengo Balozini wa Miaka 15 (2017/2018 – 2031/2032) ambao unatumika kama mwongozo wa kuendeleza viwanja kwa kujenga majengo ya ofisi, vitega uchumi, makazi ya watumishi pamoja na kukarabati majengo yaliyopo. Mpango huo umeainisha yapo majengo 47 yanayohitaji ukaratabati mkubwa, majengo 9 yanayohitaji kuvunjwa na kujengwa upya na viwanja 11 kujengwa. Kati yake 4 ni ajili ya Balozi na Makazi na 7 ni kwa ajili ya vitega uchumi. **Kiambatisho Na. 1**. Katika kutekeleza Mpango Mkakati huo, Serikali hutenga fedha kila mwaka katika bajeti ya maendeleo ya Wizara kwa ajili ya kutekeleza Mpango huu kulingana na uhalisia wa bajeti. Kulingana na mpango huu, ujenzi na ukarabati unaendelea katika Balozi zifuatazo: Washington (Jengo la Zamani la Ofisi za Ubalozi); Stockholm (Makazi ya Balozi na Makazi ya Mkuu wa Utawala); na Brussels (Makazi ya Balozi na Ofisi za Ubalozi). Aidha, ukarabati umepangwa kuanza katika Balozi za Khartoum (Makazi ya Balozi na Ofisi za Ubalozi); na Pretoria (Ukarabati wa majengo manne ya Ubalozi).

***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Aidha, Wizara imefanya mazungumzo na Taasisi za fedha kama vile Benki ya CRDB na NMB pamoja na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Taasisi za umma kama vile NSSF, PSSSF, WCF, WHI, na NHC ili kuingia ubia wa kutekeleza miradi ya ukarabati na ujenzi wa majengo ya Serikali Balozini, Katika mazungumzo hayo, Taaisi zimeonesha nia ya kuingia ubia na Wizara kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati katika Balozi za Nairobi – Kenya (NSSF); Kinshasa – Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (NSSF na CRDB); Muscat – Oman (NHC na NMB); Addis Ababa – Ethiopia (NHC na NMB); Kampala –

Uganda (WHI, PSSSF na WCF); Bujumbura – Burundi (CRDB); Abuja – Nigeria (NHC na NMB); London – Uingereza (CRDB, WCF, WHI na NHC); New York – Marekani (CRDB); na Geneva – Uswisi (NMB). Pamoja na nia iliyoonyeshwa, utekelezaji haujaanza kutokana na changamoto kadhaa zilizobainika ikiwa ni pamoja na, kubadilisha matumizi ya maeneo kutoka shughuli za kibalozi kwenda kwenye shughuli za kibiashara huhitaji ridhaa ya nchi mwenyeji. Katika kutekeleza hitaji hili katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Wizara imeweza kupata ridhaa ya mamlaka ya Serikali ya Zambia jijini Lusaka ya kubadili matumizi ya viwanja nane (8) vya Ubalozi kwa ajili ya kutekeleza miradi kumi (10) ya Kimkakati ya ujenzi wa majengo ya makazi na ofisi kwa ajili ya matumizi ya kibiashara.

***Mheshimiwa Mwenyekiti***, ili kukabiliana na changamoto hizo, Wizara iliunda Kamati ya Wataalmu iliyojumuisha Sekta ya Umma (Wizara na Wizara ya Fedha na Mipango), na sekta Binafsi (CRDB, NMB, NSSF, PSSSF, Ardhi) ili kuchambua na kutoa mapendekezo. Kamati hiyo imetoa mapendekezo yafuatayo, ambayo yanafanyiwa kazi:

i) Wizara iunde kampuni itakayosimamia uendelezaji wa milki zake na usimamizi wa vitega uchumi vya Serikali nje ya nchi. Kampuni hiyo iundwe ifikapo mwezi Julai 2023 ili iweze kusimamia na kuendeleza miradi iliyopangwa kutekelezwa. Pamoja na mambo mengine, kampuni hiyo itakuwa na majukumu yafuatayo:-

(a) Kusimamia na kuendesha miradi ya vitega uchumi iliyopendekezwa;

(b) Kutafuta vyanzo mbadala vya fedha kwa ajili ya kugharamia miradi balozini; na

(c) Kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuchangia katika bajeti ya Wizara ya ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi ya watumishi balozini ambayo uendeshaji wake siyo wa kibiashara.

ii) Wizara ihuishe muundo wake ili Sehemu ya Uratibu na Usimamizi wa Milki iwe kitengo kinachojitegemea kitakachokuwa na wataalam wenye sifa na ujuzi wa kusimamia uendelezaji wa milki

za Wizara. Wataalamu waliopo waendelee kujengewa uwezo kwenye maeneo yao ya uweledi kupitia mafunzo stahiki. Aidha, kitengo hiki kitakuwa na jukumu la kuisimamia (oversight) kampuni itakayoanzishwa kwa kuwa vitega uchumi na milki nyinginezo zitabaki kuwa chini ya usimamizi wa Wizara. Vile vile kitengo hicho kitakuwa na jukumu la kuandaa sera na miongozo mbalimbali kuhusu uendelezaji, usimamizi na utunzaji wa milki za Wizara. Mapendekezo ya Kamati ni Muundo wa Wizara uhuishwe ifikapo Julai 2023;

iii) Kwa kuwa Wizara haina fedha za kuandaa maandiko yanayotakiwa, maombi maalum ya fedha kiasi cha shilingi 2,000,000,000 yawasilishwe Serikalini kugharamia maandalizi ya maandiko ya miradi ya kipaumbele;

iv) Wizara iombe kibali maalum cha kulegezwa (waiver) kwa maeneo saba (7) ya sheria, kanuni na taratibu za ndani zinapunguza ufanisi katika utekelezaji na ugharamiaji wa miradi ya uendelezaji wa viwanja na ukarabati wa majengo ya serikali nje ya nchi;

v) Wizara itumie vyanzo mbadala vya kugharamia utekelezaji wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa majengo Balozini kwa kutafuta wabia/wafadhili mbalimbali kutoka sekta ya umma na Sekta Binafisi. Katika kufanikisha pendekezo hili, kamati imeweza kupendekeza jumla ya miradi kumi (10) ya kipaumbele ya ujenzi na ukarabati majengo balozini itakayotekelezwa kwa njia ya ubia na kwa njia mikopo ya masharti nafuu isiyokuza deni kuu la serikali. Miradi hiyo na wabia walioonesha nia ya kugharamia ni katika Balozi za Nairobi – Kenya (NSSF); Kinshasa – Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (NSSF na CRDB); Muscat – Oman (NHC na NMB); Addis Ababa – Ethiopia (NHC na NMB); Kampala – Uganda (WHI, PSSSF na WCF); Bujumbura – Burundi (CRDB); Abuja – Nigeria (NHC na NMB); London – Uingereza (CRDB, WCF, WHI na NHC); New York – Marekani (CRDB); na Geneva – Uswisi (NMB). Mpango kazi ulioandaliwa umelenga utekelezaji wa miradi hiyo uanze Mwezi Julai 2023.

vi) Kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia masuala ya bajeti na matumizi ya fedha za umma, mipango na bajeti ya Serikali inayoidhinishwa na Bunge hujumuisha makadirio ya makusanyo ya fedha kutoka vyanzo vyote ikiwemo vyanzo vitokanavyo na mikopo, ubia na/au misaada mbalimbali. Hivyo, Kamati imependekeza fedha zitakazotokana na vyanzo mbadala kutekeleza miradi iliyoainishwa, ijumuishwe katika Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ili kukidhi matakwa ya kisheria na

vii) Wizara iruhusiwe kubakisha sehemu ya sehemu ya maduhuli (Retention) yanayokusanywa kutoka kwenye majengo ya vitega uchumi Balozini kugharamia ukarabati na matengenezo ya majengo hayo. Hatua hiyo itasaidia kulinda hadhi ya majengo hayo na hivyo kuhifandhi wateja waliopo na kuendelea kuvutia wapya.

***Mheshimiwa Mwenyekiti***, vilevile kutokana mazungumzo kati ya Serikali yetu na Serikali ya Ethiopia, Tanzania imerejeshewa viwanja viwili vilivyochukuliwa na Serikali hiyo vyenye Hati Na. 04/007/22827 cha ukubwa wa mita za mraba 2000 na Hati Na. 04/006/19855 cha ukubwa wa mita za mraba 1,414 jijini Addis Ababa kwa masharti ya kuanza ujenzi ndani ya miezi tisa tangu Mwezi Februari 2023. Wizara inaendelea na mipango ya kuendeleza viwanja hivyo kwa ubia na NHC wakishirikiana na Benki ya NMB ndani ya muda uliotolewa.

**c) Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango iandae Mkakati Maalum wa kukarabati majengo ya Balozi kwa awamu ili yaendane na hadhi ya Tanzania iliyonayo nje ya nchi.**

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** maelezo kuhusu agizo hili ni kama ilivyoelezewa katika aya ya 9 hapo juu ambapo Wizara iliunda Kamati ya Wataalmu iliyojumuisha Sekta ya Umma (Wizara na Wizara ya Fedha na Mipango), na sekta Binafsi (CRDB, NMB, NSSF, PSSSF, Ardhi) ili kuchambua na kutoa mapendekezo. Kamati hiyo imetoa mapendekezo ambayo yanafanyiwa kazi.

d) **Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali ziandae utaratibu maalum wa kuwa na Database ya wanafunzi wa Kitanzania wanaokwenda kusoma nje ya nchi, pamoja na Watanzania wanaoishi nje ya nchi.**

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Wizara kupitia Balozi zake nje inaendelea kuhamasisha wanafunzi wote wa Kitanzania waliopo nje ya nchi kuhakikisha wanajiandikisha katika Ofisi za Balozi zetu. Kwa sasa Wizara imeendelea kutengeneza Mfumo wa Kukusanya na Kutunza Taarifa za Diaspora Kidigitali (*Diaspora Digital Hub*) pamoja na wanafunzi wa kitanzania wanaokwenda kusoma nje ya nchi. Hadi kufikia Mwezi Juni 2023, Wizara itakuwa imekamilisha kutengeneza Mfumo huo ambao utaiwezesha Serikali kupata takwimu sahihi za idadi ya Diaspora, mahali walipo, ujuzi na uzoefu walionao. Mfumo huo utaiwezesha Serikali kupata takwimu sahihi za mchango wa Diaspora na kuwawezesha Diaspora kupata taarifa na huduma mbalimbali nchini.

e) **Serikali izidishe juhudi katika kuzisimamia Balozi zetu nje ya nchi kutangaza fursa za kitalii na vivutio mbalimbali zilizopo nchini kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii.**

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Wizara kupitia Balozi zetu nje ya nchi imeendelea kutangaza fursa zetu ikiwemo vivutio vya utalii, biashara na uwekezaji. Vilevile, katika kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Mheshimiwa Rais, Wizara imechukua jitihada za kutafsiri Filamu Maalum ya ***Tanzania the Royal Tour*** katika lugha mbalimbali na kuiweka kwenye tovuti za Balozi za Tanzania. Jitihada hizi zimewezesha kuongeza biashara na kuvutia uwekezaji katika sekta mbalimbali na pia kuvutia watalii.

f) **Wizara ianze mapema michakato ya kukamilisha taratibu zote muhimu ili kuhakikisha miradi ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 inatekelezeka kwa ukamilifu.**

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara ilitengewa kiasi cha shilingi 4,700,000,000 kwenye Fungu la Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 700,000,000 ni kwa ajili ya

Ukarabati wa majengo manne (4) katika Ubalozi wa Tanzania Pretoria na shilingi 4,000,000,000 zimetengwa kwa ajili ya Ujenzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu eneo la Lakilaki jijini Arusha.

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Majengo yanayokusudiwa kukarabatiwa katika ubalozi wa Tanzania Jijini, Pretoria ni yafuatayo:-

i) Jengo la Ofisi za Ubalozi, 822 George Avenue- Acardia – Pretoria;

ii) Jengo la Makazi ya Balozi, 318 Aries Street Waterkloof- Pretoria;

iii) Jengo la Makazi ya Mkuu wa Utawala (HOC), 818 Jacques Street – Molerata Park, Pretoria; na

iv) Jengo la Makazi ya Mwambata Utawala (AA), 845 Government Avenue- Acardia Pretoria.

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** kufuatia zabuni iliyotangazwa kumpata Mkandarasi Kampuni ya TS Solutions SA Pty ya Afrika Kusini ilishinda kwa gharama ya Dola za Marekani 523,561.43 sawa na takriban shilingi 1,293,950.000.00 (pamoja na kodi). Mkataba wa Ukarabati kati ya Wizara na Mkandarasi utasainiwa tarehe 29 Machi 2023 na Kazi ya ukarabati kuanza rasmi tarehe 15 Aprili 2023.

***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Mradi wa ujenzi wa Mahakama ya Afrika ya haki za Binadamu na Watu eneo la Lakilaki Jijini Arusha utahusisha ujenzi wa majengo yafuatayo:

i. Jengo Kuu;
ii. Mgahawa na Eneo la Mazoezi;
iii. Ukumbi wa Mikutano na Vyumba vya Mihadhara;
iv. Zahanati na Duka la Dawa;
v. Kituo cha Kulelea Watoto; na
vi. Karakana na Kituo cha Mafuta.

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Wizara imekamilisha kazi ya usanifu wa majengo yanayokusudiwa kujengwa kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa

Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu katika eneo la Lakilaki jijini Arusha. Kufuatia kukamilika kwa usanifu, tarehe 6 Machi 2023, Wizara ilitangaza zabuni ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi ambapo zabuni inatarajiwa kufunguliwa tarehe 28 Machi 2023. Mkandarasi wa kutekeleza ujenzi huo anatarajiwa kupatikana mwezi Aprili 2023.

**g) Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine iandae Mkakati unaotekelezeka wa kutoa elimu juu ya Diplomasia ya Uchumi na namna inavyotekelezwa kwa vitendo. Mkakati huu uende sambamba na kupeleka Wataalamu wa Diplomasia ya Uchumi katika sekta muhimu kwa uwekezaji na biashara.**

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Wizara inaendelea na maandalizi ya Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi. Zoezi hili limeanza kwa kufanya tathmini ya utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi. Mkakati huo utajumuisha Sekta mbalimbali kwa kuainisha maeneo muhimu ya kisekta katika utekelezaji wa Dipolomasia ya Uchumi, wadau husika (Sekta ya Umma na Sekta Binafsi) na nyanja ya elimu kwa umma. Mkakati huu unatarajiwa kukamilika kufikia mwezi Desemba, 2023.

**h) Ofisi ya Rais Manejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kushirikiana na Wizara ziandae Mkakati wa kupeleka watumishi wenye fani husika katika Balozi.**

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Wizara mwaka 2020 ilifanya tathmni ya mahitaji ya watumishi balozi na Kuanza mahitaji wa watumishi 116 na watumishi 33 walirejea nyumbani na hivyo kuwa na mahitaji ya jumla ya watumishi 149. Katika Mwaka wa Fedha 2021/22 jumla ya Watumishi 138 wa kada mbalimbali wamepelekwa Balozini kulingana na mahitaji ili kuimarisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi katika Balozi zetu. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Manejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora itaendelea kuhakikisha kuwa watumishi zaidi wanapelekwa Ubalozini kwa kuzingatia weledi na mahitaji.

**i) Ili kutatua baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji, Serikali ikamilishe Mchakato wa kuandaa Sera ya Mambo ya Nje katika Mwaka wa fedha 2022/2023**

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Marejeo ya Sera ya Mambo ya Nje yanaendelea. Kufuatia maoni ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, kuwa hakuna haja ya kutunga Sera Mpya kwani misingi ya Sera bado ni ile ile. Wizara imeendelea kurejea Sera iliyopo ili misingi hii iendane kwa matakwa ya sasa. Uchambuzi umekamilika, Rasimu inatarajiwa kuwasilishwa kwenye
Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri hapo tarehe 15 Aprili 2023 ili ianze kujadiliwa.

**j) Serikali iendelee kuhamasisha sekta binafsi kutumia fursa za biashara na uwekezaji zitokanazo na Mtangamano wa Afrika Mashariki pamoja na Jumuiya za Kikanda.**

***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Serikali kupitia Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, imeendelea kuelimisha Watanzania kuhusu fursa mbalimbali zitokanazo na Mtangamano wa Kikanda. Jitihada hizi zimewezesha watanzania wengi zaidi kuzifahamu fursa za biashara na uwekezaji zilizopo katika Jumuiya za Kikanda.

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** kama nilivyoeleza katika utangulizi, majukumu ya Wizara ni kuratibu ushirikiano wa Kikanda, hivyo utekelezaji unahusisha Wizara na Taasisi mbalimbali kuhusiana na utumiaji wa fursa za kibiashara na uwekezaji. Ni matumaini ya Wizara kuwa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biasharaa itaweza kutoa takwimu kadri itakavyohitajika.

**k) Wizara iendelee kutekeleza maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali ambayo hayajatekelezwa.**

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Ninaomba nikuhakikishie kwamba Wizara itaendelea kutekeleza maoni na mapendekezo ya Kamati yanayotolewa katika vipindi mbalimbali. Aidha, ninapenda kuipongeza na kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya

Nje, Ulinzi na Usalama (NUU) kwa kuendelea kuishauri Wizara katika kuboresha na kuimarisha utendaji kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa kwa wasilisho hilo, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na shughuli zetu tunao wageni ambao wameingia Bungeni muda huu. Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni wa Mheshimiwa Ally Makoa ambao ni wanafunzi 52 na walimu watatu wa *Embeko Lutheran* Sekondari kutoka Dodoma, karibuni sana wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Wapo wageni 58 wa Mheshimiwa Justin Nyamoga, walimu na wanafunzi wa *Range Primary School* kutoka Mkoa wa Iringa, wako pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 15 na mwalimu kutoka Shule ya Msingi Amani ya Jijini Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Pia tunao wanafunzi 10 na mwalimu mmoja kutoka Shule ya Msingi Makole Jijini Dodoma pia, karibuni. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 15 na walimu watatu kutoka Shule ya Msingi Msabangalale kutoka Jijini Dodoma wale pale juu, karibuni sana wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 30 na walimu wawili kutoka Shule ya Sekondari Viwandani ya Jijini Dodoma, karibuni sana wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wanafunzi tisa na mwalimu mmoja wa Shule ya Sekondari Sechelela ya Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunae mwanafunzi wa kidato cha tano kutoka Shule ya Sekondari *St. Joseph* ya Jijini Dar es Salaam, Ndugu Debora Marandu, karibu sana mwanafunzi wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Dkt. Kimei ambao hawakuwa wamepata nafasi, washindi wa *Vunjo Cup* ya mwaka 2022, timu ya Kata za Makuyuni na Njia Panda, makocha wa timu ambao ni Ally Msangi na Lawrence Stanley, wale pale karibuni sana. *(Makofi)*

Viongozi wa timu nne, Afisa Mtendaji wa Kata ya Njia Panda, viongozi wa UVCCM wa Kata wote kwa pamoja, wawakilishi wa mashirika ya ufadhili wa *Help Age,* wote hao ni wageni Mheshimiwa Dkt. Kimei ambao ni Ndugu Yunis Temu na Sadam Mosha, pia Katibu wa Mbunge yuko hapa, karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Dkt. Kimei. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo sasa tunaanza uchangiaji wetu wa taarifa hii ya leo. Tunaanza na Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Kabudi, Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mheshimiwa Fakharia Shomar ajiandae.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim kwa kuturuzuku uhai na kutujalia afya ya kukutana leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Nshirikiano wa Afrika Mashariki. Nichukue hatua hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa *Diplomat Number One* kwa kuimarisha sauti ya Tanzania katika medani ya uhusiano wa Kikanda na Kimataifa pia kwa msukumo mkubwa aliouweka katika diplomasia ya uchumi na matunda ya juhudi hizo yako dhahiri kwetu sote. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza *diplomat number two* Mheshimiwa Dkt. Stergomena Lawrence Tax, Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa umahiri alioudhihirisha katika kuendeleza na kuimarisha diplomasia ya

Tanzania, leo kwa hotuba yake ya kwanza katika Bunge hili aliyoitoa kwa ustadi na umahiri mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja naye nawapongeza Naibu Waziri Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, Katibu Mkuu Balozi Dkt. Samwel William Shelukindo, Naibu Katibu Mkuu Balozi Tatma Mohammed Rajab na watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri mnayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo mawili ambayo na mimi ningependa niongeze sauti yangu na Wizara imeyafanya vizuri sana. Moja ni eneo la *diaspora* na la pili ni eneo kuhusu diplomasia ya utamaduni *(cultural diplomacy)* ikiwa ni sehemu na nguzo muhimu ya diplomasia ya uchumi *(economic diplomacy)*. Hapa nikiazima maneno ya Prof. Ali Mazrui, diplomasia ya utamaduni itatupa *soft power* ambayo yeye aliita *Parks Tanzaniana* akituweka katika kundi moja na *Parks Americana* na *Parks Britannica.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Uhusiano wa Afrika Mashariki kwa kuanzisha hii *digital hub* ya kuwaandikisha *diaspora*. Hatua hiyo ni hatua muhimu sana ya kuwasajili *diaspora* wote wa Tanzania walioko nje ili tuweze kujua wako wapi, wanafanya nini na kujua mchango wanaoweza kuutoa katika maendeleo ya uchumi na kijamii ya nchi yetu, hiyo itaiwezesha Serikali kuwa na mkakati wa kushirikisha *diaspora* ya Tanzania katika maendelo ya uchumi na jamii ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalisema hili mimi mwenyewe nikiwa na uzoefu kwa kuwa nimeishi Ujerumani kwa miaka tisa, siku sita na siku tatu. Kwa hiyo hii hatua ni muhimu na ninaipongeza sana na niwashukuru washiriki wote ambao wamewezesha Wizara kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naipongeza Wizara kwa kuwa katika hatua za mwisho za maandalizi ya kuwapatia hadhi maalumu watu wenye asili na nasaba ya Tanzania ambao wameacha kuwa raia wa Tanzania baada ya kuchukua uraia wa nchi nyingine. Hiyo itakuwa ni hatua muhimu ya kuondoa usumbufu na changamoto za

watu hawa wanazozipata hasa wanaporejea nyumbani kuja kuona ndugu zao au kufanya shughuli nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la hadhi maalumu ndilo lenye muafaka hapa Tanzania, nami nasema ni bora kama wanavyosema waswahili ni bora kenda mkononi kuliko kumi porini. Sasa tuna kenda mkononi ambayo ni hadhi maalumu. Mimi ningeomba Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje pia Wizara ya Mambo ya Ndani ikamilishe jambo hili ili hawa wenzetu waweze kupata hadhi maalumu waondokane na usumbufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni bora kuliko lile ambalo tunaendelea kulisema na tunajua bado halina muafaka, suala la uraia pacha bado halina muafaka hapa nchini lakini halina muafaka duniani, kwa hiyo tushikilie hili ambalo tuna muafaka nalo tulisukume kwa haraka ili liende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti nilioufanya huko duniani ni asilimia 49 tu ya nchi duniani zinaruhusu uraia pacha na asilimia 51 duniani hazirihuisu uraia pacha. Utaona asilimia 51 bado haziruhusu uraia pacha, maana yake jambo hili hata katika ngazi ya dunia bado halijapata muafaka. Hii ni pamoja na nchi ambazo tuna uhusiano nao wa karibu ambapo wako Watanzania wenye asili ya nasaba ya Tanzania bara, asili ya nasaba ya Tanzania Zanzibar ambao wako Oman. Oman hairuhusu uraia pacha, Saudi Arabia hairuhusu uraia pacha, lakini pia ziko nchi ambazo zina *diaspora* wengi sana duniani ambazo pia haziruhusu uraia pacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni India, ina *diaspora* wengi sana nje lakini katika Katiba yake imekataza kabisa uraia pacha lakini imekuja na hadhi maalumu kuwatambua watu wanaowaita *Persons of India Origin* au *Overseas Indians* ambao wanapewa kitambulisho na wanakuwa na haki zote. Nchi nyingine ya kiafrika ambayo ina *diaspora* wengi sana duniani Ethiopia, ina *diaspora* karibuni milioni tatu Marekani na Ulaya na yenyewe pia haikubali uraia pacha, lakini inatoa kitambulisho maalumu kwa waethiopia waliokuwa nje, ambao wakirudi nchini kwao Ethiopia wanakuwa na haki zote ambazo wanazihitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika nchi za Umoja wa Ulaya. *(Europian Union)*. Nchi 15 zinakubali uraia pacha, nchi 12 hazikubali uraia pacha na ambazo hazikubali uraia pacha ni pamoja na Ujerumani, Uholanzi, Austria na Denmark. Kwa upande wa Ujerumani, wao hata mtoto aliyezaliwa Ujerumani na watu ambao siyo raia wa Ujerumani hapewi hadhi yoyote, ndiyo maana baadhi ya sisi ambao watoto wetu wamezaliwa Ujerumani tuliporudi hapa walivyofikisha miaka 18 tulipoambiwa twende Ubalozini kuomba wakane uraia wa Ujerumani, Wajerumani walishangaa kwa sababu toka walipozaliwa wao hawakuwa raia wa nchi hiyo, kwa sababu kwa Wajerumani uraia ni damu. Aina yao ya uraia ni *Jus Sanguinis* ni uraia wa damu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hapa Tanzania suala la uraia pacha lina hisia kali, *it is an emotive issue*. Katika utafiti nilioufanya nimeona kwamba Bunge Oktoba Mwaka 1960 wakati tuna Serikali ya Madaraka, ulileta Muswada Bungeni kuhusu uraia wa Tanganyika na aliyekuwa Waziri Kiongozi wa wakati huo au *Chief Minister* Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na hiyo iliwekwa kwenye *Hansard* katika suala la uraia, lilileta msuguano mkubwa na hasa baada ya kuwa mwaka 1958 Waingereza walipotupa masharti ya uchaguzi wa kura tatu. Kila Jimbo liwe lina Mbunge Mzungu, Muafrika na Muasia na kundi kubwa la vijana wa *TANU,* kujitoa *TANU* na kuunda Chama Cha *African National Congress of* Tanganyika wakisema Tanganyika ni kwa Waafrika tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu aliyasema haya Tarehe 28 Oktoba Mwaka 1961 katika Hansard na naomba nimnukuu na ndiyo msingi wa kwa nini uraia pacha Tanzania haukukubalika wakati huo. *"Now Sir, what we are trying to do, we are establishing a citizenship of Tanganyika, what is going to be the best of this citizenship of Tanganyika. We, the Government* kwa sababu alikuwa *Chief Minister, elected by the people of Tanganyika say loyalty to the country is going to be the basis of determining the citizenship of Tanganyika. In order to be certain as far as human responsible to be certain, the citizens of Tanganyika are going to be loyal to Tanganyika and Tanganyika only. We have said although other countries do accept it, we are not going to accept dual citizenship in Tanganyika"* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni maneno ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akiwa Waziri Kiongozi katika Bunge la Tanganyika, Bunge la Madaraka tukijiandaa kupata uhuru wa nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Prof. Palamagamba Kabudi.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea nilimtaja Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, ajiandae.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje. Kwanza kabisa napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada kubwa alizoweka za kubeba ajenda ya diplomasia ya uchumi na tayari tumeona matokeo chanya katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nitajikita eneo hili la diplomasia ya uchumi. Tunaposema na diplomasia ya uchumi ina maeneo mengi na mimi kwa muktadha wa mchango huu nitagusia maeneo matano. Eneo la kwanza ni ziara za viongozi wetu wa Kitaifa kwenda nje ya nchi. Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara hizi zimeleta mafanikio makubwa ambayo tumekuwa tukiyaona, jambo ambalo bado linahitaji litiliwe mkazo na liimarishwe ni namna gani Wizara ya Mambo ya Nje, itatupa taarifa ya utekelezaji wa yale mambo makubwa na mafanikio yanayotokana na ziara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni uwekezaji kutoka nje ya nchi. Kupitia diplomasia ya uchumi Tanzania imefunguka na tumekuwa tukiona wawekezaji wengi wakija Tanzania, lakini jambo

ambalo bado linahitaji kutiliwa mkazo ni kituo chetu cha uwekezaji - *TIC* bado hakina mamlaka ya kutoa huduama ya *one stop center,* kwa muktadha huo wawekezaji wanakuwa wanakuja ndani ya nchi wakiwa na matarajio ya yale ambayo yalikubaliana katika aidha *TIC* au kupitia ziara za viongozi wetu, lakini wanapokuja hapa nchini kunakuwa na mkanganyiko baina ya yale yaliyokubaliwa pamoja na utekelezaji aidha ngazi ya Tawala za Mikoa au Serikali za Mitaa kwa maana ya Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hapa tunahitaji kuweka jitihada za maksudi kabisa ili kuhakikisha kwamba uwekezaji wa kutoka nje ya nchi wanapokuja hapa nchini mambo yawe mororo kusiwe kuna vikwazo au mkwamo wa aina mabalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ni biashara kati ya Tanzania na nchi zingine. Nawapongeza sana Wizara ya Mambo ya Nje, tumekuwa tukiona kila ziara za Wakuu wetu wa nchi sekta binafsi pia inakuwa inashiriki. Naomba nisisitize ushirikishwaji na ushiriki wa sekta binafsi hautakiwi kuwa tu pale ambapo kuna ziara za viongozi wetu wakuu, bali lazima tuweke jitihada za kuhakikisha kwamba sekta binafsi inatambua fika fursa zilizoko nje ya nchi na sekta binafsi kule nchi za nje na wenyewe wanatambua fursa zilizoko ndani ya Tanzania ili Wizara ya Mambo ya Nje iendelee kuwa kiungo baina ya sekta binafsi nchini Tanzania na sekta binafsi nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu Wizara hii ya Mambo ya Nje inaifungulia njia Tanzania duniani, lakini utekelezaji wa mambo mengi yanafanyika kwenye Wizara za kisekta, hapa ndipo iko changamoto bado hakuna mkakati thabiti wa namna gani ambavyo Wizara ya Mambo ya Nje itaendelea kusimamia utekelezaji wa fursa mbalimbali. Utekelezaji wa maazimio mbalimbali katika Wizara zingine za kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la nne ni misaada kwa ajili ya maendeleo ya jamii. Tumekuwa tukiona kupitia ziara za viongozi wetu, Wakuu wa Nchi, pia tumekuwa tukiona kupitia ziara za Wakuu wa Nchi zingine wanapokuja hapa Tanzania. Zinatolewa rasilimali fedha kwa maana ya misaada kwa ajili ya maendeleo ya jamii, lakini jambo

ambalo bado linahitaji kutiliwa mkazo ni fedha zile za misaada bado utekelezaji wake zinakabidhiwa katika mashirika yasiyo ya kiserikali kwa maana *NGO's* za nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Wizara hii inalo jukumu la kuona namna gani ambavyo wanaweza wakaisemea sekta ya *NGOS* za Tanzania, ili asilimia kubwa, zile rasilimali fedha zinazoingia Tanzania ziweze kutekelezwa na sekta ya *NGOS* za Tanzania. Kwa kufanya hivyo ndivyo ambavyo tutajihakikishia kwamba misaada inayoingia nchini inafanya kazi kwa kulinda na kwa kuzingatia misingi ya mila, desturi, tamaduni pamoja na yale ambayo yako kwenye Katiba yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili naamini kabisa halipaswi kuachiwa kwenye Wizara za kisekta kwa sababu, Wizara ya Mambo ya Nje ndiyo inaweza ikajadiliana na nchi nyingine kwa kutumia diplomasia ya uchumi kuona namna gani ambavyo fedha hizi za misaada zinapoingia nchini, basi *NGOS* za Tanzania ziweze kupata jukumu la kutekeleza ili kulinda; moja, ajira za Tanzania; na pili, fedha hizi ziendelee kuzunguka katika mnyororo wa thamani wa uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tano ni suala la masomo na ajira za nje ya nchi. Tumesikia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri pamoja na hotuba ya Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu suala la *diaspora*. Tunapoongelea *diaspora* kuna Watanzania wenye uraia wa Tanzania, kuna Watanzania ambao wana asili ya Tanzania, lakini wana uraia wa nchi nyingine na kuna Watanzania ambao wako masomoni nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara, imezindua *Diaspora Digital Hub* tarehe 22 mwezi wa tano. Hii itatuwezesha kujua idadi halisi ya *diaspora* tulionao na wana taaluma zipi? Halikadhalika, liko jambo ambalo bado Wizara hii inahitaji kufanya. Nikiongelea kwa upande wa masomo, wapo vijana ambao wanapata fursa za masomo na wanapata fursa za *scholarship* kwa maana ya ufadhili wa masomo, lakini vijana hawa wanapoomba *visa* wanapata changamoto na wanajikuta wananyimwa *visa*. Sasa wanaponyimwa

*visa* wakati wamekidhi vile vigezo vya msingi, kijana huyu anakuwa hana pa kwenda. Napendekeza Wizara hii ione namna gani ambavyo itasaidia vijana ambao wanakidhi vigezo vya msingi wasinyimwe fursa ya kupata masomo nje ya nchi pasipo sababu maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija pia kwenye ajira. Lazima kama Tanzania, maadamu tumeamua kuingia kwenye diplomasia ya uchumi, lazima tuangalie kada zipi ambazo sisi kama Tanzania tuna ujuzi nazo; na ni nchi zipi ambazo zinahitaji kada hizo; ili Wizara hii ya Mambo ya Nje iweze kujadiliana kupitia diplomasia ya kiuchumi, Tanzania itaweza kupata kada zipi katika nchi hizo? Kwa kufanya hivyo, tutaweza kupata diplomasia ya uchumi kwa maana ya kuwa na ajira ya Watanzania wengi zaidi ambao wanafanya nchi za nje, kwa mfano, kwenye kada ya Udaktari, Unesi, Ualimu, na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina zaidi ya wananchi milioni 60. Kwa takwimu ambazo zilitajwa mapema mwaka huu hapa Bungeni, tunao *diaspora* 1,500,000 tu. Kwa nchi yenye wananchi milioni 60, bado hapa tunahitaji kuweka jitihada za nguvu zaidi ili kuhakikisha tunaongeza tija ya Watanzania ambao wako nje ya nchi, na ziko fursa nyingi katika ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kwenye ajira, nitilie mkazo umuhimu wa Wizara hii ya Mambo ya Nje ione namna gani ambavyo Watanzania watapata fursa za ajira katika mashirika ya kimataifa. Miaka ya nyuma tulikuwa tuna Watanzania wengi sana kwenye mashirika ya kimataifa, nami naamini kupitia jitihada za makusudi kabisa za Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, tutaweza kupata fursa hizi za ajira kwenye mashirika ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kumteua Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula kuwa mgombea wa nafasi ya Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola. Hii ni nafasi nyeti sana. Hivyo, naiomba sana Wizara ya Mambo ya Nje, kupitia balozi zake na *machineries* nyingine tuweke jitihada kubwa kuhakikisha tunapata fursa hizi za ajira. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja tu ya kuhitimisha. Naomba niishauri Wizara hii ianzishe kurugenzi ya fursa ili kurugenzi hii itoe fursa kwa Watanzania, Watanzania waweze kuelewa fursa pamoja na sekta binafsi. Wizara hii itoe elimu kwa Watanzania tuweze kuelewa diplomasia ya uchumi maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado suala hili halieleweki ndani ya Serikali, Taasisi za Serikali, katika Halmashauri zetu, sekta binafsi na hata na sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha. Suala hili la hadhi maalum, nawapongeza sana Serikali kwa hatua ambazo wamechukua, lakini naomba sana tulinde kwa wivu mkubwa suala la ushiriki kwenye masuala ya kisiasa pamoja na ajira kwenye vyombo vya ulinzi na usalama. Ajira hizi na ushiriki wa kisiasa lazima ulindwe na uwe ni kwa ajili tu ya Watanzania. Haiwezekani mtu mwenye uraia wa nchi nyingine apate fursa ya kushiriki kwenye shughuli za kisiasa au apate fursa ya kupata ajira kwenye vyombo vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Serikali na Wizara hii, tulinde maeneo haya mawili kwa wivu mkubwa. Masuala ya kushiriki katika siasa, masuala ya ajira katika vyombo vya ulinzi na usalama, hizi zilindwe ni kwa ajili ya Watanzania na Watanzania pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Neema. Tunaendelea na Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, atafuatiwa na Mheshimiwa Fakharia Shomari na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ajiandae.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wa Ta'aala* aliyenipa *satua* na nguvu ya kusimama hapa mbele ya Bunge lako tukufu kuchangia hotuba hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ya mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna alivyojitahidi kuchukua hatua ya kuifanya Tanzania yetu kupaa katika mizani ya kisiasa. Kazungumzia mambo muhimu sana katika jitihada zake, tumeweza kuona ile diplomasia ya mashirikiano ya kimataifa, kuchochea diplomasia ya kiuchumi, kuvutia wawekezaji, kushamirisha uchumi wa Bluu, kufungua masoko na kuhusiana na kuweka masuala ya tabianchi. Mheshimiwa Dkt. Samia kwa kweli ameipaisha Tanzania yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee napongeza sana jitihada za Waziri wetu mahiri na hodari, Mheshimiwa Dkt. Stergomena Tax, pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Mbaruok, Makatibu wake Wakuu, watendaji, maofisa na wachocheaji wa *protocol* na wawakilishi mabalozi wetu wote wa Tanzania duniani kote kwa jitihada zao wanazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri shughuli za Wizara yetu hii zinakwenda vizuri sana. Serikali imefanya jambo zuri sana la kuhakikisha hadhi maalum hii kutolewa, kwa sababu kilio hiki cha uraia pacha kilikuwa ni cha muda mrefu cha ndugu zetu hawa wa *diaspora.* Leo Serikali imekuja na hili. Niwashauri tu wana-*diaspora* wapokee hii, mengine mazuri yatakuja baadaye. Wapokee kwa moyo mkunjufu, wajiandikishe kama walivyoelekezwa. Serikali yetu ina nia nzuri na mambo mema yatapatikana baadaye. Kwa sababu jambo hili wamelitaka siku nyingi. Inawezekana wasifurahie sana kuambiwa wapate hadhi maalum, lakini hadhi maalum ni nzuri kwa sababu bora moja kuliko kukosa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhusiana na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, tunajua sote Wizara hii ni miongoni mwa Wizara kongwe ambazo zimekuwa na mchango mkubwa katika ustawi wa Taifa letu hasa katika nyanja za kitaifa, kikanda na kimataifa. Sambamba na hilo, Wizara hii imekuwa na mchango mkubwa katika kuhakikisha ulinzi na usalama wa nchi yetu ambapo Maofisa wa Mambo ya Nchi za Nje wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana kuhakikisha wanakusanya taarifa za kiintelijensia, kudumisha ujirani mwema na hata kutoa taarifa za awali *(early warning)* ambazo zinaisaidia nchi yetu kuepukana vita au majanga mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na unyeti wa kazi ambazo zinafanywa na Maofisa wa Mambo ya Nchi za Nje, kuna mambo kadhaa ambayo Serikali inapaswa kuangalia upya kuhusu *status* za maafisa hawa ambapo nahisi wakati umefika sasa kada hii ya Maafisa wa Mambo ya Nje ikapewa hadhi maalum, *special recognition* na kumtofautisha Ofisa Mambo ya Nchi za Nje na ofisa mwingine wa Serikali. Ni dhahiri hali ya Maafisa wa Mambo ya Nchi za Nje zinakuwa ni bora pale tu ambapo wanakuwa nje ya nchi ambapo hupokea posho maalum *(special allowance),* lakini wanaporejea ndani ya nchi, maafisa hawa wanakuwa wanyonge kutokana na maslahi duni wanayoyapata licha ya kazi kubwa na ngumu ambazo wanafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisa Mambo ya Nchi za Nje, haheshimiki kama wenzao wa Idara ya Usalama wa Taifa ama Wizara ya Fedha. Naomba Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ipitie upya kada hii na kutoa maslahi sawasawa na wanayopatiwa Idara ya usalama wa Taifa. Afisa huyu wa Mambo ya Nchi za Nje naye anahusika na masuala ya kiintelijensia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ningependa kugusia ni kuhusu *scheme of service* hasa inapofika wakati wa kupandishwa vyeo au uteuzi wa mabalozi. Kwa heshima sana, kipekee, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kurejesha hadhi na heshima ndani ya Wizara hii ambayo kwa muda mrefu ilitoweka. Kipekee nampongeza Rais kwa kuendelea kuwaamini vijana waliokulia ndani

ya kada na kuwateua Maafisa wa Mambo ya Nchi za Nje kuwa Mabalozi. Hili ni jambo zuri sana na linafaa kupongezwa, kwani linachangia kurudisha *morale* na imani kwa maafisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza tena Mheshimiwa Rais kwa hatua ya kuona umuhimu wa kuteua kikosi kazi maalum cha jopo la mabalozi wabobezi, ambao wamepewa kazi mahususi ya kuangalia mwenendo na utendaji wa kazi za Wizara hii. Jambo ambalo naamini mwisho wa siku itasaidia kutoa mwelekeo chanya na ufanisi kwa utendaji wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *scheme of service* napenda kusisitiza Wizara kuzingatia kikamilifu taratibu za Utumishi wa Umma, kwani eneo hili limekuwa na changamoto kubwa. Maafisa wengi ambao walipaswa kupandishwa vyeo, bado wengi hawajapandishwa, hali hii inawanyima fursa mbalimbali ikiwemo kupata uwezekano wa kuteuliwa kuwa Mabalozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Foreign Service Regulation* iliyokuwepo imepitwa na wakati na haiendani kabisa na matakwa ya mazingira ya sasa kwa Maofisa Mambo ya Nchi za Nje. Nashauri Wizara kama bado hawajaanza kuifanyia kazi, mapitio ya *regulation* hii iliyopo, waanze na wahimize ili kuweza kuendeleza na kuleta ufanisi katika utendaji wa kazi wa Maafisa wa Mambo ya Nchi za Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Wizara iongeze mashirikiano na kuweka karibu Waziri, Makatibu Wakuu, watendaji, kwa kuandaa *retreats* angalau mwaka mara mbili, kuandaa masomo mafupi mafupi ili kuwaweka hawa watu *in order.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine muhimu sana. Tunazungumzia diplomasia ya uchumi, lakini tunapowachukua wachumi wabobezi ambao wamekuwa kwenye *foreign service* na wamekuwa ubalozini kwa miaka kadhaa isiyopungua kumi pengine, halafu unamtoa unampeleka ukamfanye Kaimu Katibu Tarafa, ina maana umepoteza ile *potential.* Huyu ana uzoefu wa ku-*deal,* ku-*lobby* na kufanya vitu fulani kwenye *foreign service,* wewe unampeleka kule. Inakuwa sawa sawa na kumchukua *surgeon*

unamwambia akafanye kazi ya ofisa ugani. Naomba watazamwe wale wote ambao walikuwa *displaced,* wakapelekwa kwenye sehemu wasizohusika warudishwe kwenye *career* yao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwapatia fursa hawa *foreign service* waendelee kwenye *career* yao ni jambo bora, kwa sababu mtu ameshakaribia kufika awe balozi, wewe unamtoa unampeleka Katibu Tarafa, *is that fair* jamani! Hii siyo haki. Unampeleka kwenye *line* nyingine hana uzoefu nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kabisa mimi naunga mkono hili jambo la *diaspora* na ninaomba tufanye kazi zaidi ili tusije tukajiingia katika jambo ambalo litahatarisha usalama wetu na nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi naona kama nimalize mambo yangu hayo. Ah, jambo moja nimesahau, kweli. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku nyingi tuliambiwa kama majengo ya ubalozi ya nchi zetu yatakarabatiwa, lakini hii imekuwa ahadi ya siku nyingi, sijui lini itakamilishwa. Bahati nzuri mimi nimebahatika pia, msinione hivi, nimeshakuwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, tuliwahi kuwa kwenye msafara na Makamu wa Rais, *by then* Mheshimiwa Dkt. Shein, tukaambiwa kule ubalozini Abuja, kama kiwanja kipo na kila kitu tayari, ubalozi utajengwa; na kwingine hivyo hivyo. Sasa jambo hili lifanyiwe kazi. Kwa sababu tukiwa na majengo yetu tutapata faida nyingi. Tutapangisha, tutafanya shughuli zetu pamoja na makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu Chuo cha Diplomasia. Hiki chuo kilikuwa kinaendeshwa kwa ushirikiano baina yetu sisi na *Mozambique*, lakini inaonekana kama ushirikiano ule umetetereka kidogo. Sasa Serikali imejipangaje kukiendeza chuo hiki ili kiwe na hadhi kubwa na kiwe cha kileo zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Baada ya hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Asha Abdullah Juma. Nilimtaja Mheshimiwa Fakharia Shomar, atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo na Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka ajiandae.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kweli, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo kusimama mbele ya Bunge hili na kuweza kuichangia Wizara hii. Sina budi kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri aliyoifanya pamoja na Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na wote wa Wizara yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu, kwa kazi zake nzuri. Ameiweka Tanzania katika ramani iliyo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi pia, kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kazi yake nzuri anayoifanya Zanzibar na tunajiringia Wazanzibari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka niipongeze Wizara kwa pesa walizozipata safari hii, Shilingi bilioni 17.8 ambazo ni fedha za maendeleo. Wizara hii inakwama, kwani kwa miaka mitatu mfululizo pesa za maendeleo wanazopatiwa ni ndogo; na hiyo ndogo wanayopewa, pia haifanyi kazi. Wanaweza wakapewa robo yake, hata nusu haifiki. Sasa tunalaumu kwamba balozi zetu hazijengwi, vitega uchumi havijengwi, na mambo mengi tu kwamba Wizara hii haiwezi kutekeleza. Tatizo siyo Wizara, tatizo pesa za kutekeleza miradi ambayo wanajipangia, hawapewi kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naiomba Wizara ya Fedha itupie jicho Wizara hii ya kimataifa. Wizara hii ni jicho, Wizara hii inafika mbali, Wizara hii ina mambo mengi. Sasa hii Wizara tuiangalie, pesa wanazotengewa wapewe kwa mujibu wa taratibu, waweze kujenga vitega uchumi katika balozi zetu ambapo tunakwenda kwenye Sera

ya Uchumi wa Diplomasia. Bila mtu kumpa pesa, hataweza kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija na suala la Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika, ya Haki za Binadamu, ambayo ilikuwa ijengwe kipindi kirefu; ina maana kuna miaka 16 mfululizo toka tumeridhia hatujafanya chochote. Tumeridhia, tumekubali, lakini hakuna kilichokuwa. Sasa tunajiuliza, tunakwenda kwenye diplomasia ya kiuchumi, ni ambayo ni ya kubana matumizi! Kwa sababu, hatuwapi pesa. Mtu haumpi pesa, hawezi kutekeleza. Tanzania tunaiweka katika picha gani au ramani gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmeahidi nyie kujenga. Miaka 16 hatujajenga, tunailaumu Wizara! Hatuilaumu Wizara, tunalaumu hawapewi fedha kulifanya hili tukio walilotakiwa wafanye. Nashukuru safari hii angalau wametengewa Shilingi bilioni 5.4, naiomba Wizara iweke alama, ifanye kitu na kazi iendelee na waweze kujenga. Isiwe sababu hampati pesa. Pesa mmeshapewa, mnatakiwa muanze jukumu la kujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija na hii *Royal Tour.* Mheshimiwa Dkt. Samia aliondoka ofisini kwake, akatembea kwenye mbuga na nyika; kwenye vielelezo vyote vya utalii; na akafanya kuipaisha Tanzania katika ramani ya utalii, lakini watalii wanakuja kwa wingi Zanzibar, wanakuja kwa wingi Tanzania Bara, na wanaotakiwa wafanye kazi kubwa ya kuhamasisha ni Wizara hii. Sasa na mtu hawezi kuhamasisha kitu kama hana pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narejea pale pale. Kazi ya mama haikuwa ya bure, kazi ya mama kajituma, inatakiwa ienziwe. Tumuenzi Mheshimiwa Dkt. Samia kwa kazi yake nzuri aliyoifanya ambayo inatuletea mapato Tanzania. Sasa ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake, lazima iwe na pesa za kutosha za kufanya kazi zake. Nampa pongezi Mheshimiwa Dkt. Samia Hassan Suluhu kwa ari yake, kwa kubuni hii ziara akaweza kuipaisha Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sera ya Mambo ya Nchi za Nje, kwanza naiomba Wizara, muda ulikuwa mrefu na ninategemea hii

2023/2024 inawezekana sera hii ikatoka maana iko katika hatua za mwisho za utendaji kutokana na maelezo yako Mheshimiwa Waziri. Nami naunga mkono itoke, aweke alama kwamba kile kitu umekisimamia na kimekuwa na kimetoka. Kwa sababu hii pia ndiyo itakayotusaidia katika diplomaisa ya uchumi, au *diaspora*, hii ndiyo itakayoleta ari na mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu hili suala la uraia pacha kwa Tanzania bado mapema. Tuikamate hii hii hadhi maalum. Hadhi maalum unapata kila kitu; tatizo liko wapi? Kwa sababu unatambulika, familia inakujua, Taifa linakujua, nyumbani wanakujua; tunataka nini tena? Kwanza hata ukisema unataka uraia pacha itakusiadia nini? Muhimu ujulikane kwenu na ufanye mambo ya kisheria ya kwenu, na sheria inakutambua kwenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri aendelee na mchakato wake. Sera inatoka na hadhi maalum inatoka zinakwenda sambamba, Tanzania oyee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, diplomasia ya uchumi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia Mheshimiwa, maana yake kengele imelia, malizia hiyo moja.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika diplomasia ya uchumi – nazungumza dogo tu – kwamba sekta mtambuka za Tanzania zishirikiane na mambo ya nje zitoe elimu kwa wananchi, kama biashara, sehemu za masoko, *investment*, kwa sababu kuna watu hawaielewi, wanakosa kujua maadili ya hilo jambo linavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Fakharia. Nilimtaja Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka na Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi wajiandae.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Naomba nianze kwa kutambua kazi kubwa ambayo wenzetu wanaifanya, na hasa nataka kutambua uamuzi wa Serikali na wa Rais wetu na Mheshimiwa Waziri wa kuweza kuwapitisha wenzetu wawili kwenda kugombea kwenye nafasi kubwa sana huko duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumzia Mheshimiwa Spika wetu, Dkt. Tulia Ackson, anayegombea Urais wa *IPU,* na mimi naamini, ninamfahamu tangu chuo kikuu, ni mtu sahihi sana kwa nafasi hiyo. Kwa hiyo tuiambie dunia kwamba amepatikana mtu sahihi wa kuongoza chombo chetu hiki muhimu na wasitie shaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini imezungumzwa hapa kwamba Mheshimiwa *Ambassador* Liberata ni mtu mahiri, muhimu sana, na hiyo nafasi itakuwa imepata mtu sahihi. Kwa hiyo niishukuru sana Serikali kwa uamuzi sahihi sana wa kuwatanguliza hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni swali kwa kweli, kwamba kwenye zile hatua nne za Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki, tulianza na *customs union,* tukaja soko la pamoja, lakini tarehe 31 Novemba, 2013, tukasaini *protocol* ya *monetary union,* ni miaka kumi, inaisha mwaka huu. Nataka kujua tupo hatua gani; na je, hatuoni haja ya kuharakisha mchakato huo tukizingatia kwamba sasa hivi tunazungumzia Dola ya Marekani ikienda kusambaratika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani mnafahamu, sasa hivi duniani, *Middle East,* hapa *BRICS* wanazungumzia kuanzisha fedha yao. Hatuoni ni muda sahihi sisi kuwa na fedha yetu Jumuiya ya Afrika Mashariki; *East African Currency,* hatuoni kama muda umefika? Ningeshukuru sana Mheshimiwa Waziri kama hili nalo ungeweza kulitolea ufafanuzi wakati una-*wind up.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nataka niongeze sauti kidogo, mimi sizungumzii uraia pacha kivile, na hili jambo lilizungumzwa vizuri sana kwenye hotuba ya Mwalimu Nyerere. Mara baada ya nchi yetu kupata uhuru na kuwa Jamhuri, tarehe 10, Desemba, kwenye

Bunge letu, Mwalimu alitoa hotuba moja muhimu sana ambapo alieleza tunakwenda kujenga Taifa la namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na wakati huo kulikuwa na matabaka makubwa kati ya Wazungu, Wahindi, Waarabu na Waafrika. Na alijaribu kuwatia moyo, kwamba ninyi Wazungu hamjapoteza chochote kwa sababu bado uchumi upo mikononi mwenu, mna elimu zaidi; na Waafrika akawaambia mna *political control,* kwa hiyo tukiunganisha hizi *forces* mbili tunaweza kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa kweli wakati huo kulikuwa na wasiwasi, suala la uraia lilikuwa kubwa, na Mwalimu alilizungumzia kwa kirefu sana. Lakini hoja ya msingi kwa upande wangu, suala kiuchumi ni zuri, lakini kwa kweli ni *secondary,* hoja ya msingi hapa tunalindaje haki za asili, haki za Kimungu? Kitila Mkumbo kuwa Mtanzania si chaguo lake, ni jambo la asili, jambo la Kimungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kati yetu hapa ambaye amechagua awe Mtanzania, au Mganda au Mkenya, uraia wa kwanza ni wa asili, unazaliwa kuwa raia wa nchi fulani. Mambo mengine ya kujitakia unaweza ukaamua uende kutafuta uraia wa nchi nyingine. Lakini kwa kweli jambo la msingi kuliko yote ni kwamba huyu mtu ambaye kwa Kimungu kabisa amezaliwa kuwa Mtanzania, na baadaye ameamua kwenda kusaka fursa, na kwa mujibu wa Katiba yetu Ibara ya 17(1) inasema hivi; 17.-(1)Kila raia wa Jamhuri ya Muungano anayo haki ya kwenda kokote katika Jamhuri ya Muungano na kuishi katika sehemu yoyote, kutoka nje ya nchi na kuingia, na pia haki ya kutoshurutishwa kuhama au kufukuzwa kutoka katika Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nimekaa hapa, mmenisomesha, nimeamua kwenda kutafuta kazi Afrika Kusini, nimepata. Lakini kule Afrika Kusini kuna hati fulani ili uzipate lazima uchukue mambo yao fulani; kitendo hicho kinaninyan'anya haki yangu ya Kimungu ya kuwa Mtanzania kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ukisoma nchi nyingi ambazo zinapinga, hazitaki uraia pacha, zipo, hata Sweden. Lakini kitu kimoja

ambacho wamekilinda ni haki ya uraia wa watu wao. Kwa hiyo wewe kachukue uraia wowote, lakini wewe ni Mtanzania, wewe ni Mswiden, wewe ni Mwingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hakuna mtu anayezungumzia hapa kwamba eti atoke mtu kutoka nchi nyingine aje apewe Uraia wa Tanzania, hilo hatulipiganii, tunachopigania na kinachozungumzwa hapa; kwa nini turuhusu Mtanzania apoteze haki yake ya Kimungu kwa sababu tu amekwenda kutafuta fursa katika nchi nyingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sasa hivi tunazungumzia, duniani, takwimu zinaonesha kabisa, moja ya njia za kutatua tatizo la *graduate unemployment,* tatizo la ajira ni kubwa, lakini tatizo kubwa la ajira kuliko yote ni tatizo la ajira ya watu ambao wamekwenda shule, wa vyuo vikuu hawa, hilo ndilo tatizo kubwa. Kwa hiyo njia ambayo zinafanya nchi nyingi ni kuwaandaa watu wao kuwa *global citizens* ili wakatafute kazi huko duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukisukuma hilo unaondoa vikwazo. Kwa hiyo hili jambo kama litakuja kwa uraia pacha, ama hadhi maalum, kwangu siyo hoja kubwa, hoja kubwa ni tunalindaje haki za watu wetu ambao ni Watanzania wanapokwenda kutafuta fursa kwenye nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hata kiuchumi, uchumi watu wengi wamesema hapa, vitu gani vinakwamisha watu wetu? Sisi watu wetu wengi wanakaa nje vizuri tu, ukiangalia idadi ya Watanzania, Waganda, Wakenya, hatutofautiani sana kwa walioko nje, lakini kwa nini *remittance* za wenzetu ni kubwa kuliko za kwetu? Kwa hiyo zimefanyika *studies* na zinaonesha, ya kwanza ni kwamba Mtanzania akiwa nje anakuwa hana *confidence*, kwa hiyo ni jambo ambalo lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile hata watu wetu kutoka nje ni changamoto, inaonesha kwamba kwa *East Africa* Watanzania ndio watu ambao wanaongoza kwa kutokupenda kutoka nje, ambayo siyo faida kwa leo. Kwa leo ungetaka kuwa na watu ambao wanachangamkia fursa duniani na ndani ya nchi yao. Kwa hiyo

nadhani hili ni jambo la msingi la kiliangalia, *whatever form we are going to decide,* kama ni uraia pacha, kama ni hadhi maalum, lakini ni jambo ambalo lazima tuliangalie kwa umakini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita nadhani *Daily News* wametoa taarifa, walikuwa wanamnukuu Mheshimiwa Rais, inaonesha kwamba ukiangalia hizo hela kutoka nje *(remittance)* na uwekezaji kutoka nje kwa Watanzania imefikia *2.5 trillion shillings;* ni pesa nyingi. Kwa hivyo lazima Mheshimiwa Waziri uangalie ni namna gani utatengeneza mazingira mambo mawili yatokee; Watanzania wengi wachangamkie fursa za kiuchumi zilizopo duniani, lakini pia waliopo kule duniani wachangamkie fursa hapa nyumbani kwa maana ya uwekezaji. Hiyo lazima tuweke mazingira mazuri ya kufanya hivyo kwa sababu ni jambo la msingi. Kwa hiyo hili jambo likamilishwe mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonesha kabisa kwamba wameshazidisha, hela ambazo zinakuja kutoka kwa hawa zinazidi hela ambayo tunapata ya kahawa, *cashewnuts*, tumbaku na chai ukiunganisha. Hela za watu waliopo nje *(diaspora*), ni kubwa, kwa hiyo siyo jambo ambalo kwa kweli tunaweza kuendelea kuliangalia kwa jicho ambalo siyo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo kwa kweli hoja yangu kubwa ni hiyo, kwamba muda umefika hili jambo lifanywe likamilike. Na tutumie fursa ambayo naisema kila siku; Mheshimiwa Rais amekuja na mambo hayo manne, suala la *reform* ni muhimu, kama kuna eneo la kufanya *reform* kubwa kuliko yote ni suala hili. Kwa saabu kwa kweli hata kama tunazungumzia Katiba mpya, itakapofika mjadala hili ni suala ambalo lazima tuliangalie kwa makini sana ili Watanzania haki zao za asili zilindwe popote walipo, iwe ni ndani ama nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo. Nilimtaja Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka na Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi na Mheshimiwa Soud Jumah wajiandae.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki katika mwaka wa fedha huu 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nipongeze Wizara hii kwa hotuba nzuri ambayo naamini kwamba kama ikitekelezwa kikamilifu italeta matunda chanya. Lakini pia niseme kwamba, kama wenzangu waliotangulia walivyosema, kuwapongeza Spika wetu, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, pamoja na Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula, kwa kupatiwa nafasi na Serikali yetu kugombea nafasi hizi za *IPU* na kuwa Katibu Mkuu katika Jumuiya ya Madola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hivi; nafasi hizi ni *very competitive,* watu wanao-*compete* ni wengi sana, tusije tukafurahi kwamba tumepeleka majina kwa hiyo *automatically* watapata. Mimi nafikiri ni vyema Serikali yetu ikajipanga vizuri, hasa ikiongozwa na Wizara yetu hii ya Mambo ya Nje kuhakikisha tunafanya kampeni ya kufa mtu ili nafasi hizi tuzipate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za Afrika Magharibi zimeweka watu wao kwenye nafasi hizi za kimataifa kiasi kwamba wame-*benefit a lot* kutokana na kwamba wale wafanyakazi wao wanarudisha nini nyumbani. Kwa hiyo ninaomba sana Serikali tusilichukulie lelemama bali tuweke nguvu tukiona kwamba tumekuwa na Katibu Mkuu katika Jumuiya ya Madola, nafasi hii itatupa nafasi kubwa sana katika nchi yetu ya Tanzania kupata mambo mengi, maana mimi nilishapata *experience* kidogo, nimefanya kazi kidogo kule, kwa hiyo najua kuna nafasi gani kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nizungumzie hotuba ya Mheshimiwa Waziri wetu aliyoileta kuhusu kwamba yeye anaweka mkazo katika diplomasia ya kiuchumi. Tukumbuke kwamba Hayati Benjamin Mkapa hii ndiyo ilikuwa *area* yake ya kipaumbele miaka 28 iliyopita. Miaka 28 iliyopita aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu alisema diplomasia ya kiuchumi ndiyo itakayoongoza Taifa letu katika kutuletea maendeleo ya haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ni miaka 28, hebu tujiulize, katika miaka 28 hii inaendana na yale ambayo tumeyafanya tangu wakati ule mpaka leo? Ni wazi kwamba tuko nyuma sana katika diplomasia ya kiuchumi. Tukiangalia yale ambayo yamefanyika kwa kipindi hicho mpaka leo, hakika utajua kwamba tuko nyuma sana kwa yale yaliyotakiwa yafanyike hadi leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Rais wetu Samia Suluhu Hassan kwamba ameunda tume ya kuangalia utendaji wa Wizara hii ya Mambo ya Nje. Ina maana kwamba kuna mapungufu makubwa ameyaona katika Wizara hii. Na hii pia inanipa picha kwamba kumekuwa na mapungufu makubwa. Nikiangalia kwamba katika kipindi hiki cha miaka mitano hii ya mwisho, maafisa masuuli wamebadilishwa badilishwa sana, takriban kila mwaka unapata Katibu Mkuu mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaashiria kwamba kuna tatizo kubwa mahali; ama wale wanaomshauri Rais, kwamba huyu anafaa kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje, au yale yaliyotegemewa siyo wanayoyafanya. Kwa hiyo hapo tuliangalie sana. Naamini kwamba tume hiyo itaweza kumshauri vizuri ili tuwe na watendaji wazuri katika Wizara hii na katika Mabalozi ambao wataweza kufanya haya tunayoyapanga hapa yatekelezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala hili la mapitio ya Sera ya Mambo ya Nje ambayo bado haijakamilika. Na hii ndiyo itakua kioo chetu, hii ndiyo itaweza kutufanya tujipime, kwamba tunakwenda wapi. Kama sera haijakamilika itakuwa pia shida kwamba tunashika lipi na tunakwenda wapi. Kwa hiyo ninashauri kwamba Mheshimiwa Dkt. Tax, uhakikishe kwamba sera hii inapita, ambayo ndiyo itatusaidia katika kuhakikisha kwamba haya yote ambayo tunataka kupitisha leo yanafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika Ripoti ya *CAG* kuhusu majengo yetu kwenye balozi zetu. Majengo yetu haya yamekuwa ni ya kutia aibu sana. Kwanza, tukumbuke kwamba takriban miaka 50 tulipata viwanja kama kumi hivi kule Zambia tulivyopewa na Hayati

Kenneth Kaunda. Viwanja hivyo hata ukifika leo ni mapori. Inatia aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikwenda Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati zetu nne; *PAC, PIC, LAAC* na Bajeti; tulitembelea maeneo yale. Tumeona ni aibu kubwa, maana wale wenye majengo yao, nyumba zao karibu na viwanja vile, kwa kweli wanasikitika sana na wanachukia sana kwamba tumewaachia mapori katika viwanja vile, kwa sababu haviendelezwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hayati Kaunda alikuwa ameona kwamba hii itatusaidia kama vitega uchumi. Na tulipotembelea kule wakati huo aliyekuwa Balozi alituambia kwamba viwanja vyetu kama vingejengwa inavyotakiwa, ni wazi vingesaidia kulipa kodi takriban Balozi zote zilizoko katika Bara la Afrika. Lakini mpaka leo ndiyo tunaambiwa bado bajeti ndiyo inapangwa viwanja hivyo vikajengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha kusikitisha zaidi ni pale ambapo jengo letu lililopo kule Washington limepoteza kinga ya kidiplomasia kwa kuwa ni chakavu mno, na kwa hiyo wakasema kule wenzetu hatuwezi kuendelea kukaa na uchafu huu, na hatutambui kama ni jengo la Balozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili hiyo tukatakiwa tulipe kodi, na imelipwa kodi kiasi cha milioni 283.3 kwa ajili ya kulipia jengo bovu. Sasa haya ndiyo kati ya mambo ya kujitathmini; hivi kweli tuko *serious* na tunayoyafanya? Tumeacha kukarabati majengo yetu, tangu miaka 29 Hayati Mkapa alivyosema uchumi wa diplomasia ndiyo utaongoza nchi yetu. Leo majengo tumeyaacha na majengo yale ndiyo ya kututambulisha, kwamba hawa ndio Watanzania. Leo majengo yale yamekuwa ni aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia pia tuna Balozi 34 ambazo hazina majengo yao. Pamoja na kwamba wamesema 14, angalia hiyo aya 20 yatajengwa lini. Kutokana na hivyo, mwaka 2021/2022 Tanzania ililipa bilioni 15.47 kwa kodi ya mapango haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo unaangalia kwamba hivi kweli diplomasia ya uchumi tunayoongelea maana yake ni nini? Maana yake ni kukuza uchumi. Lakini angalia uone kwamba uchumi wako unaukuzaje wakati una gharama nyingi kuliko ambavyo unaweza ku-*sustain* hiyo diplomasia ya uchumi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kaboyoka.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda la mwisho, tuna uhaba mkubwa wa uwakilishi wa heshima katika balozi zenye nchi zaidi ya moja. Hilo nalo naomba Wizara iliangalie, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kaboyoka. Nilimtaja Abdullah Ali Mwinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa Soud Mohamed Jumah na Mheshimiwa Condester Sichalwe ajiandae.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia katika mjadala huu muhimu na adhimu. Awali ya yote ningependa kuchukua fursa hii kutoa shukrani na pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa maendeleo makubwa sana toka alivyoingia madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyanja nyingi zimeendelea lakini kama tutakuwa tunachambua, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Sera ya Nje ni miongoni mwa vitu ambavyo Mheshimiwa Rais na timu yake imefanya kwa weledi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile pongezi zangu ziende kwa Waziri Mheshimiwa Tax na aliyemtangulia Mheshimiwa Mulamula kwa kazi kubwa waliyoifanya. Naomba nichukue fursa hii kumtakia Mheshimiwa Mulamula kila la kheri katika nia yake ya kuwania nafasi ya *General Secretary* wa *Commonwealth* kila la kheri Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia mambo matatu na nitajitahidi yote niyagusie kwa sababu ya msingi na ya dhati. Nimefarijika mno kumsikia Mheshimiwa Waziri kwamba ameyagusia mambo yote ambayo ningependa kuyachangia. Ningependa kuzungumzia *diaspora*, Sera ya Diplomasia ya Uchumi na suala la uraia pacha au hadhi maalum yote ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *diaspora* maana yake nini? *Diaspora* ni neno la Kigiriki ambalo maana yake ni kutawanyika ulimwenguni. Watu ambao wametoka sehemu yao ya asili wakatawanyika ulimwenguni, ndio maana ya *diaspora*. Watu hutawanyika ulimwenguni kwa sababu mbalimbali kuna wengine inawabidi wahame kwa sababu ya vita, mauaji ya kimbali, kwa sababu ya njaa kali *(famine),* na wengine wanakwenda tu kwenye masomo na wengine tu kuwania maisha na kutafuta riziki zao za kheri na watoto wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna ubaya kwa mtu kuhama na kwenda sehemu yoyote kujitafutia riziki yake, yote hiyo ni ruhusa. Tafiti zinaonesha kwamba *diaspora* inachangia katika nchi ya asili mambo makuu matatu mpaka manne. La kwanza, kijamii; la pili, kisiasa; na la tatu, kiuchumi au kimaendeleo. Hayo ndio maeneo ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijamii, wale ambao wako huko pengine wanajifunza ubunifu na kufanya mambo tofauti, wakirudi makwao wanafanya hivyo na kutuendeleza katika gurudumu la maendeleo. Anaweza mtu akawa Israel akawa mkulima mzuri kule, una teknolojia au njia ya kulima vyema, anarudi kwetu anatusaidia katika hilo. Huo ni mchango chanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili katika kisiasa, kuna nchi ambazo zimeingia kwenye machafuko nyingi tu, mfano Iraq, Libya, Burundi, Somalia hata Kenya katika machafuko ya 2007. *Diaspora* wa nchi hizo walichangia mchango mkubwa sana katika kupata amani. Sasa nao huo ni mchango vile vile na wanachangia maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho na la msingi zaidi ambalo nilitaka kujikita zaidi ni kiuchumi. Kiuchumi, wana-*diaspora* wanaweza kuchangia nchini mwetu kwa njia kuu mbili ya kwanza ni *remittances* ambazo zimezungumzwa na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na ya pili ni *investmen*t. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *remittances* ni zile fedha ambazo wana-*diaspora* wanawapa ndugu zao huku kuwasaidia kujikimu katika maisha yao na hizo zinapimwa. Nimefanya tafiti kidogo kwa nchi nne; Nigeria mwaka 2021/2022 *remittances* kutoka katika *diaspora* kwenda Nigeria zilikuwa dola bilioni 20, ndani ya mwaka mmoja. Ni fedha nyingi zaidi kushinda *their largest export* ya mafuta. Mafuta yanayouzwa nje yana thamani ndogo kushinda Wanaijeria waliopo nje wakileta kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya Wana-*diaspora* wapo milioni tatu, wamechangia mwaka 2021/2022 dola bilioni nne. Uganda wapo laki sita, wamechangia dola biloni 1.4. Sisi tumechangia mwaka huo huo dola bilioni 1.1 na bilioni 1.1 imeongezeka kwa kasi kubwa sana kulinganisha na mwaka uliopita ilikuwa milioni mia tano na kitu na ukiangalia cha msingi kabisa ni jinsi gani wana-*diaspora* wanajiona wanathaminika ndani ya nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nitoe pongezi kwa hatua ya kwanza ambayo imetuwezesha sisi kuongeza lakini ukiangalia wana-*diaspora* wa Uganda wako laki sita sisi tupo milioni 1.5. Wao wanachangia nchini mwao zaidi kuzidi sisi kwa nini? Hilo ndio swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nchi yetu inajikita katika Diplomasia ya Uchumi. Diplomasia ya Uchumi shamba lake kubwa ipo kwenye *diaspora*. Tukiweza kuwapa *incentives* wana-*diaspora,* tunaweza tukavuna mabilioni ya fedha mengi zaidi kushinda *export* yoyote ambayo tutaifanya hapa Tanzania.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kumalizia jambo moja tafadhali. Suala la uraia pacha na hadhi maalum. Uraia pacha tunaouzungumzia hapa Mheshimiwa Rais Nyerere kama msingi wa msimamo wetu. Tuna ahadi za Wanachama wa *TANU* au sasa CCM. Tuna ahadi mbili ambazo ni *relevant* katika hili ya kwanza binadamu wote ni ndugu na Afrika ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi huu ulitumika kuwa-*nationalize* wakimbizi 200,000 wa Burundi Tanzania awamu ya kwanza, wakimbizi hamsini elfu wa Somalia awamu ya pili. Sasa ahadi ya pili ya mwanachama sote sisi tunaijua, nitatumikia nchi yangu na watu wake wote, narudia tena nitatumikia nchi yangu na watu wake wote. Wana-*diaspora* ni watu wetu, lazima tuwatizame tuwajengee hoja, tuwasaidie, kama sio uraia pacha, hadhi maalum. Tofauti yake ni ndogo, sio tofauti kubwa. Hadhi maalum inategemea unawapa haki gani, uraia pacha unaweza kuzuia mambo makuu mawili masuala ya siasa wasiweze kushiriki katika siasa na wasiweze kufanya kazi katika vyombo vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana umeeleweka sana.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga hoja mkono, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Soud Mohamed Jumah, atafuatiwa na Mheshimiwa Condester Sichalwe, Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil, Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu na baadaye ajiandae Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara kwa uwasilisho mzuri wa bajeti pamoja na mikakati ambayo wameiweka katika bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maeneo matatu na kama muda utatosha nitaongeza moja la nne haraka haraka katika michango yangu. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake ya kule Zanzibar kwa kuweza kuifanyia marekebisho makubwa Ofisi ya Zanzibar ya Mambo ya Nchi za Nje ambayo kwa sasa angalau ina mwonekano wa kweli wa Ofisi ya Mambo za Nchi za Nje. Ni tofauti na ilivyokuwa zamani, miaka mitano iliyopita, kwa kweli ilikuwa inatia aibu kama ni ofisi ya mambo ya nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ombi langu, kwamba pamoja na marekebisho tuliyofanya kwenye ofisi hii, naomba sasa twende kwenye changamoto ambazo zinakabili hiyo ofisi. Changamoto ya kwanza hiyo ofisi ina upungufu mkubwa wa watendaji. Kwa hiyo ningeomba tukaongeza idadi ya watendaji katika Ofisi ya Mambo ya Nchi za Nje ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, suala zima la vifaa na usafiri. Kwa kweli ni aibu Ofisi ya Zanzibar ukienda suala la usafiri ni gumu katika Ofisi ya Mambo ya Nchi za Nje ya Zanzibar na halikadhalika vitendea kazi. Kwa hiyo ni tegemeo langu kwamba Mheshimiwa Waziri na timu yake wataionea huruma Ofisi ya Zanzibar kwa kuipatia vifaa na usafiri ili iweze kuonekana kuwa na hadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ningeomba pia kama kuna uwezekano tukatenga eneo hasa, sababu tumefanya marekebisho, lakini tutenge eneo tujenge Ofisi ya Zanzibar katika maeneo mengine sio katika eneo lile ambalo kidogo limejikunja hata *parking* za magari ni shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, wenzangu wameongelea kuhusu sera hapa na mimi vile vile niweke mkazo kwenye marekebisho ya sera, tuyafanye kwa haraka kwa sababu sera ya mwaka 2011, ni kipindi karibu miaka 23 sasa toka sera hii imetayarishwa. Sasa naomba tu kwamba tuweke mkazo kwenda kuitayarisha na kuitengeneza Sera ya Mambo ya Nchi za Nje ili kuweza kuakisi hii diplomasia ya uchumi ambayo tunaizungumza hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni suala zima la mambo ya *royal tour*. Mheshimiwa Waziri amefanya kazi nzuri kuzihamasisha baadhi ya balozi zetu nchi za nje na zimefanya kazi nzuri, lakini ombi langu sasa ni vyema tukawa tuna mkakati wa pamoja na miongozo ambayo itazitaka balozi zote ziwe na *target* ziwe na miongozo maalum ya kuweza kuifanyia kazi hii ripoti au hii video ya *royal tour* ili kuweza kutangaza na kufikia ile *target* au lengo la kufikia watalii elfu tano ifikapo mwaka 2025, kama ilani ya Chama cha Mapinduzi inavyozungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niongelee suala zima la ushiriki wa Tanzania katika taasisi na mikutano ya kikanda na ya nchi za nje au ya kimataifa kwa ujumla. Kama unavyojua kwamba ili kuweza kupata hizi fursa kusema vizuri za mambo ya nchi za nje, ni lazima tuwe na watendaji wazuri ambao wameandaliwa, lakini pia tuandae mazingira ya Tanzania kwa ajili ya kupata hizi fursa ambazo ziko katika taasisi pamoja na mikutano ya kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano hapa, kuna mikutano ya kikanda ya mabadiliko ya tabianchi ambayo kuna fursa nyingi za kiuchumi, lakini ukienda hivi sasa kuna tatizo kubwa kwamba hizi fursa hatujajiandaa vizuri kwa sababu kama ukiangalia, kuna *accreditation institution* moja tu Tanzania ambayo ni *Bank* ya *CRDB,* lakini bado wenzetu kuna baadhi ya nchi wana *institutions* ambazo zimesajiliwa zaidi ya nne, zaidi ya tano ambazo zinaweza zikatafuta hizi fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo na sisi Tanzania tuandae watendaji, tuandae na hizi *institutions* zetu ziweze kuchangamkia hizi fursa za kifedha na shughuli nyingine mbalimbali katika hizi Jumuiya za Kikanda pamoja na mikutano ya umoja wa kimataifa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah. Nilimwita Mheshimiwa Condester Sichalwe na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil ajiandae.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Kwanza nianze kabisa kuipongeza Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi ambayo inaongozwa na Dkt. Samia Hassan Suluhu ambaye ni mwanadiplomasia namba moja. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri lakini pia nimongeze Mheshimiwa Naibu Waziri, baba yangu Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk.

Pia nimpongeze mama yangu Mulamula Mwenyezi Mungu akutangulie ili uweze kupata hiyo nafasi. Mungu akusaidie ili uweze kuipeperusha vyema Tanzania yetu na mimi nikiwa mkubwa nitakuwa kama wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitachangia kwenye diplomasia ya uchumi ambayo ni kipaumbele namba moja kwenye Wizara. Kabla sijaongelea kwenye hilo suala la diplomasia ya uchumi, naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba bajeti iliyopita nilichangia kidogo kuhusiana na vikwazo vya wafanyabiashara ambao wanaliendea soko la Zambia, lakini wakifanya shughuli zao Zambia pamoja na kuliendea soko la Kongo kupitia Nchi ya Zambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutatamani Mheshimiwa Waziri aseme neno, je. bado anaendelea kujua kwamba wafanyabiashara hawa wanaendelea kupitia vikwazo? W iki moja iliyopita walimfuata Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Nyongo kwa ajili ya kuendelea kuelezea changamoto zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye diplomasia ya uchumi kama ambavyo Wizara wenyewe wamesema kwamba ndio kipaumbele chao namba moja, lakini na maoni ya kamati wamesema kwamba diplomasia ya uchumi bado haijaeleweka kwa ufasaha kwa wananchi na hata kwa viongozi ambao wanasimamia sekta hizo, wakataja kwa mfano. Nitataka nisimamie zaidi kwenye maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli diplomasia ya uchumi kwa wananchi wetu wa kawaida, bado hawajui diplomasia ya uchumi ni nini. Watu wengi wanafikiria diplomasia ya uchumi ni wale watu ambao wanapita kwenye *red carpet* na wale wavaa suti za *dark blue* pamoja na *white color,* lakini tunaamini kwamba diplomasia ya uchumi hapa ndio kwenye eneo ambalo limebeba ajira nyingi sana na zinaweza zikasaidia kukuza uchumi wetu kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitolee mfano, mwaka jana kama sio mwaka juzi, tulipewa soko kubwa sana kwenye nchi ya China kupeleka soya, lakini unaweza ukashangaa kwamba ilifika wakati sisi hatuwezi kupata soya hapa. Ilipelekea Watanzania wakawa wanachukua soya nyingi kutoka Zambia, yaani pale mpakani Tunduma ilikuwa ndio biashara, kila mtu anatafuta soya kutoka Zambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nikawa najiuliza sisi hapa kwetu tuna halmashauri 184, nikachukulia mfano tuchukue tu halmashauri 100 tu za wakulima mfano kule kwetu Momba, mia tu. Tungewapa *target* kwamba wazalishe tani za soya milioni moja halmashauri mia, maana yake kila halmashauri ingeweza kuzalisha soya tani elfu kumi ambayo ni kitu kinawezekana, lakini hatukuwahi kupata hilo soko kabisa na soya nyingi kwa kiwango kikubwa zilikuwa zinatoka Zambia na waliokuwa wanaenda kuchukua Zambia ni Watanzania hawa hawa. Tafsiri yake ni nini? Ni kwamba sisi tunasaidia kuwakuzia uchumi Zambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maandiko kidogo ambayo nilipata nafasi nikasoma kuhusiana na diplomasia ya uchumi namna ambavyo inaelezea, kwamba watu wenye uwezo wafanyabiashara, lakini na hata watu wa kawaida wa chini ambavyo diplomasia hii ya uchumi inawalenga. Inasema hivi diplomasia ya uchumi ni mbinu na mkakati unaotumiwa na nchi na mashirika ya kimataifa katika kukuza maslahi yao ya kiuchumi nje na mipaka yao. Lengo la diplomasia ya uchumi ni kuimarisha ushirikiano wa uchumi kibiashara, uwekezaji na ushirikiano wa kiufundi kati ya nchi na kuboresha hali ya uchumi

kitaifa. Diplomasia ya uchumi inahusisha shughuli kadhaa ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaendelea: Nchi zinatumia diplomasia ya uchumi kukuza biashara na uwekezaji kwa kuvutia wawekezaji na kujenga mazingira mazuri ya biashara. Hivyo, wafanyabiashara kusaini mikataba ya biashara na makubaliano na wawekezaji kushirikiana katika masuala ya kifedha na kibenki. Aidha, ushirikiano wa kiufundi, diplomasia ya uchumi inahusisha pia kubadilishana maarifa na teknolojia. Nchi zinaweza kuweka mikataba ya ushirikiano wa kiufundi katika maeneo ya kilimo hapa kwenye kilimo ndio tunajiongelea sisi watu wa Momba na halmashauri zingine ambazo wanalima, afya, nishati, miundombinu na teknolojia ya Habari. Kwenye teknolojia ya habari ndio kwenye mambo ya *block chain technology* na mawasiliano. Hii inaweza kuimarisha teknolojia na ujuzi na inachangia katika maendeleo ya uchumi wa nchi zinazoshirikiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameendelea wanasema, katika diplomasia ya uchumi nchi zinaweza kutuma wawakilishi wa Serikali kama mabalozi wa uchumi au wajumbe wa biashara kwenye nchi zingine. Hao hufanya mazungumzo na kuwakilisha Serikali…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia tu kidogo. Fursa za biashara na ushirikiano wa kiuchumi. Diplomasia ya uchumi kwa kumalizia anasema, malengo ya diplomasia ya uchumi ni pamoja na kuongeza mauzo ya nje na bidhaa na huduma za nchi. Kujenga mtandao wa biashara wa washirika wa kimataifa, kuvutia wawekezaji wa kigeni, kukuza viwanda vya ndani. Sasa tutakuzaje viwanda vya ndani kama hatumshirikishi mwananchi wa kawaida huyu anayefanya shughuli ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, niombe kwamba, Wizara ilikuwa inasema inatoa elimu mbalimbali kwenye mambo ya diplomasia ya uchumi kwenye magazeti, redio na vitu kadha wa

kadha. Niombe elimu hii iende kule kwenye Baraza letu la Madiwani. Wizara ya Mambo ya Nje waweke dirisha kwenye Wizara ya TAMISEMI ambao wao wanazijua halmashauri na uwezo wao. Wanajua vipato vya halmashauri ipi ina mapato kidogo, halmashauri ipi inafanya kazi gani.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Tunaomba Wizara ya Mambo ya Nje watusaidie katika hili ili diplomasia ya uchumi iende kwa wanachi wa kawaida kabisa, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester muda wako umemalizika.

Waheshimiwa Wabunge ninaongeza muda kwa mujibu wa Kanuni ya 34 hadi tumalize kazi yetu. Nilimtaja Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil, atafuatiwa na Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu na Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk ajiandae.

**MHE. AHMED YAHYA ABDULWAKIL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Wizara ambayo inatupeleka katika uso wa Dunia. Zaidi namshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Chief Hangaya, kwa namna alivyopata nafasi hii alikwenda moja kwa moja kuifungua nchi kwenye diplomasia ya uchumi ambapo sasa nchi inasonga mbele tunaelekea kwenye kipato cha kati na huenda tukaingia kwenye kipato cha kwanza. Inshaallah Mwenyezi Mungu atujalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kitu Balozi ni kitu chenye hadhi kubwa sana, nchi yetu ina hadhi kubwa sana nchi za nje tofauti na tunavyoifikiria. Jina Tanzania ni Tanzania kweli. Nchi yenye ufahari, utulivu, mito, mimea na nchi yenye mali kila siku nchi hii inavumbua mali mbalimbali. Sasa, lazima tujitafaharishe na tujifaharishe zaidi kwamba hii ni nchi tamu na nchi ya kuishi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumebatika kutemebea nchi mbalimbali kama Amerika, Bara la Ulaya na nchi mbalimbali, nilipata

bahati ya kutembea Marekani katika Mji wa Seattle kwenye ujumbe na Makamu wa Rais wa Zanzibar. Jinsi ya utamu wa nchi hii kuna Mmarekani alitusimamisha aliuliza naomba msimame nikuulizeni maswali, ninyi mnatoka wapi, tukamwambia sisi tunatoka Tanzania akasema na mimi ni Mtanzania na kwa Kichaga akasema yeye alikuwa na Kihamba kwamba ana kijishamba chake cha Tanzania. Kwa hiyo, akasema ninyi mna nchi nzuri, utulivu wenu umefanya nchi ifunguke na nchi yenu imetulia na ina amani. Kwa hiyo, hongereni sana kuja hapa America. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya hayakuja tu lazma niwampongeze Mheshimiwa Waziri na timu yako Mheshimiwa Dkt. Mbarouk kwa kuisimamia vizuri, mnafanya kazi nzuri, hamlali na hamchoki, Mwenyezi Mungu akupeni afya na muihudumie zaidi nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika diplomasia ya kiuchumi kuna mambo na fursa mbalimbali zinapatikana hasa za uchumi. Mashirika yafuatayo yameweka mkono wazi kwetu Tanzania, kama vile *World Bank, IFAD, FAO, UNDP, African Bank, BADEA, Kuwait Fund* na mashirika mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unapochukuliwa Balozi iwe unapata ripoti ya kila siku kwamba neno gani au jambo gani Tanzania lina manufaa nchi iko wazi. Kwa utundu wangu kuna siku nilikaa mgongoni kidogo World Bank kwenye corridor zile mbili, nikapata na bahati nikakaa kidogo nikachukuliwa nikaona kwamba World Bank corridor mashirika makubwa ya dunia yamekaa yanagojea tuende tukawaombe au tukakape pesa zetu. Kwa mfano, Zanzibar mradi wa *PADEP*, mradi wa *MANCEP* hii ni juhudi binafsi za Makatibu Wakuu kwa wakati ule na viongozi, mradi ule leo unawafaa Wazanzibari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi kwa hapo tu naomba Balozi zetu zichangamke fursa zipo, zituletee maendeleo ili nchi iwe na neema kwa hii fursa ya uchumi wa Bluu. *(Makofi)*

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha.

**TAARIFA**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba, anayoyazungumza kuhusiana na Balozi zetu kuiendea kwa kasi dhana nzima ya diplomasia ya uchumi, Balozi zinapaswa kukumbuka pia zitafute uwekezekano wa nchi zetu kuanzisha benki katika zile nchi ambazo tunafanya nazo biashara kwa karibu. Kwa sababu tunaingiza *intermediate currency* ambayo inampotezea Mtanzania fedha nyingi anapokwenda kununua mizigo kama China na nchi za namna hiyo, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahya, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. AHMED YAHYA ABDULWAKIL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa ya Mheshimiwa *Engineer* Ulenge kwa mikono yote miwili. Basi mimi taarifa yangu ni hiyo Balozi zichangamke fursa zipo nyingi, nchi iendelee mbele ili lengo la Rais wetu litimie la diplomasia ya uchumi, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ahmed Yahya. Nilimtaja Mheshimiwa Elibariki Kingu.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa heshima na kutoa mchango wangu mdogo katika Wizara yetu hii muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mwanadiplomasia Namba Moja ambae ni Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan. Uimara wa Wizara hii ya Mambo ya Nje, chini ya Dada yangu na Kiongozi wetu Mheshimiwa Dkt. Stergomena Tax pamoja na Naibu wake, kwa kiwango kikubwa mafanikio na kukimbia kwa kasi kubwa sana katika diplomasia ya uchumi hatuwezi kutaja mafanikio haya na kumuacha Mheshimiwa Waziri wetu wa Mambo ya Nje, Dkt. Stergomena Tax na Naibu wake. Hongereni sana viongozi wetu

wazalendo mnampa Rais wetu heshima Kubwa, mnalipa Taifa letu heshima kubwa sana katika masuala mazima ya diplomasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme mambo yafuatayo; Wizara ya Mambo ya Nje ya Tanzania ndiyo roho ya mambo yote yanayohusiana na maendeleo ya uchumi ya Taifa la Tanzania. Wizara ya Mambo ya Nje inajihusisha na mambo makubwa yafuatayo ambayo baadhi ya Wabunge wameyasema. Hauwezi kuzungumzia suala la uwekezaji kwenye nchi yetu ya Tanzania bila kuigusa Wizara ya Mambo ya Nje, hauwezi kuzungumzia masuala ya utafutaji wa masoko bila kugusia Wizara ya Mambo Nje, hauwezi kuzungumzia Mambo ya Grants and loans bila kuzungumzia Wizara ya Mambo ya Nje, hauwezi kuzungumzia habari ya kuwavuta watalii kutoka katika pande zote za dunia bila kuzungumzia Wizara ya Mambo ya Nje, hauwezi kuzungumzia mafanikio ya mikutano mikubwa ya Kitaifa na Kimataifa ambayo Viongozi wote wa Kidiplomasia wa nchi wanahudhuria bila kuigusia Wizara ya Mambo ya Nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimkakati (Strategically) Wizara ya Mambo ya Nje tukiamua kuiweka kuwa Wizara ya Kimkakati ndiyo roho ya kufanya transformation ya uchumi na uwekezaji katika Taifa letu. Nimeyasema hayo kwa sababu tumekuwa tukiichukulia Wizara ya Mambo ya Nje kama Wizara tu ya watu kwenda kwenye mikutano. Nataka nikwambie, ninatoa rai kwa Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ni Wizara inahitaji kupewa fedha za bajeti kubwa ya kwanza kwenye Taifa hili ni Wizara ya Mambo ya Nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikupe mfano mdogo, hapa tunaposema tumejenga, tumejenga barabara kubwa, tukisema tunapanua bandari, juzi tumezungumza jambo la bandari hapa, ni nani walifanya juhudi kuhakikisha kwamba wawekezaji hawa wanapatikana ni Wizara ya Mambo ya Nje. Kitu cha ajabu inapofika kwenye kuzindua miradi hii hawa watu hata hakuna mtu anayejali wala kujua kwamba kazi kubwa ya kizalendo imefanywa na Wizara ya Mambo ya Nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuambie strategically as a nation kama tunataka kufanya transformation ya kiuchumi, transformation ya uwekezaji, transformation ya kukuza diplomasia ni sharti Serikali tubadilishe mindset watu hawa wapewe fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninapozungumza ni nani anaetafuta masoko ya parachichi za Tanzania ni Mambo ya Nje. Nani anamsaidia Mheshimiwa Mwigulu kwenda kutafuta mikopo? Mambo ya nje. Halafu, nenda ukaangalie bajeti yao utaona kama nchi bado hatujadhamiria kulibadilisha Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito Serikali kama tutakuwa tumechelewa mwaka huu na tunae Mwanadiplomasia Mama Tax, Kiongozi mtulivu na mwenye uwezo mkubwa sana, yeye na Naibu wake, kama tutakuwa tumechelewa mwaka huu tujipange mwaka unaofuata tudhamirie kuleta transformation ya kiuchumi tuweze ku–*empower* Wizara yetu ya Mambo ya Nje ili *FDI* zije za kutosha Taifa letu liweze kupiga hatua ili changamoto za ajira alizozisema Daktari na watu wengine ziweze kumalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nataka nizungumzia Zanzibar leo.

**MWENYEKITI:** Malizia nusu dakika.

**MHE ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba nimalize tu Zanzibar. Zanzibar hawana Wizara ya Mambo ya Nje, hili naomba niliseme na univumilie kidogo sana. Zanzibar hawana Wizara ya Mambo ya Nje, wanategemea Wizara yetu hii ya Mambo ya Nje kuweza kuwasaidia watu wetu wa Zanzibar katika kuleta *FDI* katika kuleta utalii na masuala mazima ya uwekezaji katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Wizara ya Mambo ya Nje, chochote mnachokifanya Mambunge mengine yatakuja tutawahoji ni uwekezaji kiasi gani umekwenda kwa wenzetu wa Zanzibar ambao ni partner iko kabisa katika Muungano huu tulionao wa Tanzania. Wazanzibari wanatakiwa wasaidiwe sana kwa sababu wao hawana

Wizara inayojitegemea nje ya hii. Mheshimiwa Waziri tunaimani na wewe tunakuomba, Rais Mwinyi anafanya kazi kubwa na nitaoa rai Rais Mwinyi apatiwe utulivu Zanzibar, aendelee kuijenga Zanzibar. Choko choko ziachwe Zanzibar ili Rais Mwinyi kwa uwekezaji huu ninaouzungumza aweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwishop lakini siyo kwa umuhimu ninaunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kingu.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawaita Waheshimiwa Mawaziri naomba nimalizie wageni ambao wako muda huu wasije wakaondoka. Kuna wageni ambao wapo ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni 21 wa Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge ambao ni Chawa wa Mama kutoka Mkoa wa Tanga wakiongozwa na Ndugu Ester Maghembe. *(Makofi)*

Kuna wageni 20 wa Mheshimiwa Fatma Toufiq wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 50 wa Mheshimiwa Justine Nyamoga, Viongozi wa UWT Kata zote wakiongozwa na Mwenyekiti wa Wilaya ya Kilolo, Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, vilevile tunao wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 50 na walimu Wanne kutoka Shule ya Sekondari ya Sanza - Manyoni Mkoa wa Singida. Karibuni sana wageni wetu katika Bunge letu. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa

Afrika Mashariki Mheshimiwa Dkt. Stergomena Tax na Naibu wake Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbaroruk na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya na mchango wangu utajikita kwenye suala la uraia pacha hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Watanzania wenzetu ambao wamezaliwa hapa nchini wakiwa na uraia wa asili wa kuzaliwa hapa Tanzania. Wenzetu hawa wengi waliondoka wakiwa watu wazima na uraia wetu wa kuzaliwa kwenda nje ya nchi na kupata uraia wa nchi nyingine kama sharti la kupata ajira huko ughaibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiuhalisia tukitafakari kwa undani, hawa ndugu zetu waliomba uraia wa nchi hizo kwa sababu za kiuchumi na ustawi wao wa kijamii na hii haiondoi ukweli kwamba wao ni Watanzania kwa kuzaliwa na kwa damu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria yetu ya Tanzania hairuhusu uraia pacha. Mtanzania akishapata uraia wa nchi nyingine, moja kwa moja sheria yetu inamnyang'anya uraia wa Tanzania. Baada ya kuukosa uraia wa Tanzania, miongoni mwa haki wanazozikosa nchini walikozaliwa ni pamoja na kutokuwa na haki ya kumiliki ardhi na kutokuchagua viongozi wala kushiriki kugombea nafasi ya umma katika uchaguzi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uraia wa Tanzania unaongozwa na Sheria ya Uraia Sura ya 357 Toleo la mwaka 2002 ambapo Serikali hairuhusu uraia pacha kwa watu wazima isipokuwa kwa watoto wenye umri chini ya miaka 18 ambao wanakuwa na uraia wa Tanzania na uraia wa nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kumekuwa na kilio cha kuomba uraia pacha kutoka kwa wenzetu waliozaliwa Tanzania kiasili na kupata uraia wa nchi nyingine, wakati sasa umewadia kwa Serikali yetu kuangalia muswada huo wa sheria na kuruhusu uraia pacha nchini kwa kuyaangalia maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia, inafaa uraia pacha utolewe kwa wale ambao walizaliwa Tanzania na kupata uraia wa

nchi nyingine. Tumeona sehemu zilizoruhusu uraia pacha kwenye baadhi ya nchi kumewezesha kupata viongozi wa juu wanaoongoza mataifa makubwa na mfano mzuri ni Waziri Mkuu wa Uingereza Rishi Sunak ambaye ana asili ya Taifa la India.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uraia pacha utaruhusu yafuatayo; kwanza Watanzania wanaoishi nje ya nchi watapata haki za kumiliki mali na ardhi, kufanya biashara, kupata huduma za afya, na kushiriki katika shughuli za kisiasa; pili, itawawezesha *diaspora* kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya kijamii na kiutamaduni ya nchi yao. Diaspora hawa huko waliko tayari wameshasaidia kudumisha na kukuza utambulisho wa Kitanzania; na tatu uraia pacha utawawezesha Watanzania wenzetu kushiriki kikamilifu na kuleta miradi ya maendeleo ya jamii, elimu, afya na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, *diaspora* inayokuwa na uraia pacha inaweza kuleta ujuzi, maarifa na mtaji wa kiuchumi kutoka nchi wanazoishi kuja Tanzania. Hii inaweza kusaidia katika kukuza sekta mbalimbali za uchumi kama vile viwanda, kilimo, utalii na huduma za kitaalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, raia kutoka nchi jirani za Afrika Mashariki kama vile Kenya, Rwanda na Uganda zimeruhusu uraia pacha. Ni vyema ikiipendeza Serikali yetu kujifunza kutoka kwa majirani zetu na kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hapo juu, kuna umuhimu wa kuangalia sheria yetu ya uraia wa Tanzania na ikiipendeza Serikali ifanye mabadiliko ya sheria ili kuruhusu kuwezesha uraia pacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Spika, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Serikali katika utekelezaji wa ustawi wa jamii na maendelo endelevu, na hii ni mojawapo ya nguzo kuu katika utayari wetu wa Ushindani wa Kimataifa *(National Competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ya kuimarisha mahusiano ya kimataifa, na pia kwa mafanikio makubwa ya *Royal Tour* ambayo imeanza kuleta matunda makubwa ya kiuchumi kwa nchi yetu hususani sekta ya kitalii na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Serikali kuimarisha diplomasia ya uchumi kwa lengo la kuongeza uwekezaji toka nje *(FDIs),* masoko ya uhakika kwa mazao ya kilimo, madini na utalii, pamoja na kuongeza mapato kwa Taifa letu, itaisaidia kuongeza fedha za kigeni na kuimarisha uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Naomba sasa nimuite Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwingi wa rehema kwa kuturuzuku uhai na afya njema na kutuwezesha kujadili hotuba hii siku ya leo. Aidha, nichukue fursa hii ya kipekee kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kuhudumu katika nafasi hii ya Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pia Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushauri na maelekezo yao katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumshukuru Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na wewe binafsi pamoja na wenyeviti wote kwa namna mnavyoliongoza Bunge letu kwa hekima, busara na umahiri mkubwa. Aidha, naomba kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, ulinzi na usalama kwa maoni na ushauri wao ambao wamekuwa wakitupatia na pia kupitia taarifa iliyowasilishwa asubuhi hii ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni Kamati makini sana na Wajumbe wake wana uelewa mkubwa wa masuala ya Kidiplomasia na hivyo wamekuwa wakitoa mchango mkubwa ambao umeendelea kusaidia na kuboresha utendaji wa kazi wa Wizara yetu na diplomasia ya nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Stergomena Tax, Mbunge, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa uongozi wake mahiri na ushirikiano mkubwa anaonipatia mimi binafsi na wenzangu ndani ya Wizara. Kwa hakika uongozi wake, miongozo yake na michango yake kwa kweli inatufanya kwenda katika *direction* nzuri zaidi na kuwa chachu ya ufanisi wa Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara yetu kwa ushirikiano mkubwa ninaoupata kutoka kwao, bila kuwasahau Mabalozi wetu wote ambao wanatuwakilisha sehemu mbalimbali duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninapenda kuishukuru familia yangu kwa upendo na uvumilivu wao kwa kuendelea kuniunga mkono wakati nikitekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijielekeze kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, lakini kwanza nianze kwa kutoa shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia na kutoa maoni yao katika hoja ambayo imeletwa na Mheshimiwa Waziri wetu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirkiano wa Afrika Mashariki. Vilevile, ninashukuru kwa pongezi nyingi ambazo Waheshimiwa Wabunge mbalimbali wamezitoa kwa Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, tunawaahdi Waheshimiwa Wabunge wote kwamba tunapokea pongezi hizi na kutekeleza majukumu yetu kwa bidii na ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu nitoe ufafanuzi wa hoja iliyoelezwa hapa kuhusu kuchelewa kwa ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Kwanza naomba nieleze kwamba pamoja na kuchelewa huko Tanzania muda wote huo imekuwa ikitekeleza wajibu wake kama *Host Country Agreement* kwa kuipatia Mahakama hiyo Ofisi za Mahakama, nyumba ya Rais wa Mahakama na nyumba ya Msajili wa Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo ili Mahakama hii iwe na majengo yake ya kudumu katika mwaka huu wa fehda kiasi cha shilingi bilioni Nne tayari zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama hiyo ambazo zitakuwa katika eneo la Laki Laki huko Arusha. Hivi sasa Wizara inakamilisha malipo ya awali kwa Mkandarasi na tarehe Mosi Juni, 2023 ambapo ni kesho kutwa tu, Wizara itakabidhi eneo la ujenzi

kwa Mkandarasi ili aweze kuanza maandalizi ya awali ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuna hoja hapa ilizungumzwa kuhusiana na changamoto za *visa* hasa kwa vijana wetu wanaokwenda masomoni nje ya nchi. Naomba nikiri kwamba ni kweli baadhi ya muda kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya vijana wetu ambao wanakwenda kusoma huko nje. Hata hivyo, Wizara imekuwa ikisaidia kwa kadri inavyoweza ili wanafunzi hao wapate VISA na hivyo kupata fursa ya kwenda kusoma. Aidha, ililetwa rai hapa kwamba Wizara ianzishe Idara ya Fursa lakini naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari kuna Idara ya Diplomasia ya Uchumi na kwa hiyo tunachukua huo ushauri wake ili hizo fursa hizo ziwe katika Idara ya Diplomasia ya Uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nieleze kuhusu Ofisi ya Wizara ya Mambo ya Nje iliyoko Zanzibar. Kwanza, tunashukuru sana kwa Mheshimiwa Mbunge Soud kutambua juhudi za Serikali za kuhakikisha kwamba tuko katika maeneo mazuri ya kufanyia kazi. Pia, naomba kulifahamisha Bunge lako kwamba, suala la wafanyakazi hivi sasa liko katika hatua za mwisho la kulipatia ufumbuzi na hivi karibuni kuna Maafisa kama wanne hivi wataajiriwa hapo. Pia kuhusu suala la samani tayari Wizara imekwishaweka samani nzuri za kisasa katika Jengo la Ofisi zetu huko Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la usafiri wa gari, naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari mwezi uliopita gari aina ya *landcruiser* tayari lilishapelekwa Zanzibar kwa ajili ya Ofisi zetu.

Mwisho kuhusu kujenga Ofisi zetu za kudumu, naomba kulieleza Bunge lako tukufu kwamba, hivi sasa tuko na majadiliano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili waweze kutupatia eneo hilo na tayari eneo hilo linaweza kupatikana eneo la Tunguru kwa ajili ya ujenzi huo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda umekwisha. Kwa hayo machache, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Mbarouk, sasa namkaribisha mtoa hoja Mheshimiwa Waziri Dkt. Stergomena Lawrence Tax ambaye ni Waziri wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Ahsanteni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni. Napenda nikushukuru kwa mara nyingine tena kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa ufafanuzi na kufanya majumuisho ya mjadala ambao umeendelea asubuhi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukupongeza kwa kuongoza na kusimamia mjadala wa bajeti yetu kwa umakini na umahiri mkubwa. Aidha, naishukuru Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa ushauri na miongozo waliyotupa kufuatia hotuba niliyoiwasilisha. Nawashukuru sana pia Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu mizuri sana. Tumeipokea michango yote na yotwe tutaifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru sana, sana kwa pongezi mahususi mlizozitoa kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya na yenye tija katika kuimarisha Uhusiano wa Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi na ambazo mmezitoa kwetu sisi wasaidizi wake. Napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu na Waheshimiwa Wabunge kuwa sisi wasaidizi wake katika Wizara tutaendelea kumsaidia ipasavyo na kutekeleza majukumu yetu kwa uaminifu, uadilifu na umahiri kadri ya uwezo wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwatambue na kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja niliyoitoa leo asubuhi na tumepokea maoni na ushauri na hoja kutoka kwa wajumbe 13 ambao wamechangia wote kwa kauli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya hoja hizo ambazo Waheshimiwa Wabunge na pia Kamati imezitoa zimejibiwa kwa ufasaha na Mheshimiwa Naibu Waziri wangu Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk na kutokana na ufinyu wa muda, nitajitahidi kujibu baadhi ya hoja lakini tu niwahakikishie kwamba hoja zote zitajibiwa kwa maandishi. Wamechangia Waheshimiwa Wabunge 13 ikiwa ni pamoja na Kamati, lakini michango imekuwa mingi sana na mizuri, tunawashukuru, tutaijibu yote kimaandishi. Kwa hiyo, naomba sasa nijielekeze katika kutoa ufafanuzi katika baadhi ya hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hoja ya Mheshimiwa Kingu ambaye amesisitiza kwamba tuhakikishe tunaishirikisha Zanzibar kikamilifu. Naomba nikuhakikishie kwamba hili linafanyika na huu ndiyo msisitizo ambao tumepata muda wote kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wanaokumbuka wakati nikiapishwa, alisisitiza vitu vitatu na kimoja kilikuwa ni kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inatambua pande zote mbili za Muungano. Kwa hiyo, sio mimi tu, Wizara kwa ujumla hili tunalifahamu na tunalitekeleza asilimia 100 ikiwa ni pamoja na uwekezaji katika maeneo mbalimbali. Katika misafara yote tunahakikisha tunajumulisha pande zote mbili za Muungano, katika majadiliano yote tunahakikisha tunafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa nimetoa ufafanuzi kwenye hoja hiyo hoja, nyingine ambayo imejadiliwa kwa hisia na kwa msisitizo mkubwa ni kuhusu utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi. Hii imeongelewa na Kamati na Waheshimiwa Wabunge wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Diplomasia ya Uchumi, nianze kusema tu kwamba ni kitu mtambuka. Watekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi ni sekta zote na ni katika Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Kwa hiyo, mpaka sasa mafanikio yamekuwepo makubwa kama nilivyosema kwenye hotuba yangu katika utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi. Pia tumebaini kama mlivyosema wenyewe kwamba uelewa kuhusu Diplomasia ya Uchumi bado ni mdogo. Tunakiri hilo. Kwa kulitambua hilo na kwa msisitizo mkubwa ambao umewekwa na

Kamati yetu ya Bunge ya *NUU,* tumeanza maandalizi ya kutekeleza mpango mkakati wa utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi. Mpango huu utatoa tafsiri, nini Diplomasia ya Uchumi? Mpango huu utaainisha wadau wote katika utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposema wadau wote ni katika sekta zote; Sekta ya Umma, Sekta Binafsi, lakini katika Sekta ya Umma ninatambua kwamba tunakwenda mpaka chini. Tunakwenda mpaka TAMISEMI, tunaihusisha mikoa na Wilaya, na utaainisha majukumu na pia tutaweka mpango wa ufuatiliaji kujua inatekelezwa namna gani? Kwa sababu kulikuwa na hoja, kwamba tuwawekee malengo Balozi zetu. Wao pia watakuwa ni sehemu ya utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mtuunge mkono tukamilishe kazi hii ambayo tumejipangia kuikamilisha mwishoni mwa mwaka huu kama ambavyo pia Kamati imesema tukamilishe mwisho wa mwaka wa fedha ujao, lakini sisi lengo letu ni kukamilisha kufikia Desemba mwaka huu 2023. Kwa hiyo, baada ya kuwa tumekamilisha hili, basi tutaweka bayana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba pia ieleweke kwamba sisi kama Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kazi yetu ni kuratibu, watekelezaji ni sekta zote. Nimesikia hoja kwamba tuweke dirisha Wizarani la kufuatilia utekelezaji. Tukishamaliza mpango huu, tutajua kila mmoja anajukumu gani na mmoja atatakiwa kutekeleza mahali pake. Kwa hiyo, sisi kama Wizara, kazi yetu itakuwa ni kufuatilia tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linakwenda pamoja na hoja kwamba tuweke wataalamu mahususi kwenye maeneo muhimu katika Balozi zetu. Tutaweza kulifanya hilo baada ya ya kukamilisha huu mkakati. Kwa sababu mkakati huu pia unalenga kujua katika nchi mbalimbali tunalenga nini? Tukishajua tunalenga nini kule, tutajua pia tunaweka wataalamu wa aina gani? Kwa hiyo, tuvute Subira, tutaendelea kufanya hivyo, lakini siyo kwamba hatupeleki wataalamu, tunapeleka wataalamu hata sasa ambao ni wataalam mahususi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo imeongelewa kwa mkazo ni kuhusu Sera ya Mambo ya Nje kuikamilisha. Hili naomba tu niwahakikishie kwa kujiamini kabisa kwamba sera hii tunaikamilisha ndani ya mwaka huu wa fedha. Tuko mbali sana, tunajua umuhimu wake, Kamati imetusukuma kweli kweli na sisi tumesukumika, kwa hiyo, tunaahidi kwamba sera hii sasa itakuwa tayari. Imechukua muda kidogo kwa sababu mwanzo tulidhani kwamba tunaandaa sera mpya, lakini kadri tulivyoendelea tukabaini kwamba hatuna haja ya sera mpya. Iliyopo misingi yake inakidhi, tunachotakiwa sasa ni kuweka maeneo mapya ambayo yanapungua kama nilivyoyaainisha kwenye hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo imejitokeza kwa sana ni suala la Hadhi Maalum na Uraia Pacha. Nashukuru wachangiaji na nimefurahi kwamba alichokisema Mheshimiwa Prof. Kabudi kimejitokeza hata kwenye mijadala yetu kwamba bado hili suala halijawa na muafaka wa pamoja, siyo nchini kwetu tu, lakini hata nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kwa kutambua umuhimu wa kuhakikisha kwamba *Diaspora* ambao wapo nje ya nchi ambao ni raia na wale wenye asili, tuna *definitions* mbili za *Diaspora* kama zilivyotolewa, wote wanapata haki, kwa hiyo, akatoa msisitizo kwamba tufanye mchakato wa kutoa Hadhi Maalum. Pamoja na kwamba Katiba yetu inasema nini, lakini msingi ni kuhakikisha kwamba wote wanapata fursa tunazoweza kuziandaa katika Hadhi Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi nyingine, Mheshimiwa Prof. Kabudi ametoa takwimu kama ni nchi 49 tu zinazotoa Uraia Pacha. Sasa ukitoa Uraia Pacha kwa sasa hivi wakati hakujawa na muafaka kitaifa na kidunia, kuna wale watakaokosa fursa, kwa sababu kwenye nchi ambazo *Diaspora* zipo na zile nchi hazitambui Uraia Pacha, sisi tukitoa Uraia Pacha, wale hawatapata fursa ambazo tunatarajia kuzitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili kuweza kutoa fursa kwa wote, Mheshimiwa Rais kwa busara yake akahimiza kwamba tutoe hii Hadhi Maalum, tena kwa haraka. Huu mchakato Waheshimiwa

Wabunge umefika mbali sana, kufikia mwisho wa mwaka huu hii Hadhi Maalum itakuwa imetolewa. Inatoa fursa nyingi tu. Walileta mapendekezo kumi, mapendekezo yote hayo tumeyazingatia na yote yataingizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mchango wa Mheshimiwa Prof. Kitila, bahati mbaya katika yale mapendekezo hakukuwa na pendekezo la Haki ya Kimungu. Kwa hiyo, tutaenda kuliangalia hilo pendekezo la Haki ya Kimungu linaingia namna gani, lakini siyo miongoni mwa mapendekezo yaliyoletwa na *Diaspora*. *Diaspora* wanachotaka ni kuweza kuingia nchini, kumiliki ardhi, kupata huduma kwenye taasisi za fedha na kadhalika na yote hayo yamezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kabla sijamalizia hoja hii, napenda sana kuzishukuru Taasisi zinazotusaidia. Tumepongezwa hapa kuhusu mfumo wa kuandikisha *Diaspora* wetu kidigitali. Tumefanya kazi hii na sekta binafsi ikiwa ni pamoja na *CRDB, NMB* na *NSSF*. wanafanya hivyo kwa uzalendo wao, lakini kwa kujua kwamba na wenyewe ni wanufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa tunazoziongelea ni pamoja na huduma mbalimbali. Kwa hiyo, *diaspora* anapojiandikisha katika mfumo huu, watapata fursa za kiuchumi na kijamii, watapata fursa za ajira na pia watapata fursa zinazotolewa na taasisi mbalimbali ikiwa ni pamoja na hata Uhamiaji. Kwa hiyo, nihamasishe *diaspora* wetu waweze kujiandikisha na kutumia huu mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine iliyoongelewa ni suala la majengo kwamba Balozi zetu ziko katika hali mbaya. Ni kweli lakini hapa suala wala siyo kukosekana kwa fedha kutoka Hazina. Maana yake nisije nikarudi Hazina Mheshimiwa Mwigulu akaninyima pesa, akasema wewe umeenda kusema pesa hazitoki wakati na upungufu pia uko kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumebaini kwamba tulikuwa hatuko tayari. Ndiyo maana Kamati imesisitiza kwamba tuhakikishe taratibu zinakamilika mapema na maombi ya pesa yanapelekwa mapema. Hilo niwahakikishie Kamati tutalifanya, lakini pesa ya Serikali haitoshi.

Ndiyo maana tumeandaa huu mpango ambao nimeueleza katika hotuba yangu kwamba tuna mpango wa kushirikisha sekta binafsi. Tumeshaainisha miradi yote ya kipaumbele, tumeshaainisha changamoto zote, tumeshaainisha mfumo tutakaotumia na tumeshaainisha jinsi ya kutatua hizo changamoto. Habari njema ni kwamba tayari miradi miwili tumeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hatua kubwa sana kwamba *NSSF* wanashirikiana na sisi katika kujenga kitega uchumi chetu na Ubalozi wetu Nairobi, na sasa tuko katika hatua za mwisho pia waanze kufanya Kinshasa, lakini wapo hata na wabia waliotoka nje ya nchi ambao tuko katika mazungumzo nao. Kwa hiyo, tuna imani kwamba hili sasa linaenda kufanyika. Naomba tu mtuunge mkono na mtutafutie hao wabia ambao wako tayari kuja kufanya kazi na sisi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda wangu umeisha. Kulikuwa na hoja ya kutotumia fursa zitokanazo na ushirikiano wa kikanda, tunalipokea tunalifanyia kazi na tumeendelea kulifanyia kazi. Misaada ya asasi kutoka sekta zisizo za kiserikali tuiangalie, tumeipokea; ajira nchi za nje, Mheshimiwa Naibu Waziri amelitolea maelezo; ajira katika Mashirika ya Kimataifa, tunafanya kazi, siyo kwamba halifanyiwi kazi, ila labda tuongeze juhudi, kwa sababu hapa kuna changamoto za ndani, za nje na kuna za uelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Neema kwa kusisitiza kwamba yako maeneo ambayo hata kama tunatoa Hadhi Maalum na Uraia Pacha ni maeneo mabayo lazima kama nchi tuyalinde. Nakushukuru sana kwa msisitizo huo. Chuo cha Diplomasia tumepokea. Kuhusu vikwazo kwa wafanyabiashara, kweli ni tatizo na tunavifanyia kazi. Hapa kulikuwa na tatizo kubwa ambapo wafanyabiashara wetu walikuwa wamenyimwa vibali ili watoe mahindi Zambia ambalo limechukua muda mrefu, lakini napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba sasa suala hili limetatuliwa na wafanyabiashara hawa wamepewa vibali siku ya leo. Kwa hiyo,

tutaendelea. Haziwezi kwisha. Katika ushirikiano wa kimataifa na kikanda, vikwazo vinakuwepo. Kinachotakiwa ni kwamba muda wote kuwa macho na kushirikiana na wale wenzenu na kuhakikisha kwamba vikwazo hivyo vinatatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha, naomba niseme kwamba baadhi ya mambo ambayo yamesisitizwa hapa ni mambo ambayo yanafanyiwa kazi katika Kamati iliyoundwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, baada ya kuwa ameshazibaini changamoto mbalimbali zinazoikwaza Wizara yetu. Kamati hii isichukuliwe kwamba inapima utendaji wa Wizara kama utendaji wa Wizara kwa maana ya watumishi, inaangalia picha kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi haya mliyosema ya Diplomasia ya Uchumi, mambo mliyosema kwamba ni aina gani ya watumishi tuwe nao, mambo gani tujipange, tunajipanga namna gani, dunia ya sasa inakwenda namna gani? Twende namna gani? yote yataangaliwa katika kazi inayofanywa na hii Kamati. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba Kamati hii itakapomaliza kazi yake, basi tutakuwa tumepata suluhu ya mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa nitoe hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, hoja imeungwa mkono. Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA-KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(2) tunaingia kwenye mafungu ya jumla.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*…....................................Sh.17,654,050,819
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*.....................Sh. 2,750,375,244
Kifungu 1003 - *Foreign Affairs Office Zanzibar*.................Sh. 1,391,034,000
Kifungu 1004 - *Policy and Planning Unit*..........................Sh. 4,118,845,300
Kifungu 1005 - *International Cooperation*……..……...Sh. 1,554,994,000
Kifungu 1006 - *Europe and America*................................Sh. 4,795,173,200
Kifungu 1007 - *Asia and Australia*.....................................Sh. 5,500,512,000
Kifungu 1008 - *Africa*…………………………………………Sh. 4,801,313,013
Kifungu 1009 - *Regional Cooperation*…………………….Sh. 1,383,216,000
Kifungu 1010 - *Protocol*……………………………………..Sh. 5,967,369,052
Kifungu 1011 - *Legal Services Unit*…………………………Sh. 2,667,908,850
Kifungu 1012 - *Government Communication Unit*.............Sh. 900,903,416
Kifungu 1013 - *Middle East Division*..................................Sh. 1,607,432,000
Kifungu 1014 - *Internal Audit Unit*.......................................Sh. 782,524,797
Kifungu 1015 - *Procurement Management Unit*.................Sh. 706,778,085
Kifungu 1016 - *Information and Communication Technology Unit*..........................................Sh. 974,960,000
Kifungu 1017 - *Diaspora Engagement and Opportunity*...Sh. 968,358,080
Kifungu 1018 - *Economic Infrastructure and Social Support Services Division*...........................Sh.1,187,904,000
Kifungu 1019 - *Political, Defence and Security Affairs*.....Sh.1,079,576,000
Kifungu 1020 - *Trade, Investment and Productive Sector Division*...........................................Sh.1,372,300,000

Kifungu 1021- *Economic Diplomacy Division*.....................Sh.  641,675,000
Kifungu 2001- *Embassy of Tanzania - Addis Ababa*.........Sh.3,322,476,659
Kifungu 2002 - *Embassy of Tanzania – Berlin*.....................Sh.4,590,409,069
Kifungu 2003 - *Embassy of Tanzania – Cairo*.....................Sh.3,711,261,477
Kifungu 2004 - *Embassy of Tanzania - Kinshasa*…………..Sh.4,373,739,488
Kifungu 2005 - *High Commission of Tanzania – Abuja*.....Sh.4,549,692,840
Kifungu 2006 - *High Commission of Tanzania – London*..Sh.5,620,981,865
Kifungu 2007 - *High Commission of Tanzania – Lusaka*....Sh.2,333,076,099
Kifungu 2008 - *High Commission of Tanzania – Maputo*..Sh.2,286,865,035
Kifungu 2009 - *Embassy of Tanzania - Moscow*…………Sh. 4,022,847,955
Kifungu 2010 - *High Commission of Tanzania – New Delhi*...................................................Sh. 4,294,067,465
Kifungu 2011 - *Permanent Mission to The Un - New York*…......................................…Sh. 5,453,308,180
Kifungu 2012 - *High Commission of Tanzania -Ottawa*…Sh.3,115,525,245
Kifungu 2013 - *Embassy of Tanzania - Paris*………………Sh. 3,759,634,660
Kifungu 2014 - *Embassy of Tanzania - Beijing*……………Sh. 4,567,114,961
Kifungu 2015 - *Embassy of Tanzania - Rome*……………...Sh.4,475,773,678
Kifungu 2016 - *Embassy of Tanzania - Stockholm*………..Sh.5,052,251,586
Kifungu 2017 - *Embassy of Tanzania - Tokyo*……………..…..Sh.4,537,071,973
Kifungu 2018 - *Embassy of Tanzania - Washington*……..Sh. 4,723,445,850
Kifungu 2019 - *Embassy of Tanzania - Brussels*……………Sh.4,849,591,000
Kifungu 2020 - *Permanent Mission to The Un – Geneva*......................................Sh. 6,175,330,460
Kifungu 2021 - *High Commission of Tanzania – Kampala*..................................................Sh. 2,402,532,983
Kifungu 2022 - *High Commission of Tanzania - Harare*…Sh. 2,475,643,365
Kifungu 2023 - *High Commission of Tanzania – Nairobi*..Sh. 4,591,387,010
Kifungu 2024 - *Embassy of Tanzania - Riyadh*……………Sh. 3,475,562,190
Kifungu 2025 - *High Commission of Tanzania – Pretoria*.....................................................Sh. 3,461,159,135
Kifungu 2026 - *Embassy of Tanzania - Kigali*……………...Sh. 2,076,896,300
Kifungu 2027 - *Embassy of Tanzania - Abu-Dhabi*...........Sh. 5,340,797,843
Kifungu 2028 - *Embassy of Tanzania - Bujumbura* ………Sh.2,032,578,310
Kifungu 2029 - *Embassy of Tanzania - Muscat* …………...Sh.2,750,430,760
Kifungu 2030 - *High Commission of Tanzania – Lilongwe*.....................................................Sh.2,289,090,975
Kifungu 2031 - *Embassy of Tanzania - Brasilia*…………....Sh. 3,572,388,925

Kifungu 2032 - *High Commission of Tanzania –
Kuala Lumpa*…......................…..………Sh. 2,642,878,315
Kifungu 2033 - *Embassy of Tanzania - The Hague*...........Sh. 3,602,653,153
Kifungu 2034 - *Embassy of Tanzania – Moroni*.................Sh. 2,913,563,431
Kifungu 2035 - *Embassy of Tanzania – Kuwait*...................Sh.2,316,918,370
Kifungu 2036 - *Embassy of Tanzania - Algiers*……………Sh. 2,780,369,200
Kifungu 2037 - *Embassy of Tanzania - Ankara*……..……Sh. 3,759,755,490
Kifungu 2038 - *Embassy of Tanzania - Khartoum*……….Sh. 2,379,341,685
Kifungu 2039 - *Embassy of Tanzania - Seoul*……………...Sh. 6,218,947,098
Kifungu 2040 - *Embassy of Tanzania - Tel-Aviv*.................Sh. 3,884,584,122
Kifungu 2041 - *Embassy of Tanzania - Doha*……………...Sh.3,252,858,591
Kifungu 2042 - *Embassy of Tanzania - Havana*…………Sh. 3,121,342,210
Kifungu 2043 - *Embassy of Tanzania - Windhoek*……….Sh. 2,988,394,465
Kifungu 2044 - *Embassy of Tanzania - Jarkata*……………Sh.2,779,682,742
Kifungu 2045 - *Permanent Mission to the Un – Vienna*.....Sh.4,352,490,931

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Miradi ya Maendeleo**

Kifungu 1004 - *Policy and Planning Unit* ……………….Sh.17,887,608,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Karibu Mtoa hoja. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 122(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi yake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. Sasa natangaza rasmi kwamba Bajeti hii ya Wizara yetu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, imepitishwa na Bunge hili. Kwa hiyo, tuwapongeze sana wote ambao wameshiriki kwa njia moja ama nyingine katika kuandaa hadi kuchangia na kufikia hapa tulipofikia.

Kipekee niishukuru Kamati ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama ikiongozwa na Mwenyekiti, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Vincent Mbogo, pamoja na wajumbe wote kwa kazi kubwa wanayoifanya hadi kufikia leo kuweza kukamilisha kazi hii.

Pia nawashukuru Wabunge wote kwa michango yenu mizuri. Naamimi kabisa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na timu yao nzima wamesikiliza kwa makini kabisa na michango mingi ni yenye kujenga kwa masilahi ya Taifa letu. Basi, nami niwatakie kila la heri katika kutekeleza majukumu hayo ambayo mmeyapanga nikiamini kabisa Mwenyezi Mungu atawafanyia wepesi ili mweze kukamilisha kwa wakati kazi ambazo mmeahidi katika nchi yetu, hasa suala hili la Hadhi Maalum kwa wananchi wetu wa *Diaspora* wanaoishi nje ya nchi. Naamini huko waliko watakuwa na faraja kubwa, na ninaendelea kuomba Mungu kwamba jambo hilo liweze kukamilika kwa wakati ili na wao wapate haki yao inayostahiki kama wananchi wa Tanzania.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema maneno hayo, Mheshimiwa Balozi Mulamula anaomba yeyote ambaye ataona kishikwambi chake ambacho anahisi kimeachwa kwenye sehemu ya *security,* basi arudishiwe mwenyewe ili aweze kuwa nacho.

Waheshimiwa Wabunge, pia nawakumbusha kwamba baada ya kuahirisha shughuli za Bunge mchana huu, msisahau semina ile ya wenzetu kutoka *COSATA*.

Baada ya kusema hayo, niwatakie mchana mwema na kila la heri, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho sasa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.40 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 31 Mei, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*